

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 2 Mei, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae, tunaendelea na Mkutano wetu wa Saba, leo ni Kikao cha Kumi na Tano.

Katibu!

NDG. NENELWA M. WANKANGA – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**NDG. ALMAS A. MAIGE - MAKAMU MWENYEKITI WA
KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:**

Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shauri la Kudharau Mamlaka ya Spika

linalowahusu Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe na Mheshimiwa Halima James Mdee.

Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shauri la Kuingilia Uhuru na Haki za Bunge linalowahusu Ndugu Paul Christian Makonda na Ndugu Alexander Pastory Mnyeti.

Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shauri la Kudharau Mamlaka ya Spika linalomhusu Mheshimiwa Ester Amos Bulaya.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Naomba Katibu hizo taarifa Waheshimiwa Wabunge wagaiwe mapema. Katibu tuendelee.

NDG. NENELWA M. WANKANGA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Swali la kwanza linaulizwa na Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Kaskazini.

Na. 119

Ujenzi wa Barabara ya Mwandiga - Chenkele - Kagunga

MHE. PETER J. SERUKAMBA aliuliza:-

Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye kampeni aliahidi kuanza ujenzi wa barabara ya Mwandiga – Chankele – Kagunga.

Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mwandiga – Chankele - Kagunga yenye urefu wa kilometra 55.76 ipo katika eneo la mwambao wa Ziwa Tanganyika. Tayari upembuzi yakinifu umefanyika na kubaini kuwa zinahitajika shilingi bilioni saba kuweza kujenga barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uwezo mdogo wa Halmashauri, ilikubalika kuptitia Kikao cha Bodi ya Barabara cha Mkoa wa Kigoma, iweze kuhudumiwa na Wakala wa Barabara Mkoa (*TANROADS*). Maombi hayo yamewasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana na ujenzi kwa ajili ya kupata kibali.

SPIKA: Swali la nyongeza, Mheshimiwa Peter Serukamba.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri hakuwasiliana na watu wa ujenzi, kwa hiyo, kinachoendelea ni zaidi ya hiki alichokisema. Kwa hiyo, naomba labda hili swali nilitoe.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, swali la nyongeza.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa ameshaikagua barabara ya kutoka Gulwe – Berege – Chitemo – Mima – Chazima - Igodi Moja – Igodi Mbili mpaka Seluka; na kinachosubiri sasa hivi ni barabara hii ipandishwe hadhi ili iwe barabara ya Mkoa.

Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje na kwa ombi hilo Serikali inawaambiaje wananchi wa maeneo hayo?

SPIKA: Hili lilikuwa ni la watu wa ujenzi wenyewe, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri kama una maelezo kidogo, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lubeleje, graderla zamani, makali yale yale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lubeleje swali hili alikuwa akiliuliza mara kadhaa na hapa umesema kwamba ni kweli. Kwa sababu naamini wenzetu wa Wizara ya Ujenzi jambo hili walishalisikia na ninakumbuka Naibu Waziri wa Ujenzi siku ile alikuwa analizungumza suala hili kwamba jambo hili linafanyiwa kazi. Imani yangu ni kwamba kwa sababu barabara hii ni ya kimkakati nami nakiri wazi kwamba na wewe barabara hii inakuhusu katika eneo lako. Basi naamini Wizara ya Ujenzi itafanya kila liwezekanavyo barabara hii kuipa kipaumbele katika yale matakwa ya wananchi wa eneo hilo.

SPIKA: Ahsante sana. Swali linalofuata ni la Mheshimiwa Saumu Heri Sakala, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 120

Mpango wa Kutengeneza Magari ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani

MHE. SAUMU H. SAKALA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza magari yaliyopo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Pangani kwa haraka kutokana na uhaba wa magari unaosababishwa na ubovu wa magari?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saumu Heri Sakala, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Pangani ina jumla ya magari 15 ambapo kati ya hayo magari 11 yanafanya kazi. Matengenezo ya magari ya Halmashauri yanafanyika kupitia fedha za matumizi mengineyo zinazotengwa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri hiyo iliidhinishiwa shilingi 52,500,000 kwa ajili ya matengenezo ya magari na katika mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri hiyo imetengewa shilingi milioni 73. Hivyo, Halmashauri inashauriwa kuweka kipaumbele na kuhakikisha fedha zinazotengwa zinatumika kutengeneza magari ili kuimarisha usimamizi wa Halmashauri.

SPIKA: Mheshimiwa Saumu, nilikuona, swali la nyongeza.

MHE. SAUMU H. SAKALA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ambayo nimepata kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ningependa kumweleza kuwa Hospitali ya Wilaya ya Pangani ina magari mawili tu kati ya hayo magari 11 ambayo umeyataja, lakini magari yale ni chakavu mno kiasi kwamba yanapoenda *service* basi yanalahazimika kutengeneza kitu zaidi ya kimoja yaani sio *service* tu ya kawaida, lazima unakuta na vitu vingine vinakuwa vimeharibika pale.

Mheshimiwa Spika, Serikali pengine haioni umuhimu wa kununua magari mengine mapya badala ya kuacha magari yale chakavu yaendelee kutumikia Hospitali ya Wilaya ya Pangani? Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo la magari chakavu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, ni kweli, na mimi

nilivyofika Pangani, Mheshimiwa Mbunge anakumbuka nimefika pale nimeona changamoto hii ya magari. Magari yale ni kweli ni mionganoni mwa magari chakavu kama ilivyo katika Halmashauri nyingine. Nikijua wazi kwamba kipaumbele cha kununua magari ya Halmashauri huwa yanafanywa hasa na Halmashauri yenye we ikianzia katika mchakato wa awali. Hata hivyo, Serikali katika kuimarisha huduma ya afya, tulinunua karibu magari 50 tukapeleka katika maeneo ambayo vipo vifo vingi zaidi. Hata hivyo tuna mkakati mwingine, tukipata gari la ziada tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, suala la ununuzi wa magari naomba watu wa Halmashauri ya Pangani tuweke kipaumbele, lakini Serikali haitasita kusaidia wananchi wa Pangani tukijua wazi Jimbo lile na eneo lile jiografia yake iko tata sasa; ukitoka pale Hospitali watu wa Mwela huku na watu wa upande mwingine wana changamoto kubwa sana mpaka kwenda eneo lile.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali tunaliangalia hilo, lakini tutashirikiana vyema na wenzetu wa Pangani kuhakikisha mambo yao yanaenda vizuri. (*Makofii*)

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Saddiq Murad, swali la nyongeza.

MHE. SULEIMAN A. SADDIQ: Mheshimiwa Spika, naomba nami niulize swali moja dogo la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Waziri umetembelea Wilaya ya Mvomero na umejionea mwenyewe hali halisi ya Wilaya; leo gari la afya ambalo linatumika kwa ajili ya chanjo ndilo linatumika kwa ajili ya kukusanya mapato, lakini Idara ya Ujenzi haina gari, magari yote ni chakavu.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kutusaidia sisi watu wa Mvomero ili tuweze kuendana na kasi ya Serikali ya Awamu ya Tano?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, anachosema ni kweli. Siku ya Alhamisi tulikuwa Jimboni kwake pale na tulitembelea mpaka Hospitali ya Wilaya na kubaini changamoto na jiografia ya eneo lile kuanzia Turiani na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, eneo lile ni kweli, hata nilipokutana na wataalam pale, kuna changamoto ya magari. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama nilivyosema pale awali ni kwamba mchakato wa ununuzi wa magari mara nydingi sana unaanza na kipaumbele cha Halmashauri yenyewe, lakini kwa sababu tuko pamoja hapa na Mbunge siku ile tulikubaliana mambo mengine ya msingi. Tutaendelea kushirikiana vya kutosha kuona ni jinsi gani tutaiwezesha Halmashauri ya Mvomero iweze kufanya vizuri. Ndiyo maana Serikali hata katika suala zima la miundombinu, wewe unafahamu jinsi tunavyowekeza pale hata katika ujenzi wa lami. Lengo kubwa ni kwamba wananchi wa Mvomero wapate matunda mazuri ya Mbunge wao.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itashirikiana naye, pale kwenye mahitaji ya haraka tutafanya kwa ajili ya wananchi wake na watendaji waweze kufanya kazi vizuri katika Jimbo la Mvomero. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Afya, majibu ya nyongeza.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kutumia Bunge hili kupiga marufuku magari ya chanjo kutumika kwa shughuli tofauti na chanjo. Kuanzia sasa hivi magari ya chanjo tutayandika herufi kubwa neno "CHANJO" na lisitumike kwa matumizi mengine yoyote. Kwa sababu chanjo ni muhimu kuliko masuala mengine katika Halmashauri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, niliona nitumie Bunge lako kutoa ufanuzi. Kwa hiyo, ni marufuku Halmashauri ya Mvomero kutumia gari la chanjo kwa ajili ya kukusanya mapato. Ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa, swali moja fupi, dogo la nyongeza.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Bukoba Vijiji ni Wilaya ambayo ina jiografia kubwa na magari ya Bukoba Vijiji yote hasa ya hospitali ni mabovu. Juzi imetolewa *ambulance*, badala ya kupelekwa kwenye Hospitali ya Wilaya ya Izimbya ikapelekwa kwenye Zahanati ya Kishanji. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri ndivyo mlivyopanga au ni mipango ya Halmashauri? (*Makofi*)

SPIKA: Poleni sana Bukoba kwa tetemeko lingine tena la juzi. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, tumelisikia hili. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Afya, lengo letu kubwa ni kwamba haya magari ya chanjo yakienda katika maeneo yafanye kazi inayokusudiwa. Sasa kwako wewe kuna *scenario* tofauti kwamba gari lilitakiwa liende katika hospitali lakini limeenda katika zahanati, lakini ninachoamini ni kwamba kule kuna *DMO*, viongozi na Mkurugenzi pale, inawezekana kuna jambo ambalo tutaenda kulifanyia kazi tujue nini kilichoendelea.

Mheshimiwa Spika, letu kubwa ni kuhakikisha tunazozipeleka resourcesna hasa katika sekta ya afya, lazima watu wasimamie mwongozo huu. Gari kama ni la afya litumike kwa ajili ya afya. Ndiyo maana sasa hivi mikoa mingine hata kiwango cha chanjo wanashuka kumbe ni kwa sababu hawazingatii miongozo maalum ya Serikali ambayo tunaelekeza kila siku. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Shing'oma, Mbunge wa Nyamagana.

Na. 121

Fedha Iliyotengwa na Halmashauri kwa Ajili ya Wanawake na Vijana

MHE. STANSLAUS S. MABULA aliuliza:-

Fedha zinazotengwa na Halmashauri kutokana na mapato ya ndani; asilimia 10 ya fedha hizo zinatakiwa kwenda kwa vijana na wanawake na zinatakiwa ziwafikie walengwa kila mwaka bila kukosa.

Je, Serikali iko tayari kutoa agizo la msisitizo kwa Halmashauri zote nchini kutenga fedha hizo na wala wasichukulie kama ni hisani?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zote zinatakiwa kutekeleza agizo la kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Vijana na Wanawake. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri zilitengewa jumla ya shilingi bilioni 56.8 ambapo hadi Machi, 2017 kiasi kilichopelekwa kwenye mifuko kilikuwa ni shilingi bilioni 16.05. Halmashauri ya Jiji la Mwanza pekee imeshapeleka shilingi milioni 147.0.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuanza kutenga maeneo rafiki ya kufanya biashara kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo, kupeleka fedha kwenye mifuko na kusimamia marejesho ili ziweze kunufaisha makundi mengine. Utekelezaji wa maagizo haya

ya Serikali ni kipimo cha utendaji kwa Wakurugenzi wote nchini na kushindwa kutekeleza, sio vyema kabisa. Aidha, hatua zitachukuliwa kwa kuzingatia taratibu zilizopo.

SPIKA: Mheshimiwa Mabula, swali la nyongeza.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili madgo ya nyongeza.

Swali la kwanza, pamoja na jitihada kubwa ambazo zimeshafanywa na Halmashauri yangu ya Jiji la Mwanza, namshukuru sana tu Mkurugenzi kwa jitihada zake anazozifanya kuhakikisha anasaidia wanawake na vijana wa Jiji la Mwanza kujikomboa.

Mheshimiwa Spika, niulize tu kwamba inawezekana haya yanafanyika vizuri kwenye Halmashauri ambazo Wakurugenzi wengi wana utashi wa kusaidia makundi haya. Ni nini sasa mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba fedha hizi zinapaswa kutolewa siyo kwa hiyari, iwe ni kwa lazima kwa mujibu wa makusanyo ya mapato ya ndani ili kuwanufaisha vijana wengi zaidi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pili, je, Serikali haioni sasa ni wakati muhimu wa kuongeza asilimia hizi kutoka 10 mpaka 15 kwa sababu ni ukweli usiofichika kwamba vijana na wanawake wanaendelea kuongezeka zaidi hasa katika masuala mazima ya kujitafutia riziki na familia zao pia ili waweze kujikwamua kiuchumi? Nakushukuru. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Said Jafo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anauliza kwamba ni jinsi gani tutaweka uwe kama mkakati wa kisheria; ni kweli ukija kuangalia hata taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2013/2014, kuna *outstanding* ya fedha ambazo zilitakiwa zipelekwe karibu shilingi bilioni

37 hazikuweza kupelekwa. Ndiyo maana katika bajeti ya mwaka 2016/2017 tulitoa maelekezo mahususi kwa Wakurugenzi wote kama ndiyo mionganii mwa *guideline* kutengeneza bajeti ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, vilevile tuseme kwa kuwa tumeona kuna changamoto kwa Halmashauri nyingine kutoa hizi fedha, ndiyo maana sasa hivi katika marekebisho yetu ya Sheria ya Serikali za Mitaa Sura ya 290, tumeweka kifungu ambacho kinatoa maelekezo ya kisheria sasa kwamba tunavyoipitisha hapa kwamba Halmashauri sasa haina hiyari isipokuwa ina lazima ya kutekeleza jambo hilo la kisheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lengo kubwa ni kuwasaidia vijana na akina mama na kuzikomesha Halmashauri zote zinazoonaa kwamba kupeleka ile fedha kama ni hisani, kumbe ni utaratibu. Lazima tunataka tuingize katika utaratibu wa kisheria ambapo nina imani sheria ile ikifika ha Bungeni, Wabunge wote tutashirikiana kwa pamoja kuipitisha kwa sababu ina maslahi mapana kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, katika jambo la pili la kuongeza asilimia 10 mpaka 15; nadhani ukiangalia mgao wa *own source*, asilimia kumi nadhani tuiweke hapo hapo, kwa sababu hata hizo asilimia kumi Waheshimiwa Wabunge wengine humu walikuwa wanalamika. Jambo la kuzingatia ni kwamba tuhakikishe ile asilimia kumi inafika.

Mheshimiwa Spika, najua Mheshimiwa Mabula ni mpiganaji wa wananchi wake na mpiganaji wa Machinga pale Mwanza. Na mimi najua tukisimamia vizuri hapa kwa pamoja, jambo hili litawasaidia sana vijana na akina mama katika maeneo mbalimbali kujingiza katika shughuli za ujasiri amali. (*Makofii*)

SPIKA: Ngoja niangalie Mbunge ambaye hajauliza swali toka Bunge hili lianz. Mheshimiwa Aida Khenani. (*Kicheko/Makofii*)

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, namshukuru.

Pamoja na agizo la Serikali kwenye Halmashauri kuagiza kutenga asilimia kumi kwa vijana na wanawake, kumekuwa na utaratibu wa Halmashauri kugawa pesa hizi kipindi cha Mwenge. Kwa sababu Halmashauri nyingine wanawake wanapata changamoto sana kipindi cha kilimo, Serikali haioni ni hekima au busara kutoa pesa hizi kipindi cha msimu wa kilimo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, nilizungumza mara kadhaa hapa, fedha zile hazitoki kwa Mheshimiwa Dkt. Mpango, fedha zile zinakusanywa katika Halmashauri zetu na Kamati ya Fedha inakaa na kufanya maamuzi fedha zile ziende wapi na kwa akina nani?

Kwa hiyo, jambo hili naomba niseme wazi, kama sisi Wabunge na Madiwani wetu tukiwa *committed* kuwasaidia wananchi wetu, haitaleta shida kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, najua *concern* ya Mheshimiwa Mbunge, lakini niwaelekeze sana ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, twende sasa tukazihakikishe Kamati zetu za Fedha zinapokaa katika ile ajenda ya mapato na matumizi, katika *own source*, tutengete kabisa pale pale, tuzielekeze kwa vijana na akina mama waweze kujikomboa kwa kadri Serikali ilivyopanga. Huu ndio mchakato wa wazi kabisa, kila mtu ataona ni jinsi gani ameshiriki vyema kuhakikisha jamii yake inakwenda vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namshukuru Mheshimiwa Mbunge.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, swali la

Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba yake Mheshimiwa Hawa Ghasia.

Na. 122

**Migogoro ya Ardhi kati ya Wakulima,
Wafugaji na Mamlaka ya Hifadhi**

MHE. HAWA A. GHASIA (K.n.y. MHE. AMINA N. MAKILAGI) aliuliza:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kupima ardhi yote ya Tanzania na kuipangia matumizi yaliyo bora kufuatia kuwepo kwa tatizo kubwa la migogoro ya ardhi kati ya wakulima, wafugaji na Mamlaka ya Hifadhi?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni azma ya Serikali kuondoa migogoro ya ardhi kote nchini na ili kufikia azma hiyo, Serikali imeandaa programu ya kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa programu hii, kila kipande cha ardhi nchini kitapangiwa matumizi na kupimwa, hali ambayo itaondoa mwingiliano baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi na hivyo kupunguza uwezekano wa kuibuka kwa migogoro ya ardhi. Mpango huu utasaidia ardhi yote kutunzwa na watumiaji husika na kuhifadhi maliasili zilizopo katika mazingira kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pia jamii inayozunguka maeneo hayo yaliyohifadhiwa itawezeshwa kutambua mipaka yao na kuwa na mipango ya matumizi ya ardhi na kudhibiti

uvamizi wa maeneo ya hifadhi. Aidha, utekelezaji wa programu hii utajenga uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa kulinda ardhi inayomilikiwa dhidi ya uvamizi wowote, kuwezesha kukabliana na athari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi, kuboresha makazi ya wananchi na kuleta usalama na ustawi wa maliasili za Taifa.

Mheshimiwa Spika, programu ya kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi nchini itahusisha Halmashauri zote 181 nchini na imepangwa kufanyika katika kipindi cha miaka kumi kwa awamu ya miaka mitano kwa kila awamu kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017.

Aidha, programu hii itakuwa na miradi mikubwa miwili ambayo ni miradi ya upimaji wa kila kipande cha ardhi vijiji na mradi wa upimaji wa kila kipande cha ardhi mijini.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa programu hii kwa awamu ya kwanza, umeanza kupitia Mradi wa *Land Tenure Support Program* ambaao unatekelezwa katika Wilaya tatu za mfano katika Wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga ambayo hadi sasa jumla ya mipaka ya vijiji 50 imeshapimwa na kazi ya uandaaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi, upimaji wa vipande vya ardhi na utoaji wa hatimiliki za kimila, unaendelea. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Hawa Ghasia, swali la nyongeza.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa tatizo hili la migogoro baina ya wakulima na wafugaji siyo la Mkoa wa Morogoro peke yake, tumelishuhudia katika Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Lindi, sasa kwa nini Wilaya zote tatu za majaribio zimekuwa katika mkoa mmoja? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pili, je, Mkoa wa Pwani na Lindi zoezi hilo litafanyika lini ili kuondoa changamoto ya wakulima na wafugaji hasa katika Wilaya za Rufiji, Kilwa na yale maeneo ambayo wafugaji wapo kwa wingi? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, ikiwa ni pamoja na Kongwa na Kiteto, Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwanza napokea pongezi zake ambazo ametoa na mimi nashukuru, ni kutokana na ushirikiano wetu sote. Katika maswali yake mawili aliyozungumza; la kwanza, amesema tatizo la migogoro lipi katika mikoa mingi nchini na kwa nini tumeamua kuanzia Mkoa wa Morogoro peke yake na Wilaya zote tatu za mfano zipo Mkoa wa Morogoro?

Mheshimiwa Spika, napenda nilithibitishie Bunge lako hili, nadhani wote ni mashahidi kwamba katika ile migogoro ya wakulima na wafugaji kwa Mkoa wa Morogoro ilikuwa ni kama imekithiri.

Mheshimiwa Spika, mauaji mengi yalikuwa yanatokea kule na kila leo kulikuwa na changamoto za hapa na pale na ndiyo maana tukasema sasa kwa sababu maeneo hayo yamekuwa na mgogoro mkubwa tuanzie pale ili tuweze kupata uzoefu pia wa kuweza kutatua migogoro ya aina hiyo katika maeneo mengine.

Kwa hiyo, kuanzia Morogoro lengo lake kubwa ilikuwa tu ni katika kuhimili ile migogoro iliyokuwepo na kuona namna gani tutaweza kuisitisha ili tuweze kufanya kazi hii vizuri zaidi katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili anasema, ni lini tutakwenda katika Mkoa wa Pwani na Lindi na hususan Rufiji na Kilwa, kama alivyotolea mfano.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu, kwa sababu utatuzi wa migogoro hii na upangaji na upimaji utafanyika kwa awamu mbili na tumekwishaanza, mimi niseme pale ambapo tutakuwa tumepanga ratiba inayofuatia, basi tutaweka na mikoa ambayo ina migogoro ukiwemo na Mkoa wa Pwani ambao nao pia unaonekana una migogoro mikubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutafanya hivyo kutegemeana na uzoefu tulionao katika migogoro iliyopo lakini pia katika kuhakikisha migogoro mingine haiibuki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda tuendelee na swali linalofuata, linauliza Wizara hiyo hiyo ya Ardhi. Linaulizwa na Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 123

Makazi Bora kwa Wananchi

MHE. UPENDO F. PENEZA aliuliza:-

Tatizo la makazi duni kwa wananchi husababisha afya mbovu na hivyo kupunguza nguvu ya uzalishaji.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa wananchi wanapata makazi bora?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ripoti ya Hali Halisi ya Miji Tanzania iliyoandaliwa na Mtandao wa Miji nchini (*Tanzania Cities' Network - TACINE*) ya mwaka 2014, wastani wa kiwango cha ujenzi holela katika miji saba ya Tanzania Bara na Manispaa ya Zanzibar ilibainika kuwa ni asilimia 67 ya maneno yaliyojengeka. Mengi ya maeneo haya hayana miundombinu na huduma za msingi kama vile maji safi na salama, barabara na mifereji ya maji ya mvua na udhibiti wa maji taka na taka ngumu. Hali hiyo husababisha mafuriko, milipuko ya magonjwa, mazalio ya mbu na inzi,

na mandhari mbaya ya kuishi yanayopelekea afya duni na kupunguza nguvukazi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Serikali imeandaa programu na mikakati mbalimbali kukabiliana na hali hiyo kama ifuatavyo:-

(i) Programu ya Kitaifa ya Kurasimisha Makazi Holela Nchini ambayo inalenga mwaka 2013 mpaka 2023 inayolenga kurasimisha makazi mijini na kutoa fursa kwa maeneo kupangwa, kupimwa na kumilikishwa na kisha kutoa huduma za msingi na miundombinu.

(ii) Programu ya Kitaifa ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Kila Kipande cha Ardhi ya mwaka 2015 mpaka 2025 inayolenga, pamoja na mambo mengine, kuzuia kudhibiti ujenzi holela ambao husababisha kuwepo kwa makazi duni; na

(iii) Kuandaa mipango Kabambe katika Miji (*Master Plans*) kwa miji 30 kwa kushirikisha Halmashauri za miji na Wilaya itakayosaidia kusimamia na kudhibiti uendelezaji miji. Hadi sasa Mipango Kabambe ya Arusha, Mwanza, Singida, Tabora, Mtwara, Kibaha, Musoma, Korogwe na Songea imeandaliiwa na makampuni binafsi na ipo katika hatua za mwisho za maandalizi.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa mamlaka na Serikali za mitaa kutenga fedha za kutosha katika bajeti zao kila mwaka kwa ajili ya kuongeza kasi ya kupima, kupanga na kumilikisha ardhi katika maeneo yao ili kuwawezesha wananchi kupata makazi bora.

SPIKA: Mheshimiwa Upendo Peneza, swali la nyongeza.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Wizara inatambua kwamba makazi duni huchangia katika kuleta afya mbovu kwa wananchi. Ni lini sasa Serikali itatekeleza ahadi yake ya kupunguza kodi kwenye vifaa vya

ujenzi ili sasa wananchi waweze kujenga nyumba bora na kuepukana na nyumba za tembe na nyasi?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 inaongelea suala la *resettlement*; kwa wananchi wanaotokana na maeneo ambayo yana shughuli nyingi za wawekezaji, wakilipwa fidia hulipwa pesa na kuondoka, Sheria ya Madini ya mwaka 2010 inazungumzia kwamba ahamishwe na ahakikishe kama alikuwa na mwembe, basi ataachana naye pale ambapo mwembe utakuwa umeota na kuanza kuzaa. Ni lini sasa Serikali italeta ndani ya Bunge hili mabadiliko ili Bunge liweze kufanya mabadiliko katika Sheria ya Ardhi ili sasa hilo suala la *resettlement* liweze pia kuzungumziwa katika Sheria ya Ardhi ili wananchi wapate fidia ambayo ni sahihi na waweze kunufaika na uwekezaji huu ndani ya nchi yetu? Ahsante. (Makof)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Angeline Mabula.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA

MAKAZI: Mheshimiwa Spika, swali la kwanza amezungumzia hali duni ya makazi ya watu na kufanya pengine wasiwe na makazi bora, pengine yanachangiwa labda na vifaa kuwa na bei ya juu.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala la kupunguza kodi katika vifaa vya ujenzi ni suala ambalo linahitaji kupitiwa kwa upya katika utaratibu wake kwa sababu mwanzo Waheshimiwa Wabunge walileta suala la kutaka kupunga VAT katika vifaa vya ujenzi, lakini ilikuwa limelenga eneo moja. Katika kulitafakari ikaonekana kwamba ukishatoa *loophole* hiyo kwa sehemu moja; na ilikuwa imeongeleva upande wa *National Housing*, pengine lingeweza kuleta tatizo zaidi, watu wangetumia fursa hiyo vibaya.

Mheshimiwa Spika, tunachopendekeza pengine na kuona kwamba kina unafuu zaidi, ni pale ambapo tunaweza kutumia rasilimali tulizonazo katika maeneo yetu na hasa

katika kutumia hivi vifaa vya ujenzi ambavyo vinaletwa kwa karibu zaidi. Sasa hivi ukiangalia hata *cement* imeshuka bei kulingana na uzalishaji umekuwa mkubwa. Kadri ambavyo uzalishaji unakuwa mkubwa, ndivyo jinsi na bei inashuka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapa tunachohimiza ni ile sera ya viwanda; pale ambapo tutawezesha kuwa na viwanda vingi vitakavyoweza kutengeneza vifaa vya ujenzi bei zitashuka tu kwa sababu gharama zitakuwa zimepungua na viwanda vingi vitakuwa katika maeneo ambayo usafirishaji wa vifaa vyake utakuwa ni chini. Kwa hiyo, huwezi kusema tu kwamba utapunguza hili kwa sababu watu wengine watatumia fursa hii vibaya na tusingependa itumike hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunalipokea kama ni changamoto lakini pia tunahimiza kutumia rasilimali zilizopo katika maeneo yale ambapo pia ujenzi wa nyumba umeonekana kuwa ni nafuu zaidi.

Mheshimiwa Spika, hata ukiangalia katika ile Bodi ya Wakala wa Ujenzi wa Gharama Nafuu wa Nyumba ambayo iko kwenye Wizara yetu, wanatengeneza nyumba na vifaa vya ujenzi wanaandaa pale wanatengeneza, nyumba zake zinakuwa na gharama ya chini zaidi ukilinganisha na hali halisi.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili ameongelea habari ya Sheria ya Madini kwamba unapotaka kufanya *resettlement* kwa watu, anatakiwa afanyiwe malipo stahiki na pia kuandaliwa makazi kwa maana ya kuwezeshwa kupata makazi mengine. Suala hili kisheria lipo isipokuwa katika utekelezaji ndiyo unakuwa kidogo haupo vizuri. Hili tumesema kwamba Serikali tutalisimamia kwa sababu ni wengi wanaooneewa katika hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, unakuta kwamba unamuondoa katika makazi yake, unamlipa pengine stahiki yake ya fidia, lakini hukamilishi lile linalotakiwa kwamba umlipa fidia yake na bado pia aweze kupata *resettlement* mahali pengine. Hili tunalisisitiza kwamba lazima unapomwondoa mtu apate

kiwanja aweze kujenga katika maeneo mengine, kwa sababu unalitumia eneo lile kwa uzalishaji.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Mbunge wa Kaliua.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo kubwa ni kwamba Halmashauri zetu hazina uwezo wa kutosha wa kupima maeneo yao ili kugawa viwanja na hivyo kuwepo na makazi bora, Serikali sasa ina mpango gani mahususi wa kutoa fungu maalum kwa ajili ya Halmashauri iwe kama *revolving fund*, wakishapima maeneo waweze kuyauza *then* warudishe ile fedha na hivyo kuhamishiwa kwenye Halmashauri nyingine illi Halmashauri zote hapa nchini ziweze kupima maeneo yao na hivyo kuwa na makazi bora kwa wananchi wetu? Ahsante.

SPIKA: Majibu mafupi ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, suala alilolizungumza Mheshimiwa Sakaya, ni kweli, Halmashauri nyingi hazina uwezo wa kufanya kazi hiyo, lakini ndani ya Wilaya tulikuwa tumeanzisha mfuko huu kwa ajili ya kuwezesha Halmashauri mbalimbali kuweza kupima na kuza viwanja na baadaye kurejesha madeni yao.

Mheshimiwa Spika, lakini kumekuwa na mfano mbaya ambapo Halmashauri nyingi hazirejeshi na mpaka sasa tunadai zaidi ya Halmashauri saba ambazo zimechukua na hazijarejesha na wengine wamerejesha kiasi, na ninadhani kama Mjumbe pia anayo taarifa, tulishawasilisha wale ambao wanadaiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tusingependa pia kuendeleza kuwa na madeni haya na ndiyo maana Serikali

inahimiza makusanyo ya ndani ya Halmashauri zenyewe zinazohusika. Pia wanayo fursa ya kupata mikopo kutoka katika mabenki mbalimbali ambayo yanaweza kutumika katika zoezi hilo. Ndiyo maana pia tumeruhusu wataalam mbalimbali wa kutoka kwenye *private sector* kufanya zoezi hilo la upimaji. Katika kupima, siyo lazima ulipe *cash*, kuna ile *barter trade* tunayosema wanaweza wakafanya.

Kwa hiyo, kuna maeneo mengine ambayo wameshaanza; ukiangalia Mkoa wa Katavi, kuna maeneo mengi wanafanya kwa kukubaliana mpimaji na Halmashauri, wanaachiana asilimia kadhaa, hawalipi *cash* isipokuwa vile viwanja anavyopima anauza anapata hela yake na Halmashauri inaachiwa vingine kwa ajili ya kuweza kutengeneza miundombinu.

Mheshimiwa Spika, hata yule mmiliki wa kiwanja, kama ana kiwanja kikubwa kimetoa viwanja labda vitano, wanakubaliana asilimia kadhaa; anaachiwa viwanja vyake vingine wanachukua Halmashauri wanauzwa wanatengeneza miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, siyo lazima kuwe na *cash*, ni namna ambayo unaweza ukaifanya na hasa kwa maeneo ya vijiji. Kwa mijini inaweza ikawa ngumu kidogo, lakini vijiji inawezekana kwa kufanya *barter trade* na bado zoezi la upimaji likafanyika vizuri.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama baadhi yenu mlivyokuwa mnafahamu, kwamba Mheshimiwa Mbunge wa Ulyankulu, Mheshimiwa John Kadutu alikuwa anaumwa, lakini natambua kwamba tupo naye. Hebu asimame hapo alipo. (*Makofii*)

(Hapa Mhe. John P. Kadutu Alisimama)

SPIKA: Nashukuru sana kwamba amejiunga na sisi, nami nichukue nafasi hii kuwaambia wananchi wa Ulyankulu kwamba Mbunge wao sasa ana nafuu na anaendelea vizuri na kazi za hapa Bungeni. (*Makofii*)

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvubi, swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale. Mheshimiwa Amar. Kwa niaba yake, alijejandaa.

Na. 124

Bei za Mazao na Mbegu

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU (K.n.y. MHE. HUSSEIN N. AMAR) aliuliza:-

Ili viwanda viweze kufanya kazi kwa ufanisi vinahitaji malighafi ya kutosha.

(a) Je, Serikali iko tayari kutoa bei ya pamba mapema kabla ya msimu wa kilimo kuanza ili wakulima wawe na uhakika wa bei elekezi?

(b) Zao la pamba limekuwa na tatizo kubwa la mbegu zisizo bora na viuatilifu hafifu, je, Serikali imejipanga vipi kwa kuzingatia agizo la Mheshimiwa Rais la tarehe 31 Julai, 2016 alipokuwa akiongea na wananchi wa Geita kwamba hatavumilia kuona wananchi wakiletewa mbegu mbovu?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvubi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bei ya kuuzia pamba ya wakulima hutegemea moja kwa moja bei katika Soko la Dunia ambalo kwa bahati mbaya bei hupanda na kushuka kila wakati. Serikali haipangi bei ya pamba kwa mkulima bali huangalia hali ya bei katika Soko la Dunia katika kupanga bei elekezi ya mkulima. Bei elekezi inapangwa kwa ushirikiano kati ya Serikali, wanunuzi wa pamba na wawakilishi wa wakulima. Aidha, pamoja na mpango wa Serikali wa kujenga viwanda vyta pamba kuongeza thamani, Serikali inahamasisha

wakulima kufuata kanuni bora za kilimo cha pamba ili kuongeza tija, ubora na baadaye kuwaongezea kipato. Kwa hali hiyo, bei ya pamba hufahamika baada ya kuanza kwa msimu mpya katika Soko la Dunia na kwa hiyo, Serikali haina uwezo wa kupanga bei ya pamba bila kuangalia hali ya Soko la Dunia.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kukabiliana na tatizo la upatikanaji wa mbegu bora za pamba na viuatalifu kwa kutumia Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu Nchini (*TOSCI*) na kwa upande wa viuatalifu, Taasisi ya Utafiti na Udhibiti wa Ubora wa Dawa (*TPRI*) ili kuhakikisha kuwa wakulima wanapata mbegu na viuatalifu vyenye ubora mtawalia.

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi inafanya rejea ya mfumo bora wa kuzalisha mbegu za pamba kwa maana ya kuuboresha zaidi, hatua hii itasaidia kuongeza upatikanaji wa mbegu bora za pamba kwa wingi na kwa bei nafuu. Aidha, Serikali ina mpango wa kuutumia Wakala wa Mbegu na Mazao kwa ajili ya kufungua mashamba makubwa ya kuzalisha mbegu ya pamba.

SPIKA: Mheshimiwa Constantine Kanyasu, swali la nyongeza.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Uhaba wa mbegu bora uliokuwepo mwaka 2015/2016 na kiwango kidogo cha ubora wa dawa ya pamba uliokuwepo mwaka 2015/2016 umeendelea kuwepo 2016/2017. Sasa swali langu la kwanza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, ni kwa kiwango gani Wizara imejandaa kumaliza tatizo hilo mwaka 2017/2018?

Swali langu la pili, wakati wa kampeni Mheshimiwa Rais alipokuwa Kanda ya Ziwa aliagiza Bodi ya Pamba ihamie karibu na wazalishaji wa zao la Pamba. Sasa swali langu, ni kwa kiwango gani uwepo wa Bodi ya Pamba Kanda ya Ziwa umesaidia kuhakikisha kwamba zao hili la pamba linapata uzalishaji mkubwa? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

Mheshimiwa Spika, kuhusu ni lini Serikali itaongeza kiasi au kiwango cha mbegu za pamba ili kukidhi mahitaji ya wakulima, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika msimu unaokuja wa kupanda pamba, tayari Bodi ya Pamba kwa kushirikiana na Mfuko wa Pamba wameweke mikakati kuhakikisha kwamba kutakuwa na mbegu za kutosha.

Mheshimiwa Spika, vilevile nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba siyo suala la kuongeza tu kiasi cha mbegu inayopatikana, lakini vile vile kuhusu ubora wake.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Pamba kwa kushirikiana na Wizara na vituo vyetu vya utafiti, tayari kwa muda sasa tunafanya utafiti mbegu aina ya UKM08 ambayo haina tatizo la ugonjwa wa unyaufu na hivyo tuko mbioni kuondokana kabisa na mbegu UK91 ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikileta usumbufu.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kwamba tunapofikia mwaka 2018/2019 tayari mbegu hii mpya, yenye ubora ambayo haina magonjwa itakuwa imeingia sokoni na ifikapo mwaka 2020, mbegu aina ya UK91 itakuwa imeondoka sokoni moja kwa moja. Kwa hiyo, katika miaka hii michache inayokuja tutahakikisha kwamba tuneondokana kabisa na adha ya ugonjwa na ubora usio mzuri wa mbegu ya pamba.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu Bodi ya Pamba kuhamia katika maeneo ambayo yanazalishwa pamba, nimfahamishe tu kwamba agizo lile la Mheshimiwa Rais tayari limeshatekelezwa, Bodi ya Pamba wameshamamia Mwanza na kwa kiasi kikubwa tayari imesaidia sana kwa sababu watendaji wanaoshughulika na zao la pamba kila siku tayari wapo karibu nao. Kwa hiyo, inakuwa ni rahisi wao kuweza kufika katika Ofisi za Bodi za Pamba na kupata huduma, lakini vilevile watendaji wenyewe maana ni rahisi

wao kufika katika maeneo ya wakulima na kutoa huduma zinazotakiwa. (*Makofii*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda, bado tuna maswali matano. Swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini.

Na. 125

Ununizi wa Zao la Pareto

MHE. ORAN M. NJEZA aliuliza:-

Uhitaji wa zao la pareto duniani ni mkubwa sana kiasi kwamba inahitajika kwa takribani tani 18,000 hadi 20,000 katika Soko la Dunia na Tanzania tuna uwezo wa kuzalisha hadi tani 8,000 tukliwa na mazingira rafiki.

(a) Je, ni kwa misingi gani pareto imepangiwa mnunuzi mmoja tu wa kigeni huku ikiwafungia milango wanunuzi wadogo wa Kitanzania?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kusimamia bei ya zao hilo ambayo imeporomoka kutoka shilingi 2,400 katika kipindi cha wanunuzi wengi hadi shilingi 1,500 chini ya mnunuzi mmoja?

(c) Je, Serikali ina mkakati gani wa muda mrefu na muda mfupi wa kuwawezesha wanunuzi wadogo wa Kitanzania kuingia kwenye ushindani na wanunuzi wageni?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria na Kanuni za Pareto zinamtaka kila mnunuzi kuongeza thamani ya pareto kwa

kuzidua sumu ya pareto kupata sumu ghafi. Pia mnunuzi anatakiwa kuwa na maabara ya kupima kiwango cha sumu kwenye maua na kuwalipa wakulima kulingana na kiwango hicho cha sumu. Kwa sasa mnunuzi aliyetekeleza masharti hayo ni Kampuni ya Pareto Tanzania. Serikali inasisitiza mnunuzi yejote kutimiza vigezo vilivyopo katika sheria na kanuni ili kulinda ubora na soko.

Mheshimiwa Spika, bei ya zao la pareto hupangwa katika Mkutano Mkuu wa Wadau ambaao ni wa Kisheria na hufanyika kabla ya mwezi Julai kila mwaka kabla ya kuanza msimu mpya. Mkutano huo, huhudhuriwa na wanunuzi na wawakilishi wa wakulima na viongozi wa Halmashauri zinazolima pareto nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inasisitiza wakulima kuzingatia kanuni za kilimo bora. Kwa mfano, pamoja na bei ya juu kuwa shilingi 2,200 msimu wa 2012/2013 na shilingi 2,700 msimu wa 2014/2015 ubora wa pareto ulikuwa chini ya asilimia moja. Baada ya baadhi ya wakulima kutekeleza kanuni za kilimo bora cha pareto katika msimu wa 2015/2016, ubora ulifikia asilimia 1.8 na bei ya juu kuwa shilingi 2,700. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mkakati wa muda mrefu ni kuendelea kuhamasisha wazawa kuijunga pamoja na kukopa ili wawekeze katika viwanda vya kuongeza thamani ya zao la pareto kufikia kiwango cha *crude extract* na hatimaye kuingia kwenye ushidani na wanunuzi wa kigeni. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Njeza, swali la nyongeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupewa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo kwa mkutano tuliofanya na wakulima na wawakilishi wa Wanunuzi mwishoni mwa mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, katika mkutano huo tulikubaliana kuwa wanunuzi wadogo wapewe leseni ya muda na vile vile wajunge kwenye vikundi na pia hii Kampuni ya pareto ambayo ilikuwa imebinafishwa kutoka Serikalini kulikuwa na asilimia 10 ambazo walipewa wakulima. Vilevile katika hicho kikao tulikubaliana kuwa zichunguzwe hizo asilimia kumi ziko kwa nani kwa vile wakulima hawakupewa hizo asilimia kumi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na makubaliano yote hayo, hakuna hata kimoja kilichoizingatiwa na leo hii kuna kampuni mpya mbayo imejenga kiwanda eneo la Inyara, Mbeya ambayo imezingatia vigezo vyote na ilipewa leseni ya kununua pareto kwenye vijiji viwili tu kati ya vijiji zaidi ya 20 inavyolima pareto. Sasa ni kwa nini Serikali isiboreshe hii Bodi ya Pareto ili tuweze kuboresha kiwango cha zao la pareto?

Mheshimiwa Spika, namba mbili, tunaomba vile vile...

SPIKA: hayajawa maswali mengi sana?

MHE. ORAN M. NJEZA: Ni moja tu hilo.

SPIKA: Haya malizia.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. La pili vilevile nilitaka kupata uhakika wa Serikali, kwa sababu inavyoelekea hakuna ushindani sasa hivi, watatu haki kishia vipi ya kwamba hawa ambao wametimiza vigezo vyote wanaruhusiwa kununua pareto ili inunuliwe kwa ushindani? Ahsante sana. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Njeza. Majibu hayo kwa kifupi Naibu Waziri, Mheshimiwa William Olenasha.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri kwamba Mheshimiwa Njeza amekuwa akifuatilia sana maslahi ya wakulima wake wa pareto, kahawa na mahindi. Kwa hiyo, tumekuwa naye karibu sana. Vilevile nikiri kwamba tulifanya kikao na

wakulima, mukutano ambao ulitusaidia sana kupata makubaliano kuhusu namna bora ya kuendesha zao la pareto.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mazungumzo yetu, baadhi ya masharti ambayo wakulima na wawakilishi wao tulikubaliana watekeleze, bado wako mbioni kutekeleza na hivyo bado tunasubiri kutoka kwao.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuhusiana na leseni ya kampuni za kununua pareto; nilieleze tu Bunge lako Tukufu kwamba zao la pareto ni zao lenye masharti tofauti kidogo na mazao mengine kwa sababu tunachoruhusu kipelekwe nje siyo pareto ghafi, siyo maua, bali ni sumu ghafi. Katika maana hiyo, ili uweze kupeleka nje lile zao ni lazima uwe na kiwanda.

Mheshimiwa Spika, tunafanya hivyo kwa sababu huko nyuma wakati tulikuwa tunaruhusu kupeleka maua nje, kiwango cha pareto yetu kilishuka sana kwa sababu hatukuwa tunaweza kudhibiti ubora wa sumu inayopelekwa nje, ndio maana tukaleta ili kunusuru zao lisije likaanguka nchini. Tukaleta kigezo kwamba ni lazima uweze kuwa na kiwanda ili uweze kuzidua au kuchakata na kuwa sumu ghafi.

Kwa hiyo, kampuni yoyote ambayo imekidhi masharti hayo, katika hali ya kawaida tunaruhusu inunue pareto. Kampuni ambayo anaizungumzia ya *TAN Extract* ya Mbeya ambayo ndio imeingia tu sokoni na kutimiza masharti, tutaendelea kutoa leseni ili waweze kununua pareto maeneo mengine zaidi ya vijiji ambavyo wanatoa sasa.

Vilevile nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa hatujaona kwamba tatizo ni Bodi ya Pareto lakini ni kanuni na sheria ambayo tumewekeana wenyewe kama wadau na Serikali iko tayari kuirejea na kuangalia upya sheria na kanuni hizo kama itaonekana inafaa.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Mbunge wa Itigi, swali la nyongeza.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niulizes swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyopo huko Mbeya Vijiji yanafanana kabisa na matatizo walionayo wakulima wa Itigi. Wakulima wa Itigi wanalima mazao mbalimbali yakiwemo mazao ya biashara na mazao ya chakula, lakini wanategemea sana Kampuni hii ya *Tanganyika Packers* ambalo limetelekezwa na sasa wanalitumia. Mheshimiwa Naibu Waziri alifika pale na aliona hamasa ya wananchi kutaka shamba lile lirejeshwe kwa wananchi kupitia Halmashauri yao.

Je, ni lini sasa Wizara hii italirudisha shamba lile kwa wananchi kwa sababu kampuni hii inayolimiliki ilishafilisika? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo kama unayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati wa ziara yangu Itigi, niliona changamoto ya ardhi waliyokuvananayo wananchi, pamoja na kuwepo na shamba ambalo ni kama limetelekezwa na hivyo kuhitaji jitihada za kuangalia namna ya kuwapatia.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari mchakato wa kuangalia namna ya kuligawa shamba hilo unaendelea. Wizara yangu kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina inatayarisha waraka wa kwenda Baraza la Mawaziri ili hatimaye shamba hilo liweze kugaiwa kwa utaratibu ambao utaonekana unafaa ikiwa ni pamoja na kugawa kwa wafugaji na wakulima wa Itigi. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kwa sababu ya muda. Nawaona kabisa. Wizara ya Fedha na Mipango, swali la Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel,

Mbunge wa Siha. Hakuna wa kumuulizia swali lake, natoa huku CCM! (*Kicheko*)

Tafadhali endelea. (*Kicheko*)

Na. 126

Changamoto ya Upungufu wa Ardhi-Siha

MHE. JULIUS K. LAIZER (K.n.y MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL) aliuliza:-

Wilaya ya Siha ina changamoto ya upungufu wa ardhi jambo ambalo limesababisha wananchi kushindwa kuendesha shughuli zao za kiuchumi kwa ufanisi na pia kuendeleza makazi yao katika maeneo hatarish.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwagawia wananchi mashamba yaliyoko chini ya Hazina kama vile mashamba ya *Foster, Journey's End na Harlington* ili wananchi wayatumie kwa kilimo ikizingatiwa kuwa wananchi Kata ya Nchimeta Ngarenairobi wanaishi kwenye maporomoko hatarishi hasa wakati wa mvua na majanga ya moto?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga ardhi kwa ajili ya ufugaji kwa wananchi wa Siha ambao kwa sasa hawana maeneo ya malisho kwa mifugo yao?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godwin Oloyce Mollel, Mbunge wa Siha, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mwaka 2007 Serikali ilitoa maelekezo ya kusitisha uuzaaji wa mashamba ambayo yalikuwa hayajabinafsishwa yakiwemo mashamba ya *Forester, Journey's End, Harlington* na Kanamodo yaliyopo *NAFCO, West Kilimanjaro*. Serikali ilisitisha zoezi la uuzaaji wa

mashamba hayo baada ya wananchi wa Siha pamoja na Uongozi wa Wilaya na Mkoa kупinga zoezi la ubinafsishaji wa mashamba na kupendekeza mashamba hayo yagawiwe kwa wananchi. Serikali ilikubaliana na maoni ya wananchi na hivyo kumtafuta Mtaalam Mwelekezi kufanya utafiti na matumizi bora ya mashamba hayo.

Mheshimiwa Spika, tathmini ilifanyika na mapendekezo yalikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Kuyagawa mashamba hayo katika mashamba madogo madogo kwa ajili ya shughuli za kilimo cha mazao na ufgajji kwa wakulima wadogo na wa kati na kisha kuyauza kwa njia ya zabuni; na

(ii) Baadhi ya maeneo kukabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Siha kwa shughuli za maendeleo ikiwemo makazi, shule, vyuo, hospitali na magereza.

Mheshimiwa Spika, kwa kutilia maanani mapendekezo ya mtaalam mwelekezi, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ilielekezwa kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri wenye mapendekezo ya namna bora ya matumizi ya mashamba hayo. Waraka huo ulishawasilishwa na kufikia ngazi ya Makatibu Wakuu na kutolewa maoni kwa ajili ya marekebisho.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha marekebisho, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi itauwasilisha waraka huo kwenye Baraza la Mawaziri. Baada ya kujiridhisha na mapendekezo na ushauri, Serikali itatoa uamuzi kuhusu matumizi ya mashamba husika.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa maelekezo kwa Halmashauri zote nchini kukamilisha mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Waheshimiwa Wabunge, sisi ni sehemu ya Baraza la Madiwani katika maeneo yetu, hivyo tunapaswa kusimamia maelekezo ya Serikali ili kuhakikisha kuwa wafugaji na

wakulima wanatengewa maeneo yao. Tuhakikishe kila kundi linatengewa maeneo kwa ajili ya shughuli zao za kiuchumi. Hapo tutakuwa tumeandaa msingi bora wa maendeleo ya kiuchumi kwa watu wetu. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Kalanga Laizer, nimekuona, swalii la nyongeza.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jambo hili sasa limechukua muda mrefu tangu 2007 mpaka sasa ni zaidi ya miaka kumi na wananchi wa Enduimet na Ngarenairobi wameendelea kupata matatizo ya ardhi na maeneo ya kujenga.

Je, ni lini Serikali itakamilisha mchakato huo na kuyagawa mashamba hayo kwa wananchi hao? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; kwa kuwa jambo hili la ardhi pia limefanana na maeneo mengine ya Monduli na kwa kuwa Serikali iliyafuta mashamba 13 mwaka 2015 na mashamba hayo mpaka sasa pamoja na mapendekezo ya wananchi bado hayajagawanywa.

Je, ni nini kauli ya Serikali katika kuyagawa mashamba haya, iko katika mazingira gani ili wananchi waweze kunufaika nayo? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swalii hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swalii la nyongeza lililoulizwa na Mbunge wa Monduli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Waziri, ni wazi Monduli kuna mashamba mengi ambayo wameleta kwa ajili ya kufutwa na yaweze kupata umiliki mwengine, lakini mpaka sasa mashamba mengi bado yapo kwenye mchakato; zile hatua za awali zimeshafanyika lakini mpaka yaweze kugawiwa ni

pale ambapo umiliki wake utakuwa umeshafutwa rasmi na kuweza kuwarejeshea ili wao waweze kupanga tena matumizi kwa ajili ya wananchi wao au kwa ajili ya uwekezaji. Kwa hiyo, hatua hiyo itakapokuwa imekamilika, watapewa na watafanya zoezi la kugawa upya kama ambavyo waliomba toka awali.

SPIKA: Ahsante sana. Nilikuona Mheshimiwa Rhoda Kunchela.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Na mimi nilitaka kumwuliza Mheshimiwa Waziri, ni lini Serikali itakuja kutatua mgogoro wa wananchi katika Kata ya Kakese katika shamba la Benki ya NBC? Shamba hili ililikuwa la uwekezaji lakini mpaka sasa shamba lile lipo limekaa *dormant* na wananchi hawakuweza kuendelea kulima shamba lile na shamba lile bado lina mgogoro.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ule ni upotevu wa malighafi na wananchi wanashindwa kuendelea kuendeleza lile shamba ili waendelee kujipatia kipato? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Rhoda Kunchela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nitoe ufanuzi tu kwamba migogoro yote kwa ngazi tofauti siyo kwamba lazima itatuliwe na ngazi ya Wizara. Migogoro mingi na hasa ya kwenye kata na vijiji inatatuliwa na mamlaka zilizoko kule ikiwemo Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, kuna Ofisi ya Kanda ya Ardhi katika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu amesema mgogoro huu uko kwenye ngazi ya Kata, naomba tu Mkuu

wa Wilaya wa eneo husika pamoja na Mkurugenzi wa Halmashauri husika waende kwenye Kata yenyé mgogoro waweze kutatua mgogoro ule na wananchi waweze kupewa haki yao kama wanastahili kwa sababu amesema lilikuwa linamilikiwa na NBC, lakini siyo kila mgogoro lazima uje Wizarani.

Waheshimiwa Wabunge, nawaomba sana, migogoro mingi wakati mwingine hata tunapokwenda kufanya ziara, unakuta ni mgogoro ambao ungeweza kumalizwa na Mkuu wa Wilaya pale au Mkuu wa Mkoa au Mkurugenzi mwenyewe husika katika eneo lile. Ukienda pale unakuta wewe unakuwa kama mtazamaji, watu wanamaliza wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nashauri tu ile ambayo inahitaji Wizara basi ijulikane na ile inayohudumiwa na Mkoa na Wilaya basi nao wachukue nafasi yao kuhakikisha kwamba wanatatua migogoro hii na isiwe ni kikwazo kwa wananchi.

SPIKA: Mheshimiwa Mary Nagu, nilikuona swali la nyongeza.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Hanang kama ilivyo Wilaya ya Siha inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa Ardhi na tuna mashamba ambayo yalikuwa chini ya *NAFCO* ikiwemo *Basotu Plantation* na tuliomba kwamba shamba hili lirudi kwa wananchi; Mheshimiwa Waziri anaweza kutueleza ombi letu limefika wapi?

SPIKA: Majibu ya Swali hilo Naibu Waziri wa Kilimo.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mary Nagu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba kuna maombi ya Shamba la *Basotu Plantation* ambalo lilikuwepo

mikononi mwa *NAFCO* liweze kugaiwa kwa wananchi. Utaratibu ambao ulikuja kubadilika baadaye ni kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Hanang' ikabidhiwe hilo shamba ili wenyewe waweze kukodisha kwa wakulima wadogo, kwa sababu tayari jitihada za kugawa mashamba mengine ililileta mgogoro mkubwa sana ambao ulikuwa unatishia amani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa sasa utaratibu ambao umetumika ni huo wa kujaribu kukabidhi kwa Halmashauri huku jitihada zikiendelea za kuangalia namna bora ya kuweza kuligawa. Kwa hiyo, namtaka Mheshimiwa Mbunge aendelee kuwa mvumilivu tukiangalia utaratibu huu ili huko mbele ya safari tuweze kuligawa kwa utaratibu.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa.

Na. 127

Kucheleweshwa kwa Fedha za Miradi ya Maendeleo

MHE. GEORGE M. LUBELEJE aliuliza:-

Kila mwaka Bunge limekuwa likipitisha Bajeti ya Serikali kuhusu Wizara, Mikoa na Wilaya lakini kumekuwa na ucheleweshwaji wa fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo hususan katika Mikoa na Wilaya na kupelekea miradi mingi kutokamilika.

Je, ni sababu gani za msingi zinazofanya Serikali kuchelewa kuleta fedha za Miradi ya Maendeleo katika Mikoa na Wilaya?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa utaoji wa fedha za utekelezaji wa Bajeti ya Serikali hutegemea mapato ya Serikali kuititia ukusanyaji wa mapato kutoka katika vyanzo vya kodi na visivyo vya kodi, mikopo pamoja na misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo. Katika miaka ya hivi karibuni, mwenendo wa upatikanaji wa mapato ya Serikali umekuwa na changamoto nyingi katika miezi ya mwanzo wa mwaka wa fedha ambapo mikopo ya masharti ya biashara kutoka kwenye taasisi za fedha pamoja na misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo imekuwa haipatikani kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sababu kuu zinazochangia kutopatikana kwa wakati kwa fedha hizo ni pamoja na majadiliano na washirika wa maendeleo kuchukua muda mrefu, baadhi ya washirika wa maendeleo kutotimiza ahadi zao kutokana na sababu mbalimbali na kupanda kwa riba ya mikopo ya kibiashara katika soko la fedha la kimataifa.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazokusanywa kutokana na vyanzo vya mapato ya ndani zimekuwa zikielekezwa kugharamia matumizi mengine yasiyoepukika kama vile ulipaji wa mishahara, deni la taifa, ulipaji wa madeni ya watumishi, watoa huduma, wazabuni na wakandarasi pamoja na utekelezaji wa miradi yenye vyanzo mahususi kama vile Taasisi ya Umeme Vijijini, Mamlaka ya Elimu Tanzania, Mfuko wa Barabara, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Mfuko wa Maji na Mfuko wa Reli.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya fedha za miradi ya maendeleo katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa hutumia fedha za nje. Utoaji wa fedha hizo kutoka kwa washirika wa maendeleo huzingatia mpango kazi, masharti na vigezo mbalimbali vilivyowekwa ambavyo hupaswa kuzingatiwa na mamlaka zinazotekeleza miradi.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa miradi ya maendeleo inatekelezwa badala ya kutegemea fedha za nje ambazo uhakika wake umekuwa hautabiriki, Serikali imeendelea kuongeza fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza

miradi ya maendeleo hadi kufikia shilingi bilioni 8,702.7 kwa mwaka 2016/2017 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,366.1 mwaka 2010/2011. Aidha, Serikali yetu imeendelea kuboresha vyanzo vya ndani vya Halmashauri na kuzijengea uwezo zaidi kwa kukusanya mapato ili kutekeleza miradi mingi kwa fedha za ndani badala ya fedha za nje.

SPIKA: Mheshimiwa Lubeleje, swali la nyongeza.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa kuna miradi imeshaanza kutekelezwa, kwa mfano, Wilaya ya Mpwapwa tulikuwa na matarajio ya kujenga barabara za lami, Mpwapwa Mjini kilometra 10; na kwa kuwa fedha illyoletwa ni kidogo sana na ni karibu Majimbo yote kuna viporo; je, fedha iliyobaki Serikali italeta fedha zote kwa Wilaya zote? (*Makofii*)

Swali la pili, kwa kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya kujenga Vituo vya Afya Mima na Mbori ni kidogo sana na ndiyo maana havijakamilika sasa zaidi ya miaka kumi; je, Serikali itaongeza fedha ili tukamilishe vituo hivyo?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Lubeleje kwa jitihada zake za kufuatilia maendeleo ndani ya Mpwapwa na ndani ya Wilaya nzima ya Mpwapwa, wananchi wako wanakutegemea sana kaka yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza ni kupelekwa fedha zote. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, upelekaji wa fedha hutegemea mapato ya Serikali na hivyo fedha hizi zinapopatikana, lengo la Serikali ni kuhakikisha bajeti yetu inatekelezeka kwa asilimia 100. Kwa hiyo, fedha hizi tutakapokuwa tumezipata fedha zote zitapelekwa na

miradi yote tuliyopanga itatekelezwa kama ambavyo tulipitisha bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili la Vituo vya Afya kuongeza bajeti, ni imani yangu Wizara ya Afya watakapoleta bajeti yao hapa tutaiona na tumelizingatia hilo, vituo vyote vya afya ambavyo vimejengwa miaka mingi havijakamiliika tumevizingatia katika bajeti yetu ya mwaka huu 2017/2018.

SPIKA: Kwa sababu ya muda Waheshimiwa, nimebakiwa na maswali mawili na muda wetu umekwisha, naomba tuyatendee haki maswali haya mawili.

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wazee na Watoto, swali la Mheshimiwa Stella Alex Ikupa.

Na. 128

**Msamaha wa Uchangiaji Huduma za Afya
kwa Watu Wenye Ulemavu**

MHE. STELLA I. ALEX aliuliza:-

Asilimia kubwa ya watu wenye ulemavu wana vipato duni sana kiasi cha kushindwa kumudu ghamara za matibabu.

Je, Serikali haioni kuwa ni muda muafaka sasa wa kuwajumuisha Watanzania hawa wenye kipato duni na wenye ulemavu kwenye sera ya msamaha wa uchangiaji huduma za afya kama ilivyo kwa wanawake wajawazito, watoto chini ya miaka mitano na wazee?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Sera ya Afya ya mwaka 2007 imeainisha makundi yanayostahili kupata msamaha wa kulipia huduma za afya katika vituo vyote vya kutolea huduma.

Kulingana na Sera hiyo, Serikali inatambua kuwepo kwa wananchi wasio na uwezo wa kuchangia gharama za huduma za afya, ikiwa ni pamoja na wale walio katika makundi maalum ya kijamii, mathalan Wazee walio na umri zaidi ya miaka 60 ambaao hawana uwezo wa kipato, watoto wenye umri chini ya miaka mitano, watoto walio katika mazingira hatarishi, wanawake wajawazito na watu wasiojiweza kiuchumi. Pia watu wenye magonjwa sugu kama saratani, UKIMWI, kisukari, magonjwa ya moyo, pumu, *sickle cell*, kifua kikuu, ukoma na magonjwa ya akili. Madhumuni ya sera hii ni kuwezesha makundi maalum kupata huduma bora za afya sawa na wananchi wengine.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa watu wenye ulemavu wamezingatiwa katika makundi ya watu wanaostahili msamaha.

Mheshimiwa Spika, aidha, msamaha kwa kundi hili utatolewa kwa kuzingatia kama mlemavu huyo atabainika kuwa hana uwezo wa kulipia huduma au kuwa katika moja ya makundi yanayostahili msamaha niliyoyataja.

SPIKA: Mheshimiwa Ikupa, swal la nyongeza.

MHE. STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kutokana na majibu mazuri ya Serikali kuwa msamaha wa matibabu utatolewa kwa mtu mwenye ulemavu ambaye atabainika hana uwezo; ikumbukwe kuwa ugonjwa unampata mtu bila taarifa.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwabaini watu wenye ulemavu wasio na uwezo ili waweze kupata msamaha huu wa matibabu? (*Makofii*)

Swali la pili, je, Serikali ipo tayari kuziagiza mamlaka husika na kutoa waraka ili majibu yaliyotolewa hapa leo yawewe kutekelezwa? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo muhimu sana, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, maswali anayozungumzia Mheshimiwa Stella ni muhimu sana kama ulivyo sema wewe mwenyewe na ni maswali yanayohusu uwiano na usawa kwenye jamii yetu, ambapo kama Taifa ni lazima tutoe uwiano sawa kwa watu wote bila ubaguzi wa aina yoyote ile kama ambavyo waasisi wa Taifa letu waliweka misingi kuitia sera yetu ya ujamaa na kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, ni kwa msingi huo, Serikali kuitia Sera yake ya Afya ya mwaka 2007 inatoa matamko ya kisera ya namna ambavyo makundi maalum kwenye jamii yanalazimika kuhudumiwa ikiwemo kundi hili la watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, sasa utaratibu wa utekelezaji unawekwa na sheria na taratibu mbalimbali ndani ya Serikali. Katika awamu hii ya tano, tunakusudia kuleta hapa Bungeni mapendekezo ya Bima ya Afya ya lazima kwa watu wote ambapo ndani yake tutakuwa tumeweka utaratibu mahsus wa kuhakikisha uwiano huu tunaouzungumza unatekelezeka kuitia Bima ya Afya ambapo tutaweka utaratibu sasa kwamba watu wanaopewa msamaha kwa mujibu wa sera, basi wawe na kadi ya Bima ya Afya kuliko ilivyo sasa. Kwa sababu inajitokeza katika nyakati mbalimbali ana msamaha anastahili kupata huduma bure, lakini anapofika kwenye kituo cha kutolea huduma, anakosa dawa ama anakosa vipimo fulani na analazima kwenda kwenye *private*. Kwa hiyo, hata ile bure inayokusudiwa na sera yetu inakuwa haipo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi ndani ya Serikali tunaamini kama tutafanikiwa kuitisha sheria hii ya Bima ya Afya kwa wote, utaratibu utakuwa mzuri. Kwa hiyo,

anachokizungumzia sasa hivi tumekianzisha kwa mfano tu kwa kujaribisha kwenye kundi la wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 60 wasiojiweza ambapo Halmashauri zinalazimika kuwabaini wazee wote katika eneo lao na kuwawekea utaratibu wa kuwapa kadi za *CHF* ili kujaribisha utaratibu tunaozungumza.

Mheshimiwa Spika, kwenye kundi la wale mavu, bado hatujaanza.

SPIKA: Swali la mwisho kwa siku ya leo, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, swali la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya.

Na. 129

**Ujambazi na Unyang'anyi wa kutumia
Silaha katika Mji wa Bunda**

MHE. ESTER A. BULAYA aliuliza:-

Kumekuwa na matukio ya mara kwa mara ya ujambazi na unyang'anyi wa kutumia silaha ndani ya Mji wa Bunda na wahanga wa matukio hayo ni wafanyakia shara wadogo wadogo.

Je, ni hatua zippi za kiusalama zimechukuliwa ili kukabiliana na wimbi la ujambazi na unyang'anyi katika Mji wa Bunda?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa hivi karibuni kulikuwa na wimbi la uhalifu kwa Mkoa wa Mara na mikoa mingineyo. Jeshi la Polisi limeendelea kubuni na kutekeleza mikakakati mbalimbali ya kubaini, kuzuia na

kukabiliana na uhalifu, kadri uchambuzi wa uhalifu unavyoonesha mwenendo na mwelekeo wa uhalifu nchini ukitumika kama zana ya kutabiri uhalifu wa baadaye.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limeendelea kuwajengea uwezo Maafisa Wakaguzi na Askari kwa kuyatambua na kuyaundia mikakati ya utekelezaji mambo yafuatayo:-

(i) Kutabiri mwelekeo wa uhalifu kwa kutumia takwimu za uhalifu, kumbukumbu za uhalifu pamoja na mabadiliko ya uhalifu ili kuweza kutambua maeneo korofi, wahalifu wanaohusika, mahali walipo na namna ya kukabiliana na uhalifu huo.

(ii) Kuyatambua maeneo nyeti yenyeye vivutio vya uhalifu na kuyapangia ulinzi pamoja na misako na doria.

(iii) Kuendelea kufanya misako na doria mara kwa mara ili kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo mbalimbali nchini.

(iv) Kushirikiana na wadau wote wa ulinzi na usalama kubadilishana taarifa za Kiintelijensia pamoja na uzoefu katika kuzuia uhalifu kwa kuibua mifumo mipywa na kuboresha ya zamani.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii nitoe rai kwa wananchi wote kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi ili kuwabaini, kuwafichua na kuwakamata ili mkondo wa sheria uchukue nafasi yake kwani hatutasita kuchukua hatua kali dhidi ya vitendo hivi viovu nchini.

SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Mwenyekiti wangu wa zamani wa vijana.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwenye majibu yake, anasema moja ya mikakati ni kuhakikisha wanafanya doria imara; ni jambo zuri kabisa. Sasa huwezi kufanya doria imara kama huna magari mazuri.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Bunda kuna magari mawili na mabovu na ndiyo ambayo yanatakiwa yafanye doria kwenye Jimbo la Kangi na Jimbo la Boni. Sasa uhalifu unazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, maswali yangu, katika kuhakikisha hiyo doria imara kama Mheshimiwa Waziri amejibu, je, Serikali iko tayari sasa kutupatia gari jipya ili kupunguza vitendo vyatua uhalifu kwa kufanya hiyo doria imara? (*Makofii*)

Swali la pili, ili kuweza kukabiliana na hizi changamoto, moja ya vituo ambavyo viro hohehahe ni Kituo cha Polisi cha Bunda. Sasa wameanza mradi wa ujenzi wa jengo la upelelezi kuititia michango ya polisi, ya wadau, nami Mbunge wa Jimbo kuititia Mfuko wa Jimbo nimewachangia. Serikali mpo tayari kuungana na jitihada zetu kukamilisha jengo hilo? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa *Engineer Masauni*.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la magari, naomba nichukue nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tumepokea changamoto yake ya magari. Wakati ambapo magari yatapatikana tutatoa kipaumbele kwa Jimbo lake ili tumpatitie gari la ziada ili aweze kuongeza nguvu ya yale magari machache yaliyopo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni suala la ujenzi wa kituo cha upelelezi. Kwanza nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuamua kutoa fedha za Mfuko wake wa Jimbo kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha polisi. Natambua kwamba Mfuko wa Jimbo una fedha

kidogo na Majimbo yetu yanachangamoto nyingi. Kwa hiyo, kitendo cha Mheshimiwa Mbunge kuamua kwamba sehemu ya fedha hizo ziende kwenye ujenzi wa vituo vya polisi ambavyo vina changamoto kubwa ni jambo la kupongezwa na kuungwa mkono. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Ester kwamba jitihada zake pamoja na za wananchi zimezaa matunda, kituo hicho kimekamilika, tunatarajia wakati wowote mwaka huu tutakizindua. (*Makof*)

SPIKA: Naona Mambo ya Ndani hapa; tulibakize Bunda swali hili. Mheshimiwa Boniphace Mwita, swali la nyongeza.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa matukio ya Bunda yanazidi kuwa mengi kidogo, ni lini sasa Waziri au Naibu Waziri atatembelea Bunda ili kuona hali halisi ya mambo hayo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo. Ni lini utaenda Bunda pamoja na Mheshimiwa Boniphace Mwita na Mheshimiwa Ester Bulaya?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimuhidi kwamba tutashauriana na Mheshimiwa Waziri ili kati yangu ama yeye tuweze kwenda Bunda haraka iwezekanavyo. Tutakaa pamoja tushaurine ratiba hiyo ya kutembelea Bunda muda siyo mrefu sana. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa tafadhali, swali la mwisho la nyongeza.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Matatizo ya usalama katika eneo la Bunda yanafanana sana na Jimbo langu la Mji wa Tunduma.

Mwaka 2016 katika swali langu la msingi, niliuliza kuhusiana na ujenzi wa kituo chenye hadhi ya Wilaya, lakini pia niliuliza kuhusiana na nyumba zenyе gharama nafuu kwa ajili ya polisi wetu kwenye Mji wa Tunduma. Majibu yake ni kwamba walisema katika Bajeti ya mwaka 2016/2017 nyumba hizi zingeweza kujengwa pamoja na Kituo cha Polisi chenye hadhi ya Wilaya. Je, Serikali inasema nini kuhusiana na changamoto hizi katika mji wetu wa Tunduma? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo la Mbunge wa Tunduma, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nakiri kabisa kwamba Jimbo la Tunduma lipo mpakani na lina changamoto nydingi sana za kiusalama. Kwa hiyo, mahitaji ya kuwa na kituo cha polisi cha kisasa pamoja na nyumba za askari ni mambo ya kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi hiyo iliyotolewa na Serikali iko pale pale na hatua ambazo zitafikiwa tutamjulisha kwa kadri ambavyo upatikanaji wa fedha utakavyokuwa unaruhusu.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda, nafikiri mnaona muda wetu hauko upande wetu. Waheshimiwa Wabunge naomba tusikilizane, wanaonong'ona muendelee taratibu kidogo.

Kuhusiana na wageni mliopo Bungeni, tunawakaribisheni wote, karibuni sana hapa Bungeni. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa wale mliokuwepo hapa Dodoma, jana palikuwa na mechii ya *Bunge Sports Club* mpira wa miguu kati ya *Bunge Sports Club* na *Morogoro Combine*, mgeni rasmi akiwa ni Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Saddiq Murad. *Bunge Sports Club* ilishinda kwa kuifunga *Morogoro Combine* bao mbili na *Morogoro Combine* walipata bao tatu. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, lakini mechii hii ina marudiano, kwa hiyo, wakati mwingine tutapanga utaratibu wa kwenda ku-revenge kule Morogoro. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Anna Lupembe, Mwenyekiti wa Ibada anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo kutakuwa na ibada kwenye *chapel* yenu, Jengo la Pius Msekwa ghorofa ya pili tarehe 2 Mei, 2017 baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa 7.00 mchana. Aidha, wanamaombi wa Mkoa wa Dodoma watahudhuria ibada hiyo ili kushirikiana nanyi. Hayo ndiyo matangazo tuliyonayo siku ya leo.

Katibu, tueendelee.

NDG. NENELWA M. WANKANGA - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

Hoja ya Kamati ya Haki Maadili na Madaraka ya Bunge

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mwongozo.

SPIKA: Muda wetu ni mdogo, naomba yawe ni mambo ya maana, yasiwe mambo ambayo ni *routine*. Katibu nitajie majina.

NDG. NENELWA M. WANKANGA - KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Sakaya, Mheshimiwa Lwakatare, Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer. Basi, watatu tu.

SPIKA: Ni watatu, kwa kifupi sana, tuanze na Kamishna.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba mwongozo wako kutokana na Kanuni yetu kifungu cha 68(7) kikisomwa pamoja na kile cha 69 kuhusiana na suala la dharura la kuomba Bunge lako liahirishe shughuli zinazoendelea ili kujadili suala la msingi la dharura ambalo limetokea ndani ya jimbo langu muda huu tunavyoeendelea kuongea.

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyoongea, wananchi zaidi ya familia mia moja ndani ya Jimbo langu la Kaliua hazina makazi ya kukaa. Watoto wako chini ya miti, wanateseka, vyakula vyao vinaloa na mvua baada ya *operation ilioendeshwa* na Afisa Maliasili na Maafisa wa Mifugo Wilaya ya Kaliua, wakiongozwa kwa bahati mbaya sana na *DC*. Kwa maelekezo ya *DC* nyumba zao zimevunjwa, zimechomwa moto, watoto wanateseka.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya sana wakati zoezi hili linapoendelea, Serikali tayari ilishaunda Tume hapa kutokana na migogoro ya ardhi ya hifadhi na wananchi. Serikali imeunda Tume kuitia Wizara nne; Wizara ya Ardhi, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maliasili na TAMISEMI waweze kutembea nchi nzima waangalie matatizo kama haya waweze kuishauri Serikali njia nzuri ya kuchukua kuweza kutatua migogoro hii.

Mheshimiwa Spika, wakati zoezi linaendelea la timu hii kufanya kazi, tayari Kaliua wananchi zaidi ya 1,000 hawana pa kukaa. Tayari zaidi ya vijji sita vya kata ya Kangeme na Zugimlole wako kwenye hali mbaya. Kuna taharuki popote ninapoongea.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Bunge lako, kwa umuhimu wa suala hili, tunapojadili hapa, sisi ni Wawakilishi; tunapojadili masuala ya msingi, pale sasa hivi mvua zinanyesha, vyakula vinaoza na nchi hii hatutaki kutangaza njaa. Tunaomba sana Bunge lako lijadili suala hili la msingi hatma ya wananchi hawa zaidi ya 1,000 wanaoteseka, wanaonyanyasika, nyumba zao zimebomolewa na mabati yao kukatwakatwa na mapanga na mashoka ili angalau wasijisitiri kabisa!

Mheshimiwa Spika, hili ni suala la msingi sana. Naomba mwongozo wako ili Bunge liweze kuahirishwa lijadili suala hili ambalo ni la msingi sana kwa maendeleo ya wananchi wetu wa Tanzania. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Lwakatare.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Spika, naimama kwa mujibu wa Kanuni namba 69(1) juu ya hoja ya kuahirisha mjadala wa Bunge na niombe Bunge liahirishé shughuli zake kwa dakika 20 tu, kujadili tatizo la tetemeko ambalo usiku wa Jumamosi kuamkia Jumapili (juzi), eneo la Mkoa wa Kagera na hususan Bukoba Mjini limepata tetemeko liliokuwa na nguvu kwa muda wa sekunde tano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kwamba wakati tetemeko la kwanza liliotokea mnamo tarehe 10 Septemba, 2016 mojawapo ya hatua zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na kuunda timu ya wataalamu, wanajiolojia ambao walikwenda kule kujaribu kupima juu ya tabia na mwenendo wa hali ya tetemeko katika eneo la Mkoa wa Kagera na Mji wa Bukoba kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ninavyozungumza mpaka hivi leo, wataalamu hawa hawajatoa wazi taarifa ya nini walichochunguza na nini wanachokielekeza kwa wananchi wa Mkoa wa Kagera na *Bukoba Town* kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, sasa kutokana na hali ya tetemeko ya majuzi ni kwamba hivi sasa watu wapo katika taharuki kubwa, watu wanalala nje ya hizo nyumba zilizojiegesha na tunashukuru kwamba hali ya tetemeko la juzi ni kweli halikusababisha madhara makubwa licha nyufa kutokea kwenye nyumba na baadhi ya kuta zilizokuwa zimeanza kujengwa kudondoka; sasa wananchi wa Bukoba juu ya *dilemma* hii, wanashindwa kuelewa kwa sababu taarifa ya wataalam hajjawekwa wazi, kitu walichoambulia kwa maelekezo ya Serikali ni kwamba waanze kujenga wao wenyewe, hata wakianza kujenga wao wenyewe, kuta zinaanguka tena.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja na ninaomba iungwe mkono mjadala huu uendeshwe kwa dakika 20 ili wananchi wa Bukoba waweze kujua hatima yao na waweze kuondoa hofu ambayo imetanda katika Mkoa wa Kagera na *Buboka Town*. Naomba kuwasilisha.

WABUNGE FULANI: Toa hoja.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Spika, natoa hoja ya kuahirisha.

SPIKA: Mheshimiwa Laizer.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Spika, najielekeza katika Kanuni ya 46 kuhusu maswali kujibiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, wakati nauliza swali la nyongeza asubuhi kuhusu mashamba ya *Forest* kule Siha, niliuliza swali la nyongeza kwamba; kwa kuwa jambo hili limechukua muda zaidi ya miaka 10 tangu mwaka 2007 Serikali ikilishughulikia mpaka sasa; na kwa kuwa wananchi wa maeneo ya Ngarenairobi na Enduimet wanaendelea kuteseka katika maeneo hayo bila kuwa na makazi yao; lakini kwa masikitiko makubwa, swali hili halikujibiwa kabisa japo nilliluliza kama swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa sababu kuendelea kuliacha suala hili likiwa hewani zaidi ya miaka 10 litaweza kusababisha mgogoro na mapigano ya wananchi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako kuhusu swali hili ambalo halijajibiwa kabisa. (*Makofi*)

SPIKA: Sijakuelewa Mheshimiwa Laizer, mwongozo kuhusu nini? Kwamba *Forest* imefanya?

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Spika, swali halikujibiwa kikamilifu kama lilivyouliza katika swali la nyongeza la swali namba 126. Halikujibiwa. (*Makofi*)

SPIKA: Unajua maswali na majibu, Mheshimiwa nikianza na la kwako, unayeuliza unauliza ulivyouliza na wanaojibu wanajibu vile walivyojibu. Sasa habari ya kutokuridhika, unatuweka hapo katikati.

Tunaendelea na miongozo hii miwili mingine, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mwongozo wa Mheshimiwa Sakaya na Mheshimiwa Lwakatare.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa mujibu wa kanuni tumesikia miongozo iliyotolewa; wa kwanza ulitolewa na Mheshimiwa Sakaya na ule uliotolewa na Mheshimiwa Lwakatare.

Mheshimiwa Spika, tunayo maelezo ndani ya Serikali ya miongozo hii miwili; wa Mheshimiwa Lwakatare na Mheshimiwa Sakaya. Kikosi kazi kilichoundwa na Serikali, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) ni Wajumbe ambao ni miongoni mwa Wizara ambazo zilikuwa zinasimamia zoezi hilo. Kwa heshima sana ya kikao chako, nitaomba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI atoe maelezo ya Mwongozo huo wa Mheshimiwa Sakaya.

Mheshimiwa Profesa Muhongo, tunazo taarifa kupita Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusiana na ripoti ya wataalamu wa miamba kwenye suala zima la tetemeko la Kagera. Kwa hiyo, naomba sana kwa dakika chache tu, Serikali itoe maelezo ndani ya Bunge lako.

SPIKA: Ahsante. Tuendelee kama tulivyojipanga.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, nimesikia Mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Sakaya juu ya Jimbo la Kaliua na matukio yanayotokea, lakini nadhani siyo jambo la dharula kwa sababu jambo linalofanywa na Serikali na linasimamiwa na Serikali kuwa la dharura nadhani tutapata shida kidogo.

Mheshimiwa Spika, kubwa hapa pengine ni yale matukio anayoyasema. Nadhani kwa sababu ni jambo ndiyo limetokea bado la moto, acha twende tukusanye taarifa, tupate taarifa kutoka huko kwa sababu kule kuna Serikali.

Halafu tutakuja hapa tueleze kilichotokea na pengine anachokijua Mheshimiwa kinaweza kikawa pengine ndicho hicho au sicho hicho, lakini tukipata taarifa ile itatusaidia ili tuweze kufanya Bunge na Taifa kwa ujumla liweze kufahamu kitu gani kimetokea Kaliua.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kuhusu tetemeko la Kagera, tumeshatoa ripoti tatu ambazo zilipelekwa kwenye ngazi zote za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ripoti ya mwisho kabisa ambayo ilikuwa iwasilishwe kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkao wa Kagera, Profesa Mruma ambaye ndiye Mkuu wa Kitengo cha Jiolojia, tukapanga na tarehe na siku ya kwenda kule Kagera, zikaingia kazi za kiserikali nyingine. Akatuma wawakilishi kule, Serikali ya Mkao ikasema hapana, ingependa ye ye mwenyewe awepo.

Mheshimiwa Spika, ripoti mimi mwenyewe ninayo, nimeisoma na nikawapatia ruhusa ya kwenda kuitoa kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, tuseme hivi, haya matetemeko yakiwa yanatokea, haiwezekani kila mara liwe jambo la dharura la kusimamisha Bunge kwa sababu hili ni Bunge; narudia kusema, hayupo mtaalam yeyote duniani ambaye anaweza kusema kwamba tetemeko litatokea Musoma tarehe 2, saa mbili asubuhi, hayupo. Kama yupo, basi ni mtaalam ambaye dunia haimtambui. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kinachofanyika ni kwamba kwa ndugu zetu wa Kagera kule tumeweka *station* kubwa ambayo ina *monitor* (inafuatilia) na tuseme hiyo ndiyo kubwa kuliko zote maana yake inaenda chini kilometra 10. Hizi nyingine zote tulizoziweka zinaenda kilometra tatu, nne au tano. Kwa hiyo, tetemeko la juzi *Geological Survey* wametoa taarifa kwa vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimweleze tu Mheshimiwa Lwakatare kwamba Profesa Mruma na timu

yake wako tayari kwenda kutoa, lakini walishatoa na wameshatoa maelekezo na wanazidi kuendelea na ramani inatengenezwa. Baada ya kutengeneza ramani ya Bukoba kuangalia maeneo ambayo yatakuwa yanakumbwa na hayo matetemeko, wamehamia Mkoa wa Dodoma kuanza kutengeneza hiyo ramani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimweleze Mheshimiwa Lwakatare kwamba hali ni hiyo na kila siku tunachukua *data* tunaweka. Kwa hiyo, hiyo ripoti tutaipeleka kule mkoani ikiwa Serikali ya Mkoa iko tayari kumsikiliza mtaalam mwagine bila Profesa kuwepo.

Mheshimiwa Spika, isitoshe labda nimfahamishe, siyo tu watu wa Bukoba, sasa hivi duniani hicho kikitokea stesheni za kwanza kabisa dunia nzima zinazopata kwa haraka vipimo hivyo ni Marekani, *US GS*. Sisi hata kabla hatujapata sekunde nne, tano wanatutangulia wao.

Kwa hiyo, nadhani hilo tatizo tunalifuutilia kwa karibu na wale ndugu zetu wa Bukoba walivyoelekezwa na wataalamu kwamba wasijenge pale wawafuate wale wataalamu, walishatoa maelekezo ya mwanzo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge kama Serikali ya Mkoa itakuwa haijawa tayari kumpatia ripoti, naomba wakati wa mapumziko nimpatie hiyo ripoti, lakini aende awaeleze wenzake. (*Makofii*)

SPIKA: Nakubaliana na maelezo ya Serikali na huo ndiyo Muongozo wangu. (*Makofii*)

Kuhusu Mheshimiwa Laizer utaonana na Mheshimiwa Waziri, kama kuna majibu ambayo hukupata, mtayamaliza kantini kule. (*Kicheko/Makofii*)

Nina matangazo mawili, la kwanza linatoka kwa Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto, nalo linahusu kwamba timu yake ambayo tuliwahi kutangaza siku za nyuma hapo

imeshafika hapa Bungeni kuanzia leo tarehe 2 mpaka 9 Mei, 2017 katika zoezi la kubadilisha Vyeti vya Chanjo ya Homa ya Manjano, zile *yellow card fever*, pamoja na utoaji wa chanjo yenye we ya Homa ya Manjano kwa Waheshimiwa Bunge na Watumishi wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, huduma hizi zitatolewa katika jengo la Pius Msekwa kila siku kuanzia leo mpaka tarehe 9 Mei, kuanzia saa 2.00 mpaka saa 10.00 jioni. Utaratibu wa kubadilisha hivyo vyeti vya chanjo utazingatia mambo yafuatayo:-

Waheshimiwa Wabunge, kwanza utawasilisha kile cheti ulichonacho cha Homa ya Manjano, halafu na hati yako ya kusafiria au nakala ya hati, hilo ni jambo la pili. Kile cheti cha manjaro na hati au nakala. Gharama yake ni shilingi 5,000. Kwa hiyo, hivyo vitu vitatu uzingatlie wakati wa kwenda kwenye mabadiliko.

Waheshimiwa Wabunge, kwa wale ambao wanahitaji kupata chanjo ya ugonjwa wa Homa ya Manjano watawasilisha hati ya kusafiria, kwa maana ya kwamba hawana kile cheti cha manjano; watapeleka hati na kulipia gharama ya shilingi 20,000 kwa maana ya kupata chanjo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kama maelezo haya yanakukanganya, maelezo zaidi utayapata pale Msekwa ilipokuwa zahanati ya zamani. Kwa hiyo, wote mnakaribishwa kupata chanjo hiyo ya Homa ya Manjano. Wanashughulika na mambo hayo tu ya Homa ya Manjano, mambo mengine hawaangalii Waheshimiwa, msiwe na wasiwasi. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, jana tarehe 1 Mei, 2017 ilikuwa ni Sherehe ya Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Dunia na kila ifikapo siku hiyo huwa wanachaguliwa wafanyakazi bora kuanzia ngazi za chini hadi ngazi ya Taifa katika Ofisi mbalimbali za Umma na Taasisi za binafsi katika nchi yetu.

Kwetu sisi Ofisi ya Bunge katika kufanikisha zoezi hilo kila Idara au Kitengo ilichangua mfanyakazi bora aliyewakilisha Idara husika na badaye majina hayo ya watumishi wa kila Idara au Vitengo yakawasilishwa kwenye mukutano wa pamoja kati ya Menejimenti ya Bunge ya hapa Bungeni na Tawi la Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya (TUGHE), Tawi la Ofisi ya Bunge kwa ajili ya kupata Mfanyakazi Bora wa Ofisi ya Bunge ambapo jina hilo liliwasilishwa Ofisi ya TUGHE Taifa kwa ajili ya kumpata mfanyakazi bora wa kitaifa. Aidha, sifa za kiutendaji zilikuwa ndizo vigezo muhimu katika zoezi hilo la kumpata mfanyakazi bora wa Ofisi ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, vigezo vilivypendekezwa na kuzingatiwa ni:-

- (1) Kuwahi na kutulia mahali pake pa kazi;
- (2) Nidhamu ya hali ya juu katika utenaji wa kazi;
- (3) Heshima kwa viongozi wa kazi na kwa watumishi wenzake;
- (4) Kuchukia vitendo vya rushwa;
- (5) Utiiifu, uaminifu na ukweli katika utendaji wa kazi;
- (6) Uadilifu katika utumishi;
- (7) Utayari wa kulinda maslahi ya kiuchumi katika maeneo ya kazi kwa kufichua njama ovu zinazolenga kuhtarisha ajira yake au ya watumishi wenzake;
- (8) Nia na uwezo wa mtumishi kujiendeleza kielimu juu ya kazi anazozifanya; na
- (9) Kushiriki katika shughuli za Chama cha Wafanyakazi mahala pa kazi ambapo kinatetea maslahi ya watumishi na kuhamasisha umoja mionganii mwao.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Katika majina ya wafanyakazi bora, kwa Idara na Vitendo waliopitishwa kwa kura katika Mkutano wa pamoja baina ya Menejimenti na utaratibu ambao tumejiwekea hapa Bungeni, katika Idara ya Utawala mfanyakazi bora alikuwa Mhudumu wa Ofisi anaitwa Ndugu Stanford Gombo wapo pale *gallery*, naomba usimame Stanford, ahsante sana. (*Makofi*)

Kwenye Idara ya Sheria ni Afisa Sheria Ndugu Stephano Sebba Mbutu, ahsante sana; kwenye Kurugenzi ya Zanzibar ni Ndugu Mzee Mmanga Sherehe - Msaidizi wa Kumbukumbu, ahsante; kwenye Ofisi ya Katibu wa Bunge ni Msaidizi wa Mtendaji Mkuu Ndugu Lidya Mwaipyana; kweye Idara ya Uhasibu, Mhasibu Msaidizi Ndugu Dativa Msovela; kwenye Kitengo cha Milki ni Fundi Sanifu Ndugu Sabina Mathew; Ukaguzi wa Ndani ni Mkaguzi wa Ndani Ndugu Bira Kileo; Ofisi ya Naibu Spika ni dereva Ndugu Sheny Lupondo, Idara ya Maktaba na Utafiti ni Mtafiti Ndugu Fransisca Haule; Idara ya Bajeti ni Mchumi Ndugu Lilian Masabala na Kitengo cha Ununuzi na Ugavi ni Afisa Ugavi Ndugu Hawa Mbaya. (*Makofi*)

Kutoka Idara ya Shughuli za Bunge ni Katibu Kamati Ndugu Bakari Kishoma, Kitengo cha Ulinzi na Usalama ni mlinzi Ndugu Mtonji Melle, Ofisi ya Spika ni Msaidizi wa Ofisi Ndugu Theresia Jacob, Ofisi ya Dar es Salaam ni Mkurugenzi Ndugu Jossey Mwakasyuka na Idara ya TEHAMA ni Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Lily Mraba.

Kutoka Idara ya Uhusiano wa Kimataifa na Itifaki Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Theonest Ruhilabake, Kitengo cha Habari ni Katibu Muhtasi Ndugu Jane Munene; Idara ya Kamati za Bunge ni Katibu Kamati Ndugu Chacha Nyakega na Taarifa Rasmi za Bunge ni Mwandishi wa Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) Ndugu Emmanuel Mdidi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kati ya hao waliochaguliwa na Idara na Vitengo, mtumishi ambaye amechaguliwa sasa miongoni mwao kuwa mfanyakazi bora kabisa kwa mwaka huu ni Msaidizi wa Mtendaji Mkuu ambaye ni Bi. Lidya Mwaipyana. (*Makofi/Vigelegele*)

Kule Moshi jana Mfanyakazi Bora Tanzania nzima aliyepata zawadi kubwa nadhani ni yule aliyetoka *TANESCO*, alipata shilingi milioni kumi, kwa hiyo na sisi tunampatia Bi. Lidya Mwaipyana shilingi milioni kumi. (*Makof/ Vigelegele*)

MBUNGE FULANI: Mbunge bora je?

SPIKA: Anayefuata katika wafanyakazi bora wa pili ni Ndugu Chacha Nyakega na wa tatu ni Ndugu Jossey Mwakasyuka nao watapata zawadi zao.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kumpongeza Bi. Lidya Mwaipyana kwa utumishi uliotukuka na kuchaguliwa na wenzake kuwa mfanyakazi bora na pia wote waliochaguliwa kuwa wafanyakazi bora katika Ofisi ya Bunge. Aidha, nawapongeza watumishi wote 314 wa Ofisi ya Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutuhudumia. (*Makof/*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba mkumbuke kwamba katika zoezi la uhakiki wa vyeti *fake* kwa watumishi wa umma, Ofisi ya Bunge imekuwa ni safi asilimia 100, hakuna mfanyakazi *fake* hata mmoja na niwaambie wananchi kwamba ile lugha ya kusema kwamba Wabunge wanajua kusoma na kuandika tu, niwahakikishie Bunge langu mimi hakuna maneno ya kusoma na kuandika, hili Bunge la wasomi. (*Makof/*)

Nikisema ukweli Taasisi ya Bunge kwa maana ya Wabunge, na watumishi wake 314 tukichukua *CV* zao, tukaziweka mahali pamoja taasisi hii inaweze ika-*rank* katika taasisi tatu bora, tunazidi hata baadhi ya vyuo vikuu, kabisa kwa maana kuweka watumishi wote wa taasisi hiyo kwa pamoja halafu ukaangalia uzito wa vyeti viliviyoko pale, Bunge ni moja ya taasisi yenye wasomo wa hali ya juu kabisa. (*Makof/*)

Kwa hiyo, ningependa *massage* hii iwe inawafikia wananchi wasije wakadhani hapa, mmh. Basi baada ya hapo Katibu tunaendelea.

NDG. NENELWA M. WANKANGA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

Taarifa ya Kamati ya ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, natumaini Waheshimiwa Wabunge tayari mna nakala za baadhi ya maamuzi haya, kama huna wataendelea kuleta watu wa *Hansard* wanaendelea kufanya *printing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, tafadhalii Mheshimiwa Makamu wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Almas Maige, naomba ujitalidi najua ripoti yako ni ndefu, lakini ujaribu kutumia kama nusu saa hihi.

MHE. ALMAS A. MAIGE – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE: Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Kapteni Mstaafu George Mkuchika nisome taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu shauri ya kudharau mamlaka ya Spika, linalowahusu Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe (Mbunge) na Mheshimiwa Halima James Mdee (Mbunge).

Mheshimiwa Spika, utangulizi; kwa mujibu wa Kanuni ya 4(2) na (3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu shauri la Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe (Mbunge) la kudharau Mamlaka ya Spika kinyume na kifungu cha 26 (d) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge ya Sura 296 (*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act*) na Mheshimiwa Halima James Mdee (Mbunge) la kudharau Mamlaka ya Spika, na kutumia lugha ya matusi, kuudhi na kuzalilisha Wabunge wengine kinyume na kanuni ya 64(1) (f) na (g) pamoja na Kanuni ya 74

(1)(a) na (b) ya Kanuni za kudumu za Bunge na kifungu cha 26(d) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge - Sura 296. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, chanzo cha mashauri haya dhidi ya Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe (Mbunge) na Mheshimiwa Halima James Mdee (Mbunge) ni kuwa katika kikao cha kwanza cha Mkutano wa Saba wa Bunge kilichofanyika tarehe 04 Aprili, 2017 ulifanyika uchangazi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki (*EALA*). Baada ya uchaguzi huo Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe (Mbunge) alionekana na kunukuliwa na vyombo vyaa habari akitoa maneno ya utovu wa nidhamu kwa kudharau Mamlaka ya Spika na kutoa maneno ya kuudhi kwa Wabunge wengine. Kitendo hicho kilifanyika nje ya ukumbi wa Bunge na mara ya Uchaguzi wa *EALA*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matukio hayo katika kikao cha tatu kilichofanyika siku ya Alhamis tarehe 06 Aprili, 2017 baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, waliomba Mwongozo wa Spika kuhusu vitendo hivyo vyaa kudharau Mamlaka ya Spika. Baada ya maombi ya kutolewa na kutumia mamlaka yako chini ya Kanuni ya 4(1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge na Kanuni ya 74(a) na (b) uliwataja Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe (Mbunge) na Halima James Mdee (Mbunge) na kuwataka wafike mbele ya Kamati yangu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili kujibu tuhuma dhidi yao. Aidha, uliagiza Kamati kuchunguza vitendo hivyo na kutoa taarifa kwa Spika baada ya uchunguzi kukamilika; hii ndiyo Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilianza kuchunguza kwa kutoa hati za wito (*summons*) kwa Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe na Mheshimiwa Halima James Mdee wafike mbele ya Kamati siku ya Jumamosi tarehe 08 Aprili, 2017 ili kujibu tuhuma zao. Mheshimiwa Freeman Mbowe alituhumiwa kuwa akiwa nje ya ukumbi wa Bunge mara baada ya kumalizika Uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Masharika alinukuliwa na vyombo vyaa habari akitoa kauli za kudharau Bunge na Mamlaka ya Spika kinyume na

Kifungu cha 26 (d) cha Sheria ya kinga, Haki na Madaraka ya Bunge sura 296 (*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP 296 R.E. 2015*).

Mheshimiwa Spika, tuhuma dhidi ya Mheshimiwa Halima James Mdee ni kama ifuatavyo:-

- i. Kusema Bungeni bila idhini ya Spika, kinyume na Kanuni za Majadiliano kwa mujibu wa Kanuni za 59 na 60 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016.
- ii. Kutoa lugha ya matusi, kuudhi na kumdhalilisha Mbunge mwingine kinyume na Kanuni ya 64(1) (f) na (g) ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge, Toleo la Januari 2016.

Mheshimiwa Spika, namba tano, shauri dhidi ya Mheshimiwa Freeman Mbowe (Mbunge), katika uchunguzi Kamati iliangalia picha za video na mahojiano ya Mheshimiwa Mbowe na waandishi wa habari nje ya Ukumbi wa Bunge mara baada ya uchaguzi huo wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Alinukuliwa na vyombo vyya habari akitamka maneno yafuatayo:-

- (i) Spika amevunja Kanuni za Bunge, Sheria hazikuheshimiwa, ubabe umetumika.
- (ii) Ni mkakati wa Kiserikali, tunajua Rais anahusika, Waziri Mkuu anahusika, viongozi wa chama chao wanahusika.
- (iii) Tumeleta wagombea wazuri sana wawili, *very competent*, wamepigiwa kura za hapana kwa sababu ulikuwa ni mkakati wa Chama cha Mapinduzi, tumeona ni ujinga na upumbavu mtupu.
- (iv) Uchaguzi huu umekuwa wa kijinga.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Freeman Mbewe aliposomewa tuhuma dhidi yake alikiri wazi kuwa alitamka maneno hayo, yaliyolalamikiwa na Bunge na akaliomba radhi Bunge kwa maneno yake mwenyewe kama ifuatavyo:-

"Mheshimiwa Mwenyekiti, matamshi yangu hayakukusudia kumkwaza mtu ye yeyote, dhamira hiyo kwangu haikuwepo, na kama imemkwaza kiongozi ye yeyote hususan Mheshimiwa Spika, mimi namuomba radhi sana. Namuomba radhi kwa sababu haikuwa dhamira yangu kumkwaza Mheshimiwa Spika, namheshimu sana na ninaheshimu mamlaka yake na nayatambua."

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Freeman Mbewe pia aliomba radhi kwa Bunge kama ifuatavyo:-

"Hilo naliombea radhi sana kwa sababu halikukusudiwa katika dhamira yangu, wala sikukusudia wakati wowote, wala siwezi kulidharirisha Bunge kwa sababu najua Bunge ni chombo kikubwa ambacho nimeshiriki kipindi kirefu huko, kwa hiyo, nalielewa na najua mipaka yake na mamlaka yake, ahsanteni sana."

Mheshimiwa Spika, kutokana na kukiri kwake Mheshimiwa Freeman Mbewe na kuomba radhi kwa Mheshimiwa Spika na Bunge, Kamati iliridhia kuwa alitamka maneno ya dharau kwa Bunge na kwa Mamlaka ya Spika, hivyo Kamati ilimtia hatiani kwa kosa la kudharau Mamlaka ya Spika, huo ndio ulikuwa uchunguzi wa Kamati kuhusu shauri la kudharau Mamlaka ya Spika, lilitomhusu Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbewe (Mbunge), hivyo Bunge liutafakari ushauri uliotolewa dhidi yake na kuzingatia wakati wa kupitisha azimio la kuchukua hatua dhidi yake.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchunguzi kwa kusoma Taarifa Rasmizi za Bunge (*Hansard*) na kuangalia picha za video za ukumbini wakati wa taratibu za uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki (*EALA*) kuhusu Mheshimiwa Halima Mdee.

Mheshimiwa Spika, wakati mjadala wa hoja ya uchaguzi huo ukiendelea Mheshimiwa Halima James Mdee (Mbunge) alisikika akitoa lugha ya matusi na ya kuudhi kama ifuatavyo:-

"Hatupendi maneno ya kipumbavu hapa, Mheshimiwa Spika, unaongea nini? Fala wewe!"

Mheshimiwa Spika, katika mahojiano ya shahidi mbele ya Kamati, Mheshimiwa Halima James Mdee aliposomewa tuhuma dhidi yake, alikiri kusema Bungeni bila idhini ya Spika wakati wa uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Pia alikiri kutamka maneno ya matusi na kuudhi kama yalivyonukuliwa katika Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) na alieleza kama ifuatavyo:-

"Hilo nimeshasema kwamba nimeongea bila idhini ya Spika, nimekiri nimetoa lugha ya kuudhi na nimesema mbele ya Kamati yako kwamba malengo yangu mimi nilikuwa namu-address Kigwangalla, lakini kama Hansard ndiyo ushahidi namba moja na kwa mujibu wa Hansard imeonekana kwamba nilikuwa namu-address Spika, sasa siwezi tu ku-dispute ila kwa sababu mnasema Hansard ndiyo ushahidi namba moja, niko tayari kuomba radhi, kwa wote wawili, kwa Spika lakini vilevile kwa Mheshimiwa Kigwangalla."

Mheshimiwa Spika, Kamati ilimkumbusha Mheshimiwa Halima Mdee (Mbunge) kwamba aliwahi kutiwa hatiani kwa kosa kama hilo siku za nyuma kwa kudharau Mamlaka ya Spika na kupewa adhabu ya kutohudhuria baadhi ya vikao vya Mkutano wa Tatu wa Bunge. Mheshimiwa Halima Mdee (Mbunge), alikubali kuwa aliwahi kutiwa hatiani kwa kosa kama hili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Halima Mdee alipoulizwa kama hatarudia tena kufanya kosa hili, alijibu:-

"Nitajitahidi kutorudia ingawa ngumu sana ku-predict future itakuwaje. Kwa hiyo, naamini Mwenyezi Mungu ataniongoza kosa lisijirudie tena."

Mheshimiwa Spika, namba kumi ni kuhusu maoni ya Kamati (*findings*). Baada ya kukamilisha uchunguzi, Kamati ilibaini kuwa kweli Halima Mdee (Mbunge) alisema Bungeni bila idhini ya Spika na hivyo kukiuka Kanuni za 59 na 60 kuhusu utaratibu wa Majadiliano Bungeni. Pia alikiuka kifungu cha 29 (d) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge.

Mheshimiwa Spika, vilevile maneno au kauli za Mheshimiwa Halima Mdee Mbunge kama yalivyonukuliwa kwenye *Hansard* ni lugha ya matusi na lugha ya kuudhi kinyume na Kanuni ya 64(1)(f) na (g) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Pia kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili ya Baraza la Kiswahili la Taifa chapa ya mwaka 2015 neno "pumbavu" maana yake ni "siokuwa na uwezo wa kuelewa, jinga, zoba, zuzu" na neno 'fala" maana yake ni; "mtu ambaye akili zake hazifanyi kazi vizuri, mpumbavu, bwege, mjinga, bozi au gulagula."

Mheshimiwa Spika, kutokana na ushahidi huo, Kamati imejiridhisha bila kuacha shaka yoyote na kumtia hatiani Mheshimiwa Halima James Mdee (Mbunge) kwa kudharau Mamlaka ya Spika na kutoa lugha ya matusi na lugha ya kuudhi.

Mheshimiwa Spika, huo ndio ulikuwa uchunguzi wa Kamati kuhusu shauri la kudharau Mamlaka ya Spika linalomhusu Mheshimiwa Halima James Mdee (Mbunge). Hivyo, Bunge liutafakari ushahidi uliotolewa dhidi yake na kuuzingatia wakati wa kuitisha azimio la kutoa adhabu inayostahili kwa kosa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, na napenda nitumie nafasi hii kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge letu hili ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi

kuisimamia na kuishauri Serikali ili kuhakikisha kuwa ustawi wa wananchi ndio kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, kipekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua kwa umakini mkubwa mashauri ya kudharau Mamlaka ya Spika. Wajumbe hawa wanafanya kazi nzuri na walizingatia misingi ya haki, bila kumuoneea au kumpendelea mtu yoyote. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika taarifa hii yaingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, Aidha napenda kumshukuru kwa dhati kabisa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah na Makatibu wa Kamati kwa kusaidia Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika baada ya kusema hayo sasa naomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kupokea maoni na mapendekezo ya Kamati ili baada ya mjadala huu liazimie kuchukua hatua stahili kwa kadiri inavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kusoma Azimio la Bunge kuhusu hatua za kuchukua dhidi ya Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe (Mb) kwa kuhusika na vitendo vya kudharau Mamlaka ya Spika siku ya tarehe 4 Aprili, 2017. Limetolewa chini ya Kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge (*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, [CAP 296 R:E 2015]*).

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaongozwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge ambazo zilitungwa na Bunge lenyewe kwa ajili ya kuliongoza katika kutekeleza shughuli zake;

Na kwa kuwa, Sheria na Kanuni za uendeshaji wa shughuli za Bunge zimeweka utaratibu wa majadiliano ndani na nje ya Bunge, na kwamba kwa taratibu hizo Wabunge

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wanatakiwa kuheshimu Mamlaka ya Spika na shughuli za Bunge kwa ujumla;

Na kwa kuwa, katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Saba wa Bunge kilichofanyika tarehe 4 Aprili, 2017 ulifanyika uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki (*EALA*), na baada ya uchaguzi huo, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe (Mbunge) alitoa kauli za kudharau Mamlaka ya Spika;

Na kwa Kuwa, Mheshimiwa Spika kwa Mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge alimpeleka mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe (Mbunge) kwa kosa la kudharau Mamlaka ya Spika;

Na kwa kuwa, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilikaa tarehe 8 Aprili, 2017 hapa Dodoma kusikiliza shauri dhidi ya Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe (Mbunge);

Na kwa kuwa, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbobe alitiikia wito wa Kamati bila kuleta usumbufu wa aina yoyote, na alipohojija na Kamati alikiri wazi kosa lake na kuomba radhi kwa Mheshimiwa Spika na Bunge;

Na kwa kuwa, kosa la Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe (Mbunge) la kudharau Mamlaka ya Spika lilikuwa ni kosa lake la kwanza.

Hivyo basi, Bunge linaazimia; moja, kumsamehe Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe (Mbunge) kutokana na kitendo chake cha kuonesha ushirikiano kwa Kamati na pia kitendo chake cha kiungwana cha kuomba radhi kwa Mheshimiwa Spika, kwa Bunge na kwa wengine wote alioyawakwaza kutokana na kauli yake; na mbili hata hivyo, kwa kuwa Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe (Mbunge) ni Kiongozi yaani Mwenyekiti wa Chama cha CHADEMA, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mbunge, anatakiwa kuwa mfano bora wa kuigwa kwa Wabunge

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wengine anaowaongoza Hivyo Mheshimiwa Freeman Mboge (Mbunge) anatakiwa kujiepusha na vitendo vyaa ina yoyote vyaa kudharau Mamlaka ya Spika na Bunge ili awe mfano bora wa kuigwa katika kuzingatia sheria, Kanuni na taratibu za uendeshaji wa Bunge.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kutoa msamaha kwa Mheshimiwa Freeman Aikael Mboge (Mbunge) na kumshauri kama kiongozi kuwa mfano bora kwa Wabunge wengine katika kuheshimu sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji wa shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

MHE. ALMAS A. MAIGE – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE: Mheshimiwa Spika, naomba sasa kwa ruhusa niseme Azimio la Bunge kuhusu hatua za kuchukuliwaa dhidi ya Mheshimiwa Halima James Mdee (Mbunge) kwa kuhusika na vitendo vyaa kudharau mamlaka ya Spika na kutoa lugha ya matusi na ya kuudhi katika kikao cha kwanza cha Mkutano wa Saba wa Bunge siku ya tarehe 4 Aprili, 2017.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaongozwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge ambazo zilitungwa na Bunge lenyewe kwa ajili ya kuliongoza katika kutekeleza shughuli zake;

Na kwa kuwa, sheria na kanuni za uendeshaji wa shughuli za Bunge zimeweka utaratibu wa majadiliano ndani ya Bunge, na kwamba kwa taratibu hizo Wabunge wanatakiwa kujiheshimu na kuheshimu Mamlaka ya Spika na shughuli za Bunge kwa ujumla;

Na kwa kuwa, katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Saba wa Bunge kilichofanyika tarehe 4 Aprili,

2017 ulifanyika uchaguzi wa Mkutano wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki (*EALA*), na wakati uchaguzi ukifanyika katika Ukumbi wa Bunge, Mheshimiwa Halima James Mdee (Mbunge) alifanya vitendo vya kudharau Mamlaka ya Spika na kutoa lugha ya matusi, kuudhi na kudhalilisha Wabunge wengine;

Na kwa kuwa, Mheshimiwa Spika kwa mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge alimpeleka mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Mheshimiwa Halima James Mdee (Mbunge) kwa makosa ya kudharau Mamlaka ya Spika na kutoa lugha ya matusi, kuudhi, na kudhalilisha Wabunge wengine;

Na kwa kuwa, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilikaa kuanzia tarehe 8, Aprili, 2017 hadi tarehe 10 Aprili, 2017 hapa Dodoma na kusikiliza shauri la Mheshimiwa Halima James Mdee (Mbunge);

Na kwa kuwa, kwa kuzingatia kuwa Mheshimiwa Halima James Mdee hii ni mara ya pili kutiwa hatiani kwa kosa kama hili la kudharau Mamlaka ya Spika na kupewa adhabu na Bunge ya kutohudhuria Vikao vya Mkutano wa Tatu na Nne wa Bunge;

Na kwa kuwa, Mheshimiwa Halima James Mdee (Mb) alivunja tena Kanuni za 59, 60(2), 64(1)(f) na (g), zilizosomwa pamoja na Kanuni ya 74(1) (a) na (b) na Kifungu cha 26(d) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, sura ya 296 kwa kufanya vitendo vya kutoa kauli za kudharau Mamlaka ya Spika;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kuwa Mheshimiwa Halima James Mdee (Mbunge) asihudhurie vikao vyote vilivyobaki vya Mkutano wa Saba wa Bunge la Bajeti kuanzia tarehe ya Azimio hili la Bunge, kutohana na tabia yake ya mara kwa mara ya kufanya vitendo vya kudharau Mamlaka ya Spika na kutoa lugha ya matusi na ya kuudhi. Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba linakubaliana na kupitisha mapendekezo ya adhabu hiyo kwa Mheshimiwa Halima

James Mdee (Mbunge) kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, mbele yako.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

MHE. ALMAS A. MAIGE – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE: Mheshimiwa Spika, naomba sasa niwasilishe mbele yako Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu shauri la kudharau Mamlaka ya Spika linalomhusu Mheshimiwa Ester Amos Bulaya (Mbunge).

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 4(2) na (3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu shauri la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya (Mbunge) la kudharau mamlaka ya Spika, kinyume na kifungu cha 26(c), (d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296; (*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP. 296 R.E. 2015*) na kinyume na Kanuni ya 74(1)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, mnamo siku ya tarehe 30 Mei, 2016 katika Mkutano wa Tatu, kikao cha Thelathini na Mbili, wakati wa asubuhi Bunge lilikuwa likijadili Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha, 2016/2017. Mheshimiwa Joshua Nassari (Mbunge) aliomba Mwongozo wa Spika kwamba Bunge liahirishe kujadili Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji na badala yake lijadili suala la waliokuwa wanafunzi wa Diploma Maalum ya Sayansi, Chuo Kikuu cha Dodoma ambao walifukuzwa ndani ya saa 48.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika alitoa Mwongozo kuwa hakuona kama ni utaratibu bora wa uendeshaji wa shughuli za Bunge kwa kuahirisha shughuli za

Bunge kwa kuwa jambo hilo lilikuwa linashughulikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kufuatia Mwongozo huo wa Naibu Spika, baadhi ya Wabunge hawakuridhika na hivyo waliendelea kuomba Mwongozo bila utaratibu, walismama bila kuruhusiwa huku wakipiga kelele, jambo ambalo liliurvuga shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, mara kikao cha jioni kiliporejea, Mheshimiwa Naibu Spika alitoa maelezo kuwa baada ya kutafakari vurugu zilizotokea asubuhi, Kamati ya Uongozi iliamua kuwa, Waziri wa Elimu Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako atoe Kauli ya Serikali kuhusiana na suala la mgogoro wa Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Dodoma na Walimu, pamoja na hatma ya wanafunzi waliofukuzwa. Hata hivyo, Profesa Joyce Ndalichako hakuwepo Bungeni wakati huo, hivyo alimwita Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji kuhitimisha hoja ya Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Kufuatia hatua hiyo, baadhi ya Wabunge walismama bila kuruhusiwa na kuanza kuomba Miongozo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilianza uchunguzi kwa kutoa hati ya wito (*summons*) kwa Mheshimiwa Ester Amos Bulaya (Mbunge) kufika mbele ya Kamati siku ya Alhamisi tarehe 20 Aprili, 2017 ili kujibu tuhuma dhidi yake.

Mheshimiwa Spika, mahojiano ya shahidi, siku ya tarehe 20 Aprili, 2017 Mheshimiwa Ester Amos Bulaya Mbunge alifika mbele ya Kamati kwa mujibu wa hati ya wito aliyopewa. Mheshimiwa Ester Amos Bulaya aliposomewa tuhuma dhidi yake alikiri na kuliomba radhi Bunge kwa maneno yake mwenyewe; "*Nachukua fursa hii kuomba radhi kwa Kamati, Bunge na kwa yote yaliyotokea naomba radhi kwa moyo wa dhati kabisa, sipendi kusumbua Kamati hii naiheshimu sana, kama Kamati imeona chochote nilichokifanya, kwa moyo wa dhati naomba radhi.*"

Mheshimiwa Spika, Kamati ilimkumbusha Mheshimiwa Ester Bulaya kwamba hapo awali aliwahi kutiwa hatiani na

Kamati kwa kosa kama hili la kudharau Mamlaka ya Spika na alipewa adhabu ya kutohudhuria baadhi ya vikao.

Mheshimiwa Spika, kuititia mkanda wa video wa tukio la tarehe 30 Mei, 2016 iliyorekodiwa ukumbini Mheshimiwa Ester Bulaya (Mbunge) alionekana akipiga makofii bila utaratibu, akitaidi maelekezo ya Spika ya kumtaka atulie ili shughuli iliyokuwa mezani iendelee. Wakati Kambi nzima ya Upinzani ilipoamuliwa kutoka nje ndipo Mheshimiwa Ester Bulaya alionekana akirusha ovyo kwa nia ya kutawanya vitabu ovyo na kwa makusudi, jambo ambalo ni kitendo cha kuleta vurugu na ni dharau kwa Mamlaka ya Spika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuangalia mkanda wa video, Mheshimiwa Ester Bulaya kwa hiari yake alikiri mbele ya Kamati kutenda kitendo hicho kiovu na aliomba radhi kwa Bunge kutokana na vitendo vyake hivyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ushahidi uliopo, Kamati iliridhia bila kuacha shaka yoyote kwamba Mheshimiwa Ester Bulaya Mbunge alifanya kosa kinyume cha kifungu cha 26(c),(d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 pamoja na Kanuni ya 74 ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua dhidi ya Mheshimiwa Ester Bulaya (Mbunge) Kamati ilizingatia yafuatayo:-

(a) Kitendo cha Mheshimiwa Ester Bulaya Mbunge kukiri kutenda kosa;

(b) Mheshimiwa Ester Bulaya Mbunge ni mkosaji wa mara ya pili;

(c) Athari za vitendo vilivyofanywa na ambavyo vingevuruga shughuli za Bunge na kushusha hadhi ya Bunge; na

(d)Mheshimiwa Ester Bulaya tangu alipoadhibiwa na Bunge lako tukufu mnamo tarehe 30 Mei, 2016, hajaacha kufanya vitendo vya uvunjaji wa Kanuni lakini kwa kiasi fulani amepunguza vitendo hivyo tofauti na alivyokuwa kabla ya kupewa adhabu ile ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge kinaeleza kuwa Mbunge yeoyote atakayefanya kosa la kudharau Mamlaka ya Spika au shughuli za Bunge kwa mujibu wa kifungu cha 26 au kifungu kingine chochote, Bunge linaweza kuazimia kumuelekeza Spika kumpa karipio kali (*reprimand*) au kumsimamisha asihudhurie vikao vya Bunge kwa muda litakaloona unafaa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia sheria zilizotawala suala hili pamoja na mashauri yaliyowahi kuamuliwa na Kamati, pamoja na kitendo cha Mheshimiwa Bulaya kukiri na kuomba radhi huku akiahidi kutorudia tena vitendo hivi, hivyo tunapendekeza Bunge litafakari ushahidi uliotolewa dhidi yake na kuzingatia wakati wa kuitisha azimio la kutoa adhabu inayostahili kwa kosa hilo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuongoza Bunge vizuri na kipekee nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili, kuchambua na kwa umakini na nimeshawataja katika maelezo yangu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kujadili na kupokea maoni na mapendekezo ya Kamati ili baada ya mjadala liazimie kuchukua hatua stahiki kwa kadri litakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nisome Azimio la Bunge kuhusu hatua za kuchukua dhidi ya Mheshimiwa Ester Amos Bulaya (Mbunge) kwa kuhusika na vitendo vya

kudharau Mamlaka ya Spika katika Mkutano wa Tatu, Kikao cha Thelathini na Mbili kilichofanyika tarehe 30 Mei, 2016. Azimio hili ilimetolewa chini ya Kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge (*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, [CAP 296 R.E 2015]*).

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaongozwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge ambazo zilitungwa na Bunge lenyewe kwa ajili ya kuliongoza katika kutekeleza shughuli zake;

Na kwa kuwa, sheria na kanuni za uendeshaji wa shughuli za Bunge zimeweka utaratibu wa majadiliano ndani ya Bunge, na kwamba kwa taratibu hizo Wabunge wanatakiwa kuheshimu Mamlaka ya Spika na shughuli za Bunge kwa ujumla;

Na kwa kuwa, katika Kikao cha Thelathini na Mbili cha Mkutano wa Tatu wa Bunge kilichofanyika tarehe 30 Mei, 2016 Bunge ilikuwa likijadili Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha, 2016/2017, na Mheshimiwa Ester Amos Bulaya alifanya vitendo vya kudharau Mamlaka ya Spika kwa kurusha na kutawanya ovyo karatasi za vitabu, kumbukumbu wakati Bunge likiwa linaendelea hivyo kuvuruga shughuli za Bunge;

Na kwa kuwa, Mheshimiwa Spika kwa mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge alimpeleka mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Mheshimiwa Ester Bulaya (Mbunge) kwa makosa ya kudharau Mamlaka ya Spika;

Na kwa kuwa, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilikaa tarehe 20 Aprili, 2017 hapa Dodoma na kusikiliza shauri la Mheshimiwa Ester Bulaya;

Na kwa kuwa, Mheshimiwa Ester Bulaya (Mbunge) kwa kuzingatia kuwa hii ni mara yake pili kutiwa hatiani kwa kosa kama hili la kudharau Mamlaka ya Spika na kupewa

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

adhabu na Bunge ya kutohudhuria Vikao vya Mkutano wa Tatu na Nne wa Bunge;

Na kwa kuwa, Mheshimiwa Ester Bulaya alivunja tena Kanuni ya 74(1)(a) na (b) na kifungu cha 26(d) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge Sura ya 296, kwa kufanya vitendo vya kudharau Mamlaka ya Spika;

Na kwa kuwa, Mheshimiwa Ester Bulaya Mbunge kwa hiari yake alikiri, alitikia wito wa Kamati bila kuleta usumbufu wa aina yoyote, na alipohojwa na Kamati alikiri wazi kosa lake na kuomba radhi kwa Mheshimiwa Spika;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kumpa karipio kali Mheshimiwa Ester Bulaya kutokana na kitendo chake cha kuonesha ushirikiano kwa Kamati na pia kitendo chake cha kuomba radhi kwa Mheshimiwa Spika, kwa Bunge na wengine wote aliowakwaza kutokana na matendo yake hayo.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba linakubaliana na kuitisha mapendekezo ya adhabu hiyo kwa Mheshimiwa Ester Amos Bulaya kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Naomba kutoa hoja.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

MHE. ALMAS A. MAIGE – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya MwenyeKITI wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge naomba sasa nisome shauri la kuingilia uhuru wa haki za Bunge lililowahusu Ndugu Paul Christian Makonda na Ndugu Alexander Pastory Mnyeti.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu shauri la kuingilia uhuru na haki za Bunge lililowahusu Ndugu Paul Christian Makonda na Ndugu Alexander Pastory Mnyeti.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa fasili ya 4(2) na (3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati kuhusu uchunguzi wa tuhuma zinazowahusu Ndugu Paul Christian Makonda, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na Ndugu Alexander Pastory Mnyeti, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru kuhusu kudharau, kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mamlaka uliyonayo chini ya fasili ya 4(1)(a) na (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, uliiagiza Kamati yangu kukutana kwa ajili ya kushughulikia suala la tuhuma za kudharau, kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge zinazowahusu Ndugu Paul Makonda na Ndugu Alexander Mnyeti.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelekezo hayo, Ndugu Paul Makonda na Ndugu Alexander Mnyeti waliitwa kwa hati ya wito (*summons*) ili wafike mbele ya Kamati kujibu tuhuma zinazowakabili kwa kukiuka Kifungu cha 26(e) na 34(1)(j) vya Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge Sura ya 296.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la shauri; mnamo tarehe 8 Februari, 2017 katika Kikao cha Nne cha Mkutano wa Sita, Bunge lilipitisha Maazimio yaliyotokana na hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara (Mbunge) iliyowasilishwa chini ya Kanuni ya 51 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waitara alitoa hoja kwamba Ndugu Paul Christian Makonda ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam alinukuliwa na Kituo cha Televisheni cha Clouds akisema Wabunge wanasingzia Bungeni. Aidha, Mheshimiwa Waitara aliendelea kueleza kwamba pia Mkuu wa wilaya ya Arumeru Ndugu Alexander Pastory Mnyeti aliandika katika mtandao wa kijamii wa *facebook* kuwa Azimio la Bunge lililotokana na pendekezo la Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa la kuwapatia semina Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuhusu namna ya

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kutekeleza majukumu yao ni upuuzi mtupu na kwamba Wabunge hawajielewi na anashauri wafanye kazi zao na za wengine waachiwe wenyewe.

Mheshimiwa Spika, katika kujadili hoja hiyo, Bunge liliona kuwa Ndugu Makonda na Ndugu Mnyeti wana tuhuma za kujibu kuhusu kulidharau Bunge, kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge na hivyo Bunge liliazimia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI atoe waraka mahsus kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuhusu namna ya kutekeleza majukumu yao bila kuingilia mihimili mingine; mbili, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Ndugu Paul Christian Makonda na Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Ndugu Alexander Pastory Mnyeti waitwe mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge; na tatu, endapo itathibitika na Bunge kuridhia, wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria na taratibu za Bunge zilizopo.

Mheshimiwa Spika, shauri kuhusu Ndugu Paul Christian Makonda; tuhuma dhidi ya Ndugu Makonda zinatokana na kauli yake aliyoitoa mnamo tarehe 2 Februari 2017 katika mukutano wake na vyombo vya habari uliofanyika ofisini kwake. Ambapo aliulizwa swali lifuatalo na mwandishi wa habari:-

"Mheshimiwa, ni kwamba tumeona Bungeni kuna ushahidi mbalimbali uliotolewa, wanasema wanajuana, wanatajana lakini mpaka muda huu hatujaua hatua gani zitachukuliwa kwa wale wanaosema wanajuana wenyewe kwa wenyewe."

Akijibu swali hilo Ndugu Makonda alikaririwa akisema:-

"... zingine ni mbwembwe tu, unajua mle ndani wakati mwingine wanachoka na kusinzia lazima kuwe na watu kidogo akili zao zinawasaidia kuamka, kucheka na kufurahi maisha yanaendelea."

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Ndugu Makonda alifika mbele ya Kamati tarehe 29 Machi, 2017 na kusomewa tuhuma dhidi yake ambapo alikiri kwamba ni kweli alitoa kauli hiyo. Katika maelezo yake alionesha kujutia kauli hiyo ambayo iliakwaza na kuwavunja heshima Wabunge. Hivyo, aliomba radhi kwa kueleza kuwa hata kabla ya kuitwa na Kamati hii tayari alishaandika barua kwa Mheshimiwa Spika ya kuliomba radhi Bunge.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya maelezo yake ya kukiri kosa mbele ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

"Mheshimiwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge na Wajumbe wa Kamati hii ambaao ni Waheshimiwa Wabunge, pamoja na timu nzima ya Sekretarieti, awali ya yote nawashukuru na nawapongeza kwa kazi kubwa mnayoifanya. Wengi wenu tumefahamiana na wengi wenu ni walezi wangu. Kwa hiyo, ninajisikia vibaya sana kusimama mbele yenu kwa kuwakwaza na kuwavunja heshima ambayo sikupaswa kufanya hivyo hasa kwa watu ambaao mmekuwa walezi wangu na ni watu ambaao mnanitegemea nifanye vizuri kwa ajili ya kuwawakilisha vijana wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa baada ya kauli yangu, nilichukua jukumu la kuandika barua kwa Mheshimiwa Spika, baada ya kusikiliza mjadala katika Bunge na kumwomba radhi Mheshimiwa Spika kwa kitendo cha kauli yangu niliyoitoa wakati nikijibu swali pale ambapo mwandishi alitaka kujuu mambo kadhaa yaliyofanyika."

Mheshimiwa Spika, Ndugu Makonda alimalizia maelezo yake kwa kusema:-

"Kwa hiyo, akili yangu ilikuwa na mtazamo wa namna hiyo, haikuwa na mtazamo wa kulidharau Bunge, haikuwa na mtazamo wa kumvunja heshima Mbunge ye yote yule, na kwa kweli najisikia vibaya sana kusimama mbele yenu na ninaomba radhi sana sana kwa kauli niliyoitoa na tafsiri iliyopatikana."

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ushahidi wa kukiri kwa shahidi huyu, Kamati iliridhia kuwa Ndugu Paul Christian Makonda, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, alitamka maneno yaliyolalamikiwa na Wabunge na hivyo kumtia hatiani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shauri kuhusu Ndugu Alexander Pastory Mnyeti; chanzo cha malalamiko kuhusu shahidi huyu ni Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa iliyowasilishwa tarehe 3 Februari, 2017. Katika taarifa hiyo Kamati ilipendekeza kuwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa awapatie semina Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuhusu namna ya kutekeleza majukumu yao. Mapendekezo hayo yaliridhiwa na Bunge na kuwa Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kutohana na masuala mbalimbali yaliyojadiliwa Bungeni kuhusiana na taarifa hilo, Ndugu Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Alexander Pastory Mnyeti alipoandika katika ukurasa wake wa mtandao (*facebook*) aliyaита mapendekezo hayo ni upuuzi mtupu na kwamba Wabunge hawajielewi, anawashauri wafanye kazi zao. Maneno aliyoandaika katika ukurasa huo ni haya yafuatayo:-

"Upuuzi mtupu. Wabunge hawa hawajielewi. Nawashauri fanyeni kazi zenu za wengine waachieni wenywewe."

Mheshimiwa Spika, siku ya tarehe 6 Aprili, 2017 Ndugu Mnyeti alifika mbele ya Kamati yangu na kuhojiwa kuhusiana na tuhuma zilizomkibili ambapo alikiri kuandika maneno hayo katika ukurasa wake wa *facebook*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, shahidi aliomba radhi kwa Bunge na kusema kuwa hana ubavu wa kushindana na Bunge. Baadhi ya maneno yake mbele ya Kamati ni yafuatayo:-

"Mheshimiwa Mwenyekiti, basi naomba sasa Kamati yako itumie busara, na ninaomba radhi kwamba limekuwa

ni kubwa lakini halikuwa kusudio langu tangu awali kwamba sasa nilikwaze Bunge kwa style hiyo. Mimi naomba radhi Kamati yako itumie busara zake lakini lengo kutoka moyoni kwangu halikuwa katika hali hiyo ambayo limefikia. Naomba radhi, jambo limekuwa kubwa lengo halikuwa katika hali hii liliivyo chukuliwa. Nikiri kuwa ni madhaifu yangu sikutenda kiungwana, naomba Kamati inisamehe kuanzia sasa na kuendelea haitajirudia tena. Kwa hiyo, binafsi niombe Kamati yako kwa nafasi ya kipekee ione umuhimu wa kunisamehe.”

Mheshimiwa Spika, baada ya kumsikiliza shahidi huyo Kamati imejiridhisha bila kuacha shaka yoyote kwamba shahidi huyo aliandika maneno yaliyolalamikiwa ya kuingilia uhuru na kuvunja haki za Bunge kinyume na kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, vilevile maneno aliyoyaandika Ndugu Alexander Mnyeti yalikiuka kifungu cha 34(1)(j) kinachokataza mtu ye yeyote kuchapisha kwa madhumuni ya kumkashifu (*libel*) Mbunge kuhusu tabia au mwenendo wake kutokana na kitendo cha Mbunge huyo, au maneno aliyo yasema wakati akitekeleza majukumu yake ya kibunge. Hivyo Kamati ilimtia hatiani.

Mheshimiwa Spika, katika kupendekeza hatua za kuchukua, Kamati ilizingatia na kutafakari kwa kina kuhusu ushahidi wa shauri hili pamoja na maeleo ya kukiri yaliyotolewa na mashahidi wote wawili. Vilevile kamati ilizingatia hatua ya mashahidi kukiri na kujutia vitendo vyao walivyofanya vyta ukiukwaji wa sheria za nchi kwa kuingilia uhuru na kuvunja haki za Bunge.

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo ulikuwa uchunguzi wa Kamati kuhusu shauri la kudharau Bunge, kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge linalowahu Ndugu Paul Christian Makonda na Ndugu Alexander Pastory Mnyeti. Hivyo, Bunge iliutafakari ushahidi huu uliotolewa dhidi yao na kuzingatia wakati wa kupitisha azimio na hatua za kuchukua dhidi yao.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kusoma taarifa hii kwa niaba ya Mwenyekiti wangu Kapteni George Mkuchika na kuwasilisha maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, na napenda nitumie nafasi hii tena kukupongeza wewe kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge letu hili ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi katika kusimamia na kushauri Serikali kuhakikisha kuwa ustawi wa wananchi tunaowawakilisha ndicho kipaumbele chetu.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Wajumbi wete wa Kamati hii sasa kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua kwa umakini mkubwa sana shauri la kuingilia uhuru wa kuvunja Haki za Bunge. Wabunge hao walifanya kazi nzuri na walizingatia misingi ya haki bila kumuonea au kumpendelea mtu yeoyote. Naomba majina yao ya Kamati yaliyoorodheshwa kwenye Taarifa hii yaingie kwenye *Hansard*.

Aidha, napenda kumshukuru sana kwa dhati Katibu wa Bunge Ndugu Thomas Kashililah na Makatibu wa Kamati kwa kusaidia Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupokea maoni na mapendekezo ya Kamati hii na baada ya mjadalaliazimie kuchukua hatua stahiki kwa kadri linavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nisome Azimio la Bunge kuhusu hatua za kuchukua dhidi ya Ndugu Paul Christian Makonda aliyetiwa hatiani kwa kosa la kudharau, kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge. Azimio hili limetolewa chini ya kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge (*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, [CAP 296 R.E 2015]*).

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa aligiza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ikutane na kulifanya kazi

suala la tuhuma dhidi ya Ndugu Paul Christian Makonda kuhusu kudharau, kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge;

Na kwa kuwa, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilikaa tarehe 29 Machi, 2017 na tarehe 9 -10 Aprili, 2017 kufanya uchunguzi wa suala hilo uliowezesha Kamati kubaini kuwa Ndugu Paul Christian Makonda amekiuka masharti ya kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge, Sura ya 296 kwa kutamka maneno yanayoonesha kudharau, kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge;

Na kwa kuwa kitendo cha kutamka maneno hayo ni kitendo cha dharau, kudhalilisha na kulifiedhehesha Bunge;

Na kwa kuwa Kamati imezingatia ukweli kwamba Ndugu Paul Christian Makonda hakuisumbua Kamati kwa namna yoyote ile bali alikuwa mtii na alitoa ushirikiano mkubwa kwa Kamati;

Na kwa kuwa Kamati imezingatia kwamba Ndugu Paul Christian Makonda hakuwa na dhamira ya kulidharau wala kulidhalisha Bunge kama ambavyo ilichukuliwa;

Na kwa kuwa Kamati imezingatia kuwa Ndugu Paul Christian Makonda hajawahi kutenda kosa kama hilo na kufikishwa mbele ya Kamati;

Na kwa kuwa Ndugu Paul Christian Makonda amekiri makosa yake na kuliomba radhi Bunge;

Na kwa kuwa Ndugu Paul Christian Makonda alionesha nia ya kukiri kosa na kuamua kumwandikia Mheshimiwa Spika barua ya kuomba radhi hata kabla hajafika mbele ya Kamati;

Na kwa kuwa Kamati imezingatia usoefu wa Mabunge mengine kuhusu adhabu kwa mtu ambaye amekiri kosa la kudharau Bunge na kuomba msamaha wa kosa hilo;

Na kwa kuwa uzoefu wa Mabunge mengine ya Jumuiya ya Madola kama vile Bunge la Lok Sabha la nchini India unaonesha kuwa Bunge hilo liliwahi kutoa msamaha kwa watu waliopatikana na hatia ya kulidhalilisha Bunge au Mbunge na baada ya kukiri kutenda kosa waliomba msamaha na kusamehewa;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Ndugu Paul Christian Makonda asamehewe na Bunge kutokana na kitendo chake cha kiungwana cha kukiri na kujutia kosa lake na kuliomba radhi Bunge mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nisome kwa pamoja na azimio la pili.

Mheshimiwa Spika, sasa nisome azimio la Bunge kuhusu hatua za kuchukuliwa dhidi ya Ndugu Alexander Pastory Mnyeti aliyetiwa hatiani kwa kosa la kudharau, kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge kama liliyotolewa chini ya kifungu cha 26(e) na 34(1)(j) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge (*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, [CAP 296 R.E 2015]*).

Kwa kuwa Mheshimiwa Spika aliagiza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ikutane na kufanya kazi suala la tuhuma dhidi ya Ndugu Alexander Pastory Mnyeti kuhusu kudharau, kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge;

Na kwa Kuwa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilikaa tarehe 06 Aprili, 2017 na tarehe 9 -10 Aprili, 2017 kufanya uchunguzi wa suala hilo uliowezesha Kamati kubaini kuwa Ndugu Alexander Pastory Mnyeti amekiuka masharti ya kifungu cha 26(e) na 34(1)(j) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge, Sura ya 296 kwa kuandika maneno kwenye ukurasa wa *facebook* yanayoonesha kudharau, kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge;

Mheshimiwa Spika, na kwa kuwa kitendo cha kuandika maneno hayo ni kitendo cha kudharau, kudhalilisha na kulifedhehesha Bunge;

Na kwa kuwa Kamati imezingatia ukweli kwamba Ndugu Alexander Pastory Mnyeti hakuisumbua Kamati kwa namna yoyote ile bali alikuwa mtii na alitoa ushirikiano mkubwa kwa Kamati;

Na kwa kuwa Kamati imezingatia ushahidi wa Ndugu Alexander Pastory Mnyeti kwamba hakuwa na dhamira ya kulidharau wala kulidhalilisha Bunge kama ambavyo ilichukuliwa;

Na kwa kuwa Kamati imezingatia kuwa Ndugu Alexander Pastory Mnyeti hajawahi kutenda kosa kama hilo na kuflikishwa mbele ya Kamati yetu;

Na kwa kuwa Ndugu Alexander Pastory Mnyeti amekiri makosa yake na kuliomba radhi Bunge;

Na kwa kuwa Kamati imezingatia uzoefu wa Mabunge mengine kuhusu adhabu kwa mtu ambaye amekiri kosa la kulidharau Bunge na kuomba msamaha wa kosa hilo;

Na kwa kuwa uzoefu wa Mabunge mengine ya Jumuiya ya Madola kama vile Bunge la Lok Sabha la nchini India unaonesha kuwa Bunge hilo limewahi kutoa msamaha kwa watu waliopatikana na hatia ya kumdhaliilisha Mbunge na baada ya kukiri kutenda kosa hilo waliomba msamaha na kusamehewa;

Kwa hiyo, Bunge linaazimia kwamba, Ndugu Alexander Pastory Mnyeti asamehewe na Bunge kutockana na kitendo chake cha kiungwana cha kukiri na kujutia kosa lake na kuliomba radhi Bunge mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba tena kutoa hoja. (*Makof*)

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante sana hoja imetolewa na imeungwa mkono.

**TAARIFA YA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA
BUNGE KUHUSU SHAURI LA KUDHARAU MAMLAKA YA SPIKA
LINALOWAHUSU MHE. FREEMAN AIKAEL MBOWE (MB) NA
MHE. HALIMA JAMES MDEE (MB) – KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

1.1 **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 4 (2) na (3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shauri la Mhe. Freeman Aikael Mbowa (Mb) la kudharau mamlaka ya Spika na Mhe. Halima James Mdee (Mb) la kudharau Mamlaka ya Spika na kutumia lugha ya matusi, kuudhi na kudhalilisha Wabunge wengine, kinyume na kifungu cha 26 (d) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 [*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP. 296 R.E. 2015*]; na kinyume na Kanuni ya 74 (1) (a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

1.2 **Mheshimiwa Spika**, kwa Mamlaka yako chini ya Kanuni ya 4(1) (a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, katika Kikao cha Tatu cha Mkutano wa Saba wa Bunge la 11 kilichofanyika tarehe 6 Aprili, 2017 uliagiza Mhe. Freeman Aikael Mbowa (Mb) afike mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kujibu tuhuma za kudharau Mamlaka ya Spika na kulidharau Bunge.

1.3 **Mheshimiwa Spika**, pia kwa Mamlaka yako kwa mujibu wa Kanuni ya 74(1) (a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, katika Kikao cha Tatu cha Mkutano wa Saba wa Bunge la 11 kilichofanyika tarehe 6 Aprili, 2017, ulimtaja Mhe.

Halima Mdee (Mb) kwamba amedharau Mamlaka ya Spika, na uliagiza afike mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kujibu tuhuma za kudharau Mamlaka ya Spika.

**2.0 CHANZO CHA MASHAURI HAYA DHIDI YA
MHE. FREEMAN AIKAEL MBOWE (MB) NA MHE. HALIMA
JAMES MDEE (MB)**

2.1. Mheshimiwa Spika, katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Saba wa Bunge kilichofanyika tarehe 4 Aprili, 2017 ulifanyika uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Nne la Afrika Mashariki (EALA). Wakati mchakato wa uchaguzi huo ukiendelea, baadhi ya Wabunge walionekana kufanya vitendo vyta utovu wa nidhamu kwa kudharau Mamlaka ya Spika na kutoa lugha za matusi na kudhalilisha Wabunge wengine.

2.2. Mheshimiwa Spika, Mhe. Freeman Mbowa (Mb) alioneekana na kunukuliwa na vyombo vyta habari akitoa maneno ya utovu wa nidhamu kwa kudharau Mamlaka ya Spika na kutoa maneno ya kuudhi kwa Wabunge wengine. Kitendo hicho kilifanyika nje ya Ukumbi wa Bunge mara baada ya uchaguzi wa Wabunge wa EALA kumalizika.

2.3. Mheshimiwa Spika, kutokana na matukio hayo, katika Kikao cha Tatu kilichofanyika siku ya Alhamisi tarehe 06 Aprili, 2017, baadhi ya waheshimiwa Wabunge waliomba Mwongozo wa Spika kuhusu vitendo hivyo vyta kudharau Mamlaka ya Spika. Wabunge walioomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo hili ni pamoja na Mhe. Kangi A. Lugola (Mb):

2.4. Mheshimiwa Spika, baada ya maombi hayo kutolewa, ndipo Mheshimiwa Spika aliwataja Mhe. Freeman Aikael Mbowa (Mb) na Mhe. Halima James Mdee (Mb) na kuwataka wafike mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili kujibu tuhuma dhidi yao. Aidha uliagiza Kamati kuchunguza vitendo hivyo na kutoa taarifa kwa

Spika. Baada ya uchunguzi kukamilika, hii ndiyo taarifa ya Kamati.

3.0 UCHUNGUZI WA KAMATI

3.1 Mheshimiwa Spika, katika Waraka wako kwa Kamati wa kutaka kufanya uchunguzi kwa Wabunge waliobainika kufanya vitendo vya kudharau Mamlaka ya Spika, ulielekeza kama ifuatavyo:-

3.1.1 *Kwa kuzingatia Kanuni ya 74 (1) (a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, nimemtaja Mhe. Halima James Mdee, (Mb).kwamba amedharau mamlaka ya Spika na naelekeza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ikutane mara moja na kufanya uchunguzi wa vitendo hivyo.*

3.1.2 *Naelekeza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuchunguza vitendo vya kudharau Mamlaka ya Spika vilivyofanywa na Mhe. Freeman Aikael Mbowa, (Mb).nje ya Ukumbi wa Bunge mara baada ya uchaguzi huo kufanyika kinyume na kifungu cha 26 (d) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296.*

3.2 Mheshimiwa Spika, Kamati ilianza uchunguzi kwa kutoa wito (*summons*) kwa Mhe. Freeman Aikael Mbowa (Mb) na Mhe. Halima James Mdee wafike mbele ya Kamati siku ya Jumamosi tarehe 08 Aprili, 2017 katika Ukumbi wa Spika (Dodoma) saa 4 kamili asubuhi ili kujibu tuhuma dhidi yao kama ifuatavyo:-

3.2.1 Mhe. Freeman Mbowa (Mb), alituhumiwa kuwa, akiwa nje ya Ukumbi wa Bunge mara baada ya kumalizika uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, alinukuliwa na vyombo vya habari akitoa kauli za kudharau Bunge na Mamlaka ya Spika, kinyume na Kifungu cha 26 (d) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 [*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP 296 R.E 2015*].

3.2.2 Tuhuma dhidi ya Mhe. Halima James Mdee (Mb) ni kama ifuatavyo:-

i. Kusema Bungeni bila idhini ya Spika, kinyume na Kanuni za Majadiliano kwa mujibu wa Kanuni za 59 na 60 za Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016.

ii. Kutoa lugha ya matusi, kuudhi na kudhalilisha Mbunge mwingine, kinyume na Kanuni ya 64(1) (f) na (g) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016.

3.3 **Mheshimiwa Spika**, ili Kamati iweze kufanya uchunguzi wa kina wa tuhuma hizo, ilijelekeza kwenye hoja za uchunguzi (*issues*) zifuatazo:

3.3.1 Kama ni kweli Mhe. Freeman Aikael Mbewe (Mb) alifanya vitendo vya utovu wa nidhamu na dharau kwa Mamlaka ya Spika, na kutoa maneno ya kuudhi nje ya Ukumbi wa Bunge alipokuwa akihojiwa na vyombo vya habari mara baada ya kumalizika kwa uchaguzi wa EALA.

3.3.2 Kama ni kweli Mhe. Halima James Mdee (Mb) alifanya vitendo vya utovu wa nidhamu, kutoa lugha ya matusi na ya kuudhi na dharau kwa Mamlaka ya Spika wakati wa Kikao cha uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki.

3.3.3 Kama itathibitika ni kweli walifanya vitendo hivyo, ni hatua gani wanatakiwa kuchukuliwa?

3.4 **Mheshimiwa Spika**, katika kujibu hoja hizo, Kamati ilifanya uchunguzi na uchambuzi wa shauri la kila mmoja ili kubaini jinsi alivyohusika na vitendo vilivyolalamikiwa.

3.5 **Mheshimiwa Spika**, Kamati katika uchunguzi wake, ilifanya rejea za Sheria, Kanuni za Kudumu za Bunge, mashauri mbalimbali yaliyoamuliwa na Bunge siku za nyuma (*case law*), Taarifa Rasmi za Bunge na ushahidi wa picha za *video* za Ukumbini na picha za video nje ya Ukumbi wa Bunge katika mkutano wa waandishi wa habari na Mhe. Freeman Mbewe, kama ifuatavyo:

3.5.1 Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki [*The Treaty for the Establishment of the East African Community*].

3.5.2 Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge [*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP. 296 R.E. 2015*].

3.5.3 Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

3.5.4 Shauri la la nchini India la K.M Kaushik L.S Deb 2-2-19703.5.5 Shauri la Waheshimiwa Wabunge Halima James Mdee (Mb), Godbless Lema (Mb), Tundu Lissu (Mb), Ester Bulaya (Mb), Pauline Gekul (Mb) na Zitto Kabwe (Mb) kudharau Mamlaka ya Spika Bungeni tarehe 27 Januari, 2016.

3.5.6 Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) za tarehe 4 Aprili, 2017.

3.5.7 Picha za video (*video clip*) za Ukumbini na picha za video nje ya Ukumbi wa Bunge katika mukutano waandishi wa habari na Mhe.Freeman Mbowe.

3.5.8 Kitabu cha *Parliamentary Privileges – Digest of Cases 1950 – 2000, Vol II, Lok Sabha Secretariat New Delhi, 2001;*

5.0 SHAURI DHIDI YA MHE. FREEMAN AIKAEL MBOWE (MB)

5.1 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilianza kuchunguza Shauri la Mhe. Freeman Mbowe (Mb). Katika uchunguzi huo Kamati iliangalia picha za video na mahojiano ya Mhe. Freeman Mbowe (Mb) na waandishi wa habari nje ya Ukumbi wa Bunge mara baada ya uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kumalizika, alinukuliwa na vyombo vyaa habari akitamka maneno, ambayo baadhi yake ni kama yafuatayo:

(i) “..... *Spika amevunja Kanuni za Bunge, Sheria hazikuheshimiwa, ubabe umetumika.....*”.

- (ii) “..... ni mkakati wa Kiserikali, tunajua Rais anahusika, Waziri Mkuu anahusika, viongozi wa chama chao wanahusika.....”
- (iii) “..... tumeleta wagombea wazuri sana wawili “very competent”, wamepigiwa kura za hapana kwasababu ulikuwa ni mkakati wa Chama Cha Mapinduzi, tumeona ni ujinga na upumbavu mtupu”.
- (iv) “..... uchaguzi huu umekuwa wa kijinga”

6.0 MAHOJIANO YA SHAHIDI MBELE YA KAMATI

6.1 **Mheshimiwa Spika**, Mhe. Freeman Aikael Mbewe (Mb) alifika mbele ya Kamati kwa mujibu wa wito (*summons*) aliopewa. Mhe. Freeman Mbewe (Mb) aliposomewa tuhuma dhidi yake alikiri wazi kuwa alitamka maneno hayo yaliyolalamikiwa na Bunge na akaliomba radhi Bunge. Kwa maneno yake mwenyewe kama alivyonukuliwa kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) alisema yafuatayo:-

“Mheshimiwa Mwenyekiti, matamshi yangu hayakukusudia kumkwaza mtu yeyote; dhamira hiyo kwangu haikuwepo na kama imemkwaza kiongozi yeyote hususan Mheshimiwa Spika, mimi namwomba radhi sana. Namwomba radhi kwa sababu haikuwa dhamira yangu kumkwaza Mheshimiwa Spika, namheshimu sana na naheshimu mamlaka yake na natambua”.

Mheshimiwa Spika, Mhe. Mbewe pia aliomba radhi kwa Bunge kama ifuatavyo:-

“.....hilo naliombea radhi sana kwa sababu halikukusudiwa katika dhamira yangu, wala sikusudii wakati wowote wala siwezi kulidharau Bunge kwa sababu najua Bunge ni chombo kikubwa ambacho nimeshiriki kipindi kirefu huko, kwa hiyo nalielewa na najua mipaka yake na mamlaka yake. Ahasante.”

7.0 MAONI YA KAMATI (*FINDINGS*)

7.1 **Mheshimiwa Spika**, Pamoja na Mhe. Freeman Aikael Mbewe (Mb) kukiri na kuomba radhi kwa Mhe. Spika na Bunge, Kamati ilibaini ni kweli kauli alizotoa ni dharau kwa Bunge na kwa Mamlaka ya Spika, kinyume na Kifungu cha 26(d) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296.

Kifungu tajwa kinaeleza kuwa:-

26. Any person who:
- (a)
 - (b)
 - (c)
 - (d) *Shows disrespect in speech or manner towards the Speaker; or*
 - (e) *Commits an offence.*

7.2 **Mheshimiwa Spika**, Uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki uliandaliwa na kufanyika kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 50 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki [*The Treaty for the Establishment of the East African Community*], Kanuni ya 12 ya Kanuni za Kudumu za Bunge na Nyongeza ya Tatu ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

7.3 **Mheshimiwa Spika**, kitendo cha Mhe. Freeman Mbewe (Mb) kutamka kuwa uchaguzi huo ni wa kijinga na kwamba Spika amevunja Kanuni za Bunge katika kuendesha shughuli za uchaguzi huo, kilikuwa ni kitendo cha kulidharau Bunge na kudharau Mamlaka ya Spika. Si sahihi kuhoji uamuji uliofanywa na Bunge kinyume na taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 15 ya Nyongeza ya Tatu ya Kanuni za Kudumu za Bunge kuhusu kupinga uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Kanuni tajwa inaelekeza kuwa:

15. *Pursuant to the provisions of Article 52(1) of the Treaty, the election of a candidate as a*

member of the East African Legislative Assembly may be declared null and void on an Election Petition".

7.4 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni hiyo inaelekeza kuwa mapingamizi yoyote dhidi ya uchaguzi huo ni kwa njia ya maombi mahakamani (*Election Petition*).

7.5 **Mheshimiwa Spika**, ni kinyume cha taratibu kipinga uchaguzi huo kwa njia aliyotumia Mhe. Mbewe (Mb) kwa kuongea na vyombo vya habari na kusema kuwa ni uchaguzi wa kijinga na kuwa Spika amevunja Kanuni. Alitakiwa kufuata utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa Kanuni tajwa.

7.6 **Mheshimiwa Spika**, kutokana na ushahidi huo, Kamati imemkuta na hatia Mhe. Freeman Mbewe kwa kosa la kudharau Mamlaka ya Spika, kinyume na Kifungu cha 26 (d) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 [*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP. 296 R.E. 2015*] kama alivyokiri mwenyewe mbele ya Kamati.

8.0 MASHAURI MBALIMBALI YA NYUMA (CASE LAW)

8.1 **Mheshimiwa Spika**, katika kujadili hatua za kuchukua dhidi ya Mhe. Freeman Aikael Mbewe (Mb), Kamati illichambua uamuzi wa Bunge la *Lok Sabha* la nchini India. Bunge hilo katika shauri la **K.M Kaushik L.S Deb 18-11-1970** liliowahu su Maafisa wawili wa polisi ambao walituhumiwa kuvunja haki za Bunge kwa kumshambulia na kumdhalilisha Mbunge, Bunge liliwaita Maafisa polisi hao mbele ya Bunge ambapo walihojiwa na wakakiri kutenda kosa hilo na kuomba radhi kwa kitendo hicho. Bunge liliwasamehe na kufunga shauri hilo.

8.2 **Mheshimiwa Spika**, nanukuu shauri hilo kama ifuatavyo:

K.M Kaushik L.S Deb 18-11-1970

“....Two police officers of the State of Maharashtra were summoned to the bar of the House to answer the charge of breach of privilege and contempt of the House for allegedly assaulting and abusing a member. The officers expressed apologies to the member concerned and to the House for whatever happened on that day. In view of the apologies tendered by them, the House decided to treat the matter as closed”.

8.3 **Mheshimiwa Spika**, huo ndio ulikuwa uchunguzi wa Kamati kuhusu shauri la kudharau Mamlaka ya Spika linalomhusu Mhe. Freeman Aikael Mbewe (Mb). Hivyo, Bunge liutafakari ushahidi uliotolewa dhidi yake na kuizingatia wakati wa kupitisha Azimio la kuchukua hatua dhidi yake.

9.0 SHAURI DHIDI YA MHE. HALIMA JAMES MDEE (MB)

9.1 **Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilichunguza Shauri la Mhe. Halima James Mdee (Mb). Kamati ilianza kufanya uchunguzi kwa kusoma Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) na kuangalia picha za *video* za Ukumbini wakati wa taratibu za uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA) zilipokuwa zikiendelea na kubaini kuwa, Mhe. Halima James Mdee (Mb) alionekana akifanya vitendo vya utovu wa nidhamu kwa kudharau Mamlaka ya Spika na kutoa lugha ya matusi nay a kuudhi.

9.2. **Mheshimiwa Spika**, wakati mjadala wa hoja ya uchaguzi huo zikiendelea Ukumbini, Mhe. Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mhe. Dkt. Hamis Andrea Kigwangallah (Mb) aliomba kuchangia, Mhe. Spika ulitoa idhini ili achangie. Kabla hajaanza kutoa maelezo yake, Mhe. Halima Mdee (Mb) alianza kusema bila idhini ya Spika, huku akitoa lugha ya matusi na kuudhi kama ifutavyo:-

“Hatupendi maneno ya kipumbavu hapa”.

9.3. Vilevile wakati Mhe. Kigwangallah (Mb) akiendelea kutoa maelezo yake, Mhe. Halima Mdee (Mb) alisema tena

bila idhini ya Spika huku akitoa lugha ya matusi na ya kuudhi kwa Mheshimiwa Spika akisema:

"Mheshimiwa Spika, unaongea nini? Fala wewe!".

10.0 MAHOJIANO YA SHAHIDI MBELE YA KAMATI

10.1 **Mheshimiwa Spika**, Mhe. Halima James Mdee (Mb) naye aliiitikia wito wa Kamati na kufika mbele ya Kamati kwa siku na muda uliopangwa kwa ajili ya mahojano.

10.2 **Mheshimiwa Spika**, aliposomewa tuhuma dhidi yake, Mhe. Halima Mdee (Mb) alikiri kusema Bungeni bila idhini ya Spika wakati wa uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Pia alikiri kutamka maneno ya matusi na kuudhi kama yalivyonukuliwa katika Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Alieleza kama ifuatavyo:-

"...Hilo nimeshasema kwamba nimeongea bila idhini ya Spika.....Nimekiri nimetoa lugha ya kuudhi na nimesema mbele ya Kamati yako kwamba malengo yangu mimi nilikuwa namu-address Kigwangala lakini kama hansard ndiyo ushahidi namba moja na kwa mujibu wa Hansard imeonekana kwamba nilikuwa namu-address Spika sasa siwezi ku dispute hilo kwa sababu mnasema Hansard ndiyo ushahidi namba moja, niko tayari kuomba radhi....kwa wote wawili, kwa Spika lakini vilevile kwa Mheshimiwa Kigwangala".

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pamoja na kukiri tuhuma dhidi yake, Mhe. Halima James Mdee alieleza mbele ya Kamati kuwa lengo lake halikuwa kumtukana Mheshimiwa Spika, bali aliyasema katika majibizano na Mhe. Kigwangallah (Mb). Alisema kama ifuatavyo:-

"Lakini nilikuwa ninalotaka kuweka kwenye record ni kwamba siku ya tukio hilo sikumtukana Spika kwa sababu namheshimu sana.....Lakini nikiri vile vile kwamba nilijibizana na Mheshimiwa Kigwangala ambaye ni Naibu Waziri wa Afya na nikiri vilevile kwamba kile kitu nilichokifanya cha kujibizana na Mbunge mwingine wakati Spika hajanipa

nafasi ya kuzungumza ni kitu ambacho siyo kizuri na kiko kinyume na Kanuni na utaratibu.....niko tayari kabisa kuomba radhi mbele ya Kamati yako nakiri yale maneno ambayo niliyazungumza siyo mema sana.”

10.3 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilimuuliza Mhe. Halima Mdee (Mb) kama lugha ya matusi inaruhusiwa kwa Mbunge mwininge. Alijibu kuwa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge kuhusu mambo yasiyoruhusiwa Bungeni, lugha ya matusi, kuudhi au kudhalilisha hairuhusiwi kutolewa kwa Mbunge mwininge. Mhe. Halima James Mdee (Mb) alikiri kuwa maneno ya kuudhi hayabagui Spika, Naibu Spika, Mwenyekiti au Mbunge mwininge.

10.4 **Mheshimiwa Spika**, Pia Kamati ilimrejesha katika ushahidi wa *Hansard* ambapo hakuna sehemu yoyote ya majibzano kati yake na Mhe. Kigwangallah (Mb) bali ushahidi unaonesha kuwa Mhe. Halima Mdee (Mb) alisema bila idhini ya Spika huku akielekeza matusi hayo kwa Mhe Spika. Mhe. Halima Mdee (Mb) alijibu kuwa kama kwenye *Hansard* inaonekana hivyo, anaomba radhi kwa maneno aliyoelekeza kwa Mheshimiwa Spika.

10.5 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilimkumbusha Mhe. Halima Mdee kwamba aliwahi kutiwa hatiani kwa kosa kama hili siku za nyuma kwa kudharau Mamlaka ya Spika na kupewa adhabu ya kutohudhuria baadhi ya vikao vya Mkutano wa tatu wa Bunge, na alikubali kuwa aliwahi kutiwa hatiani kwa kosa kama hili.

10.6 **Mheshimiwa Spika**, Katika Azimio la Bunge la tarehe 30 Juni, 2016 Bunge lilitoa adhabu kwa Mhe. Halima Mdee (Mb) na Wabunge wengine waliohusika na fujo za tarehe 27 Januari, 2016 katika Ukumbi wa Bunge, kutohudhuria vikao vya Mkutano wa tatu wa Bunge vilivyokuwa vimebaki, kutokana na kosa la kudharau Mamlaka ya Spika.

10.7 **Mheshimiwa Spika**, Mhe. Halima Mdee alipouliwa kama hatarudia tena kufanya kosa hili, alijibu kuwa:-

“....nitajitahidi kutorudia ingawa ni ngumu sana ku-predict future itakuwaje... Kwahiyo naamini Mwenyezi Mungu ataniongoza kosa lisijirudie tena.”

11.0 MAONI YA KAMATI (*FINDINGS*)

11.1 **Mheshimiwa Spika**, baada ya kukamilisha uchunguzi, kamati ilibaini kuwa kweli Mhe. Halima Mdee (Mb) alisema Bungeni bila idhini ya Spika na hivyo kukiuka Kanuni za Majadiliano. Kwa mujibu wa Kanuni ya 59 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Mbunge yejote anaweza kuchangia Bungeni kwa idhini ya Spika. Kanuni inaeleza bayana kuwa:-

“Kwa idhini ya Spika, Mbunge yejote anaweza kusimama na kuchangia Bungeni katika nyakati zifuatazo:

- (a) *Wakati wa kuchangia mjadala wa hoja yoyote iliyowasilishwa Bungeni ambayo Kanuni zinaruhusu ijadiliwe”.*

11.2 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 60 pia imeweka taratibu za jinsi ya kupata nafasi ya kusema Bungeni. Fasili ya (1) imetaja taratibu hizo kuwa ni:

- (a) *Kumpelekea Spika ombi la maandishi;*
- (b) *Kusimama kimya mahali pake; au*
- (c) *Kutumbukiza kadi ya elektroniki.*

Fasili ya (2) inafafanua bayana kuwa:

“Isipokuwa kwamba, Mbunge yejote hataanza kuzungumza hadi aitwe na Spika ama kwa jina au wadhifa wake na kumruhusu kusema na wakati wa kusema ataaelekeza maneno yake kwa Spika”.

Mhe. Halima Mdee (Mb) alikiuka Kanuni hiyo kwa kuanza kuzungumza bila kuitwa na Spika kwa jina na kuruhusiwa kusema, kitendo ambacho ni dharau kwa Mamlaka ya Spika.

11.3 **Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 26(d) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 [*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP. 296 R.E 2015*] kimetaja kuwa ni kosa kuonesha dharau kwa kauli au matendo dhidi ya Spika. Nanukuu:-

26. Any person who:

- (a)
- (b)
- (c)
- (d) *Shows disrespect in speech or manner towards the Speaker; or*
- (e) *commits an offence.*

Kusema Bungeni bila kuruhusiwa ni dharau (*contempt*) kwa Mhe. Spika, kama kifungu tajwa kinavyofafanua.

11.4 **Mheshimiwa Spika**, maneno au kauli za Mhe. Halima Mdee (Mb) kama zilivyonukuliwa kwenye *Hansard*, ni lugha ya matusi na lugha ya kuudhi.

Kanuni ya 64 imenorodhesha mambo yasiyoruhusiwa Bungeni. Fasili ya (1) (f) inazuia Mbunge kusema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwingine yeyote. Fasili ya (1)(g) inazuia Mbunge kutumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine.

11.5 **Mheshimiwa Spika**, Kauli za Mhe. Halima Mdee (Mb) ziliikuwa kanuni tajwa. Ni kauli za matusi na kuudhi. Mathalani, kwa mujibu wa Kamusi Kuu ya Kiswahili ya Baraza la Kiswahili la Taifa, Chapa ya 2015, neno “*pumbavu*” maana yake ni:

“.... *siokuwa na uwezo wa kuelewa, jinga, zoba, zuzu*”.

Neno ‘*fala*’ maana yake ni:

“*mtu ambaye akili zake hazifanyi kazi vizuri, mpumbavu, bwege, mjinga, bozi, gulagula*”.

11.6 **Mheshimiwa Spika**, kutohana na ushahidi huu, Kamati imejiridhisha bila kuacha shaka yoyote kuwa ni kweli Mhe. Halima James Mdee (Mb) alitoa lugha ya matusi na lugha ya kuudhi kinyume na Kanuni ya 64 (1) (f) na (g); zikisomwa pamoja na Kanuni ya 74 (1) (a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 na kifungu cha 26(d) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 [*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP. 296 R.E 2015*]). Hivyo Kamati inamtia hatiani

12.0 MASHAURI MBALIMBALI YA NYUMA (CASE LAW)

12.1 **Mheshimiwa Spika**, ili Bunge lako Tukufu liweze kupitisha Azimio la adhabu anayostahili kupewa Mhe. Halima James Mdee (Mb), Kamati imepitia shauri la nyuma ambalo Kamati hii imewahi kushughulikia kuhusu Wabunge kudharau Mamlaka ya Spika.

12.2 **Mheshimiwa Spika**, Shauri hilo lilihusu baadhi ya Wabunge kufanya fujo Bungeni mnamo tarehe 27 Januari, 2016. Awali shauri hilo lilifikishwa kwenye Kamati likiwhahu Mhe. Tundu A. Lissu (Mb), Mhe. Godbless J. Lema (Mb), Mhe. Pauline Gekul (Mb) na Mhe. Ester Bulaya (Mb) ambao walituhumiwa kufanya fujo Bungeni mnamo tarehe 27 Januari, 2016. Baadaye mnamo tarehe 10 Machi, 2016 wakati Kamati ikiendelea na kazi, Spika alieilekeza Kamati kufanya uchunguzi wa mashahidi wengine watatu zaidi ambao ni Mhe. Zitto Kabwe (Mb), Mhe John Heche (Mb) na **Mhe. Halima Mdee (Mb)**.

Katika shauri hilo, Wabunge tajwa walidaiwa kuwa mnamo tarehe 27 Januari, 2016 walipingana na mwongozo wa Kiti kwa kufanya fujo Bungeni, jambo liliatosababisha shughuli za Bunge zilizokuwa zimepangwa kwa siku hiyo, hususan mjadala wa hotuba ya Rais aliyoitoa Bungeni kushindwa kuendelea. Katika kudhibiti fujo hizo, Mheshimiwa Mwenyekiti alitumia mamlaka yake chini ya Kanuni ya 74 ya Kanuni za Kudumu za Bunge kuwataja Wabunge husika katika hili kuwa ndio walikuwa vinara wa kufanya fujo na kuwataka watoke nje ya ukumbi. Wabunge hao walikaidi uamuzi wa Kiti hali

iliyopeleka shughuli za Bunge kuahirishwa kwa muda kwa lengo la kudhibiti fujo hizo Bungeni.

Kufuatia hali hiyo, baadaye shauri hili liliwasilishwa mbele ya Kamati ambapo pamoja na mambo mengine, baadhi ya Wabunge hao walituhumiwa kwa kosa la kudharau Mamlaka ya Spika kinyume na kifungu cha 24 (c) na (d) cha Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge pamoja na Kanuni ya 74 (1) (a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Baada ya kupokea ushahidi wa shauri hilo na kuufanya uchambuzi, Kamati iliwakuta na hatia ya kudharau Mamlaka ya Spika Wabunge sita ambao ni Mhe. Halima Mdee, Mhe. Godbless Lema, Mhe. Tundu Lissu, Mhe. Ester Bulaya, Mhe. Pauline Gekul na Mhe. Zitto Kabwe.

Kamati ilishauri Wabunge hao wapewe adhabu stahiki kadri Bunge litakavyoona inafaa. Kwa Azimio la Bunge la tarehe 30 Juni, 2016 Bunge lilitoa adhabu ya kutohudhuria Vikao vya Mkutano wa Tatu na wa Nne kwa Wabunge tajwa kwa kipindi cha muda tofauti kwa kila Mbunge kulingana na alivyohusika na fujo hizo.

12.3. **Mheshimiwa Spika**, huo ndio ulikuwa uchunguzi wa Kamati kuhusu shauri la kudharau Mamlaka ya Spika linalomhusu Mhe. Halima James Mdee (Mb). Hivyo, Bunge liutafakari ushahidi uliotolewa dhidi yake na kuuzingatia wakati wa kuitisha Azimio la kutoa adhabu anayostahili kwa kosa alilotenda.

13.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge na napenda nitumie nafasi hii kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge hili ambalo ni chombo cha uwakilishi wa Wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ili kuhakikisha kuwa ustawi wa wananchi ndio kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, kipekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua kwa umakini mkubwa Mashauri ya kudharau Mamlaka ya Spika. Wajumbe hawa walifanya kazi nzuri na walizingatia misingi ya haki, bila kumwonea au kumpendelea mtu yoyote. Kwa heshima naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

- (i) Mhe. Kapt(Mst), George Huruma Mkuchika (Mb) -Mwenyekiti
- (ii) Mhe. Almas Athuman Maige (Mb) - Makamu Mwenyekiti
- (iii) Mhe. Rashid Ali Abdallah (Mb)- Mjumbe
- (iv) Mhe. Amina Nassoro Makilagi (Mb)-Mjumbe
- (v) Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma (Mb)- Mjumbe
- (vi) Mhe. Othman Omar Haji (Mb)-Mjumbe
- (vii) Mhe. Rose Kamil Sukum (Mb)-Mjumbe
- (viii) Mhe. George Malima Lubeleje (Mb)-Mjumbe
- (ix) Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf (Mb)-Mjumbe
- (x) Mhe. Susan Anselm Lyimo (Mb)-Mjumbe
- (xi) Mhe. Tunza Issa Malapo (Mb)-Mjumbe
- (xii) Mhe. Asha Abdullah Juma (Mb)-Mjumbe
- (xiii) Mhe. Augustino Manyanda Masele (Mb)- Mjumbe
- (xiv) Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka (Mb)- Mjumbe
- (xv) Mhe. Ali Hassan Omar King (Mb)- Mjumbe; na
- (xvi) Mhe. Innocent Sebba Bilakwate (Mb)- Mjumbe

Aidha, napenda kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru Ndugu Pius T. Mboya, Kaimu Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Ndugu Prudens R. Rweyongeza, Ndugu Mossy Lukuvi ambaa ni Manaibu Washauri wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Ndugu Maria Mdulugu, Katibu wa Kamati, na Ndg. Ediltruda Kilapilo kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kujadili na kupokea maoni na mapendeleko ya Kamati ili baada ya mjadala liazimie kuchukua hatua stahiki kwa kadiri litakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

Kapt (Mst) George Huruma Mkuchika

MWENYEKITI

KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE

11 Aprili, 2017

**AZIMIO LA BUNGE KUHSU HATUA ZA KUCHUKUA DHIDI YA
MHE. FREEMAN AIKAEL MBOWE (MB) KWA KUHSIKA NA
VITENDO VYA KUDHARAU MAMILAKA YA SPIKA SIKU YA
TAREHE 4 APRILI, 2017 – KAMA LILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*[Limetolewa chini ya Kifungo cha 33(1) cha Sheria ya Kinga,
Madaraka na Haki za Bunge (The Parliamentary Immunities,
Powers and Privileges Act, [CAP 296 R:E 2015].*

KWA KUWA, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaongozwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge ambazo zilitungwa na Bunge lenyewe kwa ajili ya kuliongoza katika kutekeleza shughuli zake;

NA KWA KUWA, Sheria na Kanuni za uendeshaji wa shughuli za Bunge zimeweka utaratibu wa majadiliano ndani na nje ya Bunge, na kwamba kwa taratibu hizo Wabunge wanatakiwa kuheshimu Mamlaka ya Spika na shughuli za Bunge kwa ujumla;

NA KWA KUWA, katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Saba wa Bunge kilichofanyika tarehe 4 Aprili, 2017 ulifanyika uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA), na baada ya uchaguzi huo, Mhe. Freeman Aikael Mbowa (Mb) alitoa kauli za kudharau Mamlaka ya Spika;

NA KWA KUWA, Mheshimiwa Spika kwa Mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge alimpeleka mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Mhe. Freeman Aikael Mbowa (Mb) kwa kosa la kudharau Mamlaka ya Spika;

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

NA KWA KUWA, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilikaa tarehe 8 Aprili, 2017 hapa Dodoma kusikiliza shauri dhidi ya Mhe. Freeman Aikael Mbewe (Mb);

NA KWA KUWA, Mhe. Freeman Aikael Mbewe (Mb) aliiitikia wito wa Kamati bila kuleta usumbufu wa aina yoyote, na alipohojwa na Kamati alikiri wazi kosa lake na kuomba radhi kwa Mheshimiwa Spika na Bunge;

NA KWA KUWA, kosa la Mhe. Freeman Aikael Mbewe (Mb) la kudharau Mamlaka ya Spika lilikuwa ni kosa lake la kwanza;

HIVYO BASI, Bunge linaazimia:-

i. Kumsamehe Mhe. Freeman Aikael Mbewe (Mb) kutokana na kitendo chake cha kuonesha ushirikiano kwa Kamati na pia kitendo chake cha kiungwana cha kuomba r a d h i kwa Mheshimiwa Spika, kwa Bunge na kwa wengine wote alioawakwaza kutokana na kauli yake; na

ii. Hata hivyo, kwa kuwa Mhe. Freeman Aikael Mbewe (Mb) ni Kiongozi, yaani Mwenyekitiwa chama cha CHADEMA, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Mbunge, anatakiwa kuwa mfano bora wa kuigwa kwa Wabunge wengine anaowaongoza Hivyo Mhe. Freeman Mbewe anatakiwa kujiepusha na vitendo vya aina yoyote vya kudharau Mamlaka ya Spika na Bunge ili awe mfano bora wa kuigwa katika kuzingatia sheria, Kanuni na taratibu za uendeshaji wa Bunge.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kutoa msamaha kwa Mhe. Freeman Aikael Mbewe (Mb) na kumshauri kama Kiongozi kuwa mfano bora kwa Wabunge wengine katika kuheshimu Sheria, Kanuni na taratibu za uendeshaji wa shughuli za Bunge.

Kapt. (Mst.) George Huruma Mkuchika (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE

11 Aprili, 2017

**AZIMIO LA BUNGE KUHSU HATUA ZA KUCHUKUA DHIDI YA
MHE. HALIMA JAMES MDEE (MB) KWA KUHSIKA NA
VITENDO VYA KUDHARAU MAMLAKA YA SPIKA NA KUTOA
LUGHA YA MATUSI NA YA KUUDHI KATIKA KIKAO CHA
KWANZA CHA MKUTANO WA SABA WA BUNGE SIKU YA
TAREHE 4 APRILI, 2017 – KAMA LILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*[Limetolewa chini ya Kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Kinga,
Madaraka na Haki za Bunge (The Parliamentary Immunities,
Powers and Privileges Act, [CAP 296 R:E 2015].*

KWA KUWA, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaongozwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge ambazo zilitungwa na Bunge lenyewe kwa ajili ya kuliongoza katika kutekeleza shughuli zake;

NA KWA KUWA, Sheria na Kanuni za uendeshaji wa shughuli za Bunge zimeweka utaratibu wa majadiliano ndani ya Bunge, na kwamba kwa taratibu hizo Wabunge wanatakiwa kuheshimu Mamlaka ya Spika na shughuli za Bunge kwa ujumla;

NA KWA KUWA, katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Saba wa Bunge kilichofanyika tarehe 4 Aprili, 2017 ulifanyika uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA), na wakati uchaguzi ukifanyika katika Ukumbi wa Bunge, Mhe. Halima James Mdee (Mb) alifanya vitendo vya kudharau Mamlaka ya Spika na kutoa lugha ya matusi, kuudhi na kudhalilisha Wabunge wengine;

NA KWA KUWA, Mheshimiwa Spika kwa Mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge alimpeleka mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Mhe. Halima James Mdee (Mb) kwa makosa ya kudharau Mamlaka ya Spika na kutoa lugha ya matusi, kuudhi, na kudhalilisha Wabunge wengine;

NA KWA KUWA, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilikaa kuanzia tarehe 8, Aprili, 2017 hadi tarehe 10 Aprili, 2017 hapa Dodoma na kusikiliza shauri la Mhe. Halima James Mdee (Mb);

NA KWA KUWA, kwa kuzingatia kuwa Mhe. Halima James Mdee (Mb) hii ni mara ya pili kutiwa hatiani kwa kosa kama hili la kudharau Mamlaka ya Spika na kupewa adhabu na Bunge ya kutohudhuria Vikao vya Mkutano wa Tatoo na Nne wa Bunge;

NA KWA KUWA, Mhe. Halima James Mdee (Mb) alivunja tena Kanuni ya 59, 60(2), Kanuni ya 64 (1) (f) na (g); zikisomwa pamoja na Kanuni ya 74(1) (a) na (b) na Kifungu cha 26(d) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 kwa kufanya vitendo na kutoa kauli za kudharau Mamlaka ya Spika;

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kuwa:-

Mhe. Halima James Mdee (Mb) asihudhurie vikao vyote vilivyobaki vya Mkutano wa Saba (wa Bunge la Bajeti) kuanzia tarehe ya Azimio hili la Bunge, kutokana na tabia yake ya mara kwa mara ya kufanya vitendo vya kudharau Mamlaka ya Spika na kutoa lugha ya matusi na ya kuudhi.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, linakubaliana na kuitisha mapendekezo ya adhabu hiyo kwa Mhe. Halima James Mdee (Mb) kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Kapt. (Mst.) George Huruma Mkuchika (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE

11 Aprili, 2017

**TAARIFA YA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA
BUNGE KUHUSU SHAURI LA KUDHARAU MAMLAKA YA SPIKA
LINALOMHUSU MHE. ESTER AMOS BULAYA (MB) – KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1:0 UTANGULIZI

1.1. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 4 (2) na (3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shauri la Mhe. Ester Amos Bulaya (Mb) la kudharau mamlaka ya Spika , kinyume na kifungu cha 26 (c) (d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 [*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP. 296 R.E. 2015*]; na kinyume na Kanuni ya 74 (1) (a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

1.2. Mheshimiwa Spika, kwa Mamlaka yako kwa mujibu wa Kanuni ya 74(1) (a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge katika 2016 katika Mkutano wa Tatu, Kikao cha Thelathini na Mbili kilichofanyika tarehe 30 Mei,2016 ulimtaja Mhe. Ester Amos Bulaya (Mb) kwamba amedharau Mamlaka ya Spika, na uliagiza afike mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kujibu tuhuma za kudharau Mamlaka ya Spika.

**2.0. CHANZO CHA SHAURI DHIDI YA MHE. ESTER AMOS
BULAYA (MB)**

2.1. Mheshimiwa Spika, mnamo siku ya tarehe 30 Mei, 2016 katika Mkutano wa Tatu, Kikao cha Thelathini na Mbili, wakati wa asubuhi Bunge lilikuwa likijadili Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha, 2016/2017, Mhe. Juma Nkamia (Mb) aliomba Mwongozo wa Spika kupitia Kanuni ya 68(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 akitaka kujua ni kwanini Serikali imewafukuza Wanafunzi wa Diploma Maalum ya Sayansi katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Mhe. Nkamia alieleza kuwa

wanafunzi waliofukuzwa hawakuwa na kosa lolote, isipokuwa Serikali ndiyo iliyokuwa na mgogoro na Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Dodoma, hivyo alitaka kujua ni kwanini wanafunzi waadhibiwe kwa makosa ya watu wengine?

2.2. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika alitoa Mwongozo wake kwa kueleza pamoja na mambo mengine kuwa, Mwongozo wa Spika unapaswa kuombwa kwa mambo yaliyotokea Bungeni mapema na sio mambo yanayotokea nje ya Bunge. Hata hivyo, alitaka Serikali kuangalia namna bora ya kushughulikia suala husika.

2.3. Mheshimiwa Spika, baada ya Mheshimiwa Naibu Spika kutoa majibu ya Mwongozo ulioombwa na Mhe. Nkamia (Mb), Mheshimiwa Joshua Nassari (Mb) alisimama kwa kutumia Kanuni ya 69 na kuomba Mwongozo wa Spika kwamba Bunge liahirishe kujadili Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji na badala yake lijadili suala la waliokuwa wanafunzi wa Diploma Maalumu ya Sayansi, Chuo Kikuu cha Dodoma ambao walifukuzwa ndani ya masaa 48. Alieleza zaidi kuwa, wanafunzi hao ni watoto wadogo ambao walikuwa wanapata shida hapa Dodoma baada ya kufukuzwa.

2.4. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika alitoa Mwongozo kuwa hakuona kama ni utaratibu bora wa uendeshaji wa shughuli za Bunge kuahirisha shughuli za Bunge kwa kuwa jambo hilo lilikuwa linashughulikiwa na Serikali.

2.5. Mheshimiwa Spika, kufuatia Mwongozo huo wa Naibu Spika, baadhi ya Wabunge hawakuridhika na hivyo waliendelea kuomba Miongozo huku wakipiga kelele, jambo ambalo lilivuruga shughuli za Bunge zilizokuwa zinaendelea. Mhe. Naibu Spika alilazimika kuahirisha shughuli za Bunge na aliiitisha kikao cha Kamati ya Uongozi ili ijadili suala hilo.

2.6. Mheshimiwa Spika, mara kikao cha jioni kiliporejea, Mheshimiwa Naibu Spika alitoa maelezo kuwa, baada ya kutafakari vurugu zilizotokea asubuhi, Kamati ya Uongozi iliamua kuwa, Waziri wa Elimu Mhe. Profesa Joyce Ndalichako

(Mb) atoe Kauli ya Serikali kuhusiana na suala la mgogoro wa Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Dodoma na Walimu, pamoa na hatma ya wanafunzi waliofukuzwa. Hata hivyo, Prof. Joyce Ndalichako (Mb) hakuwepo Bungeni wakati huo, hivyo alimwita Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliji kuhitimisha hoja ya Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

2.7. Mheshimiwa Spika, kufuatia hatua hiyo, baadhi ya Wabunge walismama na kuanza kuomba Miongozo, kupiga kelele, kugonga meza, kurusha vitabu hovyo na kukataa kutii maelekezo ya Naibu Spika yaliyowataka kutulia ili kumruhusu Mheshimiwa Naibu Waziri kuhitimisha hoja yake. Vitendo hivyo vilivuruga shughuli za Bunge kwa muda, jambo lililopelekea Mheshimiwa Naibu Spika kumtaja kwa jina Mhe. Ester Bulaya (Mb) amefanya vitendo vya kudharau Mamlaka ya Spika na kuagiza afike mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

3.0. UCHUNGUZI WA KAMATI

3.1. Mheshimiwa Spika, katika Waraka wako kwa Kamati wa kutaka kufanya uchunguzi kwa Wabunge waliobainika kufanya vitendo vya kudharau Mamlaka ya Spika, ulielekeza kama ifuatavyo:-

...kwa mamlaka nilyopewa chini ya Fasili ya 4(1) (a) na(b) ya nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge .Toleo la Januari,2016,naiagiza Kamati ya Haki,Maadili na Madaraka ya Bunge ichunguze na kutoa mapendekizo kuhusu suala hill"

3.2. Mheshimiwa Spika, Kamati ilianza uchunguzi kwa kutoa Hati ya Wito (*summons*) kwa Mhe. Ester Amos Bulaya kufika mbele ya Kamati siku ya Alhamis tarehe 20 Aprili, 2017 katika Ukumbi Na. 227 Ghorofa ya Pili, Jengo la Utawala (Dodoma saa 7 kamili mchana ili kujibu tuhuma dhidi yake kama ifuatavyo:-

- (a) Kuvuruga shughuli za Bunge kwa kupiga kelele na kupiga makofi kwa vurugu jambo ambalo lilimfanya Naibu Waziri wa Maji aliyekuwa ameruhusiwa kuzungumza kushindwa kuendelea kuzungumza kutokana na vitendo hivyo.
- (b) Kukaidi maelekezo ya Naibu Spika aliyeutaka utulie ili kumruhusu Naibu Waziri wa Maji kuhitimisha hoja iliyokuwa mezani.
- (c) Kuendelea kusimama na kupiga kelele wakati Spika amekutaka utulie.
- (d) Kusambaza karatasi na vitabu hovyo kwa makusudi kitendo ambacho ni dharau kwa Bunge na kudharau Mamlaka ya Spika.

4.0. HOJA ZA MSINGI (ISSUES)

4.1. Mheshimiwa Spika, ili Kamati iweze kufanya uchunguzi wa kina wa tuhuma hizo ilijielekeza kwenye hoja za uchunguzi (*issues*) zifuatazo:

- (a) Kama ni kweli Mhe. Ester Amos Bulaya (Mb) alifanya vitendo vya utovu wa nidhamu na dharau kwa Mamlaka ya Spika.
- (b) Kama itathibitika ni kweli alifanya vitendo hivyo, ni hatua gani anatakiwa kuchukuliwa?

4.2. Mheshimiwa Spika, Kamati katika uchunguzi wake, ilifanya rejea za Sheria, Kanuni za Kudumu za Bunge, mashauri mbalimbali yaliyoamuliwa na Bunge siku za nyuma (*case law*), na ushahidi wa picha za *video* za Ukumbini kama ifuatavyo:-

4.2.1. Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge [*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP. 296 R.E. 2015*].

4.2.2. Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

4.2.3. Picha za video (*video clip*) za Ukumbini.

5.0. MAHOJIANO YA SHAHIDI MBELE YA KAMATI

5.1. **Mheshimiwa Spika**, siku ya tarehe 20 Aprili, 2017 Mhe. Ester Amos Bulaya (Mb) alifika mbele ya Kamati kwa mujibu wa Hati ya Wito (*summons*) aliyopewa. Mhe. Ester Amos Bulaya (Mb) aliposomewa tuhuma dhidi yake alieleza kuwa kwa kuwa suala hili limekuwa la muda mrefu kwa kiasi fulani hakumbuki vema, inawezekana alitenda kosa hilo kutokana na mhemuko uliokuwepo kufuatia tukio la kufukuzwa wanafunzi wa Diploma Maalum ya Sayansi, Chuo Kikuu cha Dodoma kwani pia walikuwemo wapiga kura wake. Hata hivyo alikiri wazi kuwa yawezekana kabisa alitenda matendo yaliyolalamikiwa na Bunge. Hivyo analiomba radhi Bunge kwa maneno yake mwenyewe kama yafuatayo:-

...yawezekana ni muda mrefu sana nimesahau kutokana na hasira naweza nikawa nimefanya vitendo vya kuvunja Kanuni nachukua fursa hii, kuomba radhi kwa Kamati, Bunge kwa yote yaliyotokea, naomba radhi kwa moyo wa dhati kabisa ... sipendi kusumbua Kamati hii naiheshimu, ... kama Kamati imeona chochote nilichofanya, kwa moyo wa dhati naomba radhi".

5.2. **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilimkumbusha Mhe. Ester Bulaya kwamba aliwahi kutiwa hatiani kwa kosa kama hili siku za nyuma kwa kudharau Mamlaka ya Spika na kupewa adhabu ya kutohudhuria baadhi ya vikao vya Mkutano wa Tatoo wa Bunge, na alikubali kuwa aliwahi kutiwa hatiani kwa kosa kama hili na alisisitiza kuomba radhi tena na kuahidi kuwa hatarudia tena kosa hili.

6.0. MAONI YA KAMATI (*FINDINGS*)

6.1. **Mheshimiwa Spika**, kupitia mkanda wa video wa tukio la siku hiyo, Mhe. Ester Bulaya (Mb) anaonekana akipiga makofi bila utaratibusi, akikaidi maelekezo ya Spika ya kumtaka atulie ili shughuli iliyokuwa mezani iendelee, na mara alipoamriwa kutoka nje alionekana kurusha kwa

kutawanya vitabu hovyo na kwa makusudi jambo ambalo ni dharau kwa Mamlaka ya Spika.

6.2. Mheshimiwa Spika, pamoja na kuangalia mkanda wa video, Mhe. Ester Amos Bulaya (Mb) alikiri mbele ya Kamati na kuomba radhi Bunge kwa vitendo vya utovu wa nidhamu vinavyoonesha dharau kwa Bunge na Mamlaka ya Spika.

6.3. Mheshimiwa Spika, kutokana na ushahidi huu, Kamati imejiridhisha bila kuacha shaka yoyote kuwa ni kweli Mhe. Mhe. Ester Bulaya (Mb) alifanya vitendo ambavyo ni kudharau Mamlaka ya Spika kinyume na Kifungu cha 26(c) (d) (e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 pamoja na Kanuni ya 74 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

6.4. Mheshimiwa Spika, Kwa urahisi wa rejea nanukuu:

26. Any person who-

- (a)
- (b)

(c) Causes an obstruction or disturbance within the precincts of the Assembly Chamber during a sitting of the Assembly or of the Committee thereof; or

(d) Shows disrespect in speech or manner towards the Speaker; or

(e) Commit any other act of intentional disrespect to or with reference to the proceedings of the Assembly or to any person proceeding at such proceedings, Commits an offense

74 (1) Spika anaweza kutaja jina la Mbunge kwamba amedharau mamlaka ya Spika na kisha kupeleka jina hilo kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ikiwa;

(a) Kwa maneno au vitendo, Mbunge huyo anaonyesha dharau kwa Mamlaka ya Spika; au

(b) *Mbunge huyo anafanya kitendo chochote kwa makusudi cha kudharau Shughuli za Bunge au Mbunge yoyote anayeongoza shughuli hiyo.*

6.5. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mantiki hiyo, Kamati inamтиа hatiani Mhe. Ester Bulaya (Mb) kwa Kudharau Mamlaka ya Spika.

6.6. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kujiridhisha kuwa Mhe. Ester Bulaya alikiuka sheria na Kanuni za Bunge, Kamati inajielekeza katika hoja kwamba Kama itathibitika ni kweli alifanya vitendo hivyo, ni hatua gani anatakiwa kuchukuliwa?

6.7. **Mheshimiwa Spika**, katika kujibu hoja hiyo Kamati ilizingatia yafuatayo:-

(a) Kitendo cha Mhe. Ester Bulaya (Mb) kukiri na kuomba radhi Bunge bila kuisumbua Kamati.

(b) Mhe. Ester Bulaya (Mb) ni mkosaji wa mara ya pili kwa kosa hili la kudharau mamlaka ya Spika.

(c) Athari za vitendo alivyovifanya ambavyo vilivuruga shughuli za Bunge na kushusha hadhi ya Bunge.

(d) Mhe. Ester Bulaya (Mb) tangu alipoadhibiwa na Bunge lako tukufu kwa kosa kama hili mnamo tarehe 30 Mei, 2016, hajaacha kufanya vitendo vya uvunjifu wa Kanuni lakini kwa kiasi fulani amepunguza kufanya vitendo hivyo tofauti na alivyokua awali kabla ya adhabu hiyo.

6.8. **Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 33(1) Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge kinaclekeza kuwa Mbunge yeoyote atakayefanya kosa la kudharau Mamlaka ya Spika au shughuli za Bunge kwa mujibu wa Kifungu cha 26 au Kifungu kinginecho, Bunge linaweza kuazimia kumuelekeza Spika kumpa karipio kali (*reprimand*) au kumsimamisha asihudhurie vikao vya Bunge kwa muda litakaloona unafaa, isipokuwa muda huo usizidi siku ya mwisho ya Mkutano wa

Bunge unaofuata baada ya azimio hilo. Kifungu cha 33(1) kinasomeka ifuatavyo:

"33(1) Where any member commits any contempt of the Assembly whether specified in section 26 or otherwise, the Assembly may, by resolution, either direct the Speaker to reprimand such member or suspend him from the service of the Assembly for such period as it may determine".

7.0. UZOEFU WA MASHAURI YA NYUMA

7.1. Shauri lililomhusu Bi. Zuhura Hamza ambaye alikuwa ni mfanyakazi (TANESCO).

Mheshimiwa Spika, Mtumishi huyo alinukuliwa na vyombo mbalimbali vya habari akituhumu Wabunge kuwa wanakaa ndani ya Ukumbi wa Bunge hawafanyi chochote lakini mwisho wa uhai wa Bunge miaka mitano (5) wanapata fedha nyingi (*millions of money*) wakati wengine wanalala tu Bungeni.

Alipoitwa mbele ya Kamati ya Maadili **alikiri na kuomba msamaha kwa maandishi na kwa mdomo**. Kamati ilimwandikia barua ya onyo kali.

7.2. Shauri lililomhusu **Mhe. Salim Khamis Juma**, aliyekuwa Mbunge kuititia Chama cha CUF. Wakati wa kujadili Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 1999/2000 alitamka maneno yaliyokuwa yanamtuhumu Spika wa Bunge kuwa ana maslahi ya Chama na anajihuisha na rushwa katika kuteua Wabunge kusafiri nje ya nchi kikazi, alipoitwa mbele ya Kamati kuthibitisha alishindwa hivyo Kamati ilimtia hatiani kwa kumdhara Mhe. Spika. Kamati iliwasilisha taarifa ya uchunguzi kwa Spika na shauri lilimalizika kwa Mhe. Salim K. Juma kumwomba radhi Spika na Spika aliridhia radhi aliyoomba.

Mheshimiwa. Spika, kwa kuzingatia Sheria hii, uzoefu wa mashauri ya numa pamoja na kitendo cha Mhe. Ester Bulaya (Mb) kukiri na kuomba radhi na kuahidi mbele ya Kamati kutorudia kitendo hiki, Hivyo, Bunge litafakari ushahidi

uliotolewa dhidi yake na kuuzingatia wakati wa kupitisha Azimio la kutoa adhabu anayostahili kwa kosa alilotenda.

8.0. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge na napenda nitumie nafasi hii kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge hili ambalo ni chombo cha uwakilishi wa Wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ili kuhakikisha kuwa ustawi wa wananchi ndio kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, kipekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua kwa umakini mkubwa shauri la kudharau Mamlaka ya Spika. Wajumbe hawa walifanya kazi nzuri na walizingatia misingi ya haki, bila kumwoneea au kumpendelea mtu yoyote. Kwa heshima naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

- (i) Mhe. Kapt (Mst), George Huruma Mkuchika (Mb) - Mwenyekiti
- (ii) Mhe. Almas Athuman Maige (Mb) - Makamu Mwenyekiti
- (iii) Mhe. Rashid Ali Abdallah (Mb)- Mjumbe
- (iv) Mhe. Amina Nassoro Makilagi (Mb)-Mjumbe
- (v) Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma (Mb)-Mjumbe
- (vi) Mhe. Othman Omar Haji (Mb)-Mjumbe
- (vii) Mhe. Rose Kamil Sukum (Mb)-Mjumbe
- (viii) Mhe. George Malima Lubeleje (Mb)-Mjumbe
- (ix) Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf (Mb)-Mjumbe
- (x) Mhe. Susan Anselm Lyimo (Mb)-Mjumbe
- (xi) Mhe. Tunza Issa Malapo (Mb)-Mjumbe
- (xii) Mhe. Asha Abdullah Juma (Mb)-Mjumbe
- (xiii) Mhe. Augustino Manyanda Masele (Mb)-Mjumbe
- (xiv) Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka (Mb)-Mjumbe
- (xv) Mhe. Ali Hassan Omar King (Mb)- Mjumbe; na
- (xvi) Mhe. Innocent Sebba Bilakwate (Mb)- Mjumbe

Aidha, napenda kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza

majukumu yake. Kipekee, nawashukuru Ndugu Pius T. Mboya, Kaimu Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Ndugu Prudens R. Rweyongeza, Ndugu Mossy Lukovi ambao ni Manaibu Washauri wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Ndugu Maria Mdulugu, Katibu wa Kamati, na Ndg. Editruda Kilapilo kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kujadili na kupokea maoni na mapendekozo ya Kamati ili baada ya mjadala liazimie kuchukua hatua stahiki kwa kadiri litakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

Kapt. (Mst) George Huruma Mkuchika, (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE

28 Aprili, 2017

**AZIMIO LA BUNGE KUHSU HATUA ZA KUCHUKUA DHIDI
YAMHE. ESTER AMOS BULAYA (MB) KWA KUHSIKA NA
VITENDO VYA KUDHARAU MAMILAKA YA SPIKA KATIKA
MKUTANO WA TATU, KIKAO CHA THELATHINI NA MBILI
KILICHOFANYIKA TAREHE 30 MEI, 2016 – KAMA
LILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*[Limetolewa chini ya Kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Kinga,
Madaraka na Haki za Bunge (The Parliamentary Immunities,
Powers and Privileges Act, [CAP 296 R:E 2015].*

KWA KUWA, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaongozwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge ambazo zilitungwa na Bunge lenyewe kwa ajili ya kuliongoza katika kutekeleza shughuli zake;

NA KWA KUWA, Sheria na Kanuni za uendeshaji wa shughuli za Bunge zimeweka utaratibu wa majadiliano ndani ya Bunge, na kwamba kwa taratibu hizo Wabunge wanatakiwa kuheshimu Mamlaka ya Spika na shughuli za Bunge kwa ujumla;

NA KWA KUWA, katika Kikao cha Thelathini na mbili cha Mkutano wa Tatu wa Bunge kilichofanyika tarehe 30 Mei, 2016 Bunge lilikuwa likijadili Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha, 2016/2017, Mhe. Ester Amos Bulaya (Mb) alifanya vitendo vya kudharau Mamlaka ya Spika kwa kurusha kwa kutawanya karatasi na vitabu hivyo kufanya shughuli za Bunge zilizokuwa zimepangwa kuendelea;

NA KWA KUWA, Mheshimiwa Spika kwa Mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge alimpeleka mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Mhe. Ester Bulaya (Mb) kwa makosa ya kudharau Mamlaka ya Spika;

NA KWA KUWA, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilikaa tarehe 20 Aprili, 2017 hapa Dodoma na kusikiliza shauri la Mhe. Ester A. Bulaya (Mb);

NA KWA KUWA, kwa kuzingatia kuwa Mhe. Ester Bulaya (Mb) hii ni mara ya pili kutiwa hatiani kwa kosa kama hili la kudharau Mamlaka ya Spika na kupewa adhabu na Bunge ya kutohudhuria Vikao vya Mkutano wa Tatu na Nne wa Bunge;

NA KWA KUWA, Mhe. Ester Bulaya (Mb) alivunja tena Kanuni ya 74(1) (a) na (b) na Kifungu cha 26(d) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 kwa kufanya vitendo vya kudharau Mamlaka ya Spika;

NA KWA KUWA, Mhe. Ester Bulaya (Mb) aliiitikia wito wa Kamati bila kuleta usumbufu wa aina yoyote, na alipohojiwa na Kamati alikiri wazi kosa lake na kuomba radhi kwa Mheshimiwa Spika na Bunge;

HIVYO BASI, Bunge linaazimia:-

Kumpa karipio kali Mhe. Ester Bulaya (Mb) kutokana na kitendo chake cha kuonesha ushirikiano kwa Kamati na pia kitendo chake cha kiungwana cha kuomba radhi kwa Mheshimiwa Spika, kwa Bunge na kwa wengine wote alioawakwaza kutokana na matendo yake;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, linakubaliana na kupitisha mapendekezo ya adhabu hiyo kwa Mhe. Ester Amos Bulaya (Mb) kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Kapt. (Mst.) George Huruma Mkuchika (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE

28 Aprili, 2017

**TAARIFA YA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA
BUNGE KUHUSU SHAURI LA KUINGILIA UHURUNA HAKI ZA
BUNGE LINALOWAHUSU NDG. PAUL CHRISTIAN MAKONDA
NA NDG. ALEXANDER PASTORY MNYETI – KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

1.1 **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Fasili ya 4(2) na (3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya Kamati kuhusu uchunguzi wa tuhuma zinazowahusu Ndg. Paul Christian Makonda, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na Ndg. Alexander Pastory Mnyeti, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru kuhusu kudharau, kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge.

1.2 **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kukushukuru wewe binafsi kwa weledi, busara na hekima unazozitumia katika kuliongoza Bunge letu kwa ufanisi

mkubwa. Kama tujuavyo Bunge la Kumi na Moja lina changamoto nyingi-kutokana na ukweli kwamba karibu asilimia sabini ya Bunge letu linaundwa na Wabunge wapya kabisa kwa maana ya usoefu wa masuala ya Bunge.

1.3 **Mheshimiwa Spika**, aidha, napenda kumshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge letu kwa uongozi makini.

1.4 **Mheshimiwa Spika**, kwa Mamlaka uliyonayo chini ya Fasili ya 4(1) (a) na (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, uliiagiza Kamati yangu kukutana kwa ajili ya kushughulikia suala la tuhuma za kudharau, kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge zinazowahusu Ndg. Makonda na Ndg. Mnyeti. Katika maelekezo yako uliitaka Kamati kufanya uchunguzi ili kubaini kama kweli watu hao walihusika na tuhuma hizo na kupendekeza hatua za kuchukua dhidi yao.

1.5 **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelekezo hayo, Ndg. Makonda na Ndg. Mnyeti waliitwa kwa Hati ya Wito (*Summons*) ili wafike mbele ya Kamati kujibu tuhuma zinazowakabili. Hati ya Wito ilimtaka kila shahidi kutoa maelezo juu ya kuhusika au kutohusika kwao na tuhuma zinazowakabili na kama ikibainika waeleze ni kwanini wasichukuliwe hatua kwa kukiuka Kifungu cha 26(e) na 34(1)(j) vya Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge Sura ya 296 ambavyo vinakataza kufanya matendo wanayotuhumiwa kuyafanya.

1.6 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana rasmi tarehe 29 Machi, 2017 na tarehe 6, 8-10 Aprili, 2017 kwa ajili ya kushughulikia masuala hayo.

2.0 CHIMBUKO LA SHAURI

2.1 **Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 8 Februari, 2017 katika Kikao cha Nne cha Mkutano wa Sita, Bunge lilipitisha Maazimio yaliyotokana na hoja iliyotolewa na Mhe. Mwita

Mwikwabe Waitara (Mb) aliyoiwasilisha chini ya Kanuni ya 51 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

2.2 **Mheshimiwa Spika**, Mhe.Waitara (Mb) alitoa hoja kwamba Ndg. Paul Christian Makonda ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam alinukuliwa na kituo cha televisheni cha *Clouds* akisema Wabunge wanasinzia Bungeni. Aidha, Mhe. Waitara (Mb) aliendelea kueleza kwamba pia Mkuu wa wilaya ya Arumeru Ndg. Alexander Pastory Mnyeti aliandika katika mtandao wa kijamii wa *Facebook* kuwa Azimio la Bunge lilitotokana na pendekeso la Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa la kuwapatia semina Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuhusu namna ya kutekeleza majukumu yao ni upuuzi mtupu na kwamba Wabunge hawajielewi na anashauri wafanye kazi zao na za wengine waachiwe wenyewe, jambo ambalo kwa maoni ya Mhe. Waitara (Mb) lilikuwa ni dharau kwa Bunge na pia kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge.

2.3 **Mheshimiwa Spika**, katika kujadili hoja hiyo, Bunge lilionia kuwa Ndg.Makonda na Ndg. Mnyeti wana tuhuma za kujibu kuhusu kulidharau Bunge, kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge na hivyo Bunge liliazimia kama ifuatavyo:

1. **Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI atoe Waraka mahsusni kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuhusu namna ya kutekeleza majukumu yao bila kuingilia Mihimili mingine;**

2. **Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Ndugu Paul Christian Makonda na Mkoo wa Wilaya ya Arumeru Ndugu Alexander Pastory Mnyeti waitwe mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge; na**

3. **Endapo itathibitika na Bunge kuridhia, wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.**

3.0 UCHAMBUZI WA KAMATI

3.1 **Mheshimiwa Spika**, Katika Waraka wako ulioelekeza kwa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ulirejea

Fasili ya 4(1) (a) na (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016. Kwa urahisi wa rejea nanukuu Fasili ya Kanuni hiyo:

4 (1) Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itatekeleza majukumu yafatayo:-

(a) *Kuchunguza na kutoa mapendeleko kuhusu masuala yote ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge yatakayopelekwa na Spika;*

(b) *Kushughulikia mambo yanayohusu maadili ya Wabunge yatakayopelekwa na Spika.*

3.2 **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Hati za Wito zilizotolewa kwa mashahidi kama ilivyoelezwa awali ilikuwa kama ifuatavyo: Ndg. Makonda na Ndg. Mnyeti zillieleza kukiukwa kwa masharti ya Kifungu cha 26(e) Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge Sura, 296 kinachoeleza kwamba mtu ye yeyote atakuwa ametenda kosa endapo atafanya kwa makusudi kitendo chochote chenye kudharau shughuli za Bunge au mtu ye yeyote anayeendesha shughuli hizo.

Aidha, Hati ya wito ya Ndg. Mnyeti iliongeza kueleza kosa la kukiuka kifungu cha 34 (1) (j) ambacho kinakataza mtu ye yeyote kuchapisha kwa madhumuni ya kumkashifu (*libel*) Mbunge kuhusu tabia au mwenendo wake kutokana na kitendo cha Mbunge huyo, au maneno aliyo yasema wakati akitekeleza majukumu yake ya kibunge.

3.3 **Mheshimiwa Spika**, katika kushughulikia suala hili, Kamati ilirejea nyaraka mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

(ii) Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge Sura ya 296.

(iii) Practice and Procedure of Parliament by M.N. Kaul S.L. Shakdher -Lok Sabha Secretariat pg. 230

(iv) Kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*) za tarehe 8 Februari, 2017.

(v) Hukumu za Mashauri mbalimbali yaliyoamuliwa na Bunge siku za nyuma (*case law*).

4.0 HOJA ZA MSINGI (ISSUES)

4.1 **Mheshimiwa Spika**, ili Kamati iweze kufanya uchambuzi wa malalamiko yaliyotolewa na kufikia mapendelekezo ya Maazimio Kamati ijielekeza katika kupata majibu ya maswali yafuatayo:

(a) Je, ni kweli kwamba Ndg. Paul Christian Makonda alitamka maneno yaliyolalamikiwa na Wabunge kwamba yalivunja haki na kudharau mamlaka ya Bunge?;

(b) Je, ni kweli kwamba Ndg. Alexander Pastory Mnyeti aliandika maneno yaliyolalamikiwa na Wabunge kwamba yalivunja haki na kudharau mamlaka ya Bunge? ; na

(c) Endapo hoja (a) na (b) ni kweli, Je, ni hatua gani za kisheria zinazopaswa kuchukuliwa dhidi yao?

4.2 **Mheshimiwa Spika**, katika kujibu hoja hizo, naomba tuanze kuchambua ushahidi wa shahidi mmoja baada ya mwingine.

5.0 SHAURI KUHUSU NDG. PAUL CHRISTIAN MAKONDA

5.1 **Mheshimiwa Spika**, chanzo cha malalamiko yaliyosababisha kuwepo kwa suala hili mbele ya Kamati ni hatua iliyochukuliwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Ndg. Paul Christian Makonda kupambana na watu wanaojihusisha na biashara ya madawa ya kulevyta pamoja na watumiaji wa madawa hayo.

5.2 Mnamo tarehe 2 Februari, 2017 Ndg. Makonda alinukuliwa na vyombo mbalimbali vyatuhusu ikiwemo

mitandao ya kijamii akitaja majina ya watu mbalimbali na wenyе nafasi na nyadhifa tofauti katika jamii kwamba wanadhaniwa kuwa wanajihusisha na biashara ya kuuza, kusafirisha na kutumia dawa za kulevya. Miongoni mwa watu waliotajwa walikuwa ni baadhi ya askari wa Jeshi la Polisi, wasanii mbalimbali katika tasnia ya filamu na muziki na watu wengine.

5.3 **Mheshimiwa Spika**, pamoja na pongezi hizo, wapo baadhi ya wananchi na wabunge waliokosoa utaratibu alioutumia wa kutaja majina ya watuhumiwa hadharani.

5.4 Katika Mkutano wake na vyombo vya Habari uliofanyika ofisini kwake, Ndг. Makonda aliulizwa swali lifuatalo:

"Mheshimiwa ni kwamba tumeona Bungeni kuna ushahidi mbalimbali unatolewa wanasema wanajuana, wanatajana lakini mpaka muda huu hatujajua hatua gani zitachukuliwa kwa wale wanaosema wanajuana wenyewe kwa wenyewe"?

Akijibu swali hilo Ndг. Makonda alikaririwa akisema maneno yafuatayo:-

"..... zingine ni mbwembwe tu, unajua mle ndani wakati mwininge wanachoka na kusinzia lazima kuwe na watu kidogo akili zao zinawasaidia kuamka, kucheka na kufurahi maisha yanaendelea".

5.5 **Mheshimiwa Spika**, Ndг. Makonda alifika mbele ya Kamati tarehe 29 Machi, 2017 kuanzia saa 4 asubuhi katika Ukumbi wa Spika na kusomewa tuhuma dhidi yake na kukiri kwamba ni kweli alitoa kauli hiyo. Katika maelezo yake alionyesha kujutia kauli hiyo ambayo iliwakwaza na kuwavunjia heshima Wabunge. Hivyo, aliomba radhi kwa kueleza kuwa hata kabla ya kuitwa na Kamati tayari alikuwa ameandika barua kwa Mheshimiwa Spika ya kuliomba radhi Bunge.

5.6 **Mheshimiwa Spika**, sehemu ya maelezo yake ya kukiri kosa mbele ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

"Mheshimiwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge na Wajumbe wa Kamati hii ambao ni Waheshimiwa Wabunge, pamoja na timu nzima ya Sekretarieti, awali ya yote nawashukuru na nawapongeza kwa kazi kubwa mnayoifanya. Wengi wenu tumefahamiana na wengi wenu ni walezi wangu. Kwahiyo, ninajisikia vibaya kusimama mbele yenu kwa kuwakwaza na kuwavunja heshima ambayo sikupaswa kufanya hasa kwa watu ambao mmekuwa walezi na ni watu ambao mnanitegemea nifanye vizuri kwa ajili ya kuwawakilisha vijana wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa baada ya kauli yangu, nilichukua jukumu la kuandika barua kwa Mheshimiwa Spika, baada ya kusikiliza mjadala katika Bunge na kumwomba radhi Mheshimiwa Spika kwa kitendo cha kauli yangu niliyoitao wakati nikijibu swali pale ambapo mwandishi alitaka kujua mambo kadhaa yaliyofanyika."

Ndg. Makonda alimalizia maelezo yake kwa kusema:-

"Kwahiyo, akili yangu ilikuwa na mtazamo wa namna hiyo, haikuwa na mtazamo wa kulidharau Bunge, haikuwa na mtazamo wa kumvunjia heshima Mbunge ye yote yule na kwa kweli najisikia vibaya sana kusimama mbele yenu na ninaomba radhi sana sana kwa kauli niliyoitao na tafsiri iliyopatikana."

5.7 **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia ushahidi wa kukiri kwa shahidi, Kamati imejiridhisha kuwa Ndg. Paul Christian Makonda, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, alitamka maneno yaliyolalamikiwa na Wabunge hivyo hoja (a) ya Je, ni kweli kwamba Ndg. Paul Christian Makonda alitamka maneno yaliyolalamikiwa na Wabunge kwamba yalivunja haki na kudharau mamlaka ya Bunge, IMETHIBITIKA bila kuacha shaka yoyote.

5.8 **Mheshimiwa Spika**, huo ndio ulikuwa uchunguzi wa Kamati kuhusu shauri la kudharau Bunge, kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge linalomhusu Ndg. Paul Christian Makonda. Hivyo, Bunge liutafakari ushahidi uliotolewa dhidi yake na kuuzingatia wakati wa kuitisha Azimio la hatua za kuchukua dhidi yake.

6.0 SHAURI KUHUSU NDG. ALEXANDER PASTORY MNYETI

6.1 **Mheshimiwa Spika**, chanzo cha malalamiko kuhusu Shahidi huyu ni taarifa ya Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa iliowasilishwa tarehe 3 Februari, 2017.

6.2 Taarifa hiyo ilainisha changamoto na mapendekezo ya kutatua changamoto hizo. Miiongoni mwa changamoto na mapendekezo yaliyoainishwa ni suala la Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kutumia vibaya mamlaka yao chini ya Kifungu cha 7(1) (2) na Kifungu cha 15(1) na (2) vya Sheria ya Tawala za Mikoa Na. 19 ya 1997 (*The Regional Administration Act*), No. 19 of 1997) kwa kukamata na kuwaweka mahabusu Wabunge, Madiwani na Watumishi wa Umma.

6.3 Katika Taarifa hiyo Kamati ilipendekeza kuwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa awapatie semina Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuhusu namna ya kutekeleza majukumu yao. Mapendekezo hayo yaliridhiwa na Bunge na kuwa Maazimio ya Bunge.

6.4 **Mheshimiwa Spika**, kutokana na masuala mbalimbali yaliyojadiliwa Bungeni kuhusiana na jambo hilo, ndipo Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Alexander Pastory Mnyeti alipoandika katika ukurasa wake wa mtandao wa (*Facebook*) akiyaita mapendekezo hayo ni upuuzi mtupu na kwamba Wabunge hawajielewi anawashauri wafanye kazi zao. Maneno aliyoanda katika ukurasa huo ni haya yafuatayo:

"Upuuzi mtupu. Wabunge hawa hawajielewi. Nawashauri fanyeni kazi zenu za wengine waachieni wenywewe".

6.5 **Mheshimiwa Spika**, siku ya tarehe 6 Aprili 2017 Ndg. Mnyeti alifika mbele ya Kamati yangu na kuhojiwa kuhusiana na tuhuma zilizomkabili ambapo alikiri kuandika maneno hayo na kwamba anamiliki akaunti ya *facebook* iliyoandika maneno yanayolalamikiwa.

6.6 **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, shahidi aliomba radhi kwa Bunge na kusema kuwa hana ubavu wa kushindana na Bunge. Shahidi aliomba radhi kwa baadhi ya maneno yafuatayo:

“...Mhe. Mwenyekiti, basi naomba sasa Kamati yako itumie busara na ninaomba radhi kwamba limekuwa ni kubwa lakini halikuwa kusudio langu tangu awali kwamba sasa nilikwaze Bunge kwa style hiyo. Mimi naomba radhi Kamati yako, itumie Busara zake lakini lengo kutoka moyoni kwangu halikuwa katika hali hiyo ambayo limechukuliwa...”

...naomba radhi jambo limekuwa kubwa lengo halikuwa katika hali hii lilivyo chukuliwa “nikiri kuwa ni madhaifu yangu sikutenda kiungwana naomba Kamati inisamehe kuanzia sasa na kuendelea haitajirudia tena”...

Kwa hiyo, binafsi niiombe Kamati yako kwa nafasi ya kipekee ione umuhimu wa kunisamehe...”

6.7 **Mheshimiwa Spika**, baada ya kumsikiliza shahidi huyo, Kamati imejiridhisha bila kuacha shaka yoyote kuwa Shahidi huyo aliandika maneno yaliyolalamikiwa ya kuingilia uhuru na kuvunja haki za Bunge kinyume na kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge. Kifungu hicho kinaeleza. Nukuu:

26. Any person shall be guilty of an offence who-

- (a) N/A
- (b) N/A
- (c) N/A
- (d) N/A

(e) does any other act of intentional disrespect to or with reference to the proceedings of the

Assembly or to any person presiding at such proceedings commits an offence"

6.8 **Mheshimiwa Spika**, Ndg. Mnyeti aliyaandika maneno hayo kwenye akaunti yake ya *facebook* kitendo ambacho ni kukiuka masharti ya *Kifungu cha 34 (1) (j) kinachokataza mtu yeyote kuchapisha kwa madhumuni ya kumkashifu (libel) Mbunge kuhusu tabia au mwenendo wake kutohana na kitendo cha Mbunge huyo, au maneno aliyoyasema wakati akitekeleza majukumu yake ya kibunge.*

6.9 Kifungu hicho kinasomeka kama ifuatavyo:-

"34 (1) any person who-

(j) publishes or prints any libels on any member concerning his character or conduct as a member and with regard to actions performed or words uttered by him in the course of the transaction of the business of the Assembly, commits an offence and on conviction is liable to a fine not exceeding five hundred thousand shillings or to imprisonment for a term not exceeding three years or to imprisonment for a term not exceeding three years or to both"

6.10 **Mheshimiwa Spika**, kwa mantiki hiyo, hoja (b) ya Je, ni kweli kwamba Ndg. Alexander Pastory Mnyeti aliandika maneno yaliyolalamikiwa na Wabunge kwamba yalivunja haki na kudharau mamlaka ya Bunge, IMETHIBITIKA bila kuacha shaka yoyote.

6.11 **Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi huo na baada ya kubaini kwamba Ndg. Makonda na Ndg. Mnyeti wametenda makosa yaliyolalamikiwa, **Je, ni hatua gani za kisheria zinazopaswa kuchukuliwa dhidi ya mashahidi?**

6.12 **Mheshimiwa Spika**, katika kujibu hoja hiyo, Kamati ilizingatia na kutafakari kwa kina kuhusu ushahidi wa Shauri hili pamoja na maelezo ya kukiri yaliyotolewa na Mashahidi wote wawili. Vile vile Kamati ilizingatia hatua ya mashahidi kukiri na kujutia vitendo walivyofanya vyta ukikwaji wa Sheria za nchi kwa kungilia uhuru na kuvunja haki za Bunge.

6.13 **Mheshimiwa Spika**,ili Kamati iweze kutoa mapendeleko wa kuzingatia katika masuala tajwa hapo juu hususani pale ambapo shahidi ambaye anatuhumiwa kuvunja haki za Bunge amekiri na kuomba radhi, Kamati ilifanya utafiti kuangalia uzoefu katika mabunge mengine duniani pamoja na uzoefu wa Bunge hili katika kushughulikia masuala kama haya.

7.0 UZOEFU WA MABUNGE MENGINE

7.1 **Mheshimiwa Spika**, mionganini mwa Mabunge ambayo Kamati ilifanya utafiti ni Bunge la *Lok Sabha* la nchini India. Bunge hilo katika Shauri la **K.M Kaushik L.S Deb 18-11-1970** lililowahu Maafisa wawili wa polisi ambao walituhumiwa kuvunja haki za Bunge kwa kumshambulia na kumdhalilisha Mbunge, Bunge liliwaita Maafisa polisi hao mbele ya Bunge ambapo walihojiwa na wakakiri kutenda kosa hilo na kuomba radhi kwa kitendo hicho. Bunge liliwasamehe na kufunga shauri hilo.

7.2 **Mheshimiwa Spika**, nanukuu shauri hilo kama ifuatavyo:-

Shauri la K.M Kaushik L.S Deb 18-11-1970

“....Two police officers of the State of Maharashtra were summoned to the bar of the House to answer the charge of breach of privilege and contempt of the House for allegedly assaulting and abusing a member.

The officers expressed apologies to the member concerned and to the House for whatever happened on that day. In view of the apologies tendered by them, the House decided to treat the matter as closed”.

UZOEFU WA BUNGE KATIKA KUSHUGHULIKIA MASUALA YA HAKI ZA BUNGE KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO

8.1 **Mheshimiwa Spika**, Bunge hili limewahi kufanya uchunguzi kuhusu malalamiko ya kuvunjwa kwa haki za

Bunge ambapo Kamati ya Maadili ilifanya kazi na hatimaye Spika kutoa Uamuzi kuhusiana mashauri yafuatayo:

8.1.1 Shauri jingine ni la Bw. Harold Jaffu (ailiyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha TLP)

8.1.1.1 Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 5/4/2001 aliiwtwa mbele ya Kamati ya Haki za Bunge kujibu tuhuma za kudharau Mamlaka ya Spika siku ya tarehe 29/3/2001 alipokuwa akiongea na vyombo vya habari Dar es Salaam ambapo alinukuliwa na televisheni ya ITV tarehe 30/5/2001 akimtuhumu Spika, Mheshimiwa Pius Msekwa kuwa ana nia ya kupunguza Wabunge wa upinzani kuchaguliwa kuwa wawakilishi katika Bunge la Afrika Mashariki.

8.1.1.2 Akiwa mbele ya Kamati Ndg. Jaffu alikiri na **kuomba radhi** ambapo alieleza mazingira yaliyompelekea kusema maneno hayo.

8.1.1.3 Kamati ilimkuta na hatia na kumuandikia barua ya onyo yenye kumbukumbu Na.BD.50/155/05 ya tarehe 10/4/2001.

8.1.2 Shauri liliomhusu Bi. Zuhura Hamza ambaye alikuwa ni mfanyakazi (TANESCO)

8.1.2.1 Mheshimiwa Spika, Mtumishi huyo alinukuliwa na vyombo mbalimbali vya habari akituhumu Wabunge kuwa wanakaa ndani ya Ukumbi wa Bunge hawafanyi chochote lakini mwisho wa uhai wa Bunge miaka mitano (5) wanapata fedha nyingi (*millions of money*) wakati wengine wanalala tu Bungeni.

8.1.2.2 Alipoitwa mbele ya Kamati ya Maadili **alinkiri na kuomba msamaha kwa maandishi na kwa mdomo**. Kamati ilimwandikia barua ya onyo kali.1

8.2 **Mheshimiwa Spika**, huo ndio ulikuwa uchunguzi wa Kamati kuhusu shauri la kudharau Bunge, kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge linalomhusu Ndg. Alexander Pastory

Mnyeti. Hivyo, Bunge liutafakari ushahidi uliotolewa dhidi yake na kuuzingatia wakati wa kupitisha Azimio la hatua za kuchukua dhidi yake.

8.0 HITIMISHO

9.1 **Mheshimiwa Spika**, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge na napenda nitumie nafasi hii tena kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge hili ambalo ni chombo cha uwakilishi wa Wananchi katika kuisimamia na kuishauri Serikali ili kuhakikisha kuwa ustawi wa wananchi tunaowawakilisha ndio kipaumbele cha kwanza.

9.2 **Mheshimiwa Spika**, kipekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua kwa umakini mkubwa Shauri la kuingilia uhuru na kuvunja haki za Bunge Wabumbe hawa walifanya kazi nzuri na walizingatia misingi ya haki, bila kumwonea au kumpendelea mtu yoyote. Kwa heshima naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:

- (i) Mhe. Kapt(Mst), George Huruma Mkuchika (Mb)-Mwenyekiti
- (ii) Mhe. Almas Athuman Maige (Mb)-Makamu Mwenyekiti
- (iii) Mhe. Rashid Ali Abdallah (Mb)- Mjumbe
- (iv) Mhe. Amina Nassoro Makilagi (Mb)-Mjumbe
- (v) Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma (Mb)-Mjumbe
- (vi) Mhe. Othman Omar Haji (Mb)-Mjumbe
- (vii) Mhe. Rose Kamil Sukum (Mb)-Mjumbe
- (viii) Mhe. George Malima Lubeleje (Mb)-Mjumbe
- (ix) Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf (Mb)-Mjumbe
- (x) Mhe. Susan Anselm Lyimo (Mb)-Mjumbe
- (xi) Mhe. Tunza Issa Malapo (Mb)-Mjumbe
- (xii) Mhe. Asha Abdullah Juma (Mb)-Mjumbe
- (xiii) Mhe. Augustino Manyanda Masele (Mb)-Mjumbe
- (xiv) Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka (Mb)-Mjumbe
- (xv) Mhe. Ali Hassan Omar King (Mb)- Mjumbe; na
- (xvi) Mhe. Innocent Sebba Bilakwate (Mb)- Mjumbe

9.3 Aidha, napenda kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Kipekee, nawashukuru Ndg Pius T. Mboya, Kaimu Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Ndgg. Prudens Rweyongeza, na Ndg. Mossy Lukuvi Naibu Washauri wa Bunge wa Mambo ya Sheria kwa ushauri na ufanuzi walioutoa kuhusiana na hoja mbalimbali za kisheria kuhsiana na mashauri haya. Vile vile, nawashukuru Ndg. Maria Mdulugu, Katibu wa Kamati na Ndg. Editruda Kilapilo kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

9.4 **Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kujadili na kupokea maoni na mapendekezo ya Kamati ili baada ya Mjadala liazimie kuchukua hatua stahiki kwa kadri litakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

Kapt (Mst) George Huruma Mkuchika

MWENYEKITI

KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE

....April, 2017

AZIMIO LA BUNGE KUHSU HATUA ZA KUCHUKUA DHIDI YA NDUGU PAUL CHRISTIAN MAKONDA ALIYETIWA HATIANI KWA KOSA LA KUDHARAU, KUVUNJA HAKI NA KUINGILIA UHURU WA BUNGE – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

[Limetolewa chini ya Kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge (The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, [CAP 296 R:E 2015].

KWA KUWA, Mheshimiwa Spika aligiza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ikutane na kufanya kazi suala la tuhuma dhidi ya Ndgg. Paul Christian Makonda kuhsu kudharau, kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge.

NA KWA KUWA, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilikaa tarehe 29 Machi, 2017 na tarehe 9-10 Aprili, 2017 kufanya uchunguzi wa suala hilo uliowezesha Kamati kubaini kuwa, **NDG. PAUL CHRISTIAN MAKONDA** amekiuka masharti ya kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge (Sura ya 296) kwa kutamka maneno yanayoonesha kudharau, kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge.

NA KWA KUWA, kitendo cha kutamka maneno hayo ni kitendo cha dharau, kudhalilisha na kulifedhehesha Bunge.

NA KWA KUWA, Kamati imezingatia ukweli kwamba Ndg. Paul Christian Makonda hakuisumbua Kamati kwa namna yoyote ile bali alikuwa mtii na alitoa ushirikiano mkubwa kwa Kamati.

NA KWA KUWA, Kamati imezingatia kwamba Ndg. Paul Christian Makonda hakuwa na dhamira ya kulidharau wala kulidhalisha Bunge kama ambavyo ilichukuliwa.

NA KWA KUWA, Kamati imezingatia kuwa Ndg. Paul Christian Makonda hajawahi kutenda kosa kama hilo na kufikishwa mbele ya Kamati.

NA KWA KUWA, Ndg. Paul Christian Makonda amekiri makosa lake na kuliomba radhi Bunge.

NA KWA KUWA, Ndg. Paul Christian Makonda alionesha nia ya kukiri kosa na kuamua kumwandikia Mhe. Spika barua ya kuomba radhi hata kabla hajafika mbele ya Kamati.

NA KWA KUWA, Kamati imezingatia uzoefu wa Mabunge mengine kuhusu adhabu kwa mtu ambaye amekiri kosa la kudharau Bunge na kuomba msamaha wa kosa hilo.

NA KWA KUWA, uzoefu wa Mabunge mengine ya Jumuiya Madola kama vile Bunge la Lok Sabha la nchini India unaonesha kuwa Bunge hilo liliwahi kutoa msamaha kwa watu waliopatikana na hatia ya kumdhalilisha Mbunge na baada kukiri kutenda kosa waliomba msamaha na kusamehewa.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Ndg. Paul Christian Makonda **ASAMEHEWE** na Bunge kutokana na kitendo chake cha klungwana cha kukiri na kujutia kosa lake na kuliomba radhi Bunge mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Kapt. (Mst) George Huruma Mkuchika, (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE

27 Aprili, 2017

AZIMIO LA BUNGE KUHUSU HATUA ZA KUCHUKUA DHIDI YA NDG. ALEXANDER PASTORY MNYETI ALIYETIWA HATIANI KWA KOSA LA KUDHARAU, KUVUNJA HAKI NA KUINGILIA UHURU WA BUNGE – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

[Limetolewa chini ya Kifungu cha 26(e) na 34(1) (j) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge (The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, [CAP 296 R:E 2015].

KWA KUWA, Mheshimiwa Spika aligiza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ikutane na kufanya kazi suala la tuhuma dhidi ya Ndg. Alexander Pastory Mnyeti kuhusu kudharau, kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge.

NA KWA KUWA, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilikaa tarehe 06 Aprili, 2017 na tarehe 9-10 Aprili, 2017 kufanya uchunguzi wa suala hilo uliowezesha Kamati kubaini kuwa, **NDG. ALEXANDER PASTORY MNYETI** amekiuka masharti ya kifungu cha 26(e) na 34(1) (j) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge (Sura ya 296) kwa kuandika maneno kwenye ukurasa wake wa *facebookyanayoonesha* kudharau, kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge.

NA KWA KUWA, kitendo cha kuandika maneno hayo ni kitendo cha dharau, kudhalilisha na kulifedhehesha Bunge.

NA KWA KUWA, Kamati imezingatia ukweli kwamba Ndg. Alexander Pastory Mnyeti hakuisumbua Kamati kwa namna yoyote ile bali alikuwa mtii na alitoa ushirikiano mkubwa kwa Kamati.

NA KWA KUWA, Kamati imezingatia ushahidi wa Ndg. Alexander Pastory Mnyeti kwamba hakuwa na dhamira ya kulidharau wala kulidhalisha Bunge kama ambavyo ilichukuliwa.

NA KWA KUWA, Kamati imezingatia kuwa Ndg. Alexander Pastory Mnyeti hajawahi kutenda kosa kama hilo na kufikishwa mbele ya Kamati.

NA KWA KUWA, Ndg. Alexander Pastory Mnyeti amekiri makosa yake na kuliomba radhi Bunge.

NA KWA KUWA, Kamati imezingatia uzoefu wa Mabunge mengine kuhusu adhabu kwa mtu ambaye amekiri kosa la kudharau Bunge na kuomba msamaha wa kosa hilo.

NA KWA KUWA, uzoefu wa Mabunge mengine ya Jumuiya Madola kama vile Bunge la Lok Sabha la nchini India unaonesha kuwa Bunge hilo liliwahi kutoa msamaha kwa watu waliopatikana na hatia ya kumdhaliilisha Mbunge na baada kukiri kutenda kosa waliomba msamaha na kusamehewa.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Ndg. Alexander Pastory Mnyeti **ASAMEHEWE** na Bunge kutohana na kitendo chake cha kiungwana cha kukiri na kujutia kosa lake na kuliomba radhi Bunge mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Kapt. (Mst) George Huruma Mkuchika, (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE

27 Aprili, 2017

SPIKA: Sasa Waheshimiwa Wabunge, mtaona kwamba Taarifa hii ya Kamati ya Haki, Kinga Maadili na Madaraka ya Bunge imetoa taarifa tatu. Taarifa moja inamhusu Mheshimiwa Freeman Aikael Mbewe na Mheshimiwa Halima Mdee kwa pamoja. Taarifa nyingine inamhusu Ndugu Paul Christian Makonda na Ndugu Alexander Pastory Mnyeti kwa pamoja na taarifa nyingine inamhusu Mheshimiwa Ester Amos Bulaya peke yake.

Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi hiyo tumefika kama ilivyo utaratibu wetu, baada ya kusomewa *summary* lakini maelezo marefu yamo ndani ya vitabu ambavyo naamini kila mmoja wetu amepata nakala, ambayo mnaweza mkajiridhisha wenyewe, mashauri yenye yalihusu nini na yalipoenda kwenye Kamati yalishughulikiwa namna gani, na Kamati hii ilifikia vipi mahitimisho yake; na Kwa hiyo, sasa wameleta maoni na mapendekezo yao mbele yetu ili tuyajadili na baadaye tufanye maamuzi kuhusiana na mambo haya ambayo yameletwa mbele yetu, ambayo sisi kama Bunge ndio tuna mamlaka kwayo.

Kwa jinsi hiyo naruhusu mjadala ambao hautakuwa mrefu sana. Nadhani tukimpa kila mmoja dakika tano zitakuwa zinatosha, si ndio?

Haya, tuenze na Paroko Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa napenda nichukue nafasi hii kukupongeza wewe pamoja na viongozi wetu mnaokalia hicho kiti, kwa busara na kazi nzuri mnayofanya kwa kuliongoza Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuipongeza kamati. Kamati imefanya kazi kubwa, imefanya kazi nzuri ambayo iko mbele yetu sasa kwa ajili ya mjadala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatu, nataka niwapongeze viongozi wote pamoja na Wabunge walioitwa kwenye Kamati hii na kukubali kuitika wito. Nawapongeza zaidi kwa

sababu ya unyenyekevu wao, kwa sababu sisi viongozi unyenyekevu ni jambo la msingi sana katika kuhakikisha kwamba tumetenda kazi yetu kwa ufanisi na kwa weledi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nataka niungane na Kamati, kwa uamuzi wake wa kuwasamehe wote walioomba msamaha katika Kamati. Kwa sababu hata kama unakusudia kumuadhibu mtoto akiomba msamaha, basi ni ushahidi kwamba lile alilokosea amelijua na dhamira ya kutolitenda tena amekuwa ameshaiweka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hatua ya Kamati kuwasemehe walioomba msamaha, ninapenda kuchukua nafasi hii kumuombea msamaha Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Ester Bulaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, licha ya Mheshimiwa Halima Mdee kuomba msamaha ndani ya kamati, Mheshimiwa Halima Mdee alifika ndani ya Bunge lako Tukufu, alisimama na kuomba msamaha kwa Watanzania, kwa wapiga kura wake wa Jimbo la Kawe, kwa Spika, kwa Wabunge wote. Na mtakumbuka siku akiomba msamaha kuna Mbunge mmoja alisema Halima umeokoka, kama ishara kwamba ule uamuzi wake wa kuomba msamaha na lugha aliyoitumia ilimridhisha kila mmoja wetu ndani ya Bunge na ndiyo maana siku ile tulikuwa tunampigia makofi mengi kabisa.

Mheshimiwa Spika, sisi wote humu ndani ni waumini wa dini mbalimbali, na dini zetu zinafundisha msamaha. Sasa, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, nakuomba Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu ambao Mheshimiwa Halima aliunesha ndani ya Kamati na ndani ya Bunge lako tukufu basi tumuunganishe na wenzake ambao waliomba msamaha wakasamehewa ili tumpe nafasi ya kuanza upya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa pamoja, tuendelee kutii Mamlaka ya Kiti, tuendelee kuheshimu maagizo ya Kiti na pamoja

tuendelee kusaidiana, kuheshimiana na kuweza kulifanya Bunge letu liwe ni Bunge la mfano. Kwa kusameheana itaonesha kabisa kwamba, sisi ni viongozi ambao tunaweza tukaguswa, na baadaye tukarudi tukaendelea na mambo yetu kama kawaida. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa unyenyekevu mkubwa na kama ulivytania Baba Paroko, Maparoko ni watu wa imani, ni watu wanaofundisha msamaha, basi mimi Baba Paroko nakuomba Spika msamaha, namuomba Mheshimiwa Kigwangalla msamaha, nawaomba Wabunge wote msamaha kwa niaba ya Mheshimiwa Halima tumsamehe aweze kuendelea na wenzake, ahsante sana. (*Makof*)

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa na mimi nichangie hoja iliyoko mbele yetu ambayo ni muhimu sana, si tu kwa mustakabali wa Bunge letu lakini jamii nzima ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, niungane kabisa na aliyoyasema Mheshimiwa Selasini kama tunavyomwita Baba Paroko kwa maneno ya busara kabisa.

Mheshimiwa Spika, tuna misemo mingi kwenye jamii yetu ya Kiswahili, mmojawapo ni lile tunalosema mtoto akiunyea mkono, haukatwi, lakini dini zetu tunazoziamini zinatuambia tutoe adhabu ambayo inafundisha na tusitoe adhabu ya kuumiza. Kwa kweli Kamati yetu imefanya kazi nzuri sana na imetuletea taarifa za kina kabisa. Kama nilivyosema mwanzo napita kwenye njia aliyopita Baba Paroko, kwamba niwapongeze kamati kwa maamuzi waliyoyafikia hasa yale ya kusamehe. Kwa sababu kwenye kusamehe kuna matokeo mema zaidi si duniani tu, lakini hata siku ya hukumu kwa wale tunaoamini kwamba iko siku ya kuhukumiwa na pale tunaambiwa tutapata msamaha ikiwa na sisi tutasamehe wale waliotukosea huku duniani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nisimame kwa nafasi ya mama, kuwaombea radhi watoto kwa wale ambao hawakupata

msamaha. Mama siku zote ndiye wa kulaumiwa, hata kama makosa yanafanywa na watoto kwenye nyumba baba akiwa amechangia sana lakini mwisho wa yote lawama kwa mama.

Kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hiyo ya mama, kwamba makosa waliyoyafanya watoto wangu hawa Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Ester Bulaya yachukuliwe kwa uzito huo na mama siku zote hataki kuharibikiwa kwa watoto wake, na katika jitihada za kutengeneza wala haoni kuna kosa kubwa ambalo halisameheki na kwa hiyo, maisha yakaendelea wenye familia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, na mimi naomba vilevile kwamba maisha ya familia hii ya Bunge yaendelee kwa kuwasamehe watoto hawa, tuwape adhabu ambayo itawarekebisha, na mimi naamini ni ile ambayo itawabakisha humu ndani ya hili jengo tukiwaona kila siku kwa miezi hii miwili ili tuone kweli wanabadilika, tukiwapeleka huko nje hatujui watakumbana na nani. Inawezekana akakumbana na ibilisi mbaya zaidi akawaambia wewe *keep it up* utafukuzwa leo lakini wewe Mbunge, sisi hilo siyo nia yetu, tunataka kuona watoto hawa wenye kofia hii ya uheshimiwa wakiwa ndani humu tukiwaangalia kila siku na ili wabadilike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nipongeze kwa namna ya kipekee kabisa lile ambalo amelifanya binti yangu Halima Mdee. Profesa Kabudi hapa alipokuwa anawasilisha siku ile, alisema amejifunza kitu kutoka kwa Mheshimiwa Mtemi Chenge, ambaye alimwambia ukiingia kwenye maisha haya ya umma basi *swallow your pride and suppress your ego*. Meza ile unayoona wewe ndio sifa kwako na kandamiza yale kibri ya kibinadamu.

Mheshimiwa Spika, na mimi kwa kile alichokifanya mwanangu Halima Mdee nimeona kabisa amesimama kwenye busara za Mheshimiwa Mtemi Chenge. Halima Mdee amemeza kibri ya kibanadamu, amesimama kwenye Bunge

Iako hili Tukufu akaomba msamaha na sisi wote tuliokuwemo humu tuliguswa na maneno yake.

Mheshimiwa Spika, naomba tena tuwasamehe hawa kama ambavyo tumewasamehe wengine, nakushukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana, nilishawaona wote kabisa nitawataja tu hapa. Mheshimiwa Kangi Lugola atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba.

MHE. KANGI A. N. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu kwenye taarifa zinazohusiana na maadili kwa viongozi wa Serikali, ma-DC pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru sana kwamba Kamati iliweza kufanya kazi ambayo uliagiza kufanya na wamefanya kazi yao vizuri na wamewahoji watuhumiwa wote na kuja na mapendekezo ndani ya Bunge lako Tukufu. Pamoja na hayo, pengine yako mapungufu ambayo yapo kwenye ripoti hii.

Mheshimiwa Spika, mapungufu haya yanaonesha kuwemo kwa dalili za kigugumizi katika kutoa mapendekezo. Kuna maeneo mengine wamependekeza, maeneo mengine wamesema tunaleta Bungeni humu wajaribu kuangalia, hizi ni dalili za kigugumizi. Pengine kutokana na kigugumizi hiki inawezekana baadhi ya watuhumiwa humu wakawa wamebekwa kwenye kundi la kuadhibiwa na baadhi wakawa wamesamehewa, hizi ni dalili za kigugumizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nishauri jambo moja, kwamba jana ilikuwa ni Mei Mosi, Siku ya Wafanyakazi katika nchi yetu na leo ndio maamuzi haya ya maazimio yanatolewa kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, pia leo ilikuwa ni siku ambayo umelisifia Bunge lako Tukufu kwamba limesheheni wasomi,

limesheni watu mbalimbali wenye kada mbalimbali na ukasema huenda wakitu-rank kwenye taasisi katika nchi yetu na sisi tunaweza pengine kama sio kuongoza basi tukakaribia kuongoza. Hii ni ishara kwamba Bunge hili, ni Bunge ambalo linajengwa na Waheshimiwa ambaao ni waungwana, lakini wakati mwingine inaonekana ndimi zao huteleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa wale wote ambaao waliomba msamaha na tunakwenda kuwasamehe. Pia ili tufungue ukurasa mpya, na hasa maneno ya Halima Mdee ametugusa sana alipoamua sasa kuanza kumtanguliza Mungu mbele katika kumsaidia na kumuongoza asije akarudia tena, hii ni heshima kubwa sana. Kama imefikia hatua Mheshimiwa Halima Mdee anamkumbuka Mungu na kumheshimu Mungu, mimi nadhani Mheshimiwa Halima Mdee hatarudia tena na ninashawishi Bunge hili kwa kauli moja Mheshimiwa Halima Mdee na yeze aweze kusamehewa.

Mheshikiwa Spika, kwa kuwa pia Mheshimiwa Selasini ametukumbusha siku ile amekuja hapa kwa unyenyekevu mkubwa, akakuomba msamaha wewe binafsi Mheshimiwa Spika na Wabunge wote mpaka na wananchi wake wa Kawe, kitendo ambacho hapo nyuma Mheshimiwa Halima Mdee asingweza kufanya kama tunavyomfahamu. Hizi ni dalili kwamba sasa amejirekebisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bulaya amekaripiwa na ni jirani yangu pale, hili karipio hili na wewe Mheshimiwa Bulaya, mimi nilikuwa naomba Waheshimiwa Wabunge na huyu dada yetu tumsamehe maana yake karipio nayo ni adhabu. Huyu Mheshimiwa namuona siku hizi, na kama ripoti ilivyosema ameanza kujirekebisha, ameanza kuwa mpole, kwa hiyo, nilikuwa nawaomba Waheshimiwa Wabunge na yeze tumsamehe ili leo tufungue ukurasa mpya, kwamba hawa wote tumewasamehe wameingia kwenye kitabu cha utakatifu hawatarudia tena na hawatakuwa na makandokando. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nitoe angalizo moja kwa Waheshimiwa Wabunge na viongozi wa

Serikali na wananchi kwa ujumla, kwamba Bunge hili unapolikosea, unapomkosea Spika, unakosea Bunge unatakiwa kuomba msamaha kabla halijawekwa tishio lolote la kukuchukulia hatua. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, haya mambo ya kuwa kuna tishio la Kamati yetu ya Mheshimiwa Mkuchika inataka kukaa, ndipo sasa mnakuja humu mnaanza kulialia na kuomba msamaha wakati mwingine uombaji huu wa msamaha unakuwa unatoka hapa mdomoni, hautoki rohoni. Kwa hiyo, tuwe na *spirit*, unapojikuta umeteleza sisi ni binadamu, basi ndani ya siku hiyo au kesho yake, unakuja kutuangukia na kuomba msamaha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Peter Serukamba.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, Wabunge lazima tulionee sana vivu Bunge letu. Tunakumbushwa moja ya kazi kubwa ni kulionea vivu Bunge letu. Kulionea vivu maana yake ni nini? Lazima tulilinde Bunge hili lisidhalilishwe kwa namna yoyote ile, hii ndio kazi yetu ya kwanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini ili tuweze kuifanya vizuri kazi hii ni lazima sisi Wabunge tuheshimu sana kanuni zetu. Tulivyoanza Ubunge kitu cha kwanza tulichopewa ni kanuni. Niwaombe sana tuheshimu kanuni zetu. Tukiziheshimu kanuni na taratibu tulizojiwekea kwanza sisi hapa ndani nina hakika ule ulinzi wa Bunge letu tutaufanya kwa pamoja. Nilitaka nianze kusema hayo, lakini la pili nipongeze Kamati kwa kazi kubwa waliyofanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na mimi niungane na wenzangu tuanze upya. Tukubaliane wote leo, haya yaliyotokea wazungu wanasema iwe *wake up call*. Tudhamirie kama Bunge kwamba sisi Wabunge humu ndani tutaheshimu kiti cha Spika, tutawaheshimu Mawaziri, tutaheshimu Waziri Mkuu, tutaheshimiana Wabunge

wenyewe kwa wenyewe. Bahati nzuri kanuni zimetupa nafasi ya kila mtu kusema kwa wakati wake, kanuni imetoa nafasi ya kueleza unachotaka kukisema kwa kufuata taratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaamini tukizifuata taratibu zetu tutaheshimiana; na Waheshimiwa Wabunge tumekuja hapa kufanya kazi ya Watanzania. Ili tuweze kuifanya vizuri cha kwanza lazima tuweke *discipline*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na mimi niwaombe sana Waheshimiwa tumsamehe Halima Mdee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi kilichonigusa kwa Mheshimiwa Halima ni siku ile alivyokuja hapa ndani. Kwa wale ambao tumeanza na Mheshimiwa Halima siku nyingi siku ile mimi nilishangaa sana, ile *humidity* ni kubwa sana aliyoitoa. Aliomba radhi hata kabla ya kwenda kwenye Kamati, kwenye Kamati ameomba radhi. Sasa niwaombe sana wote, kwa maana ya *spirit* hii ya kuanza upya Mheshimiwa Halima, Mheshimiwa Ester, Mheshimiwa Freeman, wote tuwasamehe tuanze upya. Tukishawasamehe tukaanza upya sasa tufanye ile kazi ya kulilinda Bunge letu na mtu yejote wa nje asilidharau. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ningeomba nitoe angalizo na ningetamani Kamati wangelisema, kwamba nadhani umefika wakati tuwaombe wenzetu viongozi Wakuu wa Wilaya kote nchini, Wakuu wa Mikoa na Watanzania wote wauheshimu huu mhimili wa Bunge. Kama ambavyo na sisi tuna jukumu la kuwaheshimu Watanzania, kuheshimu Mahakama, kuheshimu *Executive* na sisi tuheshimiwe; tukienda hivyo, kazi ya kutafuta maendeleo ya Watanzania itakuwa rahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi leo asubuhi nimefarijika sana Mheshimiwa Spika uliposema kwamba Wabunge hawa sio wanaojua kusoma na kuandika. Mimi nimefarijika sana, hili sio Bunge watu wanaojua kusoma na kuandika, nadhani sisi

tunayo heshima kubwa zaidi na ndio maana wananchi walituchagua. Na wananchi wa leo ambao zaidi ya asilimia 70 ni vijana sifa haiwezi kuwa kusoma na kuandika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, narudia tena, niwaombe Wabunge tumsamehe Mheshimiwa Halima kama ambavyo tumemsamehe Mheshimiwa Freeman, tumsamehe Mheshimiwa Ester, ili tuanze upya, lakini niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge tuheshimu Kanuni zetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Hawa Ghasia, atafuata Mheshimiwa Bulembo.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na kuweza kusimama ili niweze kuchangia hii hoja.

Mheshimiwa Spika, sina matatizo na wale wote ambao wameenda mbele ya Kamati, na ningependa kuwapongeza kwa kazi nzuri waliyoifanya na kuomba msamaha bila kigugumizi. Kwa kweli, mimi naomba wasamehewe na wajiangalie na wajirekebishe ili yale ambayo wameyafanya yasiweze kujirudia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia napenda niungane na wale ambao wameomba Mheshimiwa Ester Bulaya asamehewe. Nilikuwa nasoma pale, naomba ninukuu aliyoyasema mbele ya Kamati:-

"Yawezekana ni muda mrefu sana nimesahau kutokana na hasira naweza nikawa nimefanya vitendo vya kuvunja Kanuni, nachukua fursa hii kuomba radhi kwa Kamati, Bunge, kwa yote yaliyojitokeza. Naomba radhi kwa moyo wa dhati kabisa. Sipendi kusumbua Kamati hii, naiheshimu Kamati, nimeona chochote nilichofanya kwa moyo wa dhati naomba radhi."

Mheshimiwa Spika, naomba kwa kweli na yeye asamehewe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia nirudi kwa ndugu yangu Mheshimiwa Halima Mdee; ameomba radhi, lakini ile radhi yake ya kimtego mtego. Naomba ninukuu maneno aliyoysasema:-

"Nitajitahidi kutorudia, ingawa ni ngumu sana ku-predict future itakuwaje. Kwa hiyo, naamini Mwenyezi Mungu ataniongoza kosa lisijirudie."

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ameomba radhi, lakini anaona ni ngumu sana huko mbele kama halitajitokeza na hii si mara yake ya kwanza kutokea mbele ya Kamati. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nimuombe Mheshimiwa Halima Mdee, nimemuona alikuja mbele ya Bunge, ameomba radhi vizuri na mimi nilifikiria ndivyo alivyoomba kwenye kamati, nikaona kama amefikia hapo Mhedshimiwa Halima kwa kweli, Mwenyezi Mungu amsaidie na amuongoze asirudi kule alikotoka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nakubaliana na wanaosema asamehewe, lakini ninachomuomba ile ya kwamba, ni ngumu itajirudia, basi hilo neno ikiwezekana, hata ndani ya Bunge aliondoe. Akiri, aombe msamaha, asamehewe na aahidi kwamba kitu kama hicho hakitatokea. Kwa sababu wewe Mheshimiwa Spika ni kiongozi wetu wa huu Mhimili, tusipokuheshimu sisi hivi nani atakuheshimu huko nje? Kama sisi unaotuongoza tunakudharau, nani atakuheshimu? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba Mheshimiwa Halima Mdee asamehewe, lakini aahidi kwamba hatarudia tena. Kwa sababu kama atarudia hiyo itakuwa kama ni mara ya tatu au sijui mara ya ngapi; na Mheshimiwa Halima Mdee ni Mbunge mzoefu, hii ni *term* yake ya tatu, kama ni mtoto zaidi ya miaka 12 kama ingekuwa ndio amezaliwa hiyo 2005. Kwa hiyo, niwaombee

asamehewe, lakini akiri kwamba hatarudia tena, asiseme yale maneno kwamba hii ni ngumu kwa hiyo hawezi ku-*predict*, ni kama vile anajiwekea akiba ya kuja kufanya vile ili ionekane kwamba alishasema huko mbele hajui kutakuwaje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na mwisho nimalizie kwa kumuomba Mheshimiwa Paroko, kumuomba Hajjat mwenzangu, Mheshimiwa Mama Shahari Mngwali na wanawake wenzangu kwamba tumsaidie Mheshimiwa Halima Mdee ili kile alichokiomba kile, kwamba Mungu amsaidie basi na sisi tumsaidie, ili asiweze tena kurudia au huko anakokuona kugumu basi Mwenyezi Mungu amfanyie wepesi, aendelee kuwa Mheshimiwa Halima Mdee aliyezaliwa upya ambaye anaheshimu Kiti na kuheshimu Kanuni ambazo tumejiwekea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Bulembo atafuatiwa na Mheshimiwa Janet Mbene.

MHE. ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Spika, na mimi nichukue fursa hii kuwapongeza Kamati kwa kazi kubwa waliyofanya, lakini mimi nitaanza kwa mzee mwenzangu Mheshimiwa Mzee Mbobe. Namheshimu sana, amefanya kubwa, unajua mtu mzima ukienda mbele kwa wazee wenzako ukasema nisameheni ni neno kubwa sana, nampongeza sana kwa ujasiri huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili nikupongeze wewe na uvumilivu wako. Unapigwa mawe unavumilia, ndio raha ya Kiti hicho. Lakini Kamati imefanya kazi na walio wengi wameomba msamaha.

Mheshimiwa Spika, mimi ninachotaka kusema, tukimtoa Mheshimiwa Mbobe, hawa waliobaki wote ni vijana hawa, si ndio jamani? Eeh, ni vijana na hawa vijana ndio Taifa letu la kesho...

MBUNGE FULANI: La leo.

MHE. ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Spika, leo ndio wanaanza, kesho wakati sisi tunapumzika wao ndio watakuwa mbele ya viti vilevile.

Kwa hiyo, nampongeza Ndugu Makonda kwa kuomba samahani, Ndugu Mnyeti, bwana harusi juzi ameoa, Kamati imemsamehe, mwanangu Mheshimiwa Ester Bulaya; ni ujasiri, hawa vijana wa leo kusema naomba samahani si neno dogo ni kubwa, lakini kama wamekiri wakaomba samahani naomba Bunge hili, kama alivyosema Baba Paroko, tuwavumilie, tuwarekebishe, tuwape msamaha wa dhati.

Mheshimiwa Spika, pia na wao wajue ni watoto basi, anapokuja mkubwa siyo masharubu yanakaa juu. Ukihaitwa mtoto huwezi kumsalimia mtu shikamoo halafu ukamtukana hapo hapo, hiyo si heshima unakuwa unamjaribu tu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nirudi kwa mdogo wangu Mheshimiwa Halima Mdee, nilitaka kuelekea alikosema Mheshimiwa Ghasia pale kwamba kama Mungu atanisaidia. Mimi huko nakuacha, siku ile amesimama hapa mbele akasema kwa kadri ya uwezo wake, ni kama kutubu, pamoja na kwamba Mheshimiwa Spika, hukuwepo, lakini alikuwepo Mheshimiwa Mtemi Chenge hapo, akaahidi kukufikishia, toba ile ni kubwa sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini tuseme wanaorudia makosa, mimi naomba pale mwishoni tuweke neno, umefanya kitubio, umesamehewa, je, ukirudia kosa turudie tena kuanza kusameheana hapa au tunaelekea wapi? Maana sasa tunaweka azimio watu wasamehewe, lakini kuna mara ya kwanza, mara ya pili, mara ya tatu. Sasa mara ya nne ule si msamaha maana umezoea. Sasa kwenye kuzoea pale siku ya mwisho mpekue vizuri vitabu; kwamba kosa la kwanza limeisha, la pili, lakini la tatu hili haliwezi tena kurudi kwenye kusameheana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kingine wewe ni mlezi wetu, ndiyo maana ukawa baba hapo, ukapata kura za kutosha ukawa kiongozi wetu, ukatulea, kila mtu unajua tabia yake. Mimi nasema vijana wetu hawa tuwasamehe, lakini kama walivyosema akinamama, kaeni na watoto wenu wamekuwa hatari kidogo.

Mheshimiwa Spika, maana Mheshimiwa mama Shahari uko hapo mwanao anatukana tu, ukienda nje humkanyi, humuiti, wakati mwingine ukimuita anakataa, kuna watu wazima, Mheshimiwa Mama Sitta mko humu, kaeni na mabinti zenu hawa, ingawaje wanaitwa Waheshimiwa. Kuwa Mheshimiwa si kitu, huwezi kufika hapa unatoka mbinguni, umefika pale kuna sababu zilizokufikisha pale; sasa tusivunjane heshima kwa sababu ukija humu utaomba samahani, hapana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yaliyopita si ndwele, nashukuru Baba Paroko tumeungana wote sasa humu kama wazazi. Basi na mabinti zetu sasa waichukue ile heshima wanayopewa ni dhamana kubwa, kukaa kwenye Bunge zima kama hili ikaandikwa kwenye Hansard umesamehewa inakaa kwenye kumbukumbu, sasa si lazima usamehewe kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba tuungane wote, wote wanaonesha huruma tutengeneze huruma hiyo. Zaidi nampongeza Mheshimiwa Mbowe kwa kukiri ndani ya Kamati. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Janet Mbene atafuatiwa na Mheshimiwa Mwakasaka, halafu Mheshimiwa simbachawene.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii nyeti iliyopo mbele yetu. Namshukuru Mungu sana kwa kunipa uzima na afya njema hata kufika kuongelea hili jambo.

Mheshimiwa Spika, haya mambo yanapotokea Bungeni yanatusikitisha sana, kwa sababu sisi kama viongozi ni kioo cha jamii. Sisi humu ndani majukumu yetu yanatuweka katika nafasi maalum na mahsus kwa Taifa hili, sasa inapotokea kuwa tunaonekana kuwa kama wahuni huwa inasikitisha sana. Inasikitisha kwa sababu unaona kabisa hili jambo linafanywa kwa makusudi, kwa sababu hata pale ambapo inaonekana kabisa mtu unakosea, unanyamazishwa, unatafadhalishwa bado unaendelea kufanya fujo na huombi msamaha mpaka ile siku ambayo unaitwa kwenye Kamati. Sawa umeomba msamaha, umekiri, umetubu, lakini je, inatoka moyoni? Ilibidi mpaka ifikie kwenye Kamati ndiyo tuanze kusema tunasameheana?

Mheshimiwa Spika, hebu tuangalie sasa jamani huko tunakokwenda, leo tunakubaliana tunatoa msamaha, wote tunakubaliana kwa sababu wote tunapenda kusamehewa tunapokosa, lakini kama makosa ni ya makusudi vilevile itafika mahali tuanze kufikiria, kweli huu ni msamaha wa kweli mtu anaomba au basi tu kuepusha tu shari ya ziada? Mimi nataka kusema hivi, kweli tumeambiwa kuwa wapo akinamama, wako wazee humu ndani tunaweza tukaongea na watoto wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watoto wenyewe wanakubali kuongea na sisi? Hao watoto watakubali kuongea na sisi? Kwa sababu kwa viburi wanavyovionesha na dharau wanazozonesha kwa Kiti kikubwa kama kile nani atakayethubutu kuwaweka chini aanze kuongea nao?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunachoomba sisi, kama kweli wameomba radhi na sisi tumekubali radhi yao basi sisi tutaomba kuendelea kukaa nao tupeane mawaidha kama wazazi na watoto ili tufanye kazi ambayo imetuleta humu Bungeni si kila siku kusuluishana migogoro isiyokuwa ya lazima. Kwa kweli heshima inanza na wewe mwenyewe, kama wewe mwenyewe hujiheshimu inakuwa sio rahisi kwa mtu mwengine kuku heshimu, lakini vilevile unapokuwa hujiheshimu na wenzio hapo ndipo tatizo linakuwa kubwa zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nataka kusema hivi; nakubaliana na wenzangu wote kuwa watu wamekuja kuomba msamaha, tumekubali tuwasamehe na wale ambao wameomba msamaha kwa kinyongonyongo kama ilivyopendekezwa waombe msamaha uliokamilika wasiweke *condition*. Kwanza wewe umekosa, kwa nini unaomba msamaha wa *condition* wakati yule anayekusamehe hajakupa *condition*? Tukubaliane wote tuache tunayotaka kuyafanya tukubaliane kuwa tutajitahidi kwa uwezo wetu wote kutokurudia makosa ili mwisho wa yote wote tufanye kazi iliyotuleta Bungeni. Lakini kwa kweli uvumilivu sasa utaanza kuwa mdogo kwa wale ambao kila siku ni hao hao wanaonekana wakorofi Bungeni, hata sisi mama zenu mwisho mnatutia aibu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nimalizie hapo. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwakasaka ni Mjumbe wa Kamati, Meshimiwa Kangi Lugola amesema mlikuwa na kigugumizi baadhi ya maeneo, Mheshimiwa Mwakasaka tafadhali.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniruhusu kuzungumza lakini pia mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo. Labda nianze na hili ambalo umelianza la Mheshimiwa Kangi Lugola.

Mheshimiwa Spiika, sisi mule kwenye Kamati, kwanza Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa tunafanya kazi hii kwa niaba yenu huwa hatuko pale kwa ajili ya kumuonea mtu, hata tofauti zetu zile za kisiasa mle huwa hazimo na ndiyo maana hatujawahi kufanya maamuzi yoyote mle ndani kwa kupiga kura. Pamoja na kwamba Kambi nyingine ipo mle, huwa tunakubaliana bila mashaka yoyote na hukumu hizi zote tulikubaliana.

Mheshimiwa Spika, lakini kitabu chetu hiki cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 74(4) inaturuhusu sisi au inatua madaraka sisi ya jambo fulani, pamoja na

mapendekezo tunaweza tukayatoa, lakini haitufungi sisi hii kutoa yale ambayo sisi tunaona yanafaa na ninyi mnakuwa watu wa mwisho kuyaridhia. (*Makof*)

Mimi nzungumzie kuhusu suala la Mheshimiwa Halima Mdee; tumeangalia mambo mengi mle ndani. Kwanza unaangalia kwa kawaida kwa sababu sisi ni kama mahakama ndogo, tuko mle ndani kama *quasi-judicial*, tunaangalia mambo mengi, *motive* ya yule mtu. Hawa watuhumiwa wote wanaitwa mashahidi mle, tunaangalia ile *intention* yake anapokuja pale hata kujieleza *body language*, je, anachozungumza ndicho kilichopo, tunaangalia mambo mengi.

Mheshimiwa Spika, sasa mnaweza mkaona wote tumewasamehe lakini kwa Mheshimiwa Halima Mdee tumependekeza adhabu hiyo, ni kwa sababu ya mwonekano wake wa ushahidi alivyokuwa akitoa mle ndani ni tofauti kabisa na wengine. Kwa hiyo, bila hata kupiga kura sisi wote kama Kamati tulikubaliana adhabu hiyo, lakini humu ndani ya Bunge ndio waamuzi wa mwisho. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna swali pia ambalo tulijiliza, kwamba je, kama kila mtu atafanya makosa humu ndani ya kukikosea Kiti, kuwakosea Wabunge wenzake halafu akachukulia kigezo cha kwamba si nitaenda kuomba msamaha itakuwaje? Wote waje na misamaha hiyo hiyo. Kwa sababu Waheshimiwa Wabunge msisahau hapa kisheria tunatengeneza kitu kinachoitwa *precedent*, tunatengeneza hukumu za nyuma hapa, hiki tuakachofanya hapa tayari maamuzi haya ndiyo itakuwa kwenye Kamati ile ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge itakuwa ni miongozo yetu ya kutuongoza kwa wengine kama watafanya makosa kama haya. Sasa mimi nasema kwa jinsi tunavyofanya maamuzi mle ndani Mheshimiwa Mdee kwa kweli hakuonesha kuwa sawa na wengine. Nikisema hivyo mnanielewa kwa sababu imesomwa, wengine walionesha kwa dhati hata ukiwaangalia tu unawaona hawa kweli walikuwa wanakiri. (*Makof*)

Mheshimia Spika, lakini kwenye sheria hiyohiyo kuna muda mtu anakaa wa kufikiria, pamoja na kwamba ameshawahi kufanya makosa kama haya bado amekuwa akiendelea, na mara nydingi Mheshimiwa Spika unawasamehe hapa mpaka wakati mwengine unajaribu mpaka unajifyonya hapa kwamba jamani, lakini tuheshimiane, tunawaona.

Mheshimiwa Spika, sasa kama tutaendelea huku kwenye suala la kusema kwa kuwa kaomba msamaha na wengine wako Maparoko hapa, tunashukuru, ni vizuri wangkuwa wanatusaidia kurekebisha hizi tabia, kwa sababu sisi hatuhitaji kumkomoa mtu, sisi ni kurekebisha ili Bunge liwe na nidhamu inayotakiwa. Lakini kama kigezo kitatumika kwamba mtu kwa sababu kaomba msamaha bila kuangalia *motive* sjui kama tutafika, mimi naona bado yale maamuzi ya Kamati yako sahihi. Naomba niishie hapa. (*Makof*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOANAN SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, mimi nimesimama kwanza kabisa kuipongeza Kamati, imefanya kazi nzuri, ni kazi ndefu na hukumu hizi ni hukumu za kisheria, kwa hiyo, ni kama tafiti hivi zimefanyika na pia wamerejea mambo ya nyuma, kwa hiyo wamefanya kazi kubwa kweli nawapongeza sana.

Mimi nilikuwa najiuliza, hivi tumefikaje mpaka tunafika hatua hii ya maneno yanayotolewa kuwa yanakiuka au kugongana au kugombana na pengine wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika umepata shida sana na haya na kesi kama mbili hapa zinakuhusu wewe.

Mheshimiwa Spika, mimi nalionna tatizo, na msisitizo wagu mkubwa upo kwenye tatizo la kuzingatia Kanuni. Sehemu ya Tano na Sehemu ya Sita ya Kanuni hizi zimeeleza vizuri sana namna ya ku-*behave* kama Wabunge na namna ya kuendesha mijadala na shughuli zote ndani ya Bunge na hata pengine shughuli zinazowagusa watu wengine nje ya Bunge. Endapo haya yakizingatiwa hatutakuwa na matatizo makubwa ama na Kiti au na watu walioopo nje.

Mheshimiwa Spika, tunapata matatizo haya leo kwa sababu wako watu wengine kwa makusudi tu, wanazijua Kanuni wanaamua kutokuzifuata. Sasa kama mtu anajua hiki kitu hakiruhusiwi na mtu huyo ni kiongozi siyo mtu wa mtaani tu, kwamba ni mtu wa kawaida, ni kiongozi na kama ulivyosema Bunge hili limesheheni wasomi wakubwa kabisa kweli kabisa, ukiweka Taasisi ukaunganisha *degrees* zilizoko hapa ndani ni shughuli kubwa ni taasisi ambayo kwa kweli ina *reputation* ya hali ya juu sana. Sasa lazima tuoneshe haya hata katika kuzingatia utaratibu tuliojiwekea wa Kanuni.

Mheshimiwa Spika, kwa humu ndani nitoe rai kwa wenzangu tuzingatatie maelekezo ya Kanuni na hasa Kanuni ya 64 maana Kanuni zile zote zimeeleza utaratibu mzima wa namna ya kuongea na unaposema kitu lazima kisimuudhi mtu mwingine, kisimkere mtu mwingine, lakini mtu kwa makusudi anasema. Ni lazima Kanuni hizi pia tuone haja ya kuzipitia upya tuziongezee vitu vya ziada. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa vitu vinavyowagusa watu waliopo nje ya humu, wanaweza wakawa wafanyabiashara, wanaweza wakawa viongozi unapozungumzia Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya ni Kiongozi. Kwa mujibu wa Kanuni hizi hasa Kanuni ya 64, inasema namna ambavyo Mbunge anatakiwa kutoa lugha inayohusu watu hata walioko nje. Kwa mfano, Kanuni ya 64(f) inasema:-

"Mbunge (f) hatamsema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwingine ye yeyote." Kwa hiyo, unapozungumza uwe na *reserve* kwamba unamzungumza mtu mwingine na yeye ni binadamu. Hii itatusaidia sana kwa sababu kanuni zinataka tusizungumze ovyo ovyo tu.

Mheshimiwa Spika, *reaction* zingine tunazozipata zinatokana na aina ya uzungumzaji inaweza ikawa *massage the same*, mazingira ni yale yale ikasemwa na ikafika kwa maudhui yaleyale, lakini namna sasa ilivyozungumzwa mpaka ina-excite watu wengine. Kwa mfano, mazungumzo ya kwenye *facebook*, ukiangalia hapa DC Mnyeti anaposema, upuuzi mtupu, Wabunge hawa hawajielewi,

nawashauri fanyeni kazi zenu za wengine waachieni wenye. Ni-flowya *comments* zilizokuwa kwenye *facebook*, sasa aliyeokuwa anazisema huku hajazungumziwa kwamba ilikuwaje mpaka huyu afike aseme hivyo, *and it was very specific na waliokuwa wanazungumza naye kwenye comments* hizo wanajulikana. Ingawa sasa imechukuliwa kwamba hii yote ni kulidharau Bunge kumbe ni *specific, individuals* ambao ni Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni kweli leo hii Bunge limefanya kazi yake na kuunda Kamati na uchunguzi umefanyika na watu wamekiri wamefanya jambo zuri sana na tunawapongeza sana wote. Nitoe rai kwa sisi Viongozi tunapozungumza tujue kwamba tunapaswa kuwa na *reserve*, tuzungumze kwa nidhamu na wenzetu huko nje na wao ni viongozi.

Mheshimiwa Spika, nataka tu niliseme hili, kwa sababu pia ni muhimu kwamba tukizingatia Kanuni zetu tunakuwa salama zaidi. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Simbachawene ukumbuke katika Maazimio haya liko moja la kwako pia la kushughulika nalo, lakini muda bado unao. Mheshimiwa *Chief Whip*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Spika, nami nianze kwanza kwa kukupongeza sana kwanza wewe binafsi. Hatukufanya makosa kukuchagua kuwa Spika wa Bunge hili. Kadri tunavyokwenda umezidi kuonesha ukomavu wa hali ya juu na baba unayeweze kuongoza mhimili huu. Katika kujadili na kushughulikia hoja hii, naomba niseme nakupongeza sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nitende haki kwa Kamati ambayo imeleta hii hoja leo mbele ya Bunge lako Tukufu. Kamati kwa mara nyingine, siyo kwa mara ya kwanza, ni kwa mara nyingine, imeendelea kuonesha, ulipokuwa unaiteua kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane ya Kanuni zetu za Kudumu za Bunge Kifungu cha Nne, Kifungu kidogo (1),

(2) na (3) ulifanya uteuzi muafaka wa Kamati hii ambayo imeleta hoja yetu mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo, naipongeza sana Kamati yako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati hii kama nilivyosema ile Nyongeza ya Nane, Kifungu cha Nne, Kifungu kidogo (1), 2 na (3) imetekeleza kazi yake ya awali na Kanuni inakwambia, baada ya kupokea ile taarifa ya Kamati yako hii, utaleta taarifa kama hoja ndani ya Bunge. Hoja hii ikishawasilishwa ndani ya Bunge sasa Wabunge wana kazi moja ya kuiamua.

Mheshimiwa Spika, nimewasilikiza sana Waheshimiwa Wabunge na wote wamechangia na wala sina shida na michango yao, kimsingi naomba niseme kwa yaliyojiri, naomba nimpongeze sana Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwa ushirikiano mkubwa alioutoa kwenye Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Paul Makonda kwa ushirikiano mkubwa alioutoa ndani ya Kamati hiyo. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Ester Bulaya, mdogo wangu, kwa kuanza kukua na kuonesha ushirikiano kwenye Kamati hiyo na najua Mheshimiwa Riziki ataendelea kumkuza zaidi. Naomba nimpongeze Mheshimiwa DC Mnyeti kwa ushirikiano mkubwa aliouonesha kwenye Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, tunarudi kwa Halima Mdee pamoja na kutokuonesha ushirikiano kwenye Kamati, Halima Mdee pia alionesa ukomavu na kuja kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 57 hoja ilioletwa ndani ya Bunge hili hatuwezi kuiamulia bila kuleta hoja nyininge, ili hoja hii ilioletwa na Kamati iweze kubadilika na kuendana na mtazamo wa Wabunge ni lazima Kanuni ya 57 ichukue nafasi yake. Kanuni ya 57 nikusomea hapa kidogo kwa manufaa ya Waheshimiwa Wabunge inasema:-

"Hoja ikishatolewa ili iamuliwe inaweza kubadilishwa kwa:-

- (a) kuondoa maneno fulani kwa ajili ya kuingiza maneno mengine;
- (b) kuondoa maneno fulani bila ya kuongeza mengine; au
- (c) kuingiza au kuongeza maneno mapya."

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge hapa wamezungumza sana, wameridhishwa na *spirit* ya Bunge lako Tukufu jinsi tunavyokwenda, tukiamua kusahau yaliyopita lakini kuangalia yale yajayo.

Mheshimiwa Spika, naomba tu niseme jambo moja, kwa *spirit* hiyo ya kuangalia yale yajayo ni lazima tuendelee kukumbushana Waheshimiwa Wabunge kwamba, Kanuni hizi ziendelee kutuongoza kuyasahau yaliyopita lakini kuyangalia yajayo. Kwa hiyo sasa kuanzia leo ni lazima Wabunge waheshimu Kanuni za Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ili sasa twende sawasawa, naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu waridhie sasa, niweze kutoa hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 57 ili tufanye mabadiliko ya hoja na hasa adhabu zilizotolewa katika Kamati huku tukiwa tumewapongeza na kuwaheshimu sana Kamati kwa maamuzi waliyoyachukua na hatua waliyoifikia mpaka sasa. Vilevile, tukiendelea kukumbushana Waheshimiwa Wabunge wote kwamba msamaha huu wa leo siyo tiketi ya kuwafanya Wabunge waendelea kukosea halafu wasamehewe tena ndani ya Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, watambue, Spika una heshima yako hapo mbele na anayemdharau Spika ametudharau Wabunge wote. Watambue tunapaswa kwa mujibu wa Kanuni kuheshimiana sisi kwa wote tena pande zote mbili. Hivyo naomba nisome maneno yafuatayo ili kubadilisha hoja ya Kamati na Bunge liweze sasa kuhitimisha hoja hii kwa

mujibu wa Kanuni baada ya kuchangia na kutoa mawazo ya kimsingi kabisa leo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nitoe hoja kwamba, maneno yaliyomo katika azimio linalomhusu Mheshimiwa Halima James Mdee yabadilishwe kutoka ilivyo sasa kwa kuongeza maneno yafuatayo ambayo nitayasoma huko mbele.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tarehe 25 Aprili, 2017 Mheshimiwa Halima Mdee aliomba radhi ndani ya Bunge hili Tukufu na kwa kweli Kamati ile ilifanya kazi kwa niaba ya Bunge hili Tukufu. Kwa kuwa, Mheshimiwa Halima Mdee hilo ni lazima niliseme alikwishafanya kosa kama hili la kudharau mamlaka ya Spika na kusimamishwa kutohudhuria vikao vyote vilivyobaki nya Bunge la Bajeti, 2016, kwa hiyo, ni lazima tuendelee kukumbuka huku tukiendelea kuzingatia msamaha aliotuomba.

Mheshimiwa Spika, naomba kufanya marekebisho kwa mujibu wa Kanuni ya 57(1) na kuondoa maneno ambayo yanasmeka katika Azimio hilo na nitaomba kupendekeza hoja ya mabadiliko ili kuweka maneno mengine kwa mujibu wa Kanuni hiyo.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Bunge kwa mujibu wa taarifa ya Kamati, liliombwaliazimie kwamba Halima James Mdee, Mbunge asihudhurie vikao vyote vilivyobaki nya Mkutano wa Saba wa Bunge la Bajeti yaani Mkutano huu kuanzia tarehe ya Azimio hili la Bunge kutokana na tabia yake ya mara kwa mara ya kufanya vitendo nya kudharau mamlaka ya Spika kwa kutoa lugha za matusi na lugha ya kuudhi.

Mheshimiwa Spika, naomba nibadilishe Azimio hilo kama ifuatavyo kwa kuweka maneno yafuatayo:-

Hivyo basi, naomba Bunge liazimie yafuatayo: Mheshimiwa Halima Mdee asamehewe kosa alilolifanya, ila tu iwapo atatenda kosa lingine la kudharau mamlaka ya

Spika au kufanya kosa lingine lolote la uvunjifu wa Kanuni za Kudumu za Bunge na Kifungu cha 26(b) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki ya Bunge, Sura ya 296. Utekelezaji wa adhabu uanze mara moja akirudia kosa tena kama hili kwa maelekezo ya kiti cha Spika tena bila hata kuitisha Kamati ya Maadili. Hivyo, tutakuwa tumefanya nafasi nzuri ya kumsamehe Mheshimiwa Halima Mdee na kuweka utaratibu wa kuheshimu Kanuni ndani ya Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lengo langu ni kuzingatia uungwana mkubwa aliuonesha Mheshimiwa Halima Mdee, ameonesha uungwana mkubwa wa kuomba radhi ndani ya Bunge, lakini tuendelee kutambua mtiririko wa shughuli nzima ya Kamati ya Maadili mpaka tunapofika hapa Bungeni, lengo langu ni kuiomba Kamati ya Maadili isamehe yale maneno aliyoatumia Mheshimiwa Halima Mdee ndani ya Kamati ya Maadili, lakini izingatie maneno aliyoatumia Halima Mdee wakati akiliomba Bunge lako Tukufu radhi kwa niaba yako wewe na Kamati ya Maadili.

Mheshimiwa Spika, hivyo Maazimio haya yanapendekeza Halima James Mdee asamehewe, lakini mabadiliko yangu hayo yachukue nafasi ya mapendekezo ya adhabu ambayo Halima Mdee alipewa na Kamati ile ili aweze kuondoka na Halima Mdee aendelee na shughuli za Bunge katika Mkutano huu na Mkutano ujao utakapofika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono, kiutaratibu tutaanza kwanza kuiamulia hii hoja ya rekebisho kama ilivyosomwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Nafikiri wote tumeielewa.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Hoja ya kubadilisha Maazimio ya Kamati kama ilivyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu) ilikubaliwa na Bunge)

SPIKA: Kwa hiyo, mnataka adhabu hiyo ibakie kama ilivyopendekezwa na Kamati? Walioafikiana na Mheshimiwa Waziri wa Nchi wameshinda. Hivyo, kutakuwa na badiliko kama alivyolisema. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ili ahitimishe hoja yake, ukiweza kutozidi dakika 15 tutashukuru. Karibu hapa mbele Mheshimiwa Maige. Karibu sana Mwenyekiti.

MHE. ALMAS A. MAIGE – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE: Mheshimiwa Spika, naomba sasa nihitimishe hoja yangu inayohusu mashauri haya matatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nieleze kazi kubwa ya Kamati kama ambavyo inaletwa kwetu na Mheshimiwa Spika kwa Kanuni zetu tulizojiwekea pia nikiri kwamba Kamati yangu inafanya kazi kubwa sana ya kuchunguza matukio na masuala yote yanayoletwa kwetu hatukurupuki.

Mheshimiwa Spika, katika masuala haya matatu tulipata mtihani mkubwa sana. Tulipata mashahidi wa aina mbili, mashaidi kutoka nje ya Bunge ambao siyo Wabunge na mashahidi ambao ni Wabunge. Mashahidi wote waliotoka nje ilikuwa ni mara yao ya kwanza kufanya makosa. Mashahidi waliotoka ndani walikuwa na makosa ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imejadili mashahidi wote, maamuzi ya Kamati ni kama ambayo mmeyaona tumewasilisha leo. Hata hivyo, likatokea tatizo la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge ambaye ndani ya Kamati, Kamati ilimwona ana kosa la *mens rea*. Kamati tunafanya kazi kama *Quasi-Judicial* tulimwona ana makosa ya

kukusudia. Pia Mheshimiwa Halima alishindwa kuomba radhi hata baada ya kuongozwa (*lead questions*) ili akiri kwamba hatarudia tena na akatupeleka kwenye imani ya dini mbalimbali ndani ya Kamati. Tulikuwemo Wakristo, tulikuwemo Waislam na kila mtu ana Mungu wake. Kwa hiyo, alipoweka neno la Mungu mbele likatuchanganya tukaona kwamba haliwezi kuamuliwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifikia kumpa adhabu ndogo kuliko ambayo aliipata kwa kosa kama hili kipindi cha nyuma. Mheshimiwa Halima amewahi kusimamishwa Mabunge mawili lakini tukampa Bunge moja hili na siyo siku zote.

Mheshimiwa Spika, hivyo, tulifirkiria na tulishangazwa sana na Mheshimiwa Halima alipokuja humu ndani na kuomba radhi kama mtoto mlocole, kule ndani illkuwa tofauti. Amekuja kuomba radhi hapa baada ya hukumu kutolewa na hukumu ikajulikana. Hatuna uhakika, narudia tena Mheshimiwa Spika kwamba hatuna uhakika kama radhi aliyoiomba Mheshimiwa Mdee humu ndani ilitokana na busara yake mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati yangu haikuweza kukaa tena, kwa sababu huko nyuma tumeshakaa, tumeamua hukumu bado kusoma tu, nasi hatukai mpaka kwa amri ya Mheshimiwa Spika ndipo tukae. Baada ya kukaa na kumaliza shauri lote Mheshimiwa Halima Mdee akaja kuomba radhi kwenye aneo nje kabisa na Kamati. Ingawa alisemea humu ndani Wajumbe wa Kamati wengine hawakuwepo, walikuwa nje kikazi na wengine hawakusikia kama aliquwa anaomba radhi Kamati au aliquwa anaomba radhi Bunge na akatamka kwamba kuna watu *individual* amekwenda kuwaomba msamaha. Tumeepata taabu kuiandika upya hukumu yetu na hili ndilo tatizo limefanya tuisome hukumu yetu kama tulivyoleta.

Mheshimiwa Spika, Mashahidi wote wamesamehewa, isipokuwa tumeona Mheshimiwa Ester Bulaya apewe onyo tu basi, hili ni kosa la pili kwa Mheshimiwa

Ester Bulaya, katika makosa haya tulimtia hatiani kwa kosa la kutupa vitabu kama dhara na hilo tukasema linaweza kusamehewa. Pia aliomba msamaha asamehewe ndani ya Kamati. Hili tulilikubali na tukakubali kwamba Kamati inafanya kazi kwa kusameheana.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba yako tulifanya kazi hii kama ulivyo tuagiza na mwishoni leo, pia nakiri kukubali mapendelekezo ya mabadiliko katika Azimio linalomhusu Mheshimiwa Halima na kuindoa adhabu ambayo tulikuwa tumeiweka kama Kamati. Sasa nashauri Bunge lako likubali mabadiliko ya kutoka adhabu kuwa msamaha kama ambavyo yameletwa na *Chief Whip* wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda sana kukuachia muda wako, Kamati ya Haki na Maadili na Madaraka ya Bunge tunaunga mkono mabadiliko ya Azimio.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imeungwa mkono, sasa naomba niwahoji kwa ujumla wake kuhusiana na hoja hizi za Kamati pamoja na marekebisho yake ambayo sote tunayaelewa jinsi yalivyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Maazimio ya Kamati ya Maadili, Haki na Madaraka
ya Bunge pamoja na Marekebisho yake
yalipitishwa na Bunge)*

SPIKA: Wote kabisa mmeafiki. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa kulifikisha jambo hili hapa. Katika kumalizia hapa tuelewane jambo moja, kwamba Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe amesahemewa bila masharti yoyote. Waheshimiwa Paul Makonda na Mheshimiwa Alexander Mnyeti wamesamehewa bila masharti yoyote. Mheshimiwa

Halima Mdee amesamehewa lakini kwa sharti la kwamba akifanya kosa lingine lolote atapata adhabu bila kulazimika kumpeleka kwenye Kamati ya Maadili, itakuwa ni moja kwa moja. Kwa hiyo, amesamehewa lakini kwa masharti hayo. Mheshimiwa Ester Bulaya amesamehewa lakini bado anatakiwa kuandikiwa barua ya onyo kwa sababu pendekezo lake halikubadilika. Hapo ndipo tulipofikia, tuelewane kabisa (Makofi).

Waheshimiwa Wabunge, sasa katika kufikia hapo niseme ya kwangu haya, kuna wakati kitambo sana nimewahi kusoma kitabu cha *Autobiography* ya Nelson Mandela, *The Long Walk to Freedom* na naamini wengi mmesoma. Nilisoma siku nyingi sana, lakini nakumbuka mahali fulani ambapo yule Mzee wakati wa miaka ile ya 1960 anahangaika na ile '*Umkhonto we Sizwe*' Umoja wa Vijana ule ulloamua kuingia katika mapambano ya silaha, wakati huo ye ye amefikia katika kiwango cha kuwa na elimu ya digrii ya kwanza ya sheria na miaka ile kwa Mwanasheria wa kiwango chake alikuwa na uhakika wa maisha mazuri, bado aliamua kuyaacha hayo maisha mazuri akaingia katika *struggle* kwa ajili maisha mema na maboresho ya demokrasia katika nchi yao ya *South Africa*. Kwa hiyo, akawa anajificha wakati fulani, wakati wa mchana ili usiku wafanye hujuma fulani fulani, wakati wamekubalia sasa kwamba waingie katika mapambano.

Waheshimiwa Wabunge, nayaeleza kwa kifupi sana. Sasa katika kujificha kwake wakati fulani alikuwa kwenye lile shamba ambalo ndilo alikuja kukamatwa, linaitwa Rivonia. Shamba kama la mifugo hivi, liko karibu na Jiji la Johannesburg. Akawa anajificha kule kama kibarua wakati wa mchana lakini usiku wanafanya shughuli zao wanazozijua. Sasa wakati ule wa mchana akijificha, moja ya kazi aliyokuwa anaifanya ni kuhudumia vibarua wa shamba. Wanawagawia uji, wanagawa chakula alikuwa mmojawapo wa wale wanaogawa. Sasa wale vibarua wanajiona ni wa juu zaidi, wale wanaogawa chakula wanawaona ni wa chini zaidi. Hivyo wanapowapa chakula wengine wanamwita wewe pumbavu weka chakula hapa,

wewe mjinga fanya hivi. Sasa akawa anawaza mimi nahangaika kwa ajili ya hawa watu, lakini wao wenye we wala hata hawawaheshimu wenzao.

Kwa kifupi, nataka kusema kwamba Waafrika bado tuna changamoto moja kubwa sana ya kutokujifunza kuheshimiana, sisi tunadharauliana sana kupita kiasi! Sijui ni mila au sijui ni desturi, sijui ni nini? (*Makofi*)

Mama yake Halima Mdee alinipigia simu mara kadhaa akitaka kuja kuniona, nikamwambia wala hamna neno mama, haya mambo tutayamaliza tu, lakini nawe kosa lako pia ni malezi. Inaelekea kuna mahali hukutimiza wajibu wako vizuri. Pia huwezi kumlaumu mama moja kwa moja, wakati mwингine watoto nao wanajifunza barabarani huko kuwa na tabia za ajabu maana sisi wote wazazi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, maana yake siyo lazima awe ni Spika au ni nani, kwa neno ambalo alilisema Halima Mdee humu ndani, Kamati imeenda kwenye tafsiri ikachukua kamusi, kwa neno lilelile alilosema, ambalo maana yake huyo mtu unayemwambia “fala” ni mtu ambaye akili zake hazifanyi kazi vizuri, ni mtu mpumbavu, ni mtu bwege, ni mtu mjinga, ni mtu bozi, ni gulagula.

Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana nikasema, sisi Waafrika hata kama humpendi namna gani mwenzako huwezi kumfanya hivyo. Mradi tu yeye ni binadamu, huwezi kumfikisha hapo. Sijui awe amekufanyaje, labda awe amekubaka, au nini, labda unaweza ukasema namna hiyo. Vinginevyo *you don't do that*. Kwa hiyo ame-step over! Ni mtu ambaye kwa vyovyote vile kwa mtu wa kawaida lazima utampa adhabu. Ni busara kubwa ya Bunge hili na wote ambaao mmezungumza, kwamba kwa mtu ambaye amefanya makosa makubwa namna hii, kwa kweli adhabu yake ni kusamehewa. Ndiyo adhabu yake hasa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo ni matumaini yangu kwamba *Caucus* ya Upinzani ya Wanawake mtakaa na mwenzenu huyu na kuzungumza naye, whether

atawasikiliza au hatawasikiliza, mjenge utamaduni huu na *Caucus* ya CCM pia kwa wale ambao ni wakorofitujenge utamaduni huo pia wa kusaidiana. (*Makof*)

Wengine ni Viongozi, huyu ni Mwenyekiti wa Wanawake wa CHADEMA, una-*send* picha gani kwa wanawake nchi nzima ambao wamekuamini wewe kuwa kiongozi wao, kuna wakati unamwangalia mtu unamwonea huruma, kwa sababu hajitambui, hajielewi kabisa, dhamana aliyonayo na aliyoibeba. Wanawake ni wapiga kura wengi nchi hii, sasa Chama cha Siasa ambacho kina-*risk* namna hii ni hatari sana.

Tukija kwa Kiongozi wa Upinzani na yeye, siku ile ya uchaguzi ule akasema Spika amevuruga Kanuni za Bunge. Hivi leo tujiulize, kwenye uchaguzi ule Spika alivuruga Kanuni gani? Kanuni namba ngapi? Akasema, sheria hazikuheshimiwa, zippi? Ubabe umetumika, ubabe gani? Ninyi ni waumini wa demokrasia na wengine mnajiita Chama cha Demokrasia. Umeleta mtu wako kwenye demokrasia hakupata kura kwa uwazi, unaona watu wanapiga kura na wewe unaenda kuhesabu, unaona kabisa hazikutosha. Halafu analaumiwa Spika ambaye hana kura. Maana yake kwenye uchaguzi ule Spika hapigi kura, hata kura moja hana yeye, lakini sasa ukiwa hapa ndiyo wewe unakuwa jalala? (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, hivyo jamani, tuwe na kiasi katika mambo haya na maneno yanayozungumzwa katika maandiko yanasema tuchukuliane, tukichukuliana tutafika vizuri zaidi na salama zaidi.

Kwa hiyo, binafsi yangu naungana na ninyi wote katika kuwasamehe wenzetu wote, kama walivyosema baadhi, tukianza wenyewe kuheshimiana humu ndani itatusaidia sana na kule nje wenzetu kutuheshimu kama mhimili. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge pia nisemee baadhi ya maneno ambayo yamekuwa yakisemwa katika hotuba

ambazo zinasomwa humu ndani na kipekee hotuba za Upinzani kuhusu kudharau Kiti na kudharau Bunge. Nimefanya utafiti wangu, kwa mfano; siku moja alisoma hotuba Dada yangu Ruth Mollel. Mheshimiwa Ruth Mollel namfahamu ni mtu *Senior* hata kwangu mimi, ni mtu mwelewa sana, ni mtu *measured*. Yale maneno yaliyokuwa yameandikwa mle, najua kabisa Ruth Mollel hawezi kuyaandika, kuna mtu anaandika mahali na nilimwambia siku ile.

Kwa hiyo, nikafanya utafiti wangu, nikagundua kwamba, kama nilivyosema siku ile nilivyohisi, kwenye Ofisi ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni kuna vijana wanne, Onesphory Mbuya, Olivia Mwikila, Jonathan Wilfred na Doris Cornell. Vijana hawa waliombewa na Kiongozi wa Upinzani Bungeni kwamba wanahitaji kuongeza nguvu kidogo ya vijana kwa ajili ya kufanya utafiti na kusaidia katika *ku-draft* mambo mbalimbali *including* baadhi ya taarifa ambazo zinasomwa hapa.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hawa tunawalipa sisi Bunge, kwa maneno mengine nawalipa mimi, halafu wanakaa, wanaandika hotuba za kunituhumu mimi tena hapa, *how!* (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mimi sijawahi kuona vitu vya namna hiyo! Nanyi hamkai mkawaambia hawa watoto, siku hizi ajira hakuna. Hivi wewe unamtuhumu mwajiri wako tu kizembezeme unafikiri.... Uliona wapi duniani kitu kama hicho? Mliona wapi? (*Makofi*)

Kwa hiyo, nawaambieni ndugu zangu, nimewahi kusimama hapa kusema tena na tena, lakinisasa nimechoka, sasa tutaanza kuchukua hatua. Hawa nao nawasamehe kwa leo. Ni mambo ya ajabu, ya kijinga kabisa. Pili, wewe unayekuja kusoma hotuba hapa, isome hiyo hotuba yako wewe mwenyewe. Ukija hapa na kuanza kutuhumu Bunge hovyo, unatuhumu Spika hovyo, mimi nakuva wewe mwenyewe kwamba hayo ni ya kwako. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hatuwezi kwenda hivyo! Kuifanya Taasisi hii kila mtu tu anaropoka anavyotaka. Utatakiwa ututhibitishie hayo unayoyasema hata kama ni maoni ya Kambi. Mengine unaweza ukayasema lakini kama ni kuhusu Taasisi hii hatuwezi kuruhusu mtu ye yote kuipaka Taasisi hii anavyotaka, anavyojisikia, *we cannot do that*. Tatalinda kama mlivyosema leo kwa wivu mkubwa hii Taasisi ili ijenge heshima yake. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kama mna jambo lolote tuna vikao vingi semeni. Kiongozi wenu wa Upinzani ni Mjumbe wa Kamati ya Uongozi, ni Mjumbe wa Kamati ya Kanuni, ni Mjumbe wa Tume. Katika Uongozi wa Bunge hili, kwa maana ya Wabunge, nikishatoka mimi na Naibu Spika, anafuata yeye katika Uongozi. Kwa nini yeye mambo yanakuja tunatuhumiwa hapa, maana yake ni kwamba yeye anawatuma basi wakati yeye ni sehemu yetu. Mbona sisi hatujawahi kusimama tumtuhumu yeye? Hatuwezi kwenda hivyo. Lazima tufike mahali ambapo tunakwenda kwa utaratibu na kuheshimiana na kuchukuliana, kama kuna neno tuambiane tu.

Waheshimiwa Wabunge, mwisho tuwe tunakumbuka ndugu zangu, huyu Spika tunayejaribu kumdhara baadhi yetu, kama mlivyosema wengine ndiye baba yetu, mambo yako hapa yakikwendea mrama, vyovoyote vile utarudi kwake yeye. Ukiugua hapa, ikibidi sijui nini hapa, ukifanya nini hapa. Sasa huyo unayemtukana na kumdhara hivi naye akichukua moyo wako wewe, kama alivyosema Mheshimiwa Magufuli kule Zanzibar, wewe unaleta ya kuleta halafu mkono wangu huu uidhinishe wewe uende India wewe? Tusipende mambo mengine ya ovyo, tujenge mahusiano, tufanye kazi vizuri. *After all* mbona kule *canteen* na mahali pengine tunapendana? Mbona kwenye Kamati mnafanya kazi vizuri, kwa nini ikifika hapa tu? Kwa hiyo, hapa napo lazima tutafute namna ya kufanya kazi vizuri, kwa pamoja, bila chuki. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana, naipongeza sana Kamati yetu ya Maadili, Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe, muendelee kutusaidia.

Ningependa sana kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, tujitahidi sana kuepuka kuingia katika matatizo kwa kusoma Kanuni zetu vizuri na kuzielewa. Huwezi kuzikariri zote, utakosea hapa na pale, wala haina neno, utakapoombwa urekebishe, unarekebisha, ndivyo Mabunge yote yapo hivyo. Siku hiyo ukizidiwa sana umehemka, ni kawaida katika maisha. Tukakuomba Mheshimiwa hebu toka nje kidogo ukapumua, basi unakusanya vitu vyako unatoka kwa usalama tu, huna haja ya kugoma, mpaka aje *Sargent*, akupige, akunyanyue, Mabunge yote yapo hivyo na tunaelewa kwamba mwenzetu leo, eeh! Kama kwenye Jimbo lako hakuna maji, unamwambia Waziri hasikii, lazima uchemke! Eeh umwambie mimi sikubaliani na wewe.

Wakati mwagine unaweza kutoa hata kaneno, tunajua ameteleza huyu, Inaeleweka. Omba radhi bwana, unaomba radhi, ndivo Mabunge yalivyo. Siyo hata rekebisha, sitaki, sirekebishi, aah! Sasa tutakuwa Bunge la ajabu sana haiwezekani. Kwa sababu hapa tunachofanya *we just make a point* ili mradi umeshafikisha ujumbe wako, tatizo lako ni nini tena? Ni kuweka mambo sawasawa ili kuweze kucha, tuweze kwenda pamoja. (*Makofi*)

Waheshimiwa Mawaziri hawa wanafanya kazi kwa niaba yetu, tuwaheshimu. Kazi yao ni nzito. Wanasi mama hapa kwa niaba ya watu wengi nyuma yao. Baadhi yao wanafanya mambo ya hovyo kweli, lakini wakati mwagine siyo yeye kama yeye, kwa hiyo tukienda pamoja na tukielewana, itatuweka mahali ambapo ni pazuri sana.

Waheshimiwa Wabunge, nimalizie kwa kusema, siyo nia yangu kulifanya Bunge hili liwe ni Kanisa au Msikiti, sasa pawe yaani eeh, nafikiri mnani lewa? Nia yangu Bunge hili liwe *vigorous as possible*, watu watoe hoja zao wanavyowenza, wachemke kama inavyotakiwa, lakini kila kitu kina *limit* yake, matusi na mengine, huko tusifike, basi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, basi baada ya maneno hayo, najua muda wetu umekwisha, naomba sasa nisitishe

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni tutakapoendelea na hoja ya Serikali ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

(Saa 6.54 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia)

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. RAMADHANI ABDALLAH ISSA- KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa
Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi
na Mawasiliano**

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano. Tunaanza na Mheshimiwa Bonnah Kaluwa na Mheshimiwa Ghasia ajiandae.

MHE. BONNAH M. KALUWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hii Wizara ya Miundombinu. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri pamoja na Wizara yote katika miradi ambayo inaendelea katika Mkoa wa Dar es Salaam. Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya katika sekta ya miundombinu. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nianze mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kitabu cha Wizara ya Miundombinu lakini kuna barabara ambazo naona zinaweza zikatusaidia katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam,

mwaka 2014 hizi barabara ziliainishwa kwamba zitaanza kujengwa mwaka 2015, lakini kwa sasa hivi nimeangalia nimeona tu kwamba wamesema ndijo wanataka kufanya tathmini, ina maana hawajaweka hata hiyo bajeti ya tathmini au kujua ni lini zitaanza kujengwa. Barabara ambayo inatoka Kimara inapitia Jimbo la Kibamba na pia inakuja mpaka Banana lakini pia inakwenda mpaka Kitunda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie hizi barabara, kwa sababu hizi barabara za Dar es Salaam, inaweza ikaonekana Dar es Salaam kwamba kuna barabara nyngi zinatengenezwa lakini Dar es Salaam kuna foleni kubwa, hii barabara kama ikitengenezwa inaweza ikatusaidia wakazi wa Dar es Salaam ili foleni iweze kupungua. Kwa sababu, watu amba wanatoka Mbezi wanatumia hii barabara kupitia Jimbo la Segerea na baadaye wanapitia llala kwa ajili ya kukwepa foleni na kuongeza hata watu wafike makazini mapema. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho nilikuwa nakiangalia nilijua Mheshimiwa Waziri atakiweka ni fidia ya wakazi wa Kipunguni Kata ya Kipawa. Mwaka 2016 kwenda 2017 nilisimama nikaongea kuhusu hii fidia ya wakazi wa Kata ya Kipawa, ambao wamehamishwa kwa ajili ya kupisha upanuzi wa *Airport*, lakini naona hapa Mheshimiwa Waziri hajaweka bajeti wala hajawazungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wakazi tangu mwaka 1995 wako pale wanasubiri kuhamishwa na wanasubiri malipo yao. Mpaka sasa hivi hawajalipwa na hakuna kitu chochote ambacho kinaendelea na hakuna kitu chochote wanachokjua kwamba Serikali itawalipa lini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiingia katika Kata ya Kipawa, Mtaa wa Kipunguni sehemu ya hawa wakazi wanapokaa imeshakuwa kama vile watu wamehama kwa sababu watu hawawezi kufanya maendeleo yoyote wameambiwa wanasubiri malipo yao. Kuanzia mwaka 1995 mpaka leo hakuna kitu chochote walicholipwa na kuna watu

wengine ambao walikuwa wanasubiri hizi pesa wameshakufa na wengine ni wastaafu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu nilishakwenda na Naibu Waziri tukafanya mkuutano na hawa wananchi, akasema kwamba wampe miezi mitatu, lakini sasa hivi ni zaidi ya miezi nane, hakuna jibu lolote ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri wala Mheshimiwa Waziri amelitoa. Naomba Mheshimiwa Waziri aweze kuniambia ni lini hawa wakazi wa Kipawa wataweza kulipwa pesa zao. Kwa sababu kwanza sheria inazungumza watu wasiondoke walipwe fidia ndiyo waweze kuondoka, lakini wale watu wameondoka na mpaka sasa hivi hawajui kinachoendelea. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja kumalizia kwenye bajeti yake aniambie ni lini atawalipa wakazi wa Kipawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nataka kuzungumzia bomoa bomoa ambayo imepita Majimbo ya Ukonga, Segerea na Ilala. Nina masikitiko makubwa sana kwa Mheshimiwa Waziri, hawa wakazi ambao wamekaa walikuwa wamejenga pemberi ya reli, tunayo Serikali kuanzia Serikali ya Mtaa, Serikali ya Kata lakini wamewachia hawa watu wamejenga na baadaye mmekuja kuwabomolea, hata mlivyowabomolea hamjafuata utaratibu Mheshimiwa Waziri. Mtu amekaa kwenye nyumba yake miaka 50 unamwamsha saa 10 ya usiku akupishe unabomoa, jamani hiyo siyo haki! Kwanza tunawaonea sana wananchi, saa kumi ya usiku kuwatoa watu kwenye nyumba zao, wengine wana wagonjwa, wengine wanaumwa na wengine ni wazee mnaenda kuwabomolea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishafanya kikao na wakazi ambao waliambiwa wajiandae watabomolewa kwa sababu ya kupisha reli ya kisasa ambayo inajengwa. Nami nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri, hakuna mtu yeoyote awe anatoka Jimbo la Segerea au Ilala ambaye anakataa maendeleo, lakini watu wanakataa ile *process* walijotumia, jinsi walivyokwenda. Walisema kwamba tunawapa miezi mitatu ili waweze kujiandaa waondoche, lakini kabla ya hata

siku kumi tangu wametoa barua wameenda saa kumi ya usiku kuwavunja nyumba zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo reli wenye we wameweka jiwe kwamba mwisho wetu mtu asijenge hapa, lakini wamebomoa wameenda wamelipita mpaka lile jiwe walilojiwekea wenye we. Tunajua Sheria ya Manispaa inasema kwamba wakazi wa Mjini wanatakiwa kukaa mita 15 na wa Kijijini ni mita 30, watu wa reli wameenda wamebomoa mita 30. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri atuambie kwamba ni sheria gani imetumika kuwavunja wakazi wa Mnyamani Buguruni, Ukonga pamoja na Ilala kwako Mheshimiwa Zungu. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu hawa wakazi mpaka sasa hivi hawana sehemu ya kukaa, wako nje na hawajui kama mtawalipa au hamtawalipa. Kwa sababu sasa hivi kumezuka tabia, kila mtu ambaye anaenda kufanya kitu ambacho siyo kizuri anasema maagizo yametoka juu, ni uwongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie jamani hawa ni watu wetu, tumesema kwamba tunawasaidia watu wanyonge. Sasa tunawasaidiaje watu wanyonge kwa kuwavunja nyumba zao. Mheshimiwa Waziri naomba akija kujibu haya mambo anieleze wakazi hawa alio wavunja kupisha hii reli ya kati ametumia sheria gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nataka kuongelea ni miradi ya *DMDP* ambayo ilitakiwa barabara zijengwe Kiwalani pamoja na Minazi Mirefu. Leo ni mwaka wa nne, kila mwaka tukikaa hapa tunapanga kwamba tutaanza kujenga mwaka kesho na mpaka sasa hivi nimeangalia kitabu hakuna bajeti ya miradi ya *DMDP* kuhusu hizo barabara za Kiwalani pia barabara za Minazi Mirefu. Watu hawa wamekuwa wakikaa kwenye barabara ambazo siyo nzuri kwa muda mrefu. Sasa hivi ni miaka karibu 15 wanaahidiwa kwamba huu mradi utaanza, ulikuwa uanze

mwaka jana mwezi wa Nane lakini mpaka sasa hivi haujaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo,
Mheshimiwa Waziri naomba majibu (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri nami nimo humo kwenye malalamiko hayo. Mheshimiwa Hawa Ghasia, jiandae Mheshimiwa Joseph Mkundi.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na timu yake yote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika Wizara hii, pamoja na ukubwa na majukumu mengi lakini wanaonekana kuweza kuyamudu na kuimudu Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza napenda nipongeze kazi ya upanuzi wa Bandari ya Mtwara ambao tayari umekwishaanza. Ni imani yangu kwamba upanuzi ule wa bandari utasaidia sana katika kuharakisha maendeleo ya Mkoa wa Mtwara, Lindi na Ruvuma hasa ukizingatia kwamba sisi ni wakulima wakubwa wa korosho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupanua bandari ile sasa hivi hakutakuwa na sababu hata kilo moja kusafirishiwa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam hasa inayozalishwa katika Mikoa ile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la Liganga na Mchuchuma kwamba kule kuna uzalishaji wa makaa ya mawe, kuna chuma, tuna kiwanda kikubwa sana cha Dangote ambacho kinategemea hiyo bandari pia tunategemea chuma itakayozalishwa kule, makaa ya mawe na yenye we pia yasafirishwe kuititia Bandari ya Mtwara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwombwa Mheshimiwa Waziri suala la upanuzi wa Bandari ya Mtwara basi liende sambamba na ujenzi wa reli kutoka Mtwara hadi

Mbamba *Bayna Liganga* na Mchuchuma. Suala la upembuzi yakinifu limekamilika, tathmini ya mimea pamoja na nyumba maeneo ambapo reli itapita imeshakamilika. Kwa hiyo, namwomba sana suala hilo nalo liende pamoja ili ile bandari isije ikaleta mzigo mkubwa ukalazimika tena kusafiri kwa magari ambao utaharibu barabara ambayo kwa kweli tumekaa muda mrefu sana baina ya Mtwara na Ruvuma hatujawa na barabara ya kueleweka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine napenda kumpongeza sana Waziri na Serikali pamoja na Mheshimiwa Rais kwa kuanza kujenga reli ya katii. Reli ya katii ni sawa na mifumo ya damu au mifumo ya fahamu ndani ya mwili wa binadamu, reli hiyo ndiyo itakayoifanya bandari ya Dar es Salaam iweze kufanya kazi yake vizuri. Kwa hiyo, namwomba tu waharakishe hicho kipande cha kutoka Dar es Salaam kwenda Morogoro ambayo ni reli ya kisasa sana. Vipande vinavyobaki basi watangaze kwa haraka ili ujenzi huo ikiwezekana uweze kukamilika kwa muda mfupi sana, kwa sababu huo ndiyo ukombozi wa nchi yetu na maendeleo yetu kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine napongeza pia ndege ya *Bombardier* kuanza kutua Mtwara na Songea. Tarehe 30 imeenda kwa mara ya kwanza, nimeambiwa kwamba kutakuwa na ratiba nzuri tu zinazoeleweka. Ushauri wangu naomba ile ndege ya kwenda Mtwara inaunganisha pamoja na Ruvuma, unatoka Mtwara unaenda Ruvuma saa nzima, unatoka Ruvuma kwenda Mtwara dakika hamsini karibu na tano, halafu ndiyo utoke pale kwenda Dar es Salaam karibu tena dakika 50. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *route* ya Ruvuma ikiwezekana iwe ni ya Ruvuma peke yake ili mtu akitoka Dar es Salaam anafika Ruvuma na akitoka Ruvuma anafika Dar es Salaam. Kutoka Mtwara mpaka ufile Ruvuma upite tena Mtwara kwa kweli inachukua muda mrefu sana na kama shirika kweli linataka kushindana na mashirika mengine ambayo yanaenda Mtwara hapo hamtaweza kushindana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu ni kwamba *route* ya Mtwara iunganishwe na ya Comoro kwa sababu kutoka Mtwara kwenda Comoro ni saa moja na kutoka Comoro kwenda Mtwara ni dakika kama 25 au nusu saa. Kwa hiyo, hapo utaweza ushindani. Huo ndiyo ushauri wangu kwamba hiyo *route* ya Dar es Salaam – Ruvuma – Mtwara waiangalie tena ikiwezekana Mtwara iambatanishwe na ya Comoro. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka nilichangie ni suala la barabara ya kutoka Mtwara – Newala kwenda Masasi. Niishukuru Serikali kazi inaonekana kwamba inakaribia kuanza, Mkandarasi amepatikana na ameshaanza kukusanya vifaa tuna imani muda wowote ataanza ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika bajeti iliyotengwa mwaka huu ambao tunaenda nayo ni bilioni 21 na bajeti ambayo ipo sasa hivi ni bilioni saba. Kwa mujibu wa mkataba ule ni zaidi ya bilioni 90 na mkataba ni wa miaka miwili, sasa kwa pamoja tumetenga kwa miaka miwili bilioni 29, mkataba unataka bilioni karibu 90 na kitu. Sasa huyo Mkandarasi atajenga kwa fedha zipi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie hilo, vinginevyo tutakuwa tunamfanya Mkandarasi anakuwa *s/ite* anaondoka. Mheshimiwa Waziri tunashukuru kwa sababu lazima ushukuru kidogo ulichokipata, tunashukuru kwamba sasa hivi ile ndoto imeanza kutimia, lakini pia iangaliwe bajeti ili barabara ijengwe kwa ubora unaokusudiwa, kwa sababu kama pesa zitakuwepo mkandarasi hana kazi ya kuondoka *s/ite* na kwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni suala la Uwanja wa Ndege wa Mtwara. Uwanja ule umejengwa kabla sijaanza hata darasa la kwanza na hata sijui umejengwa lini kwa sababu nimepata akili nimeukuta ule uwanja upo tayari. Tangu kipindi hicho sidhani kama kuna ukarabati wowote

wa uhakika uliofanywa na sasa hivi ndege zikitua pamoja na kwamba ni uwanja wa lami lakini utafikiri umetua kwenye matuta. Kwa hiyo, nawaomba Wizara wauangalie uwanja ule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuna masuala ya utafiti wa gesi yanakuwa yakifanyika pamoja na kwamba sasa hivi yamesimama. Kule kazi zinafanyika usiku baharini, uwanja hauna taa na kama mnavyofahamu Mtwara juu linaanza kutoka na linawahi kuchwa. Sasa siku nyingine mnaondoka abiria mnakaribia uwanja mnaambiwa uwanja umeshaingia giza mnarudi tena Dar es Salaam. Nawaomba waukarabati uwanja ule pia wauweke taa. Taa zinazotumika pale ni za wachimbaji wa gesi na hawaruhusu taa zao kwa sababu ni *mobile* wanaziweka pale tu panapokuwa na dharura na kwa maombi maalum. Kwa hali, ambayo tumefikia sasa hivi Mtwara kwa kweli tunaomba uwanja ule ukarabatiwe na uweweke taa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kwa wale ambao wameenda Mtwara, lile jengo la abiria lipo ndani ya uwanja, nalo waliangalie waone uwezekano wa lile jengo kuliweka kama majengo mengine yalivyoojengwa. Haiwezekani jengo yaani unashuka kwenye ndege unaingia moja kwa moja kwenye jengo la abiria kwa sababu kwanza ni hatari kwa abiria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena kumpongeza Waziri pamoja na timu yake, niombe tu yale ambayo nimeuombea Mkoa wangu na kuimbea nchi yangu basi yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mkundi, jiandae Mheshimiwa Bungara.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya Waziri

wa Uchukuzi, Ujenzi na Mawasiliano ambayo ni muhimu sana. Kwanza naunga mkono hotuba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pili, nikitambua kwamba kuna maeneo nimekwishatoa mchango kwa maandishi niombe sasa nichangie hasa kwa kusisitiza kwenye maeneo kama matatu ambayo kwangu naona ni muhimu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Jimbo langu la Ukerewe. Sisi ni watu tunaotoka Visiwani, nimekuwa namsikia ndugu yangu Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau analalamika juu ya mazingira ya Mafia, mazingira ya Ukerewe kama nilivyosema ni visiwa na usafiri wetu mkuu ni lazima tu-cross maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea kutumia vyombo vyta usafiri kama meli, cha kusikitisha tuna shirika muhimu sana la Kampuni ya Huduma za Meli (*MSCL*) ni kampuni muhimu sana. Ukerewe tumekuwa na Meli za *MV*. Butiama, *MV Clarias*, bahati mbaya sana zimekuwa na matatizo kwa muda mrefu mfano *MV Clarias*, kila mara inaharibika. *MV Butiama* ina zaidi ya miaka minne haifanyi kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri nimeona wanaongelea utengenezaji wa Meli ya *MV Butiama*, haiko *specific* kwamba utengenezaji huu unatarajia kukamilika lini ili kuwasaidia wananchi wa Ukerewe wanaotaabika na usafiri usio wa uhakika wa meli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwamba kuna kampuni binafsi ya *MV*. Nyehunge ambayo ina-*operate* pale sasa hivi, lakini hii Kampuni ya Huduma za Meli ni kampuni muhimu sana, nimekuwa naongea na watumishi wa kampuni hii wanachoomba wao wanataka tu uwezeshwaji ili Kampuni hii ianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita kuna mchangiaji mmoja ametoa mfano akasema kwamba ni vigumu sana kwa kampuni za meli kupata harasa. Ni kweli nakubaliana naye, Kampuni kwa mfano hii ya Huduma ya Meli kama itawezeshwa ni moja kati ya makampuni ambayo yanaweza kutoa pesa kwa Serikali kutokana na utendaji wao, imani yangu ni kwamba watafanya kazi vizuri na kwa faida na sehemu ya faida ile wataipa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni mwaka mzima hata pesa za ruzuku *OC* Serikali imeshindwa kuwapa kampuni hii, wameshindwa kulipwa mishahara, hata Bima ya Afya wamektiwa kwa sababu wameshindwa kulipa pesa, matokeo yake naambiwa kuna wakati mpaka watumishi wanaenda kupanga foleni ili viongozi wa kampuni hii waweze kuwasaidia watumishi angalau familia zao zipate matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali wasaidieni Kampuni hii iweze kuwa imara, iweze kusimama na kufanya kazi zake, kwa sababu wanachoomba wao kampuni hii ya meli wanataka tu uvezeshwaji ili waanze kazi. Kama wataanza kufanya kazi wana uhakika wa kuendelea kulipana mishahara na kufanya shughuli zao bila matatizo. Kwa nini Serikali mnaicha Kampuni hii inataabika kiasi hiki. Hebu niombe Serikali tafadhali *MSCL* waweze kusimama *take off* kuliko kuwaacha katika mazingira wanaishi kama yatima, hawalipani mishahara, watumishi wanaugua hawawezi kwenda hospitali kwa sababu hawana bima tena, wasaidieni tafadhali. Iwezesheni *MSCL* iweze kufanya kazi, hii ni Kampuni muhimu sana kuweza kuisaidia hata Serikali kama chanzo chake cha mapato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kama nilivyo sema, kule tunaishi visiwani, kuna vivuko kwa mfano cha *MVNyerere* nimekuwa nawasiliana na Mheshimiwa Naibu Waziri mara kwa mara, ambacho kina *operate* kati ya Ukala na Bugolola. Kivuko hiki kina muda mrefu na sasa injini zake zimechakaa zimeanza kuleta matatizo. Kwa mfano, wiki

mbili zilizopita kivuko hiki kimezima katikati ya maji zaidi ya mara mbili na kuzua tataruki kwa abiria waliokuwa katika meli ile. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri wakati anafunga mjadala aweze kutuambia na hasa wananchi wa Jimbo la Ukerewe wanaotumia kivuko hiki nini suluhisho la kudumu la Kivuko cha MV Nyerere? Kinahitaji kitengenezwe ili watu wanaosafiri katika kivuko kile wawe na uhakika wa maisha yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kivuko kinasafiri, kwanza mahali kinapofanya kazi ni umbali ambao hauwezi kuzidi hata dakika arobaini na tano, lakini kivuko kile kwa sababu ya kuchoka kwa injini zake kinasafari zaidi ya masaa mawili, sasa fikiria kina safiri masaa mawili bado kinazima katikati ya maji! Hii inazua tataruki na kukatisha watu tamaa. Wakati Mheshimiwa Waziri anapokuja ku-*wind up* ningeshukuru sana kama atanipa suluhisho la kivuko hiki na kuweka mazingira ya kudumu na ya uhakika ya usafiri kwa wakazi wa Kisiwa cha Ukala. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kisiwa cha Irugwa vilevile pale Ukerewe, kina wakazi zaidi ya elfu 20, lakini wanasafiri kutoka kule kwa mfano watumishi wanasafiri kwa siku tatu. Ili atoke Irugwa aje atape huduma kwenye Makao Makuu ya Wilaya inabidi apite Musoma Vijijini kwenye Jimbo la Profesa Muhongo, aende Musoma Mjini kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mathayo, aende Bunda kwenye Jimbo la Mheshimiwa Ester Bulaya apite Kisolya ndiyo aje Nansio. Naomba Mheshimiwa Waziri mtuangalie kwenye eneo hili Kisiwa cha Irugwa lini Serikali itafikiria kuweka usafiri wa kudumu katika eneo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye eneo la barabara, nimesoma kwenye hotuba hapa sijaona chochote juu ya ujenzi wa daraja linalouganisha Kisolya na Rugezi. Serikali ina mpango gani juu ya ujenzi wa daraja hili ambalo litakuwa suluhisho la matatizo ya usafiri kwa wakazi wa Ukerewe. Ningeshukuru sana kama Mheshimiwa Waziri wakati

wa kufunga atanipa maelezo ni nini mkakati wa Serikali juu ya ujenzi wa daraja hili, kwa sababu tayari hatua za awali zilishaanza, nini kinaendelea, nitashukuru sana kama Mheshimiwa Waziri ataniambia nini kinachoendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mradi wa ujenzi wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Bunda – Nansio, nimeona kwenye hotuba kuna awamu ya pili ambayo inaongelea ujenzi wa kilometra 51 kati ya Kibala na Kisolya. Niombe sana Mheshimiwa Waziri. Kutoka Kisolya ambapo awamu hii ya pili inakomea mpaka Nansio Mjini ni kama kilomita kumi na zinabaki, naomba badala ya kujenga kilometra 51 kilometra 10 zikabaki ni bora Serikali ikaunganisha kilometra hizi katika kilometra 51 ili ufanyike mradi wa pamoja, badala ya kutengeneza kwa awamu miradi miwili tofauti ambayo naamini itakuwa ni gharama zaidi kuliko kama itaunganishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la mawasiliano; nimeona jitihada za Mfuko wa Mawasiliano kusambaza huduma hii ya mawasiliano, lakini bado kuna matatizo makubwa sana ya mawasiliano kwenye kisiwa cha Ukerewe hasa katika Kisiwa cha Ukara. Katika karne hii si jambo jema sana kwamba unaenda mahali unakuta wanakijiji wanakusanya eneo moja ili wapate mawasiliano ya kupiga simu. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri tuweze kupata mawasiliano kwenye kisiwa cha Ukerewe, maeneo yote yaweze kupata mawasiliano, ambayo yatasaidia hasa kuharakisha shughuli za kiuchumi za wananchi kwa eneo la Ukerewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Bungara dakika tano na Mheshimiwa Bobali dakika tano.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kukuwezesha wewe kuwa Mwenyekiti wa kikao hiki na

namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumpa Urais Mheshimiwa Magufuli na kuapa kwamba atailinda Katiba ya Jamhuri ya Tanzania, lakini kwa bahati mbaya tu Katiba yenewe kidogo anaipindisha pindisha kwa sababu hatoi haki kwa Vyama vyaa Siasa kufanya mikutano. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bungara zungumza hoja iliyopo mbele yako, acha mikwara.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, si nimetoa shukrani? Mimi nimetoa shukrani tu wala sikumtukana mtu yejote. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa shukrani hizi kwa Mwenyezi Mungu leo najielekeza kuchangia katika sehemu mbili tu katika hotuba hii. Tunakumbuka 2010 Rais aliyemaliza muda wake Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete Mungu amzidishie, aliahidi kwamba katika kampeni yake ya 2010 aliahidi kwamba atatengeneza barabara ya Kwa Mkochi – Kivinje barabara ya kilomita 4.2 kwa kiwango cha lami, mpaka leo nisemavyo barabara kwa mvua za jana tu na juzi gari zilikuwa hazifiki katika Hospitali ya Wilaya kutokana na barabara hiyo kuwa chafu na haipitiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya 2016/2017, tulitenga milioni 800 kwa ajili ya barabara hiyo ili ikamilike kwa kiwango cha lami, lakini mpaka sasa hivi nisemavyo ndege zimenunuliwa lakini fedha hizo za bajeti hazijaingia katika Wilaya ya Kilwa ili barabara hiyo itengenezwe. Pamoja na ndege mlizonunua hizo lakini mkumbuke kwamba kuna barabara ambazo ni muhimu sana zinaenda katika hospitali za Wilaya, nazo zikumbukwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri naomba hizo milioni 800 zipatikane ili babaraba ile iishe. Tena kwa bahati nzuri tarehe 2 Machi, 2016 Rais wa Jamhuri ya Muungano Mheshimiwa Dkt. Magufuli alifika Kilwa na nikamwambia tatizo hilo kwamba kuna kiporo cha Rais aliyepita na nikamwomba kiporo hicho amalizie yeye. Akaahidi na kumuagiza Injinia kwamba hiyo barabara iishe.

Naomba sana naomba, kwa kuwa Mheshimiwa Magufuli hasemi uwongo na alisema kwamba barabara lazima naomba barabara hiyo iishe ili watu wapate kutumia barabara hiyo na kufika katika hospitali kwa njia ya usalama. Bila hivyo watu wa Kivinje na Wilaya ya Kilwa kwa ujumla tutaona kwamba hatutendewi haki tunaonewa bila sababu ya msingi. Naomba Mheshimiwa Waziri barabara hiyo iishe na fedha hizo milioni 800 zipatikane katika mizezi mitatu iliyobaki ili barabara hii iishe. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni uwanja wa ndege. Kilwa Masoko kuna uwanja wa ndege, uwanja huo kulifanywa tathmini kwa wananchi wangu tarehe 19 Machi, 2013 ili walipwe fidia ili uwanja upanuliwe. Mpaka leo ninavyoongea tangu 2013 mpaka leo 2017 wananchi wangu hawajapata fidia. Naomba sana katika kuhitisha hotuba yake Mheshimiwa Waziri atuambie hawa wananchi wangu watapata lini fidia hiyo ya uwanja wa ndege na kama haiwezekani mseme kwamba haiwezekani. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bobali.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ingawa dakika tano hazijatimia lakini imeeleweka. (*Kicheko*)

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa nakushukuru. Kwa kuwa muda wenyewe mdogo nianze na suala la uwanja wa ndege wa Lindi. Kwa masikitiko makubwa nimepitia kitabu cha maendeleo ukurasa wa 134 mpaka 136 ambapo vimeorodhesha viwanja vya ndege ambavyo Serikali imevitengea fedha kwa ajili ya kuviedeleza. Kwa masikitiko makubwa uwanja wa ndege wa Lindi umeachwa. Sijui umeachwa kwa kuwa mmeusahau au hamuutaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja ule tangu Mheshimiwa Rais aliyetoka madarakani aondoke hatujaona tena ndege kwa sababu Mheshimiwa Salma hapa alikuwa anatua pale kama Mke wa Rais, tangu yeye ametoka madarakani uwanja wa ndege wa Lindi haujatumika tena

na ni uwanja wa kihistoria, ni uwanja wa muda mrefu. Naishangaa Serikali kuna mradi mkubwa wa *LNG* ambaao unataka kufanyaika takribani kilomita moja tu kutoka uwanja wa ndege. Hao Wazungu wanaotaka kuja watakuja kwa magari? Ama watakuja kwa usafiri gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nataka atakapokuja kuhitimisha, siku moja hapa Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu maswali alieleza kwamba uwanja wa ndege wa Lindi utafanyiwa upembuzi yakinifu na pesa itatengwa, leo nimedhihirisha kwamba taarifa alizozitoa Mheshimiwa Naibu Waziri siyo za kweli, ni taarifa za uwongo, uwanja wa ndege wa Lindi mmeusahau, hamuutaki. Kwa nini hamtaki kutenga fedha kwa ajili ya uwanja wa ndege wa Lindi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la fedha za maendeleo ya barabara, nimemweleza Mheshimiwa Waziri, haiwezekani Mkoa mkubwa kama Mkoa wa Lindi mnautengea shilingi bilioni 800, kuna mikoa mingine midogo mnaitengea shilingi triliuni mbili tena ni mikoa ambayo tayari imeendelea. Leo Mkoa wa Lindi ambaao miundombinu yake ya barabara bado ni mibovu, haijaendelea, mnautengea shilingi bilioni 800. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie mfano Mkoa wa Kilimanjaro, mmeutengea shilingi triliuni 2.2, Mkoa wa Lindi mnautengea shilingi bilioni 800 kwa sababu gani? Mheshimiwa Waziri tunaomba maeleo Mkoa wa Lindi ni mkubwa sana, mkoa ambaao haujaendelea au kwa sababu ni Kusini? Au mnaona gere kwa sababu korosho inalipa sasa? Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwa kuna korosho na inahitaji kusafirishwa, korosho hailimwi mjini Korosho inalimwa vijijini, lazima isafirishwe ipelekwe huko bandarini Mtwara ipelekwe Dar es Salaam, tunaomba miundombinu ya barabara ijengwe katika mkoa wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inasikitisha kwa sababu Majimbo nane, Majimbo yote saba hayajatengewa fedha, Jimbo moja tu la Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiyo limepata

fedha, hili jambo ni la hatari, Majimbo yetu wengine hayana fedha, yamekuwa hayana kitu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri aje atueleze kwa nini Mchingga haijatengewa fedha, kwa nini Liwale haijatengewa fedha, kwa nini Kilwa haina fedha, kwa nini Mtama haina fedha, kwa nini Nachingwea haina fedha, tunahitaji majibu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la ubovu wa barabara ya kutoka Somanga kwenda Nangurukuru. Hii barabara imejengwa miaka michache iliyopita, leo hii ukipita katika eneo lile barabara ni mbovu, inathibitisha kwamba imejengwa chini ya kiwango. Eneo hili sasa hivi la Nangurukuru kumekuwa na uharamia, majambazi wanakaa, wanateka watu na sababu, kipande kile cha barabara ni kibovu. Kwa nini Serikali inatumia fedha nydingi lakini barabara zinadumu kwa muda mfupi? Kuna harufu ya nin? Kuna harufu ya ujisadi au kuna harufu gani? Kwa sababu haiwezekani barabara ilijojengwa miaka miwili au miaka mitatu iliyopita leo barabara mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa unatembea kutoka Lindi ukifika kipande cha Nangurukuru unasahau kama upo kwenye lami, ni mashimo kwenda mbele. Tunaomba sana majibu ya kina juu ya barabara hususan kipande cha kutoka Nangurukuru kwenda Somanga. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la kumalizia ni suala la alama za (X) ambazo mmeziweka kwenye nyumba zetu katika eneo hili la barabara. Tunataka majibu (X) zile za kijani mwisho wake lini? Kama mmeshindwa kulipa tuwaambie wananchi waziendeze nyumba zao. Mnawawekea alama za (X) hawaendelezi nyumba. Leo ukiingia Jimboni kwangu kuanzia Mkajuni, Kitomanga, Kilangala, Mchingga mpaka unafika Mto Mkavu kote kuna alama za (X) za kijani. Watu wale hawaendelezi nyumba zao mpaka leo kumekuwa hakuna maendeleo tunahitaji maelezo hizi (X) mwisho wake lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Fredy Mwakibete, hayupo.

WABUNGE FULANI: Yupo.

MWENYEKITI: Yupo?

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo. Kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Wizara hii muhimu. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambazo anazifanya katika nchi yetu ya Tanzania. Tumeshuhudia jinsi ambavyo anajenga *flyovers*, tumeshuhudia jinsi ambavyo nchi yetu imeingia mikataba ya kujenga *standard gauge* katika reli ya kati, tumeshuhudia jinsi ambavyo majengo ya hosteli Dar es Salaam yamekamilika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hii kwa upande wetu wa Busokelo kuna barabara ambayo inaanzia Katumba – Luangwa - Mbambo mpaka Tukuyu, ina urefu wa kilometra 83. Hata kwa haya ambayo tumepeata si haba, tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jinsi ambavyo umeshiriki kikamilifu pamoja na wataalam wako. Bado tunaomba kwa kuwa kilometra ambazo umetupa sasa hivi bado hazijatosheleza zile kilometra 83. Kwa hiyo, tunaomba ikiwezekana katika bajeti yako uweze kutuongezea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona pia jinsi ambavyo Wizara inavyofanya kazi vizuri hasa katika suala la mawasiliano. Nitoe ushauri wangu katika mambo machache hasa *TCRA*. Tumeaona jinsi watu wengi sana tunatumia mifumo hii ya simu lakini kwa bahati mbaya inatumika hata kwa njia ya uhalifu na *TCRA* wanashindwa kudhibiti na hata wakati mwengine watu wanatuma meseji za kutukana wenzao, kwa hiyo tulitaka mifumo hii iboreshwe vizuri ili wawe na mfumo ambao unaweza uka-*filter*, maana kila utakapokwenda *TCRA* wanakwambia hatujui ama mfuate

mwenye namba fulani. Kama kutakuwa na *systems* ambazo zinaweza zikafanya kazi vizuri, bila shaka uhalifu ambao unaendelea sasa hivi nchini kwa kutumia njia ya mtandao hautakuwepo tena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichangie katika suala la mifumo ya kompyuta, ukisoma kitabu cha Waziri ukurasa wa 202, wamesema watajenga *National Internet Data Center*. Napenda nishauri kama Mtaalam wa Mifumo ya Kompyuta, unapojenga *Data Center* ya nchi ambapo mtakuwa mna-share *information* mbalimbali, haitakiwi iwe centralized sehemu moja, iwe decentralized ili ikitokea *in case* kuna any emergencies zile *backups* ziweze kufanya kazi vizuri, kama nchi za wenzetu za Ulaya wanavyofanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri katika jambo hili la mawasiliano, mara nyngi sana katika nchi yetu tunatumia *soft* ambazo tunasema ni *commercial, commercial* kwa maana ya kununua hizo *software*, lakini kama tungkuwa tunatumia *software* ambazo ni *open source* na gharama yake ni ndogo ni rahisi kuzi -*maintain* kwa maana ya *sustainability* yake inakuwa ni kubwa kuliko hizi *commercial software* ambazo tunanunua kwa gharama kubwa na kuzi-*maintain* kwake ni gharama kubwa vilevile. (*Makofii*)

Kwa hiyo, ningeshauri Serikali ianze sasa kama Mataifa mengine ambayo yameanza hasa nchi za Ulaya Magharibi zinafanya hivyo, lakini ukienda Marekani wanatumia zaidi hizi *microsoft* ambazo ni gharama kuzi-*maintain* lakini pia kuna *software* nyngi ambazo ningeweza pengine kuzitaja kuna hizi *Postgrace, Oracle, Square Server, Survey, GSMO*, kwa sababu nimeishi nazo naweza nikaishauri Serikali iweze kufanya hivyo. Pia kuna *software* nyngi, kuna nyngine ambazo zinatumika kwa ajili ya kuisaidia nchi iweze kupata mapato yake vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi sasa hivi Serikali ikitaka kupata mapato mazuri kutoka kwenye

mitandao ya simu lazima waende kwenye *mobile operator* mwenyewe kwamba sasa mwezi huu umepata kiwango gani, wakati ilitakiwa wawe na mfumo ambao wao wanapeleka *direct*. Kwa hiyo, kila muamala unaofanyika *either* uwe wa pesa ama uwe wa simu Serikali iwe inajua kwa kiwango gani inaweza kupata mapato yake kuititia kwenye mifumo hii ya simu. Kwa sasa hivi Serikali inaibiwa sana kwa sababu hatuna hiyo mifumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za wenzetu ambazo zimeendelea sasa ukienda kama Ethiopia, Afrika Kusini na nchi nyingine za Ulaya wana mifumo ambayo inakuwa *centralized* siyo kama sasa hivi ambavyo imekuwa *decentralized*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niweze kumalizia kwa upande wa *TBA*. *TBA* inafanya kazi nzuri na nimeambiwa pla kwamba mmepewa kazi ya kujenga majengo ya Halmashauri mbalimbali nchini. Kwa bahati mbaya sana *TBA* katika baadhi mikoa hampo ikiwemo hata kule kwetu katika Jimbo la Busokelo, katika mkoa mzima wapo watatu tu. Kwa hiyo, fedha za Halmashauri nyingi mpya ambazo zimepewa zipo tu kwenye akaunti za Halmashauri na karibu mwaka wa fedha unakwisha. Tunapofuatilia na kufuatilia wanakwambia wamepewa kazi *TBA*. Kwa hiyo, tunaomba kama *TBA* watajenga na kwa kweli wanajenga kwa kiwango kizuri na kwa gharama nafuu, basi longezewe uwezo zaidi ili iende hadi huko mikoani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ulega, jiandae Mheshimiwa Kandege dakika tano na Matiko dakika tano.

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naanza kwa msemo wa Waswahili tunaosema kwamba "Haja ya mja hunena muungwana ni vitendo." Namshukuru sana na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya na kila mmoja anaona kabisa. Tuseme ukweli kwamba ni lazima tukubaliane kwamba hatuwezi kufanikiwa bila ya kufunga mkanda na ku-sacrifice kwa ajili ya kizazi cha leo na cha kesho. Wazungu wanasema *no pain no gain.* (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa, tulikuwa tukitukanwa hapa, nchi kubwa ya Tanzania tunashindwa na nchi ndogo ndogo. Leo tumenunua ndege sita na mwakani tunanunua ya saba, wapo watu wanakuja na maneno sijui *terrible teen*, sijui kitu gani. Hayo ni matango pori na mimi namshauri sana Mheshimiwa Waziri akiinuka hapa aseme maneno ya kitaalam awaambie Watanzania na Waheshimiwa Wabunge wasiwe na wasiwasi, hatuna wasiwasi na Mheshimiwa Waziri Profesa aende akanunue ndege eti zenyе wasiwasi. Nina hakika kabisa kwamba akiinuka Mheshimiwa Waziri hapa atatuwekeea na kutufungia mjadala huu ili tuweze kusonga mbele. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kulisema hilo, naomba pia niishukuru sana Serikali yangu, kwa sababu nimekuwa nikiinuka mara nyngi sana kuzungumzia barabara ya kutoka Mkuranga Mjini kwenda Kisiju - Pwani na sasa kazi imeanza. Nimeona katika hotuba ya Rais ya kwamba upo uwezekano mkubwa mwaka huu tukapata pesa za kutengeneza kilomita mbili za lami, hii ndiyo Serikali ya Awamu ya Tano ya Hapa Kazi Tu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwa kuwa barabara hii imekuwa ikitengewa pesa nyngi kila mwaka kwa ajili ya *maintenance*, tunanunua kokoto zinazotoka Jaribu Mpakani takribani kilomita 65 kufika Mkuranga. Tafadhalii sana Mheshimiwa Waziri atazame jambo la namna hii. Waone kabisa kwamba huu mpango waliouanzisha wa lami ya kidogo kidogo waufanye kila mwaka badala ya kuingiza hela nyngi katika *maintenance* ambayo baada ya muda mfupi inaharibika tena. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaiona Mkuranga ya viwanda na Mheshimiwa Rais amekuja Mkuranga mara mbili, mwezi huu wa Tano au wa Sita atakuja mara ya Tatu kuja kufungua kile Kiwanda cha *Tiles*. Mvua hizi za masika zimetaka kukifanya kiwanda kile kisipate malighafi, kwa nini? Kwa sababu barabara ya Kimanzichana mpaka Mkamba, Mkamba - Mkuwili kuungana na wenzetu wa Kisarawe imekufa kwa sababu ya mvua. Naomba sasa tuliangalie jambo hili kwa umakini sana, kwa sababu kiwanda kile kinakwenda kulisha *tiles* za nchi nzima, hatutakuwa na sababu ya kununua *tiles* kutoka nje ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri iangalie hii ni barabara ya uchumi, watu walikuwa wakisema humu kwamba malighafi za kiwanda hicho zinatoka nje ya nchi. Nataka nikuhakikishie malighafi yote inatoka Kisarawe, Kilindi - Tanga, Mkuranga, Kisegese, Vianzi na Mkamba. Hivyo, naomba barabara hii ifanyiwe kazi maridadi kabisa ili tuweze kuinua uchumi wa watu wetu na watu wetu waweze kuona kwamba utengamano wa viwanda na uchumi wao unakwenda sambamba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kwa ufupi sana nizungumzie suala la kupandishwa hadhi za barabara. Ninazo barabara mbili ningependa zipandishwe hadhi. Barabara ya Kiguza - Hoyoyo, Hoyoyo mpaka kwenda kutokea Kitonga - Mvuti. Barabara hii upande mmoja ni *trunk road* ya *Natioal Road* - Kilwa Road na upande mwingine ni barabara ya Mkoa wa Dar es Salaam. Pande zote hizi mbili zinabeba mizigo mizito tena zina lami, lakini sisi barabara yetu ya Kiguza - Hoyoyo kupita pale Hoyoyo kwa Mama Salma pale ni barabara ya vumbi na barabara imechoka. Sasa tunabebehaje mizigo mikubwa barabara hii na Halmashauri hazina uwemo. Naomba sana Mheshimiwa Waziri akiona barua ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Kamanda Injinia Evarist Ndikilo aipitishe haraka barabara hii nayo pia vilevile iweze kupata kupandishwa hadhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo iko barabara ya Vikindu mpaka Vianzi – Marogoro – Sangatini,

upande wa Dar es Salaam kutoka Tundwi - Songani, Pemba Mnazi - Kibada - Mwasonga mpaka Kimbiji inawekwa lami. Upande wetu huku kilomita kama kumi bado ni barabara ya Halmashauri inabeba mzigo mzito. Naomba sasa kwa heshima kubwa na taadhima tuendelee kuthibitisha ya kwamba hii ni Serikali ya Hapa Kazi Tu na akiona barua ya *Engineer Evarist Ndikilo*, Mkuu wa Mkoa, Kamanda kabisa basi aitie mkono wake pale Mheshimiwa Waziri, ahakikishe kwamba mambo yanakaa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba nichukue fursa hii kuipongeza tena Serikali kwa kazi kubwa inayofanya ya kulipa madeni ya Wakandarasi. Tunaomba pia iendelee kuhakikisha jambo hili linafanyika kwa ufasaha kwa maana liharakishwe na pesa zinazokwenda katika Halmashauri zetu ziharakishwe, tena nafahamu kwamba Serikali ina mpango mzuri sana wa kuanzisha *Agency* ya Barabara za Vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wenzangu hapa wamezungumzia jambo la kwamba *agency* hii ikiwezekana wapewe *TANROADS*. Sasa sisi hatutaki kurudi nyumba, tunachosema tutakuja kumwambia Waziri wa Fedha aangalie uwezekano ikiwezekana hii *Agency* ya Barabara za Vijijini ipate pesa na asilimia kubwa zaidi ya ile ya thelathini. Kwa sababu uti wa mgongo wa wananchi wetu ili kuwatoa katika umaskini ni kuwatengenezea barabara zao. Watu wangu wa Mkuranga wakiboreshewa barabara zao vizuri ambacho ndiyo kipaumbele namba moja cha miundombinu, nina hakika kabisa kwamba, watainuka zaidi kiuchumi na watafanya shughuli zao wenyewe. Leo hii mananasi pale yanaharibika ni kwa sababu barabara ni mbovu za vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na taadhima naomba nichukue fursa hii kukushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kandege, jiandae Mheshimiwa Matiko. Waheshimiwa Wabunge, Wizara hii ina

Mafungu matatu, kwa hiyo, tutamaliza na Mheshimiwa Matiko. Mheshimiwa Laizer *no*, Mheshimiwa Matiko una dakika tano tu wewe.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mimi.

MWENYEKITI: Aah ni wewe? Basi anaanza Kandege kwanzia.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipatia fursa nami niweze kuchangia katika hotuba iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri. Naomba niungane na Wabunge wenzangu waliotangulia kumpongeza kwa kazi nzuri ambayo inafanyika, haihitaji ushahidi, kila mtu anaona kinachofanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze katika Jimbo langu. Kipekee nashukuru kwamba Serikali ina ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Sumbawanga kwenda Kasanga *Port* na nimeona imetengwa jumla ya shilingi bilioni 74. Naomba Serikali ihakikishe kwamba barabara hii inajengwa na ikamilike kwa wakati. Ni ukweli usiopingika kwamba mradi ukishachukua muda mrefu gharama yake inakuwa kubwa, lakini kama haitoshi kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri nimeona kuna ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Matai kwenda Kaseshe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni shahidi alikuja akatembelea barabara hii na akaahidi kwamba Kandarasi atapatikana na kazi hii itatolewa. Sasa naomba katika bajeti iliyotangulia ilikuwa imetengwa bilioni 11, safari hii imetengwa bilioni 4.9. Tafsiri yake nimesoma na kukuta kwamba Mkandarasi atapatikana muda wowote, kwa hiyo kiasi cha pesa tofauti ya bilioni 11 iliyokuwa imetengwa wakati ule na sasa hivi naamini itakuwa imetolewa na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami utaanza mara moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nimeliona ni vizuri nikampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa mara ya kwanza kivuko cha Mto Kalambo kimetengewa pesa za kutosha milioni 100 kwa ajili ya usanifu. Naamini haitaishia katika usanifu, kazi ya kujenga kivuko kile itaanza kwani ni ahadi ya Mheshimiwa Rais alipokuja kuomba kura Kalambo na akaahidi kwamba yejote ambaye hatahakikisha kivuko hiki kinajengwa basi ajiandae kupisha nafasi hiyo. Naamini Mheshimiwa Waziri bado anakumbuka, hiyo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ambayo haitakiwi kupingwa na mtu yejote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema kuhusu Jimbo langu, naomba niseme Kitaifa. Majuzi nilipata fursa ya kuuliza swali kuhusiana na suala la UDA Dar es Salaam na katika majibu ambayo nilipatiwa naomba nikwambie katika miradhi ya kutolea mfano Kusini mwa Jangwa la Sahara yenye mafanikio ni pamoja na usafiri wa mabasi yaendayo kasi Dar es Salaam, lakini pamoja na treni ya umeme *Lagos*. Kwa Watanzania wengi tunadhani kwamba mradi huu ni mradi mdogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuhakikishie ukienda duniani mionganoni mwa miradi ambayo inasifiwa ni pamoja na usafiri wa mabasi yaendayo kasi Dar es Salaam. Ninachoomba ni vizuri Serikali ikahakikisha kwamba fursa hii inatolewa kwa Watanzania walio wengi ili hisa zile ambazo zinamilikiwa na Serikali zikaja kuuzwa kwa Watanzania walio wengi ili tukashiriki kumiliki uchumi huu kwa ajili ya Taifa la Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi umekuwa ukipigia kelele kuhusiana na *TTCL*, naomba nikuhakikishie kama elimu ya kutosha haitolewi kwa Watanzania juu ya kununua hisa, basi hata hili ambalo umekuwa ukipigia kelele kwamba Watanzania washirikishwe katika kumiliki halitawezekana. Mfano tunao, hisa ambazo zimetolewa kwa ajili ya kuuza za *Vodacom* imefikia tarehe 19 ambayo ilikuwa tarehe ya mwisho bado hisa hazijaweza kununuliwa. Naomba Wizara ya Fedha ichukue jukumu la kuhakikisha

kwamba elimu kuhusiana na uwekezaji kwa maana ya kununua hisa inatolewa kwa Watanzania walio wengi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Kenya walivyokuwa wamepeleka hisa zao sokoni za *Safaricom* walikuwa wametoa kwa muda wa mwezi mzima lakini ndani ya siku kumi zile hisa zilikuwa zimeshanunuliwa kiasi kwamba wakalazimika wasitishe. Sasa kwa Watanzania imekuwa ni hadithi tofauti na kwa bahati mbaya sana unakuta wakati mwingine hata Wabunge pia hatuna elimu juu ya umiliki wa hisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa makusudi Serikali lazima ihakikishe kwamba inatoa elimu maana taarifa ambazo tunapata kutoka kwa Gavana wa Benki Kuu ni kwamba...

TAARIFA

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Kandege na kwa ajili ya recordvizuri kwenye Bunge lako. Kenya walipoamua kuza *Safaricom* waliruhusu Afrika Mashariki yote wakaenda kununua hisa zile. Sisi tumeamua kuza *Vodacom* hatujaruhusu Afrika Mashariki kuingia, maana yake ni nini? *Liquidity* ni kidogo tutapata tatizo kubwa kwa sababu ya *liquidity*.

MWENYEKITI: Ahsante, ameshakaa. Mheshimiwa Kandege muda wako umekwisha. Hapana kengele ililia wakati wa taarifa, lakini baadaye mnaweza mka-*engage*. Mheshimiwa Laizer na dakika tano za mwisho atachukua Mheshimiwa Massare.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nitumie nafasi hii kukushukuru pia kwa kunipa nafasi ya kusema maneno machache kwa dakika hizi tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni Wizara muhimu sana ni *cross cutting Ministry* kwa sababu Wizara zote zinaitegemea hii. Tuna matatizo makubwa ya upelekaji wa fedha ya miradi ya maendeleo katika Halmashauri zetu. Hili limekuwa ni tatizo sugu katika Halmashauri nyingi. Kwa mfano, katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli tumepelekewa milioni 200 tu katika shilingi bilioni 1.2 ambazo tulitengewa. Sasa katika mazingira ya sasa tunahangaika kupitisha bajeti, tunataka Waziri aje atueleze wana mikakati gani kuhakikisha kwamba fedha zote zilizobaki katika bajeti ya mwaka huu 2016/2017, zinapelekwa katika Halmashauri zetu kabla ya Juni mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitapata majibu ya kuridhisha basi nitashika shilingi ya Waziri, kwa sababu hakuna sababu ya kupitisha bajeti mpya kama bajeti tulioipitisha hatupeleki kwenye Halmashauri zetu. Haitakuwa na maana kwa sababu akinamama wajawazito watafia njiani na wakati wa mvua barabara zetu hazitapitika na hata sekta nyingine zote hazitakuwa na ustawi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nimeona katika kitabu tunashukuru kwamba barabara ya Loliondo – Monduli kwa maana ya Mto wa Mbu pamoja na Serengeti imeendelea kutengewa fedha. Barabara hii ni muhimu, tunaitengea fedha kidogo sana. Nataka Serikali ituambie mpango wa barabara hii itakamilika muda gani? Kwa maana mwaka huu itajengwa kilomita ngapi na mwaka unaofuata kilomita ngapi mpaka barabara itakapokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri namwona Waziri wa Viwanda. kule Engaruka yamepatikana magadi yenyeye ujazo wa trillioni nne, mpaka sasa hakuna barabara itakayofika katika eneo lile na wananchi wetu wapo tayari kutoa ardhi yao kwa ajili ya viwanda vile. Kwa hiyo, kama Serikali haitakuwa na *commitment* ya kupeleka miundombinu kwa maana ya angalau barabara na baadaye reli, ardhi ile tutaendelea kuitumia lakini wananchi wetu wapo tayari kutoa hata bure kwa ajili ya kujenga kiwanda kile. Kama hakuna *commitment* ya Serikali ya kupeleka miundombinu

kwenye maeneo yale mtuambie ili wananchi waendelee kutumia maeneo yale wakajenge mpaka mtakapokuwa tayari kuleta miundombinu na kwanda kianze na wakati huo gharama za fidia zitakuwa kubwa zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali ituhakikishie ni lini barabara hii itakamilika kutoka Mto wa Mbu kwenda Loliondo kwa sababu ya umuhimu wa magadi yaliyopo Engaruka ambao sisi tupo tayari kuwapa ardhi kwa ajili ya kuanzisha kwanda hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni ahadi za Rais. Naomba Waziri atuambie Rais alivyopita katika Wilaya ya Monduli wakati anaomba kura aliahidi kutujengea barabara ya lami kutoka Monduli Mjini kwenda Monduli Juu kule kwa Sokoine. Pamoja na kwamba Waziri haandiki lakini nataka Serikali iniambie ni lini mchakato wa barabara hiyo utaanza kwa sababu Rais aliahidi au Serikali ituambie kwamba labda Rais alisema uwongo ili kujitafutia kura, kama ni kweli basi tuambiwe ni lini barabara ya Monduli kwenda Monduli Juu Serikali itaijenga kwa lami kama Rais alivyoahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la mwisho ambalo naiomba Serikali iangalie ni upelekaji wa fedha za miradi katika barabara za Mkoa. Sisi tuna barabara moja ya

...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaomba utulivu ndani ya Bunge.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara ya Loksale tunaona imetengewa shilingi milioni mia tatu ambayo ina kilomita hamsini, haiwezi kusaidia chochote. Pamoja na kwamba kwa kweli tunampongeza Meneja wa Barabara wa Mkoa kwa sasa anafanya kazi nzuri na anasimamia miradi mingi ya Mkoa kuliko wakati mwingine wowote. Tunamshukuru na tunaendelea kumuunga mkono katika hili, fedha mnazompelekea ni fedha kidogo sana hazitoshii tunaiomba Serikali ione namna ya kuongeza fedha katika Mfuko wa Barabara ili barabara zetu nyingi ambazo

bado ni vumbi ziweze kuitika kwa wakati wote, tusipofanya hivyo hata huduma zingine hazipatikana na huduma hizi tunazozitoa zitakuwa hazlwafikii wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Massare, dakika tano.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie katika Wizara hii ambayo kwa hakika sasa inatenda haki na inafanya kazi ambazo zinaonekana kwa kila mtu ikiwemo katika Jimbo langu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 164 wameonesha barabara hii ya Makongorosi hadi Mkiwa kipande cha Nolanga – Itigi – Mkiwa kilomita 56.9 zitajenga kwa kiwango cha lami. Shida kubwa iliyopo pale tayari ujenzi unakaribia kuanza, lakini mpaka sasa hivi hakuna ufidiaji kwa maana ya *compensation* kwa wale ambao wanaafuatwa na barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri sasa azingatie kwamba wanapokwenda kujenga barabara, kuna wananchi wa Itigi ambao wamefuatwa na barabara hii ambayo ni kubwa inayojengwa mwaka huu, waweze kulipwa mapema kuondoa usumbufu ambao utajitekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Wizara hii kwa kazi nyingi ilizofanya, lakini katika Jimbo langu kuna changamoto kidogo. Mheshimiwa Waziri, Profesa Mbarawa wakati anatembelea barabara hii kutoka Mbeya hadi Itigi alikutana na changamoto kubwa sana ya mawasiliano. Kuna shida, hakuna minara ya mawasiliano maeneo mengi, kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri akumbuke maeneo yale aliyopita kutokea kule Rungwa, Mwamageme, Kintanula na maeneo ya Vijiji vya Mkao wa

Tabora ambavyo katikati yake vinaingiliana na eneo hili hadi kufika Kalangali. Maeneo haya mwenyewe aliona mawasiliano ni shida. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuwakumbusha waweze kuliona Jimbo la Manyoni Magharibi, kwa kweli mtandao wa barabara utasaidia lakini pia mawasiliano ni shida, hilo tu nilitaka kukumbusha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze pia Serikali yangu kwa kuamua kujenga reli ya kiwango cha *standard gauge*, pale walipoanza lakini naomba sasa wafanye jithada wasogee ifike hadi Itigi kwa kipindi kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali nampongeza Waziri kwa hotuba nzuri ya Bajeti yenyeye mwelekeo wa kuipeleka nchi yetu katika ngazi nyingine. Nawapongeza pia Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na Watumishi wote wa Wizara kwa kujituma, hali inayopelekea utekelezaji mzuri wa llani ya Chama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuendelea na mkakati wa ujenzi wa Bandari ya Mbegani Bagamoyo kama inavyooneshwa katika hotuba ya Waziri ukurasa 90. Jambo ambalo naliomba kwa niaba ya wananchi wa Bagamoyo ni kuwa, Serikali ijitahidi kumaliza malipo ya fidia kwa wanaopisha Mradi wa Bandari, pia kuwalipa fidia sahihi wale ambao wamegundulika kupunjwa fidia zao. Hiki ni kilio kikubwa kwa wananchi wanaopisha ujenzi wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kaya zipatazo 2,000 katika Kijiji cha Pande na Mlingotini zitahamishwa kupisha mradi wa Bandari. Kijiji chote cha Pande katika Kata ya Zinga kinafutwa kwenye ramani ya nchi pamoja na sehemu ya Kijiji

cha Mlingotini. Kaya hizi kuititia wafidiwa walihidiwa eneo la kuhamia katika shamba la Kidogoni Bagamoyo ambalo lilitengwa na Mamlaka ya EPZA tangu 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika makao hayo mapya ndiko kungehamishiwa miundombinu yao ya jamii ikiwemo Shule ya Msingi Pande, Zahanati ya Pande, Ofisi ya Kijiji Pande, Misikiti na Kanisa. Naomba Waziri aharakishe upatikanaji wa eneo la makazi mapya ya wananchi hawa wanaopisha mradi na pia Serikali iwajengee katika makazi mapya miundombinu yao ya huduma za jamii zikiwemo shule, zahanati na kadhalika ambavyo vitavunjwa kupisha mradi. Ni zoezi gumu kaya 2,000 kujitafutia zenyewe mahali pa kuishi. Kwa vile ilikuwa ni ahadi ya Serikali, naomba Mheshimiwa Waziri alisimamie jambo hili muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaofidiwa kwa ajili ya bandari jumla yao ni 2,211. Ukitoa taasisi na wananchi wasioishi Kijiji cha Pande na Mlingotini, kaya zinazohamishwa ni karibu 2,000. Kijiji kizima cha pande kinavunjwa na sehemu ya kijiji cha Mlingotini. Hizi ni kaya nyingi. Mwaka 2013 wananchi hawa walihidiwa eneo la makazi mpya lilitengwa na EPZA, shamba la Kidagoni. Ila kwa sasa hakuna dalili ya utekelezaji wa ahadi hii na wananchi wamepatwa na wasiwasi mkubwa! Naomba Mheshimiwa Waziri atuamble: Je, kaya hizi 2,000 zinazopisha mradi, zitapatiwa eneo la makazi mapya? Lini? Kwa Bajeti ipi? Naomba Mheshimiwa Waziri atupe jibu lenye matumaini ili kaya hizi zisige kuishi kuwa omboaomba mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fidia ya shilingi bilioni 57,670/= imelipwa shilingi bilioni 45. *Balance* ya fidia ya wanaopisha bandari haionekani katika vitabu vy'a bajeti. Je, fidia hii italipwa? Pia kuna wananchi 687 waliothibitika kupunjwa fidia zao na uhakiki umefanywa na Mthamini Mkuu. Wananchi hao wanategemea malipo halali ya fidia zao, lakini fedha hizo sizioni. Mheshimiwa Waziri atueleze kama wananchi hao watalipwa mapunjo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Bandari Bagamoyo ni mradi mkubwa na wenye manufaa makubwa kwa nchi yetu. Bandari hii ndiyo itakayoipa maana reli ya *standard gauge* inayojengwa. Hesabu za kiuchumi za reli mpya zitakuwa tofauti sana, reli hiyo ikiunganishwa na Bandari ya Bagamoyo. Naiomba Serikali yangu itenye fedha kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya Bagamoyo badala ya kuwaachia wawekezaji peke yao. Katika mradi mkubwa kama huu, Serikali iwekeze fedha zake ili iweze kuwa mshiriki kikamilifu katika mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na kazi nzuri ya ujenzi wa miundombinu ya maendeleo ya nchi yetu. Katika ukurasa wa 90 wa hotuba ya Waziri ametaja maandalizi ya ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo. Hili ni jambo zuri sana, bandari kubwa yenye uwezo wa kuhudumia shehena nyingi kwa nchi yetu na nchi jirani, ni nyenzo kubwa ya maendeleo ya uchumi wa nchi ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu, kauli hii ya ujenzi wa bandari haina bajeti. Maandalizi haya ya ujenzi wa bandari yatafanywa vipi? Waziri atueleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia Wizara hii muhimu kwa ujenzi wa uchumi wa nchi yetu. Nchi yoyote ile yenye miundombinu imara ya reli, barabara na anga, basi ni dhahiri uchumi wake huwa imara. Bila kuwa na miundombinu imara, kamwe hatutaweza kufikia Tanzania ya Viwanda kama ilivyo dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano. Tuwe na barabara zenye kuwezesha usafirishaji wa malighafi kwenda viwandani na kuwezesha mazao kwenda sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuwa na reli imara itakayoweza kusafirisha mizigo na kupunguza uharibifu wa barabara zetu, lakini kuweza kusafirisha mizigo mingi kwa wakati mmoja, kusafirisha abiria kwa wingi na kwa muda

mfupi. Vile vile tuwe na miundombinu ya anga imara ili tuweze kupokea ndege nyingi toka Mataifa mbalimbali hasa kwenye Majiji kama Dar es Salaam, Kilimanjaro, Arusha, Mbeya na Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa niweke msisitizo kwenye Uwanja wa Ndege wa Musoma tuwekewe lami kwenye *runways* na hata kupanuliwe ikiwezekana. Uwanja wa Ndege wa Mugumu Serengeti, ni wakati muafaka ukamalizika ili kuweza kuinua uchumi wa Mara kwa kuongeza idadi ya watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa bado kwenye dhamira ya kukuza utalii, ni vyema Serikali ikafanya tafiti za kina ni nini kilipelekea Shirika letu la ATCL kufanya vibaya toka kuwa na ndege kubwa zaidi ya kumi hadi kuwa na kandege ka kukodi? Sababu awamu hii Serikali limeamua kufufua ATCL kwa kununua ndege, basi ni vyema Menejimenti ya Shirika hili iweze kufumuliwa na kuundwa upya kwa kuweka wafanyakazi wenye weledi na dhamira ya kuendesha Shirika hili na kuona tunakuwa na *National Carrier* itakayoitangaza nchi yetu na hivyo kuongeza idadi ya watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa lisilokuwa na ndege zake, basi daima uchumi utayumba. Ni dhamira yangu na nadhani matumaini ya Watanzania wengi akiwemo Mheshimiwa Rais kuona tunakuwa na ndege zetu na hivyo kukuza uchumi wetu. Angalizo ni kwamba tuzingatie kanuni, taratibu za manunzi na kuepuka kununua ndege kwa *cash money*.

Mhesimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kwamba ujenzi wa barabara ya kuanzia Tarime Mjini kwenda Nyamwaga - Mto Mara hadi Ngorongoro, ijengwe kwa kiwango cha lami ili kuweza kurahisisha usafirishaji wa chakula katika Tarime na Wilaya ya Serengeti. Pia kukuza uchumi kupitia utalii, kwani watalii wengi hupitia Sirari kutoka Kenya na kupita njia hii kwenda Serengeti, Mbuga ambayo ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu la Tarime Mjini na hata Majimbo mengine, tunaomba *TANROADs*

wanapojenga barabara, basi wawe wanaingia angalau mita 20, kama kanuni inavyoolekeza, maana Jimboni kwangu barabara unganishi na *TANROADs* zimekatika kwenye maungio na kusababisha adha kubwa sana kwa watumiaji. Pia na uchimbaji wa mitaro ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. MAHAMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii nyeti katika uchumi wa wa nchi yetu. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajielekeza katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza barabara ya Kinyanambo A – Isalavanu – Sadani – Madibira - mpaka Rujewa yenye urefu wa kilometra 141 ambayo imekuwa inawekwa katika llani ya Uchaguzi za mwaka 2000, 2005, 2010, 2015. Cha kusikitisha, hata kilometra moja haijawahi kujengwa kwa kiwango cha lami. Naomba sana Mheshimiwa Waziri anapokuja kuhitimisha bajeti hii, atupe maelezo ya kina, sababu zinazofanya barabara hii isianze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, barabara ya kutoka Mtili – Ifwagi – Mdabalo – Ihanu – Isipii mpaka Mpanga *TAZARA* – Mlimba; barabara hii inaunganisha Wilaya ya Mufindi na Kilombero Mkoa wa Iringa na Morogoro. Vikao vyote muhimu katika kupandisha hadhi barabara hii vimefanyika mwaka 2013 na Mheshimiwa Rais ambaye alikuwa Waziri wakati huo anajua. Cha kusikitisha, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa ameandika barua mara nyingi Wizarani lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Ni vyema Mheshimiwa Waziri atuambie

kwa nini hajatuma wataalam wake mpaka leo? Barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu hasa wakazi wa Tarafa ya Ifwagi ambako kuna misitu mikubwa na viwanda vya chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka *John Corner* mpaka Mgololo ni barabara muhimu sana na fedha inayotumika kufanya matengenezo ni kubwa sana. Ni vema Serikali sasa ikaanza kutengeneza hata kilometra mbili mbili tu kila mwaka kuliko kuendelea kutenga fedha za kila mwaka kwenye matengenezo ya changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa Serikali kukubali kurudisha Kituo cha Reli cha Mpanga *TAZARA*, lakini naomba sana, kituo hiki pamoja na kile cha Kimbwa kifanyiwe ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie pamoja na minara iliyojengwa lkweha na Igunzi, lakini wananchi hawapati mawasiliano katika Jimbo hili. Pili, minara iliyojengwa Mapanda na Isipii haisaidii wananchi waliopo kwenye maeneo husika kupata huduma hii muhimu ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema sasa Serikali ikanza Ujenzi wa *Airport* ya Nduli pamoja na barabara ya Ruaha *National Park* ambayo ni muhimu sana kwa utalii katika nyanda za juu kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na mwingi wa huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya Rais katika Serikali ya Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Kikwete aliahidi kujenga barabara ya Singino (Kwamkocho) - Kivinje ya urefu wa kilometra 4.2, barabara hiyo inaelekea katika Hospitali ya Wilaya. Ahadi hiyo ilitolewa na Mheshimiwa Rais wa Awamu

ya Nne kwa umuhimu wa barabara hiyo ya kiwango cha lami, lakini kwa bahati mbaya mpaka leo, hiyo barabara ni tazito. Katika bajeti ya 2016/2017, ilipitishiwa sh. 800,000,000/= kwa ajili ya kumalizia barabara hiyo lakini hadi leo hakuna kilichopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli, mwaka huu wakati alipotutembelea nilitoa kilio changu hiki cha barabara ya kiwango cha lami katika Hosopitali ya Wilaya. Alimwagiza Meneja wa *TANROAD* Mkoa wa Lindi amalize kero hii ya muda mrefu. Kwa heshima na taadhima naomba fedha ya bajeti ya 2016/2017, sh. 800,000,000/= zipatikane ili mradi huu wa barabara muhimu ya Kwamkocho - Kivinje ikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, pia asimamie agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli aliyogiza Nangurukuru kuwa Meneja wa *TANROAD* kuwa awasiliane na Wizara ili kero hii imalizike. Naomba kwa heshima na taadhima asimamie barabara hii muhimu kwa ajili ya faida ya kuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujaona katika bajeti hii mwendelezo wa Uwanja wa Ndege na Bandari ya Kilwa Masoko. Naomba katika majumuisho ya Mheshimiwa Waziri anipatie taarifa ya Uwanja wa Ndege na Bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vile vile Mheshimiwa Waziri anifahamishe, malipo ya wananchi waliotathminiwa katika eneo la Uwanja wa Ndege. Katika majumuisho yake napenda kujua malipo ya wananchi hawa kwa muda sasa wa miaka mitatu hawajalipwa, ni lini watalipwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kusisitiza:-

(a) Barabara ya Kwamkocho – Hospitali, ambayo ni ahadi ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Kikwete.

- (b) Bandari na uwanja wa ndege.
- (c) Malipo ya wananchi walio tathminiwa katika eneo la Uwanja wa Ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi katika hizo kero zangu na naomba kuwasilisha.

MHE. OMARI A. KIGODA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa jitihada wanazofanya katika kuimarisha miundombinu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mikakati ya nchi ni kuhakikisha barabara za kufungua mikoa zinafanyiwa kazi kwa kujengwa kwa kiwango cha lami ili kuinua uchumi wetu katika Sekta ya Usafirishaji.

Mheshimiwa barabara ya Magole - Mziha - Handeni ni moja ya barabara zilizopo kwenye mpango huo. Licha ya kuwa kwenye mpango mkakati, pia ni barabara iliyopo kwenye llani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara kwa kutengea fedha kipande kilichobaki ambacho ni kidogo sana. Mwaka 2016 katika bajeti tuliamiwa Mkandarasi anadai; naomba Mheshimiwa Waziri akija kujumuisha, atufafanilie ile shilingi milioni 100 iliyotengewa ile barabara ni ya matumizi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kupata ufanuzi, shilingi milioni 500 iliyotengewa barabara ya Handeni – Kiberashi – Kibaya – Singida ni kwa matumizi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuunga mkono hoja.

MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Newala -Kitangari – Mtama inahudumiwa na *TANROADS*. Hii barabara inaunganisha

Mkoa wa Mtwara na Lindi, lakini ni barabara ya vumbi. Wananchi wa Newala wanaomba barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami, maana pia ndiyo njia kuu wanayotumia watu wa Newala kwenda Dare es Salaam na Dodoma. Tunashukuru kwa jitihada za Serikali maana sehemu korofi kama za Kitangari na mlima Kinolombedo zimejengwa kwa kiwango cha lami. Ni vizuri kuongeza kilomita zilizojengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu Uwanja mpya wa Ndege wa Newala. Baada ya eneo la Uwanja wa Ndege wa zamani kupima viwanja, Uongozi wa Wilaya umetenga eneo jipya la Uwanja wa Ndege. Wataalam wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege walitembelea Newala na kuelekeza ukubwa unaohitajika na mwelekeo wa Uwanja. Nilipouliza swalii Bungeni, Mheshimiwa Waziri alinijibu kuwa Serikali italipa fidia eneo la uwanja, wakati inafanya mipango ya Ujenzi. Wananchi wa Newala wanaomba Serikali ilipe fidia eneo la Uwanja wa Ndege ambalo halina mazao mengi ya kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami toka Newala Mjini kuelekea Masasi palitengenezwa mfereji wa kutolea maji barabarani. Mfereji huu umeleta uharibifu mkubwa kwa kutengeneza korongo kubwa zinazotishia usalama wa nyumba za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika katika Kijiji cha Mkunyu, korongo kubwa liliilosababishwa na mvua linahatarisha usalama wa nyumba za wananchi. Alipotembelea Wilaya ya Newala, Mheshimiwa Waziri Mbarawa alikagua eneo la korongo la Newala Mjini, akaahidi kutafuta fedha za kujenga makorongo hayo vizuri. Wananchi wa Newala tunakumbusha ahadi ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali kuzingatia mambo muhimu yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa Reli ya Kati; Dar es Salaam – Kigoma ndiyo Reli ya Kati. Matawi yake ni Tabora – Mwanza; Kaliua – Mpanda - Kasanga *Port*, Uvinza - Msongati (Burundi) na Isaka - Keza. Uchumi wa reli na hasa reli ya *standard gauge* ni kubeba mzigo mbito, siyo kubeba samaki wala abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhalii dhamira ya ujenzi wa reli ya kati izingatie msingi wa uchumi. Mzigo zaidi ya tani millioni 40 zipo nchi jirani ya *DRC* na zaldi ya mzigo tani milioni 10 zipo kwenye *deposit* ya Msongati katika *Province* ya Kusini Mashariki mwa Burundi. Mzigo upo *DRC* na sasa Burundi; na njia rahisi ya kwenda bandarini ipo kupitia Kigoma - Dar es Salaam. *Economic of Geography* zizingatiwe. Matawi yaliyobaki ya Tabora/Mwanza na Isaka -Keza yasubiri! Iwe *Second lot*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kidahwe – Kasulu - Kikondo na Nyakanazi, *speed* ya ujenzi wake inatia shaka sana. Kipande cha kilometra 50 cha Kidahwe - Nyumbigwa kimetumia sasa miaka saba. Naomba sana Serikali iharakishe ujenzi huo. Aidha, kutoka Nyumbigwa hadi Kasulu Mjini ni kilometra 9 - 10 hivi. Nashauri Mkandarasi aongezewe hizo kilometra 9 - 10 ili barabara hiyo ifike Kasulu Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Manyovu – Kasulu – Kibondo – Kabingo, usanifu wake na ujenzi wake unaanza lini? Tusubiri kwa miaka mingapi? Ishirini tena ijayo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Kamati inaonesha Shirika letu la *ATCL* siyo mwanachama wa *AITA*. Je, taarifa

hizi ni za kweli? Kama ni kweli, nini maana yake hasa kiusalama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ushauri uzingatiwe na Serikali itoe majibu yaliyo sahihi.

MHE. JOYCE J. MUKYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya mawasiliano katika Wilaya ya Ngorongoro imekuwa ya muda mrefu sasa na viongozi wamekuwa wanakuja kila mara na kuahidi kulishughulikia, lakini hawafanyi hivyo. Mfano, katika Kijiji cha Ngarasero, changamoto hii imekuwa ya muda mrefu sana. Tatizo la mtandao limekuwa sugu sasa na kufanya wananchi wanaoishi katika kijiji hiki kukosa mawasiliano ya redio tu. Naishauri sana Serikali ishirikiane katika kijiji hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ATCL*; pamoja na mafanikio yaliyooneshwa na *ATCL*, inabidi Serikali iweke mikakati madhubuti ya soko ili kuifanya Kampuni ijideshe kibashara na kuletea nchi yetu mafaniko makubwa kiuchumi kupitia Sekta ya Usafiri wa Anga. Lazima Serikali iangalie ni mikakati ipi iliyotumika na nchi nyingine ambazo zimefanikiwa kuijendeleza kiuchumi kupitia huduma ya usafiri wa anga, mfano Ethiopia, Rwanda na *UAE*. Ni lazima kuwa na mikakati ambayo italeta ushindani baina ya makampuni mengine yaliyomo ndani ya nchi yetu ya Tanzania ikiwemo kubadili sheria ambazo zinabeba Kampuni nyingine ambazo zinafanya biashara sawa na siyo wazawa kama ilivyo *ATCL*. Mfano, Kampuni ya *Fastjet*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa kuwa hata fedha za mtaji wa kuanzia hazijatolewa zote na hata zinazotolewa, zinatolewa kwa kuchelewa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madeni ya *ATCL*, tumeona ahadi ya kuchukua madeni yaliyopatikana kwa ujisadi na uzembe ikitolewa bila kutimizwa kwa kipindi kirefu na kuifanya *ATCL* ianze kutumia mapato yake kulipia uzembe

huu uliosababishwa na mipango mibaya ya usimamizi mbaya wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kubinafsisha *ATCL* kwa Shirika la Ndege la SA (Afrika Kusini), mali nydingi za *ATCL* zilichukuliwa na Serikali na nyingine kuuzwa. Hii inalifanya shirika sasa kutokuwa na mali zake binafsi na kusababisha kuongezeka kwa gharama za juu za uendeshaji. Naiomba Serikali isaidie kurudisha mali hizi ili kulipunguzia shirika mzigo mkubwa sana wa kiuendeshaji ukizingatia *ATCL* ndio kwanza inaanza kufanya kazi. Tatizo hili linaweza kuifanya Kampuni hii kufilisika tena na hatimaye kuwa *ATCL* tena kama ilivyokuwa huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itueleze, mali ziko wapi hasa? Kwa nani na lini zitarudishwa ili kuweza kulisaidia shirika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naomba kuwasilisha.

MHE. ZAYNABU M. VULU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kuwa miongoni mwa wanaochangia hoja hii kwa bajeti hii ya 2017/2018. Naanza kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa jinsi inavyotenga fedha na kuendeleza miundombini mbalimbali ya barabara, madaraja na mawasiliano. Pia pongezi kwa Waziri, Mheshimiwa Profesa Mbarawa kwa umakini na ufuatiliaji wa karibu sana katika miradi yote na bila ya kuchoka, yeye na wasaidizi wake hatimaye kuona kila liliopangwa linakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa Mbunge toka Mkao wa Pwani na kuona jinsi ambavyo nachangia kuomba kujengewa barabara za lami katika wilaya zilizozopo Mkao wa Pwani, ikiwemo barabara ya Kisarawe – Vikumburu – Mlandizi – Maneromango. Hii imekuwa adha kubwa sana

kwa wananchi wa huko hasa nyakati za mvua. Awamu zote katika ilani yetu imekuwa ikiahidi lakini hadi leo haijafika kokote. Naomba sana, barabara hii ipatiwe fungu la kutosha na kuweza kujenga. Je, ni lini ujenzi huo utaanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, pia naomba ahadi za Marais wetu zitimizwe, kwani barabara ya Nyamwage – Utete - Mkuranga – Kisiju – Bungu – Nyamisati, hizi barabara ni muhimu sana kwa wananchi wa maeneo hayo na hata kwa wasafiri wengine na kukuza biashara na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa ujenzi wa reli (*standard gauge*) ambayo Mkoa wa Pwani tutasaidiwa kwa maana mbili; ajira, usafiri na uuzaji wa vyakula na hiyo itainua kipato cha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mkiwa maeneo hayo ya ujenzi, kipaumbele cha ajira kianze kwa wananchi walioko jirani na ujenzi wa hiyo reli.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mungu ambaye amenipa nafasi hii kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambayo ni muhimu kwa Taifa letu. Pia naipongeza Serikali yangu kwa kazi nzuri zinazofanyika. Nampongeza kipekee Raís wangu na timu yake kwa muda mfupi, wameonesha uwezo mkubwa kuwatumikia Watanzania hasa hasa wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kazi nzuri wanazozifanya. Kweli naiona Tanzania mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa sababu sisi ni mashahidi, muda mfupi tumeona *hostel* za Chuo Kikuu Dar es Salaam zimekamilika, usafiri wa mwendo kasi,

barabara za juu Dar es Salaam, tumeshuhudia reli ya *standard gauge*, zinaanza kujengwa na mengine mengi. Hakika hapa kazi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jimbo la Kyerwa, naongelea suala la mawasiliano siyo mazuri. Upande wa mawasiliano ya simu, maeneo mengine hakuna mtandao wa simu, mawasiliano yote yanaenda au yanaingiliwa na mitandao ya nchi jirani, yaani nchi ya Uganda na Rwanda. Naomba sana Wizara ishughulikie tatizo hili ili tupate mawasiliano ya uhakika ukilinganisha na umuhimu wa mawasiliano na ya kuwa tunapakana na nchi jirani jambo ambalo kiusalama siyo nzuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la barabara zangu za Wilaya ya Kyerwa. Nikumbushe ahadi ya ujenzi wa barabara ya Mgakorongo - Kigarama mpaka Murongo wa kiwango cha lami, ambapo Mheshimiwa Waziri akijibu swalii nililouliza; ni lini ujenzi utaanza na ahadi ya Mheshimiwa Waziri alisema *before June, 2017* ujenzi utakuwa umeanza. Namwomba Mheshimiwa Waziri ahadi hiyo itimizwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iangalie kwa makini matengenezo ya barabara ya Murushaka mpaka Murongo ambapo barabara hii imekuwa ikisahaulika sana kufanyiwa matengenezo. Kwa sababu barabara ya Murushaka mpaka Murongo ni ya kiuchumi zaidi ya asilimia 75 ya magari yanayotumia barabara hiyo, ingawa imepewa kipaumbele cha pili kujengwa kwa kiwango cha lami. Naiomba Wizara barabara hii kwa sababu ya umuhimu wake katika kipindi hiki ambacho haijafikiwa kujengwa kiwango cha lami, Serikali iweke changarawe kuepusha usumbufu tunaoupata katika kipindi cha mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alipokuja Kyerwa aliwaahidi Wanakyerwa kilometra tano zijengwe Kata ya Nkwenda; nimejaribu kufuatilia lakini mpaka sasa hakuna mwenye jibu kamili. Naomba sana Mheshimiwa Waziri atupatie lami, hizi kilometra tano zijengwe ili kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais na lami hii ni muhimu kisiasa. Pia

namwomba sana Mheshimiwa Waziri atukamilishie kuweka lami kwenye mlima Rubunuka pande zote kuondoa usumbufo wa magari kukwama kipindi cha Mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuipunguzia mzigoto Halmashauri, tunayo barabara ya Nkwenda mpaka Mabila ambayo imejengwa kwa kiwango cha changarawe. Tunaomba ipelekwe *TANROADs* kwa sababu ya umuhimu wake kwa Wanakyerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuandika hayo, narudia kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri inazofanya. Tunawaombea sana Mungu awafanikishe katika yote mpate fedha ili na sisi Kyerwa tuone lami halisi katika barabara ya Mugakorongo – Murongo - Murushaka na Murongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na *team* yake yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda mrefu sana naomba kupandishwa hadhi kwa barabara inayoanzia Mlalo – Ngwelo – Mlole – Makanya – Milingano hadi Mashewa. Kilio changu hiki mpaka sasa hakijapata ufumbuzi; na barabara hii ni barabara ya uchumi ambayo ikifunguka itakuwa inachangia pato kubwa katika Serikali pamoja na Halmashauri yangu. Pia kutoa ajira kwa vijana, maana vijana wangu wamejajiri katika suala zima la kilimo. Mazao yao yanaharibikia mashambani kwa sababu ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtaji huu, vijana wengi wanakata tamaa ya kulima na kukimbilia mjini. Barabara hii ina kilometra 58 tu ambayo inaunganisha Majimbo matano, yaani Jimbo la Mlalo, Lushoto, Bumbuli, Korogwe Vijiji mpaka Mkinga. Naiomba Serikali yangu sikuvi itshe sasa, naomba barabara hii ipandishwe hadhi. Pia siyo vizuri Mbunge kuwaahidi wananchi wake kuwa barabara hii

itapandishwa hadhi, lakini mpaka sasa hakuna hata dalili. Kwa hiyo, naomba Serikali itoe majibu leo baada ya kuhitimisha taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya kilometa 16 inayoanzia Doch iadi Ngulwi mpaka Mombo. Nay o hii ni kilio cha muda mrefu sana na barabara hii ni muhimu sana. Kama unavyojuu, Lushoto ina barabara moja tu ya kuingia Lushoto Mjini. Kwa hiyo, barabara hii ikipandishwa hadhi itasaidia sana Mji waLushoto, utakuwa unafikika kwa wakati wote. Kwa hiyo, naomba Serikali yangu Tukufu ipandishe hadhi barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, barabara inayoanzia Mombo, Soni hadi Lushoto. Alitokea kiongozi mmoja na kutoa tamko kuwa barabara hiyo ipite magari ya uzito wa tani 10 tu. Kauli hii imesababisha ugumu wa maisha kwa wananchi wa Wilaya ya Lushoto. Kwani biashara zilizo nyingi zinauza bidhaa kwa bei ya juu na wananchi wa Lushoto kununua bidhaa hizo kwa bei ya juu kutokana na kuingizwa kwa bidhaa hizo kwa bei ghali. Wakati huo huo magari yenye uzito wa tani 40 yanapita, bila kuathiri au kuharibu barabara hiyo. Kwa mfano, magreda, magari yanayobeba *materials* yanayoenda Mtwara kwenye kiwanda cha Sementi cha Dangote. Pamoja na hayo nilimuuliza Meneja wa *TANROADs* Mkoa wa Tanga na akaniambia barabara hiyo inaweza kubeba gari lenye uwezo wa tani 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Waziri atoe tamko la kuruhusu kupita magari yenye uzito usiozidi tani 40 kwani suala hili limesababisha uchumi wa Lushoto kushuka na kunilalamikia mimi Mbunge wao kila siku. Naomba Waziri atoe tamko leo hii zaidi ya hapo nitashika shilingi ya mshahara wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri sijaona bajeti ya daraja la Mshizii pamoja na bajeti ya barabara yake ya kutoka Nyasa kuititia Gare

hadi Magamba. Kwani barabara hii ni mbadala, kukiokoea breakdownya Magamba Lushoto, magari yanatoa huduma kupitia njia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi ya Wilaya ya Lushoto ni ya milima na mabonde, kwa hiyo, minara ya simu baadhi ya maeneo hakuna. Kwa hiyo, naiomba Serikali itujengee minara hasa katika Kata ya Makanya, Malibwi, Ubiri, Ngwelo, Kwekanga na Kilole.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la upimaji wa barabara, yaani kutoa kilometra 30 kila upande, yaani jumla mita 60. Hili naomba niishauri Serikali yangu Tukufu kwamba iangalie maeneo mfano, maeneo ya Lushoto, Serikali ikisema itoe mita 60 itapata hasara kubwa. Ushauri wangu ni kwamba kuna baadhi ya maeneo kama Lushoto yajengewe kulingana na yalivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne ya kilometra nne za lami. Mpaka sasa hivi bado ahadi hiyo hajatekelezeka na ni takriban miaka minne sasa imepita. Naomba Serikali yangu itupatie ahadi hiyo ya Rais ili Mji wetu wa Lushoto angalau nao upendeze na tuwe tunajivunia na kumkumbuka Mstaafu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Naomba pia nipatiwe majibu haraka iwezekanavyo, maana wananchi mpaka sasa wanakosa uvumilivu kwangu, kwani wanadai nimewadanganya kwa muda mrefu sana.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii kutoa mchango wangu kwa kuandika katika Wizara hii. Pia napenda kuchukua fursa hii kutoa pongezi zangu kwa Serikali yetu namna inavyotekeliza kwa kasi ahadi zake na huduma za jamii. Vile vile, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na Watendaji wake kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kwa juhudzi zake za kujenga barabara na madaraja. Hii ni azma nzuri ya kuwarahisishia wananchi usafiri wa kupeleka mazao yao katika sehemu moja kwenda nyingine. Ushauri wangu katika jambo hili ni kushauri Serikali iwe makini katika kuwasimamia Makandarasi ili kukidhi viwango vya miundombinu hii. Miundombinu hii itakapokidhi viwango, itaiepushia Serikali gharama za ukarabati wa muda mfupi baada ya kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Posta Tanzania (*TCL*) ni chombo muhimu katika kila nchi pamoja na Tanzania. Naipongeza Serikali kwa kuonesha nia ya kuliboresha shirika hili. Ushauri wangu katika uimarishaji wa shirika hili ni kwamba Serikali ilipatie shirika vifaa vya kisasa ili kwenda sambamba na ushahidi mkubwa uliopo katika wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kusaini ujenzi wa gati moja la Bandari ya Mtwara ambayo ndiyo chachu ya uchumi Kanda yote ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, *Mtwara Corridor* inategemea kwa kiasi kikubwa ujenzi huu wa bandari ulioanza kwa kusafisha maeneo ya ujenzi huo. Ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba, ahakikishe mara tu baada ya kumalizika ujenzi huo, basi magati mengine yawekwe kwenye orodha ya kujengwa ambayo ni matatu. Gati moja halitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba utanuzi wa bandari uendane na ujenzi wa reli ya Kusini ambayo itaanzia Mtwara – Liganga – Mchuchuma – Mbamba Bay na

nchi nyingine za Kusini mwa Afrika. Ujenzi wa reli hii utasaidia sana kufungua uchumi na Bandari yetu ya Mtwara itapata mizigo ya kutosha, hivyo kuliingizia Taifa pato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitandao ya simu kwa baadhi ya maeneo ya Mtwara Mjini haipo. Mfano, Mbawala Chini, Mkangala, Naulongo, Namayanga, Dimbuzi; maeneo haya *network* hakuna kabisa na yapo Mtwara Mjini. Sambamba na hilo, Mtwara Mjini hakuna network ya *TBC* kabisa. Hii inafanya Wanamtware wakose huduma ya taarifa mbalimbali hivyo kuwa nyuma ya wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Ulinzi; mwaka 2016 tuliongea sana juu ya umuhimu wa barabara hii ambayo inaanzia Mtwara Mjini mpaka Ruvuma. Tunaomba iwekwe kwenye bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Viwanja vya Ndege ambavyo havimilikiwi na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, naomba kujua, kwa nini Serikali imeruhusu hili? Haioni kama ni hatari kwa Taifa letu na uchumi? Naomba Wizara itoe tamko juu ya hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna eneo ambalo hivi sasa Jijini Dar es Salaam ambalo lina msongamano mkubwa kama Mbagala hasa njia panda ya Charamble. Hapa kuna ulazima wa kujenga *flyover* haraka sana. Naomba bajeti ieleze, ujenzi wake utaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya *Kilwa Road* hasa eneo la Somanga - Nangurukuru imeharibika sana na ina mashimo na mabonde makubwa na sioni ujenzi au ukarabati kabambe unafanyika hasa eneo hili. Tunaomba majibu ya Waziri ili nayo ianze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya uchumi imesainiwa kwa kilomita 50. Tunaomba Mkandarasi asimamiwe kama alivyosema Mheshimiwa Rais alipokuja

Mtwara Machi, 2017 na kusema kuwa Mkandarasi hayuko *sharp*, tunaomba asimamiwe barabara hii ijengwe haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa kuna utanuzi wa bandari unaanza, tunaomba Wanamtware Kusini tupatiwe usafiri wa meli hasa kwa ajili ya mizigo, kwa kuwa barabara inaharibika kwa *cement* kupitia barabara ya lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Ndege wa Mtwara ni mbovu, hauna taa za kuongozea ndege; ndege hazitui usiku na inaleta usumbufu sana sambamba na kudumaza uchumi. Naomba bajeti hii ianze kukarabati na kuweka taa katika bajeti hii.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpungeza mtoa hoja, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa na timu yote illyofanikisha mchakato wa Makadirio ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Mwenyekiti, barabara ya *Airport Access Road* - Kilindoni mpaka Utende Wilayani Mafia yenyeye urefu wa kilometra 14 pamoja na kukamilika kwake, lakini kwa masikitiko makubwa imejengwa chini ya kiwango. Ni matumaini yangu Mkandarasi atalazimishwa kuirudia barabara ile na hatua kali za kisheria zichukuliwe kwa kuitia hasara Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafia kutohana na jiografia yake kuwa ni kisiwa, tunategemea sana Uwanja wa Ndege. Ikitokea dharura hususan nyakati za usiku, ndege haziwezi kuruka kwa kuwa uwanja hauna taa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikitokea dharura ya mgonjwa kukimbizwa Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili, anaweza kupoteza maisha, kwani ili afike Dar es Salaam, atahitaji kusafiri kwa boti kwa takriban masaa nane hadi kumi ili afike katika Hospitali ya Rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, boti ya uokoaji katika Bandari za Kilindoni na Nyamisati ndiyo usafiri wa wengi katika

Kisiwa cha Mafia. Ila hatari kubwa iliyo mbele ni kwamba hatuna huduma za uokoaji, yaani *Coast guard* kutokana na idadi kubwa ya wasafiri kati ya bandari hizi mbili. Tunaiomba sana Serikali iweke Kituo cha *Coast guard* ili likitokea jambo la dharura waweze kutoa msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu boti ya abiria kati ya bandari ya Nyamisati na Kilindoni Mafia. Wananchi wa Mafia tupo katika wakati mgumu kwenye usafiri wa kuingia na kutoka Mafia. Tumejaribu kushawishi wafanyabiashara waje wawekeze kwenye usafiri wa baharini, lakini mwitikio mpaka sasa umekuwa ni hasi mno. Hivyo tunaiomba Serikali ichukue jukumu la kutuletea kivuko cha kisasa baina ya bandari hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwa kutenga kiasi cha shilingi bilioni 2.5 na *tender* ya ujenzi imeshatangazwa na ujenzi utaanza muda siyo mrefu. Kwa kuwa ujenzi utachukua zaidi ya mwaka, mazingira ya sasa ya bandari ile siyo mazuri kabisa. Hakuna vyoo, hakuna jengo la abiria na ngazi ya kupanda na kushukia abiria. Niliani barua kwa Katibu Mkuu wa Ujenzi kuomba ngazi iliyokuwa ya Dar es Salaam ambayo kwa sasa haitumiki ili itusaidie pale Nyamisati. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, wakati wa kujibu hoja, nipate ufanuzi juu ya ombi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara kutoka Kilindoni mpaka Rasi Mkumbi yenyeye urefu wa kilometra 55, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne aliahidi; na imo katika llani ya CCM 2015 -2020. Nimeangalia kwenye kitabu hiki sijaona fedha zozote zilizotengwa kwa ujenzi wa barabara hii. Naomba Mheshimiwa Waziri atupe majibu wananchi wa Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ELIAS J. KWANDIKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja. Naomba kuchangia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ahadi ya Rais, ujenzi wa barabara ya lami. Wakati wa kampeni Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliahidi ujenzi wa barabara ya lami kilometra 10 Ushetu. Je, barabara hii itajengwa lini ukizingatia Jimbo la Ushetu halina barabara hata mita moja? Zaidi kuna vumbi jingi sana Makao Makuu ya Halmashauri ya Ushetu. Naomba Serikali itilie mkazo ujenzi wa barabara kama Mheshimiwa Rais alivyoahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ujenzi wa minara ya mawasiliano. Halmashauri yetu ni mpya, tumefanikiwa kuwa na Wilaya ya Kipolisi, tumehamia Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya, Kijiji cha Nyamilangano, Kata ya Nyamilangano. Mawasiliano ni hafifu na tunapata shida kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ya TEHAMA yanakwama ikiwemo mfumo wa malipo na mifumo mingine ya Halmashauri ya Wilaya yetu. Inalazimika wakati mwingine kazi zifanyikie kwenye Halmashauri huko Mjini Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ya kudhibiti usalama kwa Jeshi letu la Polisi pamoja na ulinzi shirikishi; niliwahi kuwa na swalii nikaomba Kata za Nyamilangano, Uyogo, Chona, Ushetu na Kata nyingine, Serikali itsaide tupate minara ili tukimbizane na maendeleo katika Jimbo la Ushetu. Naomba sana *priority* iwe Makao Makuu, yaani Kijiji cha Nyamilangano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kupandisha hadhi barabara; tumekuwa na maombi ya kupandishiwa barabara hadi ya *TANROAD* barabara zinazounganisha mikoa hususani:-

(i) Barabara ya kutoka Tulelo - Mhulidede - Tabora kilometra 21. Barabara hii inaunganisha Mkoa wa Shinyanga na Tabora.

(ii) Barabara ya Chambo hadi Mambari. Barabara hii inaunganisha Mkoa wa Shinyanga hadi Tabora.

(iii) Barabara ya Masumbwe (Mbongwe – Geita), Mwabomba, Ulowa, Kaliua (Tabora). Barabara hii inaunganisha Mkoa wa Geita, Shinyanga hadi Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizi ni muhimu kwani maeneo haya yatachochea utalii, tutasafirisha mazao ya chakula na biashara na mambo mengi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kuhuisha Kamusi ya Barabara; naomba sana Wizara hii ihuishe Kamusi ya Barabara kwani inatunyima fursa ya kugawanya rasilimali vizuri. Mfano, Kamusi inayotumika, inaonyesha Ushetu ina mtandao wa barabara wa kilometra 416 tu wakati hali halisi tuna mtandao wa barabara kilometra 1,600. Tunaomba Serikali iboreshe Kamusi ya Barabara ili tushughulikie barabara na kupewa rasilimali kwa mtawanyiko ulio mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba mambo hayo manne yashughulikiwe. Ahsante na naunga mkono hoja.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa utendaji mzuri, yeye na Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji Waandamizi wa Wizara. Kazi inayofanywa na Wizara inaonekana na inaheshimiwa kwa umma wa Watanzania. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni kwangu nina barabara mbili za Kitosi - Wampembe yenye urefu wa kilometra 68 na ile ya Nkana – Kala yenye urefu wa kilometra 67. Barabara hizi zote mbili za Mkoa wa Rukwa, kupitia Bodi ya Barabara na RCC tuliomba zipandishwe hadhi na Kamati ya Kitaifa ilikuja na kuridhia. Aliyekuja ni Katibu Mkuu wa sasa wa TAMISEMI (Mussa Iyombe), lakini hazijapandishwa licha ya Serikali kupandisha hadhi barabara nyingi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba zipandishwe hasa ya Kitosi na Wampembe. Mheshimiwa Rais alitoa ahadi kusaidia barabara hizi na wakati alipokuwa Waziri, aliweza

pia kutoa fedha shilingi milioni 500 kwa barabara ya Kitosi na Wampembe kuboresha matengenezo. Nashangaa hamjaipatia fedha ya kutosha na inaenda mipakani. Naomba iongezewe fedha, sh. 84,000,000/= hazitoshi. Inaweza kusababisha barabara kufunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Kata ya Kala ipate mawasiliano ya simu. Ni Kata iliyoko mpakani mwa Ziwa Tanganyika. Nimefanya ufuatilaji mkubwa bila mafanikio. Je, ni lini Mheshimiwa Waziri atanisaidia Kala iwe na mawasiliano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari Kata ya Ninde, Wampembe na Kala ziko kando ya Ziwa Tanganyika, hazina bandari hata moja. Kuna umuhimu mkubwa kupata Bandari Wampembe na pia kujenga Gati Ninde na Kala ili wananchi waweze kupata huduma ya usafiri wa meli kwa usalama. Kwa hiyo, nawasilisha maombi Serikalini kuwa bandari ijengwe Wampembe na gati zijengwe Ninde na Kala. Ahsante.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji katika Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa miundombinu ya uhakika ya barabara katika maeneo ya vijiji una umuhimu mkubwa katika kufungua fursa za kiuchumi na hivyo kuharakisha maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapojojwekeia lengo la ujenzi wa barabara za lami kuunganisha Mkoa kwa Mkoa, tuna wajibu vile vile wa kutoa msukumo kwa barabara za aina hiyo zenyetumuhimu wa kimkakati katika usalama na kukuza fursa ya kuongeza/kuunganisha vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabokweni – Gombero – Maramba – Bombo Mtoni – Kitivo – Mlalo hadi Same ni

barabara mbadala ya kuunganisha Mkoa wa Tanga na Mkoa wa Kilimanjaro. Barabara hii inapita kwenye maeneo makuu ya uzalishaji mazao ya chakula na biashara. Ni barabara inayounganisha maeneo haya ya Bandari ya Tanga na nchi jirani ya Kenya. Aidha, kwa upande wa usalama wa nchi, barabara hii ni barabara ambayo ina umuhimu wa kiusalama kwa nchi yetu kutokana na ukweli kuwa inaambaa katika mpaka wetu na nchi ya Kenya. Hivyo, kufanya zoezi la kukagua na kulinda mpaka wetu kuwa na uhakika zaidi kinyume na ilivyo sasa ambavyo tunalazimika maeneo mengi kupitia Kenya ili kuweza kukagua mpaka wetu na Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mabokweni – Maramba – Bomba Mtoni – Mlalo hadi Same ni barabara muhimu kwa kukuza utalii, kwa kuunganisha Mbuga ya Saadani na Mkomazi ambayo inagusa Wilaya ya Mkinga eneo la Mwakijembe ambako yapo maeneo ya asili ya mazalla ya faru. Kwenye *Umba Game Reserve*, Wilaya ya Lushoto eneo la Mlalo hadi Wilaya ya Same kwenye Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kutaimarisha na kuunganisha Sekta ya Utalii siyo tu kwa Mbuga ya Sadaani na Mkomazi, bali kutaunganisha utalii kwa watalii kutoka Zanzibar kuweza kutembelea vivutio kutoka Saadani, Amani, *Nature Reserves*, Mapango ya Amboni hadi maeneo ya utalii ya Ngorongoro, Mlima Kilimanjaro na kadhalika. Aidha, barabara hii itavutia watalii toka Mombasa, Kenya; kuvutika kwa urahisi zaidi kuja Tanzania kupitia Horohoro, Mbuga ya Mkomazi kuanzia Mkinga hadi Kilimanjaro. Naiomba Serikali kuipa kipaumbele barabara hii kwa kuanza kufanya upembuzi yakinifu ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuanza ujenzi wa reli kwa *standard gauge*. Naishauri Serikali kwamba, umefika wakati sasa tuanze kuweka mfumo wa *infrastructure bond* katika ujenzi wa reli na barabara zetu. Nashauri tujifunze kwa wenzetu wa Nigeria, India na Israel katika kutumia *infrastructure bonds* katika kujenga miundombinu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kutenga shilingi milioni 865 kwa ajili ya fidia kwa wananchi katika barabara ya Tanga - Horohoro. Hata hivyo, naisihi Serikali ihakikishe fedha hizi zinapatikana kwa sababu hii imekuwa kero ya muda mrefu kwa wananchi. Aidha, ni vyema kukawa na ushirikishaji wa karibu kwa uongozi wa eneo husika pindi malipo yatakapokuwa yanafanyika ili kuhakikisha kila anayestahili kuliwa anapata haki yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kutenga fedha, shilingi millioni 120 ku-*upgrade* Mkinga *Township Road* kilometa nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nikikumbusha kuwa bado barabara ya *TANROADS* kuunganisha Maramba na Makao Makuu ya Wilaya katika Mji wa Kasero halijakamili. Aldha, eneo la Magoli bado ambalo barabara itapita pembeni ya Kijiji halijakamili.

MHE. DKT. GERTRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu wengi kwa kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa uongozi wake mzuri. Naomba nimpongeze kwa kipekee Waziri wa Ujenzi na wasaidizi wake wote kwa hotuba nzuri na kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa juhudzi za Mheshimiwa Rais wetu kutuletea Ndege mbili jumlisha nne, jumla yake sita. Hii imeturahisishia usafiri mikoani na imetuondolea aibu Kitaifa, nasi tuna ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa ujenzi wa daraja la Kilombero, limekamili na limekuwa kiunganishi kati ya Wilaya ya Kilombero na Ulanga. Ni ukombozi mkubwa, Tunampongeza Mheshimiwa Rais wetu na Mheshimiwa Waziri na timu yake. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kuona barabara ya Kidatu – Ifakara – Malinyi –Songea; Ifakara – *Kihansi Road*

zote ziko ndani ya Bajeti ya 2017/2018 na Dumila – Kilosa – Mikumi, kweli mnachapa kazi

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaombea Mungu awape uwezo na afya mfanikiwe, Mungu aibariki Wizara ya Ujenzi, Waziri wake na timu nzima. Amina.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo yangu ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kuna uwanja wa ndege ambaao kwa sasa umezilliwa kutumika kwa kuwa upo katika Kata ya Mji. Halmashauri imetenga eneo lingine la kujenga uwanja wa ndege. Hivyo tunaomba uwanja ule wa zamani upewe Halmashauri ili kujenga majengo ya huduma za jamii. Kwa kuwa eneo la Hospitali ya Wilaya limebana sana, hilo eneo linaweza kutumika kuongezea eneo la Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majengo ya Halmashauri ya Wilaya limebana, hivyo sehemu ya uwanja huo inaweza kusaidia Halmashauri ya Wilaya kuongeza majengo kwa ajili ya kutolea huduma. Magereza nao eneo limebana sana kiasi kwamba hawana uwezo wa kujenga chochote. Hivyo eneo hili litasaidia Magereza kupata eneo la kuongeza majengo hasa nyumba za Askari wa Magereza na nyumba za Askari Polisi. Hivyo, tunaliomba sana eneo hili likabidhiwe kwa Halmashauri ili litumike kuongeza majengo mbalimbali ya Halmashauri na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tunduru Kusini imepakana na Msumbiji kupitia Mto Ruvuma, maeneo mengi ya Vijiji hayana huduma ya simu. Maeneo hayo ni Makade, Msinji, Semei, Chikomo, Lukala, Misyaje, Mbati, Nasumba na Likweso. Naomba sana maeneo hayo yajengewe minara ya simu ili iwe rahisi kuwasiliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la usikivu wa redio katika Wilaya ya Tunduru *TBC*, haipatikani kabisa. Hivyo tunaomba mdau aliyejitokeza kuweka Kituo cha Redio Tunduru, apewe *frequency* haraka ili wananchi wa Tunduru wapate huduma ya redio, kwani ni muda mrefu sana anapeleka maombi lakini hajapewa kibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa barabara, Jimbo la Tunduru Kusini lina barabara kuu inaunganisha na Wilaya ya Namtumbo kutokea Mtwaro – Pachani – Lusewa – Lingusenguse – Nalasi mpaka Tunduru Mjini. Nashukuru kwa kipande cha Mtwaro – Pachani mpaka Nalasi, kipo katika mchakato wa upembuzi yakinifu. Hivyo naomba kipande kilichobaki cha Nalasi – Mbesa Tunduru chenye urefu wa kilomita 64 nacho kiingie kwenye mpango huu wa kufanya upembuzi yakinifu, tayari kwa kujengwa kwa kiwango cha lami kwani kipande hiki ni korofi na kinasumbua sana wakati wa kifuku na Tarafa hii ndiyo yenye idadi kubwa ya watu ambao wanatumia barabara kufuata huduma za kijamii Tunduru Mjini. Barabara hii ndiyo inayotumiwa na wananchi wa Tunduru kwenda kwenye Hospitali ya *Mission* Mbesa ambayo inahudumia zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wa Wilaya ya Tunduru pamoja na Wilaya jirani ya Namtumbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Njombe – Songea ina umri wa zaidi ya miaka 30 tangu ianze kutumika na sasa imechakaa sana, ina viraka vingi ambavyo vinaweza kusababisha magari kupata ajali. Barabara hii inapaswa ijengwe upya kwa kuwa ni muda mrefu sana na imechoka sana na sasa magari yanaumia sana kutokana na ubovu wa barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mji wa Tunduru kuna eneo la makutano ya barabara inayotoka Masasi na Songea (*cross road*). Mahali hapa panatakiwa kujenga *round about*, lakini kuna sheli imejengwa hapo kimakosa, kwa sababu ipo ndani ya eneo la barabara. Hivyo tunaomba sheli ile

ibomolewe na ijengwe *round about*, kwa sababu eneo hili limejengwa vibaya na linasababisha ajali za mara kwa mara na kusababisha vifo kutokana na makutano haya kujengwa bila mpangilio wa kiusalama kwa watumiaji.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa barabara ya kutoka Mlowo (Mbezi) kwenda Kamsamba (Momba) kuelekea Kilyamatundi (Kwela) hadi Kasansa na hatimaye Kibaoni (Katavi). Ni vyema Serikali itengeneze barabara hii kwa kiwango cha lami. Mosi, hii barabara inaunganisha Mikoa mitatu ya Songwe, Rukwa na Katavi na kwa kuwa ni Sera ya Serikali kutengeneza kwa kiwango cha lami barabara zinazounganisha mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wananchi wanaoishi maeneo yanayopitiwa na njia hii wanalima mazao ya kahawa, mpunga, mahindi, ufuta, alizeti, mtama, maharage na mazao mengineyo. Naishauri Serikali itengeneze barabara hii kwa kiwango cha lami ili wananchi waweze kusafirisha mazao yao kupeleka sokoni kirahisi. Soko kuu la mazao katika ukanda huu linapatikana Mlowo – Mbozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na barabara hiyo hapo juu, pia kuna barabara ya kutoka Mji Mdogo wa Mlowo, Wilaya ya Mbozi kupitia Vijiiji vya Shiwinga – Isansa - Magamba na kuelekea Kata ya Magamba, Wilaya ya Songwe. Hii barabara ni ya muhimu kwa sababu inaunganisha Halmashauri ya Mbozi na Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mazao mbalimbali kama vile kahawa, mahindi, maharage, alizeti, ufuta na mengineyo yatasafirishwa kirahisi. Pia makaa ya mawe yanayochimbwa Kijiji cha Magamba yatasafirishwa kirahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa usimamizi wa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kwa kazi nzuri inayofanya kusimamia ujenzi wa miundombinu

katika Taifa letu. Kazi yao ni nzuri sana. Namwomba Mungu awape nguvu na afya walipeleke Taifa la Tanzania kwenye nchi ya viwanda yenye miundombinu ya barabara za kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali, Jimbo la Igunga ni Jimbo ambalo halina barabara ya kuitika wakati wote (majira ya masika na kiangazi). Wananchi wa Jimbo la Igunga inapofika wakati wa masika (mvua) huwa hawana miundombinu ya barabara kuwawezesha kufika kwenye vijiji na hata kata za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, wakati nachangia hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba eneo la Wilaya ya Igunga miaka 60,000 kabla ya Kristo lilikuwa ziwa na lilikuwa ziwa na lilitauka kwa sababu za kijiolojia na kuacha tope jeusi ambalo wakati wa mvua huwa tope ambalo hufanya barabara kutopitika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa Halmashauri kujenga barabara inayohitaji ujenzi wa tuta kubwa kwa urefu mkubwa ni mdogo sana; matokeo yake barabara zinazounganisha vijiji na kata hazipitiki kabisa. Pia barabara zinazounganisha Wilaya za Meatu na Igunga, Kishapu na Igunga, Uyui na Igunga, hazipitiki kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Igunga linayo barabara moja tu ya lami ambayo ni barabara kuu ya Dar es Salaam kwenda Mwanza inayopita katikati ya Jimbo la Igunga. Pia Jimbo la Igunga lina kilometra zipatazo 10 tu za barabara ya changarawe inayotoka Kata ya Itunduru kwenda Kata ya Igurubi inayohudumiwa na TANROADs.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zote za Jimbo la Igunga zinahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Igunga yenye uwezo mdogo sana kifedha wa kujenga barabara za changarawe kwenye eneo la mbuga. Kimsingi Jimbo la Igunga halina barabara za vijijini na kwenye kata na hasa wakati wa masika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka 2012 Halmashauri ya Wilaya ya Igunga iliomba kupandishwa hadhi kwa barabara itokayo Igurubi (mpakani mwa Wilaya ya Kishapu) kuititia Igunga na Itumba kuelekea Loya na kufika Tura katika Wilaya ya Uyui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha tu ya kuwa barabara hii inapitika katika maeneo makubwa ya uchumi wa Mikoa ya Shinyanga na Tabora, sehemu ambazo wananchi wa maeneo hayo wanalima pamba, mpunga na tumbaku, lakini pia wanafuga ng'ombe kwa wingi. Kufunguliwa kwa barabara hii kutakuza uchumi wa Wilaya ya Igunga na Jimbo la Igunga, lakini pia uchumi wa Mikoa ya Tabora, Shinyanga na Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara kadhaa nimewahi kuuliza maswali humu Bungeni juu ya lini barabara hii inaweza kupandishwa hadhi ili kufungua Wilaya ya Igunga na kuunganisha Mikoa ya Shinyanga, Singida na Tabora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ikipandishwa hadhi, inaweza kujengwa kwa kiwango cha lami ikitokea Kolandoto kuititia Ukenyenge katika Jimbo la Kishapu na kuititia Igurubi hadi Mbutu - Igunga na Itumba katika Jimbo la Igunga kuelekea Miswaki - Loya hadi Turu katika Jimbo la Igalula. Barabara hii itaunganisha kwa upande wa kaskazini barabara ya lami itokayo Shinyanga kwenda Mwanza na kwa upande wa kusini barabara ya lami itokayo Manyoni kwenda Tabora. Kujengwa kwa barabara hii kwa kiwango cha lami kutaunganisha barabara hizi kuu za lami nchini kwetu na kufungua fursa za kiuchumi za Mikoa ya Tabora, Shinyanga na Singida. Fursa hizo ni pamoja na kilimo cha pamba, tumbaku, alizeti na mpunga, mazao yanayozalishwa kwa wingi katika mikoa hii. Pia biashara ya mifugo katika minada nayo itaimarika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwombwa sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ifike wakati atume wataalam wakaitathmini barabara hii muhimu kwa mikoa hii na ikiwezekana katika bajeti ya

mwaka huu wa fedha 2017/2018 tupate hata fedha kidogo za kufanya upembuzi yakinifu ili bajeti ijayo iweze kupandishwa hadhi na baadaye kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, barabara ya Kininginila – Mwabakima – Mwanyagula – Mbutu hadi Igunga nayo inao umuhimu wa pekee sana kwa sababu inaunganisha Wilaya ya Meatu katika Mkoa wa Simiyu na Wilaya ya Igunga Mkoani Tabora. Pia barabara hii inapitia katika maeneo ya kilimo cha pamba na ufugaji wa ng’ombe. Tunaomba barabara hii nayo kupandishwa hadhi kuwa ya *TANROADS*ili iweze kujengwa kwa kiwango cha changarawe na kuitika wakati wote ili kuwaondolea adha ya ukosefu wa miundombinu ya barabara hasa wakati wa masika wananchi wa Kata za Kininginila, Isakamaliwa, Mwamashimba, Mbutu na Igunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa barabara za kiwango cha changarawe chini ya usimamizi wa *TANROADS* katika Jimbo la Igunga ni changamoto kubwa inayosumbua na kukera sana wananchi wa Jimbo la Igunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa heshima kubwa, naiomba sana Serikali ilisaidie Jimbo la Igunga kupata barabara za kutosha za kiwango cha changarawe na kiwango cha lami ili kuwaondolea adha ya usafiri wananchi wa Jimbo la Igunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja.

MHE. DKT. HADJI H. MPONDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Naipongeza Serikali katika ukamilishaji wa daraja la Mto Kilombero. Hakika daraja hili ni ukombozi mkubwa sana kwa wakazi wa Wilaya ya Malinyi, Ulanga na Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliahidi kujenga na kumaliza barabara ya Ifakara – Lupiro – Malinyi – Kilosa Mpepo – Londo

–Namtumbo (Tl6) katika kiwango cha lami. Naiomba Serikali kutekeleza ahadi hii ya ujenzi wa kiwango cha lami kwa kuwa kuwa barabara hii inahudumia maeneo muhimu ya uzalishaji wa mazao ya nafaka (mpunga). Ni eneo ambalo Taifa linategemea chakula (mpunga). Hivyo kuwepo kwa barabara ya lami itaongeza tija sana kwa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii, aidha itakuwa ni njia ya mkato, hivyo kuokoa muda na fedha kwa wakazi wa Mikoa ya Ruvuma na Njombe kuja Dar es Salaam na Dodoma (*HQ*). Wakati mchakato wa ujenzi wa barabara ya lami (Tl6) unaendelea, naiomba Serikali kutoa kipaumbele na kuongeza bajeti ya ukarabati ya maeneo korofii, kwani fedha iliyotengwa haitoshi kabisa. Ni kipande cha kilomita 25 tu za changarawe, zimetengwa kwa urefu wa barabara yenyе urefu zaidi ya kilomita 300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Wilaya ya Malinyi ina changamoto ya mawasiliano ya simu katika Kata za Ngoheranga, Kilosa Mpepo, Biro na Sofi. Aidha, minara iliyotengwa na *TIGO* kuititia ruzuku ya *UCAF* haifanyi kazi kwa kiwango cha kuridhisha na baadhi ya minara hiyo haifanyi kazi kabisa kutokana na hitilafu/upungufu wa kiufundi. Ahsante.

MHE. NJALU D. SILANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Nawapongeza Wataalamu wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya na *TANROAD* kwa ufanisi mzuri wa kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie upande wa *marine*. Hii Taasisi ni kubwa, inazo meli 15 ambazo zinatakiwa zifanye kazi katika maziwa yetu matatu kwa maana ya Ziwa Nyasa, Tanganyika na Victoria. Hizi meli zinaweza zikafanya kazi katika maeneo haya na kupata mapato makubwa ya kuongeza kuwa *GDP*. Itasaidia kuongeza ufanisi wa maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika lina madeni ya wazabuni karibu shilingi bilioni saba. Pamoja na hayo, wafanyakazi nao hawajalipwa zaidi ya miezi 11. Hii inasababisha kukatisha tamaa watumishi wa Shirika hilo. Ikumbukwe hawa watumishi wanategemewa na familia zao. Fedha iliyotengwa mwaka 2016 kwenye bajeti ya shilingi bilioni 1.4 hajitatoka hata moja. Hii inasababisha watumishi kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi.

Pamoja na kuwa wanadai, wafanyakazi wamekuwa na moyo wa kizalendo wa kufufua meli moja inayoenda Ukerewe ambayo imeweza kusaidia wananchi kwa huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, Watumishi hao hawajalipia Bima za Afya tangu mwaka 2014. Wafanyakazi hawapati huduma za afya pamoja na michango ya Mashirika ya Umma; *NSSF* na *PPF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani na Shirika hili kubwa lili na meli 15 ambazo fedha nyingi zimetumika lakini hazifanyi kazi? Kwenye bajeti ilioisha Serikali ilitenga Bajeti ya shilingi bilioni 50 nayo hajapata hatma za fedha hizo zimefanya kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kwa kutenga fedha kilomita 49.7 toka Bariadi kwenda Maswa. Tunashukuru sana kwa kazi hiyo nzuri. Naipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi hiyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri mnayofanya kwa kufufua mashirika haya ya Serikali yanayoweza kuifanya nchi kuwa na mapato mengi. Mfano, *TRL*, *ATCL*, *TTCL* na *TPA*. *Marine* mkiitunza hakika nchi hii itakuwa inapata mapato mengi. Tunayo meli ya *MV Umoja* ina uwezo mkubwa wa kubeba behewa zaidi ya 20 kupeleka Uganda moja kwa moja.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, chini ya uongozi wake Mheshimiwa Profesa Mbarawa. Pia nampongeza Naibu Waziri Mheshimiwa *Engineer E. Ngonyani* kwa namna wanavyoshirikiana na Waziri wake. Nawapongeza Watendaji wote Wakuu wa Wizara hii na bila kumsahau Kaimu Meneja wa *TANROADS* Ruvuma Ndugu Razaq kwa kazi kubwa anayofanya hususan katika Jimbo langu la Nyasa ambalo lina changamoto kubwa sana ya miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona barabara ya Mbinga – *Mbamba Bay*kiwa kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami. Barabara hii imo katika ahadi za Mheshimiwa Rais, siku anaomba kura alisema itajengwa kuanzia mwezi Aprili, 2016. Naomba sana ijengwe. Vile vile barabara ya Kitai – Lituhi na Lituhi – *Mbamba Bay* ambazo zilikuwa zimefanyiwa upembizi yakinifu, sijui zimefikia wapi?

Vilevile nashauri barabara hiyo ichukuliwe ni Chiwindi (mpakani na Msumbiji) – *Mbamba Bay* - Lituhi badala ya *Mbamba Bay* - Lituhi kutokana na unyeti wake kuwa ni barabara ya mpakani na pia yenye fursa za utalii wa fukwe za Ziwa Nyasa. Hali kadhalika, naomba kuanza upembizi wa barabara ya Kingirikitii hadi Liparamba - Mitomoni na kuunganishwa na daraja kuvuka Mkenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aliahidi kusaidiwa kujenga daraja baada ya vifo vya waliozama na boti Mto Ruvuma, kwenye bajeti hii, sijaona chochote! Tumeshawasahau wale watu tisa waliokufa. Mto ule hauna kivuko chochote cha uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Mheshimiwa Jenista Mhagama barabara ya Likuyu Fuso - Mkenda inayounganisha na Msumbiji. Jimbo la Nyasa pia tutanufaika na barabara hii endapo itajengwa kwa kiwango cha lami, pamoa daraja la Mto Ruvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile niliomba kupandishwa hadhi barabara ya Chemeni - Kipapa Matuta – Mengo - Kihagara hadi Bandari ya Njambe kuwa ya *TANROADS* au *Trunk road* kwani inakidhi vigezo; pia imeunganisha fursa za kiuchumi kwa Jimbo la Nyasa na Mbanga Vijijini. Vile vile kupandisha hadhi kipande cha barabara ya Mpapo hadi Darpori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizidi kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kukamilisha ujenzi wa meli mbili na hiyo ya abiria zinazoendelea kujengwa, pamoja na Bandari ya Ndumbi na Daraja la Mtu Ruhuhu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri inayoendelea kufanyika nchi nzima na ambayo tayari imekwisha kufanyika. Mawaziri hawa ni mahiri, wasikivu na wachapakazi sana. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mengi yaliyofanywa na yanayoendelea kufanywa na Wizara hii, naomba nishauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyombo vyaa Usafiri kwa Watu Wenye Ulemavu (Mabasi). Ipo haja kwa Serikali kuliangalia hili kwa kuwaagiza wamiliki wa *Public Transport* kuhakikisha vyombo vyao vinazingatia mahitaji maalum. Hili litawezekana endapo kutakuwa na Sheria ya kuwabana wamiliki hawa wakati wa usajili; kuwa chombo hakitasajiliwa kwa huduma za kijamii kama kitakuwa hakijakidhi vigezo ama kama kitakuwa hakina miundombinu ya kuwezesha mtu mwenye ulemavu hasa wa viungo kupanda pasipo shida yoyote ama pasipo kubebwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ndege. Kwa ndege ndogo (kati ya abiria 5 – 25) zinazofanya safari zake ndani ya nchi yetu miundombinu yake si rafiki kwa watu wenye ulemavu kwani upana wa ngazi zake ni mdogo sana na hakuna

Ambulift. Ushauri wangu ni; Unguja wana ngazi pana (Uwanja wa Unguja) ngazi hii ni ya mbao, inatumika pale inapotokea mtu hawesi kupanda kwa kutumia ngazi za ndege husika (yaani zile ndege ndogo hasa *coastal* na kadhalika)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu kumpakia kwenye ndege si sahihi kabisa, hivyo naomba sana Serikali yangu sikivu ihakikishe uwepo wa *Ambulift* na hizi ngazi za mbao kwenye viwanja vya ndege kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa *Ambulift*, *lift* na hizi ngazi za mbao kwa ndege ndogo zitasaidia wagonjwa, wazee na watu wenye ulemavu kutobebwa wakati wa kupanda ndege kitu ambacho ni hatari kwa anayebebwa na anayebeba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa kwa hotuba nzuri ya Bajeti. Aidha, hotuba hii nzuri inatokana na kazi nzuri ya timu hii mahiri ya Wizara hii inayojumuisha Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na Wafanyakazi wa Wizara na Mashirika yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Kilimanjaro una majimbo ya uchaguzi tisa. Kati ya hayo majimbo mawili tu ndiyo ya Chama Tawala cha CCM na yaliyobaki saba yako chini ya Chama cha Upinzani cha CHADEMA. Kwa bahati mbaya majimbo yanayoongozwa na CCM yalikuwa hayapewi fedha za utengenezaji wa barabara. Fedha karibu zote za kutengenezea barabara zinapangwa kutengeneza barabara katika Majimbo yanaongozwa na Upinzani. Msemo wa Wananchi wa Kilimanjaro umekuwa, kama mnataka barabara zenu zitengenezwe muwe chini ya CHADEMA. Napenda sasa nichukue fursa hii kuishukuru Serikali na hasa Wizara ya Ujenzi kuwa Bajeti ya mwaka huu 2017/2018 imejibu kilio cha wananchi wa Mwanga kwa kutenga fedha kuhudumia barabara ya Mwanga – Kikweni – Lomwe na Vuchama – Ngofi. Tuna imani kubwa kuwa hatua hii itasaidia

sana kuleta imani ya wananchi wa Mwanga kwa Serikali yao na Chama chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa sasa zinatekeleza ahadi za Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano aliyetembelea barabara hii mwaka 2015 akiwa Waziri wa Ujenzi. Hivyo napenda kwa niaba ya wananchi wa Mwanga kumshukuru sana Mheshimiwa Rais.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Wizara hii ndiyo uti wa mgongo wa Tanzania ya Viwanda. Sekta zote za uzalishaji wa kilimo na sekta nyingine zote, za biashara, utalii, miundombinu ya umeme usafirishaji wa bidhaa na watu, vifaa ya ujenzi illi viweze kufikiwa na kusafirishwa Wizara hii ina mchango mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na Watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri. Kipekee nimpongeze kwa dhati Mhandisi Patrick Mfugale kwa utumishi wake uliotukuka na mchango wake wa kipekee katika ujenzi wa barabara za lami na sasa amekuwa kiongozi wa timu ya wahandisi ambao wamefanya upembuzi yakinifu na upembuzi wa kina hadi kuanza kwa ujenzi wa reli ya *standard gauge* unaofanywa na Kampuni za *Yapi Merkez Insaat Ve Sanayina Mota-Engil* inayojenga reli aina hii kutoka Dar es Salaam – Morogoro, hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Wizara hii kwa kazi nzuri ya ujenzi wa barabara za lami chini ya usimamizi wa Mhandisi Patrick Mfugale. Niiombe Serikali ione uwezekano wa kumpatia nishani kwa ajili ya kuutambua mchango wake kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa ujenzi wa madaraja makubwa pamoja na *flyovers*, mradi wa *DART*,

pamoja na Daraja la Mwalimu Nyerere – Kigamboni. Niombi pia Mradi wa Daraja la Kigongo – Busisi lisaniifiwe na kujengwa ili kurahisisha mawasiliano katika Kanda ya Afrika Mashariki na kuondoa vikwazo vya vivuko kwenye Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali na Wizara izipandishe hadhi barabara za Bwelwa – Ushirombo – Ibumwa, Nyaruyeye, Nyarugusu, Nyabulolo – Buyegu, Geita. Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Butengolumasa, Iparamasa, Mbogwe, Masumbwe. Barabara hii ni kiungo cha barabara ya Isaka – Masumbwe, Mbogwe, Iparamasa, Butengo Lumasa, Chato, Muleba, Bukoba, Mtukula hadi nchini Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ununuzi wa ndege ni hatua maridhawa katika kuitangaza nchi yetu Kimataifa na hivyo kusaldla kukuza sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iendelee kutenga pesa kwa ajili ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) ili ujenzi wa minara katika maeneo yenye usikivu hafifu yapatiwe huduma hii hasa katika Kata za Ilolangulu, Ikobe, Isebya, Nyasato, Ikunguigazi (Kagera). Shirika la Simu Tanzania (*TTCL*) lipatiwe uungaji mkono kifedha ili liwekeze zaidi na limudu ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa hotuba yao nzuri sana. Pia naipongeza Serikali kwa kutimiza baadhi ya ahadi zake, hasa kwenye miundombinu ya barabara. Kwa Wilaya ya Nyang'hwale kuna barabara mbili za *TANROADs*, moja inayotoka Wilaya ya Geita – Nyang'hwale na ya pili inayotoka Busisi – Sengerema – Nyang'hwale – Kahama hizi zina hali nzuri kwa sababu zina matengenezo ya kila mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukumbusha kwamba kuna ahadi ambazo zilahidiwa katika Kampeni ya

Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne mwaka 2010. Katika ahadi hizo ni pamoja na kujenga barabara ya kutoka Kahama - Nyang'holongo – Bukwimba – Karumwa – Nyijundu – Busolwa – Ngoma – Busisi Wilayani Sengerema; kwa kiwango cha Lami. Kifupi kutoka Kahama – Nyang'hwale – Sengerema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano alipokuja kujinadi katika Jimbo la Nyang'hwale aliahidi pia kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; napenda kujua, je ni lini upembuzi yakinifu utaanza na kukamilika? Swalii la pili; je ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza na kukamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Rejea ukurasa wa 148 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Barabara ya Marangu – Tarakea, Rongai, Kamwanga - Bomang'ombe – Sanya Juu (kilomita 171); kwenye kila kifungu 259, mwisho wa *paragraph*; kuhusu kazi nyingine za kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kiboriloni – Tsuduni – Kidia (kilomita 10. 8).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua kipaumbele hicho kimetengewa shilingi ngapi na ni lini Ujenzi huo utaanza? Wananchi wanasubiri kwa hamu sana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yaliyo kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kuwa barabara ambazo Mheshimiwa Rais alipokuwa Njombe, alitoa ahadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Moshi Vijijini, barabara ya RAU –Shimbwe juu kilometra 10; Vunjo – Barabara ya Himo – Mandaka, Kilema Maua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kukumbushia ahadi hizo naomba pia kukumbushia madeni ya *Contractor* wa Kichina aliyejenga Barabara ya Dumila – Kilosa ambaye alitulilia sana Kamati ya *PAC* tulipawatembelea. Kwa umoja wetu tuliona kuwa kusitishwa kwa Ujenzi ni gharama kubwa kwa Serikali. Ref. (*Interest accumulation*). Ushauri wangu kwa siku za baadaye, tujenge miradi michache na tuimalize kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa Hotuba nzuri na kazi nzuri pia, *keep it up engineers*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. VEDASTUS M. MANYINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi yake nzuri. Mheshimiwa Waziri, kama atakumbuka miezi miwili iliyopita alipata nafasi ya kutembelea Uwanja wa Musoma ambapo aliahidi kuujenga kwa kiwango cha lami. Nashukuru kwamba ametenga fedha kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja inawasumbua watu wa Musoma kwa sababu wataalam walikuja kuangalia maeneo ya kupanua uwanja huo, wakavuka barabara upande wa pili wakasema hapo patafanyiwa tathmini. Napenda kufahamu ni kweli uwanja huo utavuka barabara kuelekea upande wa magharibi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, kuna kitega uchumi chetu cha mwalo wa kupokelea samaki Mwigobero. Mwalo huu ulichukuliwa na bandari na tuliomba turudishiwe; tulimweleza Mheshimiwa Waziri na akatukubalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa tunasubiri bado hatujapata jibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Nategemea majibu mazuri.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Road Fund* iwe *re-allocated*. Kwa sasa asilimia 70 barabara kuu na asilimia 30 barabara za halmashauri, hazitendi haki kwa barabara za vitongojini. Halmashauri zimeishia kuchonga barabara chache sana zinazounganisha kata; vijiji na vitongoji bado sana.

Miamala ya simu kwa kutumia fedha. Utumiaji kutoka Mtandao mmoja kwenda mwingine haufanyi kazi, fedha nyiningine za wananchi zinapotea na watu wa kampuni wanatoa maelezo tu lakini fedha zinapotea

Tunashukuru kwa ujenzi unaoendelea katika barabara ya Bwanga – Kelebezo. Hata hivyo kasi inaendelea kuwa ndogo, vile vile Mkandarasi haweki alama barabarani na hivyo kusababisha ajali.

MHE. CHARLES J. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia njia ya maandishi naomba kuchangia Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Muhutwe – Kamachumu – Muleba (kilomita 53). Barabara tajwa imeainishwa katika Ilani ya CCM ya mwaka 2015 kuwa itajengwa kwa kiwango cha lami. Umuhimu wa barabara hii kwa vipindi tofauti nimeelezea hapa Bungeni. Pamoja na mpango huu kwa sasa barabara hii imeharibika sana maeneo ya Rukono (Muhutwe – Kyabakoba) na Malele (Kyabakoba – Nyawaibewa). Uharibifu ni mkubwa sana kiasi kwamba kuna wakati watu watokao Muhutwe kwenda Kamachumu (15km) wamelazimika kuzunguka kupitia Muleba, umbali wa kilomita zaidi 110.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi yangu ni kuwa mradi huu utekelezwe kama ilivyoanishwa katika Ilani yetu. Aidha, kutokana na hali ya barabara kutoruhusu usafiri kuwa salama naomba bajeti ya barabara tajwa kama inavyoonekana ukurasa 286 sehemu kubwa ihamishiwe chini

ya mpango wa *upgrading* to DSD. Nyongeza za fedha itasaidia kujenga maeneo korofi kwa zaidi ya kilometra sita zilizopangwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako nieleze kutokuridhika na utendaji usioridhisha katika barabara hiyo kwa mwaka huu (2016/2017) hali iliyopelekea maeneo niliyoyaeleza hapo awali kuharibika. Muhimu watendaji wajiuilize ni kwa nini kwa kipindi cha zaidi ya miaka 10 eneo hilo halijapata tatizo kama la sasa katika maeneo ya Rukomo, Ruhanda na Malele. Kutokana na hali ya udongo wa eneo husika mkandarasi atafanya kazi hewa, ufanisi hewa. Kuongeza na kushindilia tabaka la changarawe badala ya kupalula tabaka la changarawe ambalo limewekwa kabla. Siridhiki na utendaji wa eneo hilo na limekuwa chini ya mategemeo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*). Yamekuwepo mawazo ya kuanzisha mamlaka ya kusimamia barabara zilizoko chini ya Halmashauri. Hii ni kutokana na utendaji mzuri na wenye ufanisi wa *TANROADS*.

Mheshimi Mwenyekiti, utendaji na ufanisi wa *TANROADS* umefikiwa baada ya kujifunza na uzoefu wa muda mrefu. Hivyo badala ya kuanzisha Mamlaka Nyingine, basi baadhi ya barabara za halmashauri zipandishwe kwenda *TANROADS* na mgawo wa fedha za Bajeti uongezeka sawia. Halmashauri wabaki na eneo dogo la mtando wa barabara; na kama nilivyoelekeza awali kwamba mgawo wao kutoka *Road Fund* upungue. Hata kwa mgao huu kwa halmashauri bado ufanisi wa barabara si wa viwango na si mzuri kutokana na upungufu katika kufanya maamuzi au kutokuwepo mafundi, wahandisi na zana zenyetumaini viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Muleba, Kanyambozo na Rubuja. Kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Muleba kupitia Bunge lako nitoe shukrani kwa Mheshimiwa Rais na Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kutoa pole kwa wahanga wa tetemeko Mkoani Kagera Mheshimiwa Rais Dkt.. John Pombe Magufuli, alisikia ombi la wananchi na kuagiza kuanza ujenzi wa barabara ya Muleba Kanyamaboga – Rubya Hospital. Ni maoni yetu kuwa kiasi cha fedha kilichopangwa kwenye Bajeti ya 2017/2018 zitatolewa kwa wakati na mradi utatekelezwa. Aidha, ni mombi yetu kuwa usimamizi makini ufanyike ili tupate ufanisi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuchangia hotuba hii kwa kuanza na hali za barabara zetu hapa nchini. Hali ya barabara zetu nydingi ni mbaya hasa majira ya masika ambapo barabara nydingi zinajifunga hasa kwa zile za changarawe na udongo. Hali hii huchangiwa zaidi na wakandarasi kuzijenga chini ya kiwango. Kwa barabara za lami hali ni mbaya pia, barabara nydingi hujengwa chini ya kiwango. Jambo linalo igharimu nchi yetu kutumia fedha nydingi za matengenezo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubovu wa barabara za lami nchini huchangiwa kwa kiasi kikubwa na kukosa umakini au utaalalim wakati wa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambapo ndio humwongoza Mkandarasi. Kwa ajili hiyo wakandarasi wengi inashindikana kuwatia hatiani kwa sababu mara zote kosa sio lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijikite kwenye Sera ya Kitaifa juu ya kuunganisha mikoa yetu kwa barabara za lami. Hadi leo kuna baadhi ya mikoa haijaunganishwa japo mikoa mingine sasa inaunganishwa kati ya wilaya hadi wilaya wakati mikoa mingine haijaunganishwa. Kwa mfano Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Morogoro au Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Ruvuma. Barabara ya Lindi – Morogoro kuititia Wilaya za Liwale na Ulanga ni muhimu sana hasa kwa sasa ambapo Serikali imehamia Dodoma, kwa sababu Mikoa ya Lindi na Mtwara kuja Dodoma kuititia njia hiyo ni fupi sana; hivyo

kuipunguzia Serikali Matumizi ya Mafuta kwa watumishi wa mikoa hiyo, kuja Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijielekeza Jimboni kwangu Liwale. Liwale ni Wilaya yenye umri wa miaka 42, lakini hadi leo Wilaya hiyo inakabiliwa na tatizo kubwa la mawasilino ya simu na barabaram jambo linalofanya Wilaya hii kuwa nyuma kimaendeleo. Katika Mkoa wa Lindi Liwale ndiyo Wilaya iliyo mbali zaidi kutoka Mkoani, kama kilomita zaidi ya 300. Barabara ya Liwale – Nachingwea, japo imetajwa katika llani ya CCM Lakini sioni juhudhi za Serikali katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Nanguruku – Liwale ni kama mshipa wa damu kwa Wilaya ya Liwale. Pamoja na kwamba Liwale inaongoza kwa zao la korosho na ufuta katika Mkoa wa Lindi lakini bado wakulima hao wanapata bei ndogo ya mazao yao, jambo linalopunguza pato la Halmashauri na Serikali kwa ujumla kwani wafanyabiashara hutoa bei ndogo kwa sababu ya ubovu wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakazi wa Wilaya za Masasi, Tunduru na Nachingwea wangeweza kutumia barabara hii ya Nangurukuru – Liwale kwani ndiyo barabara fupi kwao kwa kwenda na kutoka Dar es Salaam kuititia Liwale, hivyo kuongeza umuhimu wa barabara hii. Pamoja na Liwale kupakana na hifadhi ya Selou, watalii wanashindwa kuja Liwale kwa sababu ya ukosefu wa miundobinu ya barabara na simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naomba kupata maelezo ni kipi kianze kati ya miundobinu na simu maendeleo ya watu. Naomba barabara hii ijengwe ili ufuta, viazi na korosho za Wanaliwale ili zipate bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ya simu ni muhimu sana lakini hadi sasa ni chini ya asilimia 40 tu ya vijiji 76 vya Wilaya ya Liwale, vina mawasiliano ya simu. Ukiiondoa mawasiliano ya simu na barabara hakuna namna nyingine

ya mawasiliano kwa wakazi wa Liwale kwani hakuna redio inayosikika Liwale.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakamilisha mchango wangu wa maneno kuhusu barabara. Mabasi yaendayo kasi yaendelee kwa haraka kwenda Mbagala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari; ajira ndogo ndogo. Kuwe na mpango madhubuti wa kuzitambua ajira hizo na vijana wa Dar es Salaam hususani Temeke wapate ajira hizo, vile vile mwisho wa siku tupate takwimu za ajira hizo. Fungu la Bandari la *Corporate Social Responsibility* litolewe kwenye makundi mbalimbali ya wasiojiweza na wazee. Pia akinamama wajasiriamali wadogo watoto wa Kurasini, mama lishe na wauza vinywaji. Bandari iwajengee uwezo na kuwawekea mazingira mazuri ya kuuzia bidhaa zao. Vile vile hata *Canteen* ya Bandari iwajengee uwezo akinamama walete bidhaa kama vitafunwa ili nao wafaidike na bandari yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa ndege. Ni vyema Serikali ikaelekeza mpango wa mabasi ya mwendo kasi kwenye uwanja huo. Hata hivyo sijaona eneo la biashara kuonesha bidhaa za Tanzania na utalii, je Serikali imepanga viyi eneo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Reli; maeneo ya Shirika la Reli yaliyo mengi yametekelezwa kiasi cha kuwa Mafichio ya wezi na vibaka. Maeneo yatunzwe vizuri ili yatumike baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano; matumizi makubwa ya simu yanafanyika Dar es Salaam, lakini ukitoa kodi tunayokata kama wana Dar es Salaam wanatusaidia nini moja kwa moja kama wananchi wa Dara es Salaam? Naomba Makampuni ya simu wakae na sisi Wabunge kuangalia namna bora ya kutuchangia watu wa Mkoa wa Dar es Salaam katika mipango ya maendeleo ya Mkoa wetu. Kikubwa na kuongezeka kwa gharama za simu kumekuwa

na matangazo ya uongo kuwa kuna nafuu ya matumizi, ukiangalia dakika hakuna kitu badala yake *weekend* kuna ongezeko kubwa la gherama za simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. ABDALLAH HAJI ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa mambo yote duniani. Pili, nampongeza Mheshimiwa Spika kwa kusimamia majukumu yake vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia angalau machache kati ya mengi kwa Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Kwa nia njema kabisa Serikali katika kutafuta changamoto ya usafiri ilileta meli ya kisasa ili kupunguza tatizo la usafiri kati ya Dar es Salaam na Bagamoyo. Lengo kuu la ujio wa meli ile ni kupunguza tatizo la usafiri kati ya Dar es Salaam na Bagamoyo, lakini cha kushangaza meli ile haionekani ikifanya huduma iliyokusudiwa na tatizo lile la usafiri bado lipo vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba malengo na nia njema iliyokusudiwa haikufikiwa, lakini kubwa ni kwamba meli ile Wizara husika na Serikali kwa ujumla wanafahamu ilipo na matumizi yake. Hivyo ni vyema wananchi wakapata maelezo sahihi ili wafahamu meli ile iko wapi na inatumika vipi? Naomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo japo kidogo juu ya kutolefikiwa kwa dhamira nzuri iliyokusudiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala zima la viwanja vya ndege. Kumekuwa na malalamiko makubwa kwamba viwanja vingi havina taa hivyo ndege zetu zinashindwa kutua usiku. Katika ulimwengu huu wa sasa wa sayansi na teknologia safari ni wakati wowote iwe usiku au mchana ili kwenda na wakati na kurahisisha mambo yawe sawa. Naishauri Serikali kuliona suala hili na kuwapatia huduma walipa kodi wa nchi hii ili waweze kwenda na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuweka taa katika viwanja vyetu vya ndege ni mionganini mwa kuboresha miundombini ili iwe mizuri na kuwaweka watu wetu katika hali ya kisasa zaidi.

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii adhimu na muhimu kumshukuru *Allah Subhanahu Wataala*, kwa neema kubwa ya uhai na uzima. Pia nikushukuru kwa kuniruhusu nichangie mada iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya niliyazungumza katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini kwa umuhimu wa jambo lenyewe na Mheshimiwa Waziri ndiye mhusika mkubwa, naomba nirejee ili nipate jawabu muafaka. Mimi binafsi nimekufta Mheshimiwa Waziri zadi ya mara tatu kukuelezea malalamiko ya wasafirishaji wa majahazi katika Bandari ya Dar es Salaam. Kwa bahati mbaya sana hukuwahi kukutana na wadau wa majahazi hata mara moja, jambo ambalo sikulaumu sana kwa sababu mchakato wa hapa kazi ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa majahazi wanalamika kipimo cha (*CDM*) ambacho *CDM* moja (1) wanalipa 7,500/=, ambapo (fuso) gari moja linajaa kwa *CDM* 80. Kwa fuso moja *CDM* 80 wanalipa sh. 600,000 ambapo mzigo huu walilipia Sh. 600,000/= wao wanabeba kwa thamani ya milioni moja 1,000,000/. Kwa maana hiyo kama jahazi lina uwezo wa kubeba *CDM* 160 ama mafuso mawili Serikali inachukua 1,200,000/= na wenye jahazi wanabakiwa na laki 800,000/=, kwa hiyo wanalamika hawapati kitu na biashara hii inawashinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Mheshimiwa Waziri akutane nao wenyewe ili ajue kiini cha tatizo hili. Hata hivyo, naomba aiangalie suala hili na atoe tamko kuhusu malalamiko yao haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie usafiri wa bahari kati ya Tanga – Pemba – Nungwi. Usafiri wa

sehemu hizi wa bahari umekuwa na matatizo makubwa na husababisha ajali nyangi kwa kutumia vyombo duni na hafifu sana. Wananchi wamelalamikia Serikali yao kuhusu kuwapatia usafiri wa hakika mwishowe mfanyakibashara mkubwa Said Bakhresa ameleta meli kubwa ambayo itatoa huduma katika maeneo hayo. Nichukue fursa hii kupongeza Kampuni ya Bakhresa kwa ufumbuzi wa tatizo hili. Angalizo, Bakhresa ni mfanyakibashara. Kwa hiyo, anahitaji faida katika biashara yake. Abiria wa Tanga na Pemba kuna wakati wanakuwa wengi na wakati mwingine wanapungua. Wasiwasi wangu kama upungufu wa abiria na mizigo utakuwa mkubwa unawenza kukatisha usafirishaji na wananchi kukosa usafiri wa hakika. Je, Serikali ina mpango gani kwa wananchi hawa kama hali itakuwa kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri akisimama anitoe wasiwasi wangu huu.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Madaraja; nashauri Serikali na Wizara hii kuweka kipaumbele cha ujenzi wa madaraja yaliyo katika mipaka ya nchi hasa Malawi kwani hakuna madaraja yatakayoweza kusaidia tukipata dharura kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usumbufu kwa magari katika mpaka. Kumekuwa na usumbufu wa foleni ndefu katika mipaka hasa magari makubwa ya usafirishaji ya *transit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa vya Uokoaji. Kumekuwa na uhaba wa vifaa vya uokoaji majini hasa katika boti katika ziwa Tanganyika. Tunaomba Wizara ihakikishe inaweka vifaa hivyo kwani waathirika wakubwa ni wanawake na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ni kidogo katika Halmashauri ya Rungwe. Katika Wilaya ya Rungwe hakuna fedha za ujenzi/ukarabati wa barabara za ndani wakati Halmashauri hii ni muhimu kwa mazao ya chakula yanayozalishwa hapo.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwa ujumla kwa jitahada kubwa wanazochukua kwa kuleta maendeleo ya dhati hususan katika kujikita katika suala la usafiri wa anga kwa ununuzi wa ndege mpya pamoja na ujenzi wa reli iendayo kwa umeme (*standard gauge*). Aidha, dhamira ya dhati ya kujenga na kukarabati viwanja vyatia ndege, ujenzi wa bandari za ndani, Mtwara na mwisho ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hotuba hii katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Handeni – Kibrashi – Kijungu – Njiro – Mrijo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwamtoro – Singida (kilomita 460). Barabara hii ni muhimu sana kwa sababu ipo katika llani ya Chama cha Mapinduzi na kwa sababu inapita katika mikoa minne. Nishukuru kwa mwaka huu wa fedha Wizara imetenga kiasi cha sh. 500,000,000/=. Je, kiasi hiki ni kwa ajili ya fidia au jibu gani? Maana ni kiasi kidogo sana kwa ujenzi wa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii kipindi cha mvua inapitika kwa shida sana, barabara hii ina shughuli nydingi za kiuchumi. Wananchi katika maeneo yote yaliyotajwa ni wazalishaji wakubwa wa mazao mbalimbali hususan mahindi. Wananchi hawa hawapatil faida ya mazao yao kwa sababu wanazimika kuuza chini ya bei ambapo kama barabara ingekuwa ya kiwango cha lami, wigo na fursa ya kuuza kwenye masoko watakayokuza ingekuwa kubwa sana. Niombwe Wizara yangu watafute wadhamini wa kutujengea barabara hii au Serikali itoe fedha za kutosha kutujengea barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine katika ujenzi wa barabara ni ujenzi wa barabara kwa kilometra tatu kwenye Makao Makuu ya Wilaya. Mwaka wa jana tulitengewa fedha kiasi cha sh. 150,000,000. Kiwango hiki ni kidogo sana.

Nimeshangazwa sana kwa mwaka huu wa fedha hakuna fedha zilizotengwa, hivi Kilindi kuna tatizo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Tanga, Wilaya ya Kilindi ndiyo wilaya pekee ambayo haina kilometra tatu au tano za barabara katika Makao Makuu ya Wilaya ambayo haina lami. Naomba majibu kutoka kwa Waziri mwenye dhamana, ni kwa nini hatujapewa fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Songe – Kwekivu – lyogwe – Gairo. Barabara hii kwanza ni *shortcut* kwenda Dodoma, ni mto unaotoka Arusha, Tanga kuja Dodoma. Barabara hii ina shughuli za kiuchumi na pia ina wigo wa magari. Naomba Mheshimiwa Waziri barabara hii nayo ingeingia katika utaratibu wa kujengwa katika kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upandishwaji wa madaraja wa barabara kutoka ngazi ya kijiji kwenda wilaya na wilaya kwenda mkoa. Tunazo barabara nyngi ambazo kwa muda mrefu hazijapandishwa hadhi. Mfano katika Jimbo langu la Kilindi tunaomba barabara zipandishwe hadhi kwa sababu zinakidhi sifa na tayari Meneja wa *TANROADs* alikwisha fikisha maombi Wizarani. Barabara hizi za vijijini ndizo zilizo na shughuli nyngi za kiuchumi, zikijengwa vema na kuhudumiwa ni dhahiri uchumi wa wananchi wetu utakua. Ni vyema Serikali ilipe uzito mkubwa jibu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ENG. GERSON H. LWENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi wanayoifanya na kuliletea Taifa letu sifa kubwa. Hotuba ni nzuri na naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Wanging'ombe ina changamoto kwenye eneo la barabara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza barabara ya Njombe – Mironga – Makete (kilomita 109). Hii ni ahadi ya llani ya Chama Tawala. Mheshimiwa Rais aliwaahidi wapiga kura wangu kwamba wakimpa kura na akaingia Ikulu itakuwa ni barabara ya kwanza kuanza kujenga. Ni zaidi ya mwaka mmoja na nusu sasa yuko Ikulu na barabara hii haijaanza kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Njombe (Ramadhani) – lyayi (kilomita 74). Barabara hii ni ya muhimu kwa uchumi wa Mkoa wa Njombe na hususan Wilaya ya Wanging’ombe. Barabara hii ilifanyiwa usanifu tangu Mwaka 2014 lakini sijaona kwenye Randama ya 2017/2018 kutengewa fedha za kujenga. Ni lini barabara hii itatengewa fedha za kujenga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Halali – llembula – Igwachanya - Itulahumba (kilometra 35). Barabara hii ni ya wilaya na nimemwomba Mheshimiwa Waziri kwamba ipandishwe daraja au ihamishiwe kwa Wakala wa Barabara (*TANROADS*). Barabara hii ni kiungo cha hospitali ya llembula (*DDH*) na Makao Makuu ya Wilaya (Igwachanya). Barabara hii ilifunguliwa na *TANROADS* kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara tangu mwaka 2013 kwa maombi maalum. Sasa barabara hii kwa takriban miaka minne haijapata *routine maintenance*. Naomba sana Mheshimiwa Waziri ombi langu lifikiriwe kwani sijaona kwenye Randama kutengewa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Wizara hii eneo la Makao Makuu ya Wilaya ya Wanging’ombe hayana mawasiliano ya uhakika ya simu. Mnara wa *Vodacom* umewekwa lakini hauna nguvu kabisa.

MHE. LUCIA M. MILOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uchukuzi, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara na wataalam wake, naomba nishauri kwamba viwanja vya ndege vikarabatiwe na hasa kiwanja cha ndege cha Mkoa wa Njombe. Kiwanja hiki kimeharibiwa sana na watu wanaopita katikati ya

kiwanja, hata magari yanapita uwanjani. Hii ni kutokana na uwanja kuwa katikati ya mji. Naiomba Serikali itengeneze uwanja huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kusikiliza kilio cha watu wa Njombe na kutenga fedha kwa ajili ya barabara ya Itoni – Ludewa – Njombe – Makete – Kibena – Lupembe – Madeke. Naiomba Serikali kuhakikisha kwamba fedha hiyo iliyotengwa inapelekwa ili kazi ianze kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa barabara za vijijini katika maeneo mengi na hasa katika Mkoa wa Njombe ni mbovu, naiomba Serikali kuangalia tatizo la wananchi vijijini hasa wanawake wajawazito ambao wanapoteza maisha kwa sababu ya barabara mbovu. Naiomba Serikali itengeneze barabara za vijijini ili kupunguza vifo vya akinamama na watoto wachanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akinamama wengi ni wakulima wanaojitahidi kuzalisha mazao ya chakula na biashara lakini wanashindwa kusafirisha kwa sababu barabara hazipitiki, hasa wakati wa masika. Kwa mfano wananchi wa Mamongolo, Makovo, Ng'elamo, Matola, Iwungilo. Maeneo hayo yanazalisha kwa wingi viazi, ngano pamoja na chai lakini kipindi cha kifuku hayapitiki. Naiomba Serikali itusaidie ili maeneo hayo yaweze kupitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mawasiliano. Maeneo mengi katika Mkoa wa Njombe hakuna mawasiliano ya simu. Kwa mfano, katika Wilaya ya Ludewa maeneo yote ya mwambao kama Vijiji vya Lupingu, Ibumi, Lifuma na Kilondo hayana kabisa mawasiliano, naiomba Serikali iweke minara ya simu katika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Wilaya ya Makete, maeneo ya Matamba, Kiteto na maeneo mengine mengi hakuna mawasiliano kabisa, naiomba Serikali kupeleka minara katika maeneo hayo. Kutokana na ukosefu wa mawasiliano husababisha akinamama kupata matatizo

makubwa ya kupata msaada wakati wa kujifungua kwa sababu wanashindwa kuwasiliana na vyombo vyaa usafiri ili wawahishwe hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 22 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri inazungumzia upanuzi wa barabara ya *New Bagamoyo* (*Morocco JC1*) – Mwenge – Tegeta (12.9 kilomita). Barabara hii ilishakamilika na kuzinduliwa katika kipindi cha mwaka 2010/2015. Kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri barabara hii iko katika kupindi cha uangalizi kinachotarajia kukamilika 30 Julai, 2017. Ni ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake, wapite na kufanya uhakiki katika barabara husika kutokana na ukweli kwamba kuna maeneo ambayo tayari yameshaharibika (hayako katika hali nzuri).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo ambayo wakati wa ujenzi wa barabara mapokea na matoleo ya maji hayakujengwa katika kiwango ambacho kinakidhi. Kiwango cha maji wakati wa mvua kinachotoka maeneo ya Goba ni kikubwa na hatari zaidi iko Tangi Bovu maeneo ya Mbuyuni, Kunduchi, Africana pamoja na Salasala. Kutokana na ufinyu huu kuna hatari ya barabara kupasuka na kuharibika. Ni ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri na kwa Wizara kuchukua hatua za dharura ili kunusuru kazi iliyokwishafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba kuna kazi inayoendelea ya Ujenzi wa *service road* katika barabara husika. Kwa muktadha huo huo, ningependa kujua kwamba ni lini taa za barabarani zitakamilika kwa kuwa ajali nydingi zinasababishwa na kutokuwepo kwa taa barabarani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 22 na 23 inaonesha kwamba kipande cha *Morocco* – Mwenge kitajengwa kwa kiwango cha *dual carriage way*. Baada ya kupata msaada wa fedha kutoka Serikali ya Japan kuititia Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (*JICA*). Hata hivyo, hotuba za bajeti za

miaka minne iliyopitia ilionesha kwamba Serikali ya Japan ilitoa bilioni 88 ambapo pamoja na mambo mengine ingejenga barabara ya Mwenge – Tegeta (*first phase*) na Mwenge – Morocco (*second phase*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufanuzi juu ya utata uliojitekeza kutokana na kauli mbiu zinazotofautiana kutoka kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni utamaduni kwa Mfuko wa Barabara kutoa kiasi fulani cha fedha kwenda halmashauri, lengo likiwa ni kuziwezesha halmashauri zetu ambazo zina uwezo mdogo. Hata hivyo, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Manispaa ya Kinondoni ilitarajia kupata Shilingi bilioni 10.5 kutoka Mfuko wa Barabara. Mpaka kikao chetu cha mwisho cha Baraza la Madiwani taarifa tulizopewa ni kwamba hakuna hata shillingi iliyowasilishwa Halmashauri, hali ambayo imeathiri kwa kiwango kikubwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Naomba ufanuzi ni lini fedha husika zitaletwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TAZARA*. Kwa muda wa miaka miwili/mitatu mfululizo nimekuwa nikizungumza juu ya uuzwaji wa nyumba za *TAZARA* kinyume na utaratibu halikadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvamizi wa maeneo ya *TAZARA* yaliyofanywa pasipo hatua zozote kuchukuliwa. Mheshimiwa Samwel Sitta (marehemu) akiwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Uchukuzi nilimpatia *Audit Report* ikizungumzia kwa kina suala tajwa hapo juu lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa mpaka sasa kuhusiana na suala husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua hatua zilizoanza za ujenzi wa barabara za Tegeta kibaoni – Wazo Hill – Goba. Taarifa zinaonesha kwamba kumpata mkandarasi kwa ajili ya sehemu ya Maendeleo – Goba (kilometra tano) zinaendelea. Ni imani yangu ahadi hii ya muda mrefu,

itaanza kufanyiwa utekelezaji katika hatua ya kwanza kuelekea kukamilisha ujenzi mpaka Kibaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufanunu wa barabara kuu kuelekea Ruaha *National Park* itajengwa?

MHE. MARIA N. KANGOYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipatia uhai na nguvu ya kusimama ndani ya Bunge hili Tukufu. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya ya kujenga Tanzania mpya kuititia llani ya Chama cha Mapinduzi CCM. Namwombea kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yake pamoja na wasaidizi wake, Mawaziri, Naibu Mawaziri na watendaji wote wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nianze kuchangia hoja iliyoko mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TTCL* ni moja ya mashirika yaliyo chini ya Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Taasisi hii ya *TTCL* ni kampuni Kongwa, kuliko kampuni zote za mawasiliano Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni jambo la kusikitisha kwamba *TTCL* imetuwa nyuma sana katika masuala ya kiteknolojia kiasi kwamba imetuwa na wateja wachache sana ikilinganishwa na kampuni nyingine za simu. Napenda kutumia fursa hii kuishauri Serikali yangu kuongeza nguvu ya uwekezaji katika Kampuni hii kama ilivyofanya kwa *ATCL* kwa kununua ndege ili kusaidia kui-boost *ATCL*. Ni wakati sasa wa kuiboresha *TTCL* na sina mashaka na nia nzuri ya Mheshimiwa Rais kwani tayari mmeshamteua kijana mahiri kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto kubwa hasa katika suala zima la kuongeza nguvu ya *ringtones* na mimi binafsi nimekuwa nikijiuliza, je, Serikali inanufaika kiasi gani na *ringtones* hizi? Kwa kuwa zimekuwa

zikiingizwa kwenye simu zetu bila hata idhini zetu. Kwa mtazamo wa haraka, ni hakika Kampuni za Simu zinapata fedha za kutosha kutokana na huduma hii. Mashaka yangu makubwa yapo kwenye malipo kwa vijana wenzangu na wasanii wote kwa ujumla pale nyimbo zao zinapotumika kama *ringtones*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kuishauri Serikali yangu kuanza kulifuatilia suala hili kwa ukaribu kwa kuhakikisha Kampuni za Simu zinalipa mapato yanayotokana na *ringtones* kwa Serikali na wasanii ambao nyimbo zao zinatumika wanapata stahili zao kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake kwa jitihada walizofanya na hasa kutukumbuka sisi watu wa Moshi Vijijiini. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika *Sub-vote 2005 - Roads development divisions* kasma 4115 (vii) inaonesha tumetengewa sh. 811,000/= Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia kilomita 10.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha unaoishia wa 2016/2017, tulitengewa shilingi bilioni 2.583; lakini mpaka leo hakuna hata shilingi moja iliyotolewa kwa barabara hii ambayo ni muhimu sana. Ukiacha shughuli nyingine za kiuchumi zilizopo katika maeneo inapopita barabara hii ambazo nyingi ni za kitalii, barabara hii ndiyo iendayo kwa wakwe wa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, nyumbani kwa Mama Anna Mkapa. Ni imani yangu kuwa inafaa sana kuwaenzi wazee wetu hawa kwa kuwapa barabara nzuri. Naomba sana bajeti ya mwaka jana isipotee, zifanyike jitihada za makusudi ili kazi hii iweze kuanza kuititia fedha za mwaka unaoishia wa 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya miradi ya barabara za mikoa (kasma 4132) 2017/2018, Mkoa wa Kilimnjiro kuna

ukarabati wa Kibosho *Shine* – Mto Sere *Road*). *Upgrading* to Dar es Salaam of Kibosho *Shine* – kwa Raphael *International School Road*, kilomita 27.5 zimetengwa shilingi milioni 128.00.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ilikuwa ni ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na ilianza kujengwa kwa kiwango cha lami takribani kilometra saba. Naomba sana Mheshimiwa Waziri aangalie uwezekano wa kukamilisha ahadi hii kwa ukamilifu wake kwa kiwango cha lami. Aidha, tumetengewa *Rehab*, Uru – Kishumudu Parish – Materuni *Road*, kilometra nane shilingi milioni 61.00. Barabara hii ilijengwa kwa kiwango cha lami miaka ya 1970 mwanzoni, imebomoka karibu yote. Mwaka wa jana 2016 ilijengwa sehemu ndogo kwa kuondoa lami ya zamani na kuweka mpya urefu wa takribani kilometra 1.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi hiki cha shillingi milioni 61.00 ni kidogo mno kuendeleza kazi hii ambayo imeliliwa mno na wananchi wa maeneo hayo. Barabara hii ni njia ya utalii kwenda Mlima Kilimanjaro Maanguko ya Mnambeni na katika mashamba ya kahawa. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie upya suala hili la barabara hii, si vema kurudi nyuma, yaani kutoka lami kwenda changarawe. Tuko tayari kusubiri kwa kujengewa kidogo kidogo lakini lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kuhusu kujengwa kwa kiwango cha lami barabara ya Mamboleo – Shimbwe ambapo ni ahadi ya Rais wa Awamu ya Tano, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, mikakati ya kuanza kutekeleza ahadi hii ianze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa kiumbla. Ingekuwa ni vema sana kama Wizara ingefanya *survey* ambayo ingeiwezesha Wizara kutambua mahitaji halisi ya kila barabara kwa maana ya kazi/mahitaji mahususi eneo kwa eneo. Mara nyingi nimeona kazi zikifanyika kwa mazoea tu wakati ingewezakana labda barabara A katika eneo fulani ikajengwa kwa kiwango cha lami hata kwa robo kilometra ikasaidia sana barabara hiyo kudumu kuliko

kuiwekeea changarawe na kushindilia na mvua moja tu ikaibomoa yote au ikaacha kupidika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza sana Wizara hii kwa kazi nzuri inayoendelea. Ilani ya CCM inaelekeza vizuri kuwa barabara zilizounganisha wilaya na mikoa zitajengwa kwa lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anajua hii barabara ya Iringa – Kilolo – Dabaga – Idete. Mheshimiwa Waziri alifika Kilolo anajua; ipo kama kilometra 27, lakini barabara hii kilometra tano ni za Jimbo la Iringa na kilometra 15 ni Jimbo la Kalenga na kilometra saba ni Kilolo. Hizi zote kwa pamoja ndiyo unapata barabara ya Iringa – Kilolo – Dabaga – Idete. Barabara hii ina mchango mkubwa kwa uchumi wa Taifa, ndiko ambako mbao nyingi zinatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila nilipouliza swali kuhusu barabara hii jibu linakuwa la kutia matumaini lakini utekelezaji wake hakuna. Naomba sana barabara hii itengewe fedha ili ianzé kujengwa kwa kiwango cha lami. Barabara ambayo inatakiwa ipandishwe daraja ni Dabaga - Ng'ang'ange, Bomalang'ombe – Mwatasi – Mufindi. Vikao vyote vilipitisha ombi la barabara hii. Hivyo tunaomba barabara hii ipande daraja iwe ya mkoa.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia yafuatayo:-

Kwanza, Usafiri wa Majini. Vivuko; Kivuko, cha *MV Nyerere* kinachofanya kazi kati ya Bugorola – Ukara, kina matatizo makubwa ya kuchoka/ubovu wa *engine* zake zote mbili, hali iliyopelekea mara kwa mara kuzua taharuki kwa wasafiri kutohana na kuzima ikiwa katikati ya maji. Jambo hili ni hatari sana kwa maisha ya abiria na hata kinapofanya safari zake kivuko hiki kinatumia karibu masaa mawili kwa umbali huo badala ya nusu saa hadi dakika 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri; zinunuliwe *engine* nyingine kwa ajili ya kivuko cha *MV Nyerere* ili kuepusha matatizo yanayoweza kuhatarisha maisha, pia Serikali ione umuhimu wa kutengeneza kivuko kwa ajili ya wakazi zaidi ya 20,000 wa Kisiwa cha Irungwa na Nansio ambao wanatumia mitumbwi na hivyo kusafiri kwa zadi ya masaa matano (5) wakiwa majini. Awali *MV* Ukara ilikuwa inafanya kazi eneo hili kabla ya kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu meli; kuharibika kwa meli ya *MV Butiama* na uchakavu wa meli ya *MV Clarius* kumepunguza ufanisi na kuleta shida ya usafiri kati ya Mwanza – Nansio. Ushauri wangu ni kwamba, mchakato wa matengenezo ya meli ya *MV Butiama* ukamilike haraka ili meli hii iweze kutoa huduma na kupunguza tatizo liliopo la usafiri. *MSC* ipewe fedha za kutosha ili iweze kuboresha meli ya *MV Clarius* ili meli hiyo iweze kumudu ushindani na kushindanishwa kibia shara.

Pili, Mawasiliano; kuna tatizo kubwa la mawasiliano kwenye baadhi ya maeneo yakiwemo eneo la Bwasa na Bukiko, wananchi katika maeneo haya hupanda vilimani ili kupata mawasiliano. Ombi langu, ijengwe minara kwa ajili ya mawasiliano; Bukiko katika Kata ya Bukiko na Bwasa katika kata ya Igalla.

Tatu, Barabara; barabara ya Bunda – Kisorya – Nansio ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa maeneo haya inajengwa kwa kasi ndogo sana. Barabara hii ikamilike mapema ili iweze kutoa huduma kwa wananchi wa maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke katika bajeti ya kila mwaka mpango wa kujenga kilomita moja kila mwaka kwenye barabara ya Bulamba – Mavutunguru – Kakukuru badala ya kutumia fedha nyingi kila mwaka kwa ajili ya kufanya ukarabati usio na tija katika barabara hiyo. Fedha hiyo iongeze kilomita moja (1) ya lami kila mwaka kwenye hiyo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *formula* ya ugawaji wa fedha za Mfuko wa Barabara ibadilishwe na kutoa mgao ulio sawa katи ya *TANROADS* na Halmashauri za Wilaya. Hii itawezesha Halmashauri kuwa na uwezo wa kutengeneza barabara nyingi zinazosimamiwa na Halmashauri zetu ambazo zinakabiliwa na uharibifu mkubwa lakini hazina uwezo wa kuzihudumia kikamilifu.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi za maendeleo zinakuwa nyingi, pamoja na hayo Wizara inaomba bajeti ya kukidhi miradi hiyo na bado fedha hazitoki kwa wakati na kinachotoka ni kidogo mno kukidhi mahitaji. Ni kwa nini Wizara isipange au kuona sasa ni wakati wa kumaliza viforo kuliko kuendelea na miradi mipyä?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Uwanja wa Ndege Kajunguti umekuwa kwenye bajeti kwa muda mrefu sana lakini katika bajeti hii sikuona sehemu ilipotengewa fedha ya kujenga uwanja huu. Serikali ingekuwa inatenga angalau kila mwaka kwa ajili ya kufidia wananchi watakaoathirika na suala hilo. Kipindi uwanja wa Taifa wa Mwalimu Nyerere unaanza kujengwa vile vile uwanja wa Kajunguti ulikuwa kwenye malengo ya kutengenezwa, ila suaona wala kusikia sehemu yoyote kuwa uwanja huu utafanyiwa marekebisho yoyote. Suala hili la uwanja wa Kajunguti limekaliwa kimya sana. Huo uwanja ni tegemeo kubwa sana kwa Wanakagera. Kama tunavyotegemea uwanja wa nchi jirani ya Uganda Entebbe sasa uwanja wetu wa Kajunguti uboreshwe ili Wanakagera wasitegemee nchi jirani kama Uganda, Burundi na Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu sahihi ya maswali haya:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zinazojengwa hazijengwi kwa viwango stahiki, ni kwa nini Wizara wakati inatengeneza tenda isijiridhishe kwanza kazi anazopewa huyo mwombaji wa tenda ana usoefu nazo wa kutosha? Nimeona barabara ya Ushirombo – Lunziwe – Nyakanazi – Rushounga hadi Benako, barabara hii ni mbovu kuititia kiasi,

kilomita ulizotaja zilizokarabatiwa kweli ni aibu, ukizingatia kwamba barabara hii ni rasilimali kubwa sana kwa kuwa inapitisha magari makubwa yanayokwenda mikoani na nchi jirani zinazotuzunguka. Hivi kwa makusanyo yetu Serikali inashindwa nini kutengeneza barabara kwa viwango stahiki? Kutengeneza barabara vipande vipande ni aibu kubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia za majini (katika Ziwa Victoria) kwa Mkoa wetu limekuwa ni tatizo kubwa, tulikuwa na meli za usafirishaji mizigo zilizokuwa zinawasaidia wafanyabiashara kusafirisha bidhaa zao mbalimbali, tulikuwa na meli aina ya Nyangumi, Umoja, MV Butiama na MV Victoria lakini kwa sasa meli hizo zote zimekuwa chakavu na nyingine mpaka kusimama kabisa. Je, ni lini Serikali itajielekeza katika kuzitengeneza meli hizo? Kwa sababu wafanyabiashara kutoka sehemu jirani kama vile Uganda, Kenya na Burundi wanashindwa kufanya shughuli za kiuchumi kutokana na tatizo la usafirishaji wa majini. Ni lini Serikali yetu italeta wawekezaji kama ilivyo Dar es Salaam ambako wana mwekezaji ambaye ni Azam? Wakati wa Serikali ya Awamu ya Tatu na Nne kulitokea mwekezaji ambaye alileta *Speed boat* ambazo zilikuwa zinafanya safari yake Bukoba kwenda Mwanza lakini zilizuiliwa. Kwa hiyo, ni lini Serikali itamruhusu mwekezaji huyo kuendelea na usafirishaji huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nimekuwa nikipiga kelele mara kwa mara kuhusu kivuko cha Kyenyabasi kinachounganisha vijiji vitatu vya Bujugo, Kanazi na Kasharu. Wananchi wa vijiji hivyo vya Bukoba Vijiji wanateseka kwa kuwa kivuko hicho kimekuwa kikikarabatiwa na TEMESA kila wakati lakini bado tatizo lipo pale pale. Je, ni lini Serikali italeta kivuko kingine kusaidia wananchi wangu wa Mkoa wa Kagera?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wananchi wangu wa Bukoba Vijiji wanateseka sana na barabara za vumbi kama vile barabara za Kanazi, Karebe, Ibwera, Katunjo, Nyakibimbili, Katoro hadi Kyaka. Je, ni lini Serikali itaweka mikakati na mipango ya kutengeneza barabara hizo tajwa

zinazounganisha vijji mbalimbali ikiwemo na Hospitali ya Izimbya ambayo iko kwenye barabara ya vumbi ili kuwasaidia wananchi? Naomba majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya ukanda wa Ziwa Victoria imekuwa matatani sana maana ziwa linazidi kusogea mpaka kwenye makazi ya watu na maeneo ya mashule. Kwa mfano, *Lake View Secondary School*, sehemu za vivutio vya watalii kama vile *Space Hotel, Kloyera tours*, Bukoba *Club Yasila Hotel* na Shule ya Nyashenye vyote viko hatarini kukumbwa na maji. Je, ni lini Serikali itajenga ukuta kuzuia maji ya ziwa yanayowasogelea wananchi wa Bukoba hususan waishio Kando kando ya ziwa? Naomba majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko kwa wananchi juu ya kuweka minara katikati ya nyumba. Migogoro hii imekuwa mikubwa na haitafutiwi ufumbuzi mwaka hadi mwaka kiasi kwamba imekuwa kero kubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Kagera. Minara hiyo kwa nini isiwekwe juu ya milima ili wananchi wakae kwa amani hususani ni wananchi wa Kata ya Kashi Manispaa ya Bukoba? Vile vile naomba nijue hii migogoro ya wananchi ni lini itakwisha? Kwa sababu imekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wa Kagera. Kuweka minara kuna madhara makubwa kwa wananchi kutokana na miungurumo yake pamoja na mionzi ya minara hiyo kukaa karibu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala la minara nipate majibu. Naomba kuwasilisha.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingi zilizopo katika Jimbo la Vwawa zimekuwa hazipitiki kipindi cha masika. Tunaomba Serikali kupitia Mfuko wa Barabara kuzifanyia matengenezo ya mara kwa mara. Kuna barabara ya kilometra 10 alizoahidi Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni. Pia ili Mkoa mpya wa Songwe uunganishwe vizuri ni vyema Serikali ikajenga barabara zifuatazo kwa kiwango cha lami:-

- (a) Barabara ya Njiapanda ya lyula – Idiwili – Itezya hadi leje.
- (b) Barabara ya Vwawa – Nyimbili – Hezya hadi lleje.
- (c) Barabara ya Viwawa - Igamba Magamba hadi Mkwajuni Songwe.
- (d) Barabara ya Ihanda – Chindi hadi Chitete – Momba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha reli ya *TAZARA* ili iweze kutoa mchango mkubwa wa uchumi katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Hali ya Shirika hili si nzuri kabisa na wakati huo huo barabara nyingi zimekuwa zinaharibika sana kutokana na mizigo mikubwa. Ili kuimarisha kilimo, madini, ufugaji ni vizuri reli hii ikahudumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa majengo ya ofisi na nyumba za watumishi katika Mkoa wa Songwe. Nini hasa mpango wa Serikali katika kujenga nyumba na majengo ya ofisi katika mkoa huo mpya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa huduma wa Wakala wa Umeme na Ufundi uimarishe ili kutoa huduma nzuri za utengenezaji wa magari ya Serikali na umeme kwenye majengo ya Serikali. Hivi sasa gharama ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *TTCL* na *TCRA* yaimarishwe ili yaweze kutoa mchango mkubwa katika utoaji huduma na kuchangia kukuza mapato ya nchi yetu. Ni vyema Serikali ikayasaidia zaidi.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kilometra 149 iliyomo kwenye llani ya CCM ya mwaka 2015 – 2020 inayoanzia Tabora – Mambali – Bukene – Kagongwa haimo kabisa katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri cha bajeti ya 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ilishindikana kufanyiwa upembuzi yakinifu mwaka wa jana kwa kuwa

fedha iliyokuwepo kwa kazi hii milioni 400 haikutosha. Nilitarajia kuwa mwaka ujao wa fedha wa 2017/2018 barabara hii ingeongezewa fedha shilingi milioni 400 zingine ili zifike milioni 800 ambazo zingetosha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu. Nimepitia kitabu chote na nimepitia miradi yote ya barabara kwa mwaka 2017/2018 lakini sijaona barabara hii ya Tabora – Mambali – Bukene – Kagogwa kilometa 149.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwasilisha jambo hili kwa Naibu Waziri Mheshimiwa Edwin Ngonyani ambaye aliongea na Meneja na *TANROADS*wa Tabora Ndugu Ndabalinde, lakini sijapata mrejesho wowote. Naomba barabara hii ipate fedha za kufanya upembuzi yakinifu ili tutimize ahadi ya CCM kama ilivyo kwenye llani ya Uchaguzi ya CCM.

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kutoa mchango wangu kwa maandishi katika Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa meli mpya katika Ziwa Victoria, kutafungua fursa za biashara katika Mikoa ya Mwanza na Kagera kwani mazao mengi kutoka mikoa hiyo hutegemea usafiri wa maji. Vile vile meli hiyo itasaidia usafirishaji wa abiria na mizigo. Hivyo niiombe Serikali kutenga fedha katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya ununuzi wa meli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa upanuzi wa barabara ya Furahisha hadi Pasiansi Airport, hii imesaidia kupunguza foleni na msongamano wa magari. Naomba Serikali ianze kufanya tathmini ya kuendelea kupunguza msongamano katika Jiji la Mwanza kwa kufungua barabara zitakazoondoa msongamano katikati ya Jiji. Barabara hizo ni za:- Buhongwa – Rwanhima – Kishiri – Igoma na barabara ya Mkuyuni – Mahina – Nyakato – Buzuruga na barabara ya Butimba – Fisheries – SAUT – Mkolani. Kwa kufungua barabara hizi kutaondoa msongamano katikati ya Jiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia hotuba ya Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii lakini sijaona fedha zilizotengwa kwa ajili ya ununuzi wa kivuko cha *base* Wilaya ya Illemela kwenye Jimbo la Mheshimiwa Angelina Mabula ambapo pia Mheshimiwa Rais aliahidi wakati wa kampeni za uchaguzi 2015. Katika vikao vya RCC tulikubaliana kununua kivuko hicho. Niiombe Serikali itenge fedha za kununua kivuko hicho ambacho kitawasaidia wakazi wa kisiwa hicho cha *base* wapatao 600 na zaidi hususan akinamama ambao wanahitaji kuvuka kuja mjini kwa ajili ya kujifungua hasa wanapopata rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nashukuru na naunga mkono hoja.

MHE. AIDA J. KHENAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawasiliano ya Simu. Kulingana na umuhimu wa mawasiliano kwa binadamu ili kuweza kutimiza malengo yao kwa wakati ni vema Serikali ikamaliza tatizo kwa kupeleka minara ya simu kwenye maeneo ambayo bado hayajapata mawasiliano. Kwa mfano Jimbo la Nkasi Kusini, Wilaya ya Nkasi iliyopo Mkoa wa Rukwa, Kata ya Kala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Meli ya *MVLiemba*. Meli hii imekuwa ya muda mrefu na imechoka, Serikali kwa nini isituletee meli mpya ili kuokoa maisha ya wananchi wa Ziwa Tanganyika? Suala la barabara inayotoka Sumbawanga – Kanazi limechukua muda mrefu na kuleta usumbufu mkubwa kwa wananchi wanaotoka Namanyere, Kilando, Kabwe na maeneo mengine ya Wilaya ya Nkasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Kiwanja cha Ndege cha Manispaa ya Sumbawanga. Mpaka sasa wananchi wa Sumbawanga wanashindwa kuendelea na shughuli zao wakisubiri kulipwa baada ya tathmini. Nashauri Serikali baada ya tathmini, iwalipe wananchi hawa na kama kuna matatizo ya kifedha basi waruhusiwe kuendelea na shughuli zao za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usalama katika Bandari; kuna kila sababu ya Serikali kufanya tathmini ya kutosha katika maeneo ya bandari, kwa sababu kumekuwa na changamoto na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi na wafanyakazi wa bandari. Suala la fedha kutofika kwa wakati, nalo linakera, ni tatizo kwenye maeneo mengi nchini na kupelekea usumbu mkubwa kwa kutomaliza miradi mbalimbali ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Barabara Kujengwa Chini ya Kiwango; suala hili limikuwa endelevu katika mikoa yetu. Nashauri Serikali iwachukulie hatua wakandarasi wote wanaofanya kazi chini ya kiwango na kutoa taarifa kwenye maeneo mengine ili wawafahamu wakandarasi wazuri na wabaya ili wasirudie kuwapa kazi wakandarasi wasio na sifa.

MHE. LOLESTIA J.M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kipongeza Serikali na Wizara ya ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa kazi nzuri inayofanyika katika Taifa letu hasa katika ujenzi wa barabara na reli. Katika hotuba nimeona jinsi ambavyo Serikali imepanga kuanza rasmi ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Geita – Bukoli – Kahama. Napongeza kwa mpango huo mzuri kwani utaongeza na kuimarisha uchumi kwa Mikoa ya Geita na Shinyanga. Vile vile nashukuru kwa kilomita moja ya lami kwa barabara ya Geita – Bukombe. Pamoja na shukrani hizo ningependa kupata ufanuzi, ni lini ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kilomita 10 za lami katika mamlaka ya Mji mdogo wa Katoro/Buserere itaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni upandishwaji hadhi wa barabara ya Katoro – Kamena – Mwingiro. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita kwa kipindi kirefu sasa tumeomba barabara ya Katoro – Kamena – Mwingiro, ipandishwe hadhi kuwa barabara ya Mkao. Mapendekezo hayo yamepitishwa katika ngazi zote kuanzia kwenye Baraza la Madiwani pamoja na DCC. Nilipoangalia kwenye bajeti ya 2017/2018 sijaona hatua yoyote ya Wizara katika utekelezaji wa ombi. Hivyo, napenda kujua ni lini sasa barabara ya Katoro – Kamena – Mwingiro itapandishwa hadhi kuwa

barabara ya Mkoa? Barabara hii ni kiunganishi muhimu sana kati ya Wilaya ya Geita na Wilaya ya Nyang'hwale na kwa msingi huo ikiboreshw (ikipandishwa hadhi) itasaidia sana kuimarisha uchumi ndani ya Mkoa wa Geita. Kwa sababu hiyo, nashauri Serikali kupitia Wizara ilichukue ombi letu na kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja.

MHE. JUMAA H. AWESO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hotuba hii muhimu ambayo ni sekta yenye mchango mkubwa kwa maendeleo ya Taifa letu. Pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na watumishi wote wa Wizara hii. Binafsi nimevutiwa na utendaji wao wa kazi kama kauli ya Mheshimiwa Rais wetu ya Hapa Kazi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Rais kwa ahadi zake kwenye Jimbo la Pangani na kuzitekeleza kwa wakati kwa kutupatia kivuko kipycha cha MVTanga na kutupatia fedha za ujenzi wa geti, umetugawia na tumekabidhiwa mradi huu muhimu wa geti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara; ujenzi wa barabara ni kichocheo cha shughuli za kiuchumi na hata kuongeza ajira. Maeneo ambayo yamebadilika kwa kiasi kikubwa katika uchumi hata huduma za kijamii yana barabara nzuri. Niombe Wizara hii iangalie kwa umuhimu wake Ujenzi wa barabara ya Tanga – Pangani – Saadani – Bagamoyo, ambayo ni ahadi ya muda mrefu. Hivyo ni wakati wa kujenga barabara hii ili iifanye Wilaya ya Pangani ipate maendeleo kutokana na fursa nyigine 21 zilizopo Pangani, ikiwemo Mbuga ya Wanyama ya Saadani. Pia ujenzi wa barabara hii uende sambamba na ulipaji wa hatua kwa hatua kwa wananchi wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gati ya Pangani. Tunashukuru kwa kutujengea gati hili. Pia naomba Serikali ili gati hili liwe na tija na kuweza kupata mapato kuanzishwe usafiri wa majini, kwa maana ya kutupatia *fast boat* ya kutoka Pangani kwenda Mkokotoni. Mwekezaji ameshapatikana, cha muhimu ni kumpa ushirikiano wa dhati katika kufanikisha upatikanaji wa *boat* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mawasiliano; jamii ili ipige hatua ya maendeleo lazima iwe na mawasiliano ya uhakika, hii itachangia urahisishaji katika shughuli za kijamii na kiuchumi. Hivyo, Serikali itusaidie mawasiliano kwa maeneo ya Mkalamo, Mrozo na Bushori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. STEPHEN J. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na tabia ya kusahau barabara ya Korogwe – Dindira – Bumbuli - Somi kwa kiwango cha lami tangu mwaka 2010 hadi leo wakati barabara hii imo ndani ya Ilani Uchaguzi ya Cham cha Mapinduzi ya mwaka 2010. Kila siku inasahaulika na cha kusikitisha mwaka huu wa fedha 2017/2018 imetengewa kiwango kidogo cha fedha cha sh. 130,000,000/=, hii haina msaada wowote. Pili, Mji Mdogo wa Mombo uliahidiwa kuweka kiwango cha lami tangu mwaka 2014 hadi leo hakuna msaada wowote ambao umefanyika, kila kukicha maneno tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za mkoa hadi leo zinajengwa chini ya kiwango kiasi ambacho fedha zinatengwa lakini utengenezaji wake si wa kuridhisha. Fedha zinahamishwa bila sababu yoyote, kwa mfano barabara ya Korogwe – Magoma – Maramba – Mabokwemi kuna sehemu hazikumaliziwa kabisa. Barabara ya Korogwe – Mnyuzi – Maguzoni kuna kama kilometa 15 zilitakiwa *heavy grading* lakini hata kilometa tisa hazikufanyika. Sasa Serikali ili angalie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara zinatakiwa kupandishwa hadhi kutoka za Wilaya kuwa za Mkoa. Hadi leo hakifanyiki chochote wakati *DCC* imepitisha *RCC* imepitisha. Barabara hizo ni hizi zifuatazo:-

- (a) Barabara ya kutoka Mombo hadi Mzeli inaunganisha wilaya mbili na Mkoa kwa ujumla;
- (b) Barabara kutoka Makuyuni hadi Mpakani Bumbuli; na
- (c) Barabara ya kutoka Msambiazi hadi Bungu na kuunganisha Wilaya Bumbuli haijafanyiwa chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawasiliano. Kuna Kata ya Kizara mawasiliano hakuna, kuna Kata ya Kalalami katika Kijiji cha Kigwasi (wachimbaji wa madini) na inapakana na Mbuga ya Wanyama ya Mkomazi hakuna mawasiliano. Serikali isiangalie tu mjini na huku wapo wananchi wenu. Nategemea Mheshimiwa Waziri atakuja na majibu mazuri.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yangu yote ya Ofisini kwa Naibu Waziri na Katibu Mkuu yazingatiwe.

- (i) Kukasimu barabara ya Mugeta – Misingo – Mekomario (Bunda) hadi Sirorisimba (Butiama) na Serengeti.
- (ii) Kutangaza mkandarasi wa barabara ya Nyamuswa – Bunda (ahadi ya Mheshimiwa Waziri 31/12/2016) aliposimama Kata ya Nyamuswa na kuahidi kutangaza mkandarasi ifikapo Februari, 2017.
- (iii) Kutangaza mkandarasi kipande cha Sanzate hadi Nata. Nasikitika kuona kipande hiki kimerukwa badala yake Wizara ilitangaza barabara ya Nata. Kwangu naona kama sikutendewa haki na hasa ikizingatiwa hii *Lot* ilitakiwa kwisha kabla ya kutangaza huku. Naomba haki itendeke.

(iv) Uwanja wa Ndege Musoma, Mheshimiwa Waziri alishasema anatafuta shilingi bilioni 10 za ukarabati wa uwanja huu mapema 2016/2017. Nasikitika kuona bajeti iliyotengwa ni shilingi bilioni tatu badala ya shilingi bilioni 10. Naomba suala hili lizingatiwe.

(v) Reli ya Arusha – Musoma. Reli hii toka mwaka 1975 inapewa ahadi hadi leo. Tunaomba kwa miaka mitano watu wa Musoma waone jitihada ya Serikali katika kujenga reli hii.

(vi) Bandari ya Musoma ilikuwa ikipokea meli ya *MV Victoria*, *MV Butiama* na *MV Umoja*. Nimeona juhudzi za Wizara za kutengeneza meli hizo, tunaomba meli hizo zikitengenezwa zifike Musoma. Matengenezo ya Bandari ni kidogo sana.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi nzuri ya kutuongoza Watanzania. Pili, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na watendaji wote wa Wizara yake kwa jinsi wanavyowajibika kuwashudumia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite katika hoja tatu.

(i) Wakazi waliopo pembezoni mwa Uwanja wa Ndege Njombe.

(ii) Ujenzi wa Uwanja wa Ndege Njombe.

(iii) Ujenzi wa barabara ya Itoni - Manda kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi waishio pembezoni mwa Uwanja wa Ndege Njombe Mjini hawatendewi haki na hawajui hatma yao. Naiomba Serikali itoe ufanuzi juu ya wananchi hawa kwani hawafanyi

maendelezo, hawapewi hati na wala hawakopesheki. Hii kwa kweli ni kuwanyima maendeleo, ni vizuri sana Serikali ikatoa ufanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Ndege wa Njombe katika llani ya CCM umetamkwa kwamba utawekwa lami. Niombe Serikali sasa itekeleze ahadi hii. Njombe sasa inakua kisiwani kwa kukosa huduma ya usafiri wa ndege kwa kukosa uwanja. Naiomba Serikali ituone na sisi Wanajombe tunahitaji uwanja ili tuendane na kasi na mafanikio ya nchi yetu kwa kupata usafiri wa ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Itoni - Manda nayo imo kwenye llani ya CCM. Ukiacha miradi ya kielelezo iliyopo Ludewa, maeneo ambayo barabara hii inapita ndiyo maeneo muhimu sana ya uzalishaji wa chakula, mbao, nguzo na chai. Wakulima na wafanyakishara wametaabika kwa miaka mingi sana kwa kusafirisha mazao katika barabara hii. Serikali imeanza kazi ya kuweka zege barabara hii eneo la Mkia hadi Mawengi kilometra 50 ndani ya Jimbo la Ludewa. Niishauri Serikali, kazi hii ianzie Itoni kuelekea Mkia kwani itasaidia kuondoa ugumu wa usafirishaji wa mazao ya wananchi katika Kata za Uwembe, Luponde, Matola ndani ya Jimbo la Njombe Mjini na Kata ya Madope, Jimbo la Ludewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango wangu nillochangia kwa kuongea, napenda pia niongeze mchango wangu kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia magari ya zimamoto katika viwanja vya ndege. Viwanja vingi vina changamoto kubwa sana ya magari ya kuzima moto kikiwepo na Kiwanja cha Nduli, Mkoa wa Iringa. Gari lilloletwa Mkoa wa Iringa lilitokea Kiwanja cha Tabora likiwa bovu na halijawahi kufanya kazi toka limeletwa. Hivyo kiwanja hakina gari la kuzimia moto, gari linalotumika ni la

Ofisi ya Zimamoto kama kukiwa na ugeni wa viongozi na sasa hivi gari lile limepata ajali. Napenda kufahamishwa utaratibu unaotumika kupeleka haya magari katika viwanja au kama kuna vigezo vinavyotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nizungumzie *TCRA* na mtambo wa *TTMS*. Nashukuru sana kwa uongozi wa *TCRA* kwa kutupatia semina ya uelewa wa taasisi yao ikiwemo na matumizi ya huu mtambo wa *TTMS*. Pamoja na huu mtambo kuwa ndio mtambuzi wa namna bora ya kupata taarifa za makusanyo ya makampuni ya simu ili Serikali iweze kutoza kodi stahiki kutokana na miamala ya fedha inayofanyika kuititia simu za mikononi, je, ni lini sasa ule mfumo wa *Revenue Assurance Management System (RAMS)* utafungwa? Tulipotembelea *TCRA* tuliambiwa kuwa wana mazungumzo na mkandarasi, nini mkakati wa Serikali kuhusiana na hilo? Napenda kujua kuhusu suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, niongelee kuhusu madeni ya *TTCL*. Pamoja na Serikali kumiliki hisa kwa 100% lakini bado shirika hili linatakiwa liendelee kuijendesha. Je, ni lini Serikali itaweka mkakati wa kuhakikisha madeni yote yanalipwa, sababu imeamua kulipa madeni yake? Wizara zote zilishafanya uhakiki wa madai, je, haya madeni ya *TTCL* Wizara wameshaanza kulipa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ni *Internet Data Center*. Niipongeza Serikali kwa ujenzi wa kituo hiki kwa ajili ya kutunza na kuhifadhi kumbukumbu. Hata hivyo, ukiangalia katika bajeti zetu kuna baadhi ya Wizara na Taasisi za Serikali pia zinatenga bajeti kwa ajili ya kuwa na *data center* zao. Je, ni kwa nini kituo hiki kisitumike kwa taasisi zote za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, ni *TAZARA*. Nataka kujua ni lini ule upungufu wa ile Sheria Na. 23 ya mwaka 1975 kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria Na. 4 ya mwaka 1995 itafanyiwa marekebisho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na afya na kuweza kuchangia hoja hii. Mchango wangu ni kama ifuatavyo:

(i) Fedha zinazotengwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ujenzi wa barabara zinachukua muda mrefu sana kutolewa na Hazina na pengine itolewe kidogo sana na hivyo kutokidhi ukamilishaji wa barabara zetu. Hali hii imeathiri sana ujenzi wa barabara zinazounganisha Mkoa wetu wa Manyara Makao Makuu Babati na Wilaya zake zote kwa kiwango cha lami. Matokeo yake hali hii ya kutokuwa na barabara za uhakika, hasa wakati wa masika, inarudisha nyuma uchumi wa mkoa na wilaya zote za mkoa wetu ambazo ziko pembezoni, bila barabara hali ya wananchi inabaki kuwa duni sana, hususani Wilaya za Mbulu, Simanjiro, Kiteto na Babati Vijiijini. Tunaomba Serikali itoe fedha kwa wakati kwa barabara zote zilizo ndani ya Ilani ya CCM 2015-2020 mfano barabara ya Kondoa – Kibaya – Kongowa; barabara za Babati – Dareda – Haydom - Mbulu na barabara zote zilizoko kwenye njia kuu za kiuchumi.

(ii) Serikali ibuni utaratibu mzuri wa kuboresha manunuzi ya umma. Uzembe na kukosa uaminifu kunasababisha kujenga miundombinu hafifu ya barabara na sekta nyinginezo zilizo ndani ya Wizara ya Ujenzi.

(iii) Serikali pia iweke fedha ya kuboresha Uwanja wa Ndege wa Arusha ambao sasa hivi hauruhusu ndege kubwa kutua. Uwanja huo utasaidia sana kwa sababu sasa hivi wageni wengi, wakiwepo watalii wengi wanatua *KIA* wanaelekea Arusha. Hivyo wakitua Arusha moja kwa moja itawawia rahisi kufika Arusha saa 1.30 bila adha ya kuandaa *shuttle* na kuchukua muda mrefu kuliko muda waliotumia toka Dar es Salaam *KIA* kwa ndege (dakika 45-50).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia kwenye Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Busokelo lipo Mkao wa Mbeya, Wilaya ya Rungwe. Kwa bahati mbaya sana miundombinu ya barabara haipo vizuri. Jimbo hilo tunalima mazao mbalimbali, kwa mfano, ndizi, kokoa, chai, viazi mviringo na vitamu, mihogo, mahindi, ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, kilimo cha matunda, maparachichi, upasuaji wa mbaao na shughuli zingine mbalimbali. Hata hivyo, miundombinu ya barabara ni mibovu sana, imesababisha mazao mengi kuoza, kuharibikia shambani na hivyo kuwafanya wananchi wa Busokelo kuwa maskini kwa sababu ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara tunazoomba kupandishwa hadhi ziwe chini ya *TANROAD* Mkao wa Mbeya ni zifuatazo:-

- (i) Barabara ya Lwangwa – Tiete-Lufilyo (kilomita15).
- (ii) Barabara ya Kanyelele (Gesi) – Mpata –Ipembe –Suma (kilomita15).
- (iii) Barabara ya Kyejo (Gesi) – Lwangwa (kilomita 5.7).
- (iv) Barabara ya Lugombo-Bujingijira – Ngumbulu - Mbeya Vijijini (kilomita10).
- (v) Barabara ya Itete – Kisegese – Ntaba - Ngeleka - Matema (kilomita 30).
- (vi) Barabara ya Kilasi – Kitulo (Livingstone) - Makete (Njombe) (kilomita 30).

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya lami kutoka Katumba (Tukuyu) - Lwangwa - Mbambo Tukuyu, tunaomba

sana iendelee kujengwa kwa kiwango cha lami kutoka Busokelo – Isange - Katumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu *TCRA* waweke mifumo ya kukusanya kodi toka kwa *mobile operators*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Ndege wa Songwe. Uwanja huu ni muhimu sana kwa Nyanda za Juu Kusini. Uwanja unahudumia Mbeya, Njombe, Rukwa, Katavi na Ruvuma pamoja na nchi jirani kama Malawi, Zambia, Congo na nyinginezo. Tunaomba kuwekewa taa za kuongozea ndege, kwa hali ilivyo hivi sasa, ndege haziwezi kutua wakati wa usiku na wakati wa ukungu na hivyo kusababisha hatari kwa abiria na usalama kwa ndege zenyewe. Aidha, naomba jengo la utawala liliopo Songwe limaliziwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuundwa kwa Bodi ya Wanasyansi waliomaliza masomo ya *computer Science and Information Technology*. Nchi yetu inapita kwenye sayansi na teknolojia. Asilimia kubwa ya pato la Taifa ni kutokana na mifumo ya *IT*. Napendekeza kuwepo na Bodi ya wana-*IT* ambayo itasimamia uvumbuzi wa teknolojia ndani ya nchi yetu kuliko kutumia wataalam kutoka mataifa ya nje kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *softwares & database*; nashauri Serikali yetu ianze kutumia *Open Source* na *STO Commercial Softwares* ili kupunguza gharama za manunuzi na za uendeshaji. Kwa mfano, *Postgress*, *SQL server*, *Geo-Network*, *Geo-Server*, *Survey Gizmo* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TTCL, *National Internet Data Centre*. Pamoja na kujenga *data centre* naomba iwe very strong na ijengwe maeneo tofauti tofauti ili *back-ups* ziwe mbali na *systems*.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa pongezi kwa wale wote waliopata bahati ya kujengewa barabara kwa kiwango cha lami katika

maeneo yao nikiamini kwa kuwa wamepata wataunga mkono suala la kuhakikisha wale ambao hawajapata nao wanapata. Awamu ya Nne ililenga kufungua mikoa ya pembezoni, sambamba na kuiunganisha mikoa hiyo. Naamini wazo hilo bado ni la msingi kwa Awamu hii ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu Kitaifa unalenga kudhibiti uzito wa magari na matumizi sahihi ya mizani. Ushauri wangu, ili kulinda barabara zetu yawezakana adhabu ya *fine* imezooleka, wakati umefika wa kuangalia adhabu yenye mguso kuepuka kujirudiarudia kwa suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la hifadhi ya barabara ni jambo la msingi. Suala hili liendelee kuangaliwa katika mipango ya muda mrefu ili kuepuka bomoabomoa na uwepo wa majengo yenye mandhari mbaya pembezoni mwa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mpanda – Ugalla – Kaliua – Ulyankulu - Kahama (kilomita 457), naomba iangaliwe kwa jicho la pekee kwani mara barabara hii itakapojengwa itakuwa kwanza ni njia ya mkato/fupi lakini itakuwa ni ufumbuzi wa ziada iwapo barabara ya Mpanda – Inyonga – Koga - Tabora itapata shida ya kujifunga au vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kasi ya ujenzi wa barabara ya Ifukutwa - Vikunge (kilomita 35). Rai yangu ili ujenzi huu uwe na tija, tuone uwezekano wa upatikanaji wa fedha ili kipande kuelekea Uvinza kiweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Daraja la Kavuu na barabara unganishi. Kilomita 10 za barabara unganishi naomba ziendelee kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia malalamiko ya wakazi waliopisha ujenzi na upanuzi wa Uwanja wa Ndege Mpanda kuhusu fidia yaendeleee kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kasi ya ujenzi wa barabara ya Tabora – Ipole - Koga - Mpanda kilomita 373 iongezeke kama kweli fedha ya ujenzi huo zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho pamoja na ujenzi wa reli ya kat, napongeza matengenezo yote yanayoendelea katika reli ya Mpanda. Niombe ratiba ya treni hiyo ya abiria iendeshwe kwa kufuata ratiba sambamba na uongezaji wa mabehewa likiwemo behewa la daraja la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kunga mkono hoja kwa asilimia mia.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na timu yake kwa utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa kipindi hiki cha 2016/2017 lakini kwa maandalizi ya utekelezaji wa mpango huu wa 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa dhati kuishukuru Serikali kwa kufanya usanifu kilomita 91 za barabara za Masasi – Nachingwea - Nanganga kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, kwa barabara za mkoa ambazo zipo katika mpango wa mwaka 2017/2018 kilomita 537.9, naiomba Serikali kuiangalia barabara itokayo Nachingwea – Liwale kwani hali si shwari, kipindi cha masika barabara hiyo haipitiki kabisa. Naiomba Serikali kuingiza katika mpango wa bajeti ijayo ya mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Ndege wa Lindi ni mkongwe sana na ulitumika hata kipindi cha Ukoloni na ni kiwanja bora katika Afrika ulikuwa namba tatu. Kwa hiyo, naomba sana Serikali kuhakikisha uwanja wa Lindi unapewa kipaumbele ukizingatia Lindi sasa tunategemea uwekezaji mkubwa wa kiwanda cha *LNG*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali imeweza kutuunganisha Watanzania kupitia sekta ya mawasiliano.

Bado katika Mkoa wa Lindi tuna vijiji havina kabisa mawasiliano. Kwa mfano, Nachingwea (Kijiji na Mbondo); Ruangwa (Nangurugai na Nandandala); Kilwa (Mandete, Mandawa, Mavuji na Kandawale) na Liwale (Ngongowele, Mirui, Mlembwe na Mpigamiti). Naomba Serikali kupitia Mfuko wa *UCSAF* kuvisaidia vijiji hivi viweze kupata mawasilino.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nimpongeze Waziri na watendaji wa Wizara kwa kazi inayofanyika sasa. Pongezi hizo zinatokana na ukweli kuona Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ameonesha njia na uongozi mahiri wenye kulenga kuibadili Tanzania na kupiga hatua za haraka katika maendeleo. Yapo mambo mengi yamefanyika ikiwemo ujenzi wa reli ya *standard gauge*, kufufua *ATC*, kutenga asilimia 40 ya mapato na kuelekeza katika shughuli/miradi ya maendeleo. Pamoja na pongezi hizo, yapo maeneo muhimu ya kuchangia kama ifuatavyo:-

(i) Daraja la Sibiti linalojengwa sasa na shilingi 3.5 bilioni zimetengwa lakini barabara hiyo yenye daraja linalouanganisha Mkoa wa Simiyu na Singida lakini katika bajeti hiyo ni lini upembuzi yakinifu utafanyika?

(ii) Wilaya ya Mkalama ni mpya na haina hata kilomita moja ya lami na zipo shughuli nyingi za kiuchumi, tunaomba Wizara itenye fedha za ujenzi wa kilomita 30 za lami kutoka Iguguno -Ndugahi yalipo Makao Makuu ya Wilaya.

(iii) Badowananchi wa Mkalama wanapata shida ya mawasiliano kutokana na kutokuwepo minara ya kutosha. Tunaomba Wizara iweke mikakati ya kuhamasisha makampuni ya simu kuweka minara hasa katika Kata za Kinyampanda, Mwangeza, Ibaga, Mpambala, Msingi na Kinyangiri.

(iv) Zipo barabara ambazo hazihudumiwi na *TANROAD* wala Halmashauri pamoja na kuwa maeneo husika yana wakazi wengi pia ni maeneo yenyeye uzalishaji mkubwa mazao hasa mahindi na alizeti. Hivyo, naomba Wizara ichukue jukumu hili kwa kufungua barabara husika ya Msingi – Yulansonni – Lyelembu -Kitumbili (kilomita 25).

(v) Ipo barabara ambayo inaunganisha mikoa miwili kuititia Wilaya ya Mholame nayo tunaomba itengewe fedha, upembuzi yakinifu ufanyike. Ni barabara ya Haydom - Kidasafa – Nkungi - Ilongero - Singida (kilomita 93.4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa mipango mizuri ya kuimarisha miundombinu ya barabara zinazouanganisha mikoa na mikoa, wilaya na wilaya kwa kujenga kwa kiwango cha lami. Pia naipongeza Serikali kwa kujenga barabara ya kutoka Dodoma – Iringa na Iringa - Mafinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kumalizia kujenga barabara ya Mafinga hadi Chimara; Barabara ya Nyololo hadi Igowole - Kibao – Mtwango (kilomita 40); barabara ya Mafinga hadi Mgololo (kilomita 84) na barabara ya Igowole – Kasanga -Nyigo. Barabara hizi ni ahadi ya Rais pia mipango ya Chama cha Mapinduzi (CCM), ukurasa wa 71 imeandikwa. Barabara ya Nyololo -Igowelete - Mtwango (kilomita 40), upembuzi yakinifu ulishafanyika mwaka 2013/2014 na 2014/2015 Serikali iliahidi kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha Lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua madhubuti anazozichukua kuhakikisha kuwa kasi yetu ya uchumi inaendelea kukua kwa kusimamia mapato na kuyaelekezea katika sekta za kiuchumi na uzalishaji. Ni hatua za kupongezwa sana. Aidha nampongeza sana Waziri, Naibu

Waziri pamoja na watendaji wa Wizara na taasisi zake.
Naomba maelezo ya kina kuhusu yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ujenzi wa *flyovers* Dar es Salaam. Hii ni hatua ya kupongezwa sana kwa kuwa ujenzi wa *flyovers* ni jambo ambalo Serikali za awamu zote imetamani ilifanye. Ni hatua ambayo itawezesha harakati za kiuchumi katika mikoa ya jirani na Dar es Salaam. Hata hivyo, wananchi wangependa kufahamu juu ya ujenzi huu sasa na tafsiri yake kiuchumi ukilinganisha na maamuzi ya Serikali kuhamia Dodoma. Ukiangalia kwa sasa foleni ya Dar es Salaam imepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na uwepo wa mabasi ya mwendo kasi. Aidha, uamuzi wa Serikali kuhamia Dodoma umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza foleni pale Dar es Salaam. Swali linakuja, je, hizi *flyovers* zitaleta *economic returns* ukizingatia sababu za uwepo wa foleni pale Dar es Salaam zimetatuliwa kwa kiasi kikubwa? Je, isingewezakana fedha za ujenzi wa *flyovers* zikatumika kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali hapa Dodoma? Naomba maelezo ya kina ili wananchi wapate kuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, uuzwaji wa hisa za *Vodacom*. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kutokana na zoezi la uuzwaji wa hisa za kampuni za simu kuanza kutekelezwa. Mheshimiwa Waziri amesimamia jambo hili tokea marekebisho ya kanuni zake ingawa limechukua muda mrefu. Hata hivyo, mauzo ya hisa za *Vodacom* bado hayajatangazwa sana kwa wananchi kupata uelewa wake. Vilevile kuna hisia kwamba hisa za *Vodacom* ziko *over priced* ukilinganisha na thamani halisi ya kampuni. Tunaomba Wizara ikishirkiana na *TCRA* na Wizara ya Fedha na Mipango, waliangalie jambo hili kwa umakini ili kuondoa hisia hizi zilizopo.

Mheshimiwa Spika, tatu, Shirika la Simu Tanzania (*TTCL*). Napongeza hatua kubwa ya mabadiliko katika Shirika la Simu Tanzania. Mabadiliko haya yanapelekea Watanzania kunufaika na kujivunia kuwa na shirika lao wenywewe la simu. Hata hivyo, tunaomba, baada ya hatua hii *TTCL* iwezeshwe

kimtaji iweze kuweka miundombinu sahihi kwenye simu iweze kushindana katika soko la mawasiliano. Changamoto kubwa tunayopata sisi Watanzania ni kutokana na huduma zisizoridhisha za *TTCL*. Kwa upande wa *ISP*, *TTCL* bado hawako vizuri *despite* ya kutumia miundombinu ya umma (*fibre optic*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Pemba. Ingawa kwa muda mrefu jambo hili limekuwa likzungumzwa bado hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa hadi leo. Uwanja wa Ndege wa Pemba ambao umewekwa katika program ya ujenzi kupitia *EAC*, Waziri hajazungumza lolote kwenye hotuba yake. Naomba atupatie maelezo kama Waziri mwenye dhamana hii ya mawasiliano na ujenzi kuhusu uwanja huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii kwa kazi nzuri azifanyazo akishirikiana na Naibu Waziri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu miundombinu ya mitandao ya simu katika Kisiwa cha Pemba. Kwa kuwa Kisiwa cha Pemba mtandao unaopatikana kwa urahisi katika maeneo mengi na hasa vijiji hususani mtandao wa *Tigo* haapatikani vizuri. Naiomba Serikali kupitia Wizara hii iweze kulishughulikia suala hili la mtandao wa *Tigo* uweze kuenezwa sehemu zote katika kisiwa hiki kwa kuwa mitandao husaidia sana wananchi na hasa wafanyabiashara katika mawasiliano ya haraka na ya karibu. Naishauri Serikali kulishughulikia tatizo hili la mtandao wa simu katika Kisiwa cha Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niongelee kuhusu viwanja vyta ndege. Pamoja na Serikali kuviumarisha viwanja vyta ndege katika nchi hii sambamba na Serikali kununua ndege za kisasa za kuhudumia wananchi wake, napenda

kuomba Serikali iendelee kukifanyia ukarabati mkubwa Kiwanja cha Ndege cha Pemba na zaidi kukipanua ili kukihi huduma ya kupokea ndege kubwa za kisasa pamoja na kuziwezesha ndege hizi kuruka na kutua muda wote wa mchana na usiku. Wananchi wa Pemba wanapendelea sana kutumia ndege kwa ajili ya safari za kijamii na kibiashara, naomba marekebisho yafanywe katika kiwanja hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.
Ahsante.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja iliyio mbele yetu. Aidha, baada ya kuunga mkono hoja, naomba nichangie baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na Naibu Waziri na watendaji wote ukianzia na Katibu Mkuu (Ujenzi) na Katibu Mkuu (Uchukuzi na Mawasiliano) pamoja na wataalam wote wa Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi, naomba nichangie kwa kuanza na Jimboni kwangu. Niombé Serikali ihakikishe inajenga barabara ya kutoka Sumbawanga - Matai - Kasanga *Port* kwa kiwango cha lami. Ujenzi huu umechukua muda mrefu sana kutokana na upatikanaji wa fedha kutoka Wizara ya Ujenzi kwenda kwa mkandarasi na hivyo mradi kuwa na gharama kubwa kutokana na Serikali kulazimika kulipa fedha nyingi kutokana na mkataba. Kiasi cha fedha kilichotengwa ni cha kutosha, niiombe Serikali ihakikishe fedha zinatolewa ili mradi huu wa barabara uweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ninalopenda kuchangia ni juu ya ujenzi wa barabara ya kutoka Matai - Kasesya *border*, ambayo Mheshimiwa Waziri alipata nafasi ya kuitembelea na kuahidi kwamba mara mkandarasi atakapopatikana ujenzi utaanza. Katika mwaka huu wa fedha wa 2016/2017, Serikali iliweza kutenga kwenye bajeti

kiasi cha shilingi bilioni 11 na ukisoma taarifa ya Mheshimiwa Waziri imeonesha kwamba taratibu za kumpata mkandarasi zinaendelea. Ni imani yangu kubwa kwamba kiasi cha fedha kitawea kutolewa kabla ya mwaka huu wa fedha haujamalizika. Katika bajeti ya mwaka wa fedha wa 2017/2018 barabara hii imeweza kutengewa kiasi cha shilingi bilioni 4.9 kutoka shilingi bilioni 11 kwa mwaka wa fedha 2016/2017, sitarajii gharama za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kupungua kwa zaidi ya nusu. Naiomba Serikali iharakishe utaratibu wa kumpata mkandarasi ili aanze ujenzi wa barabara hii muhimu sana kwani siamini kwamba nchi hii ina tatizo la upatikanaji wa wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni kuhusu ujenzi wa Daraja la Mto Kalambo, ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa akiwa Waziri wa Ujenzi na akasisitiza siku alipokuja kuomba kura Kalambo akimtaka Mkurugenzi atangaze mara moja kazi ya ujenzi wa daraja hilo. Naomba niishukuru Serikali kwa kutenga kiasi cha shilingi milioni 100 japo kiasi hiki sidhani kama kinatosha kwa kuzingatia ukubwa wa daraja hili. Naiomba Serikali ihakikishe kwamba ujenzi wa daraja hili unaanza mapema na hasa kipindi cha kiangazi kwani mvua zikishaanza kunyesha siyo rahisi ujenzi kufanyaika kwani mto hufurika kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ifike mahali Serikali itimize ahadi zake kwa vitendo kuhusu ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Sumbawanga kwani ahadi hii ni ya muda mrefu sana. Umuhimu wa uwanja huu baada kukamilika kwa Uwanja wa Kimataifa wa Songwe na ule wa Mpanda Mkoani Katavi unajulikana na hakuna hata chembe ya ubishi. Naomba Serikali sasa itende haki kwani fedha za kutoka nje ni miaka zaidi ya mitatu zimekuwa zikioneshwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ngazi ya kitaifa naomba kuchangia kuhusiana na mradi wa usafirishaji wa *DART*. Ukienda kwenye mataifa ya nje mionganoni mwa miradi inayopigwa mfano Kusini mwa Jangwa la Sahara basi utakuta miradi miwili kama *one success stories* nayo ni treni ya umeme ya Lagos na Mradi wa Mabasi ya Mwendo Kasi ya

Dar es Salaam. Ni jambo la busara kwa kuwa mradi huu kama moja ya miradi ya kitaifa na wenyewe mafanikio makubwa na hivyo kutouchukua kama mradi wa watu wa Dar es Salaam. Hivyo sote tuna jukumu la kuhakikisha kwamba mradi huu unapewa upendeleo wa pekee kwa maslahi ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile uwekezaji mkubwa unafanywa na Serikali kwa maana ya ujenzi wa miundombinu kwa awamu ya kwanza, ya pili, ya tatu na hata ya nne iko haja kubwa kwa Serikali kuhakikisha uwekezaji mkubwa unafanywa kwa Serikali kuuza baadhi ya hisa zake kwa Watanzania wengi na pia kuwa na maongezi ili mbia wa Serikali naye auze hisa zake kwa kuzipeleka *DSE (Dar es Salaam Stock Exchange)* ili umiliki uwe wa wananchi wengi na ili mtaji mkubwa uweze kupatikana utakaowezesha uwekezaji mkubwa ikiwa ni pamoja na kiwanda cha kuunganisha mabasi hapa nchini pamoja na uzalishaji wa matairi, hilli litawezesha kauli ya Serikali yetu ya CCM ya Tanzania ya viwanda kutekelezeka kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mataifa ya wenzetu kama Ethiopia, Japan, Korea na kwingine wameweza kufanikiwa kwa kuweka mikakati maalum ya kuhakikisha kwamba kunakuwepo na upendeleo maalum kwa wazawa na makampuni ya wazawa wazalendo. Wakati umefika sasa kama Taifa tukafanya uamuzi huo bila ya kuchelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msemo wa Waswahili unaosema ukiona vinaelea vimeundwa. Hayo makampuni yanayotamba duniani kama vile *Samsung*, *Dangote*, *Hutchison Whampoa*, *DSM Port Operator - TICTS*na kadhalika yametokana na maamuzi yaliyofanywa na Serikali zao mahususi kuyafanya yakue kabla ya kuyataka yaanze kushindana na nguvu za soko.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa kuendelea kuamini katika maendeleo ya Mkoa wa Kigoma na hususan Mji wa Kigoma kwa

kuwekeza katika upanuzi wa Bandari ya Kigoma na ujenzi wa Bandari ndogo za Kibirizi na Ujiji. Pia nawashukuru sana kwa kumaliza kazi Bandari ya Kagunga baada ya kuhangaika nayo kwa muda mrefu sana tangu mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona zabuni za Bandari ya Kigoma - Ofisi ya Mkoa na pia taarifa ya kazi ya upembuzi yakinifu kwa upanuzi wa Bandari ya Kigoma. Nimeona zabuni ya Bandari ndogo ya Kibirizi na naamini kuwa zabuni kwa ajili ya Ujiji itakuwa imetoka ili kuwezesha gati kujengwa eneo la Ujiji na kuwezesha ndoto yetu ya kurejesha hadhi ya Ujiji katika maendeleo ya nchi yetu. Miradi hii itaingiza fedha kwenye mzunguko wa uchumi wa mji wetu, kutoa ajira kwa wananchi wetu na kupanua shughuli za uchumi za Manispaa ya Kigoma-Ujiji. Nampongeza Mkurugenzi Mkuu wa *TPA* kwa kuendeleza miradi hii na hii ni ishara ya imani yake kwa ukuaji na maendeleo ya mji wetu na Mkoa wetu wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kumpongeza Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa wa Kigoma kwa juhudni kubwa za kutekeleza miradi ya barabara katika mkoa wetu licha ya changamoto kubwa za fedha. Ujenzi wa mzunguko wa Mwanga Sokoni, taa za barabarani za umeme wajua kuelekea njia panda ya Mwandiga na kuanza kuandaa zabuni kwa ajili ya barabara ya Bangwe – Ujiji ni juhudni ambazo zinatuunga mkono katika juhudni zetu za kufanya mabadiliko makubwa katika Mji wa Kigoma Ujiji. Namwomba Waziri wa Ujenzi ahakikishe kuwa barabara ya Kasulu katika Manispaa ya Kigoma-Ujiji ambayo inaunganisha Mji wa Ujiji na barabara kuu ya Kigoma - Nyakanazi, inajengwa sasa katika orodha ya ahadi za Rais. Barabara hii yenye urefu wa kilometra 7.5 ni barabara ya kimkakati kwani itaongeza barabara mbadala ya kuingia Kigoma badala ya sasa ambapo kuna njia moja tu ambayo ni hatari kiulinzi na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo hapo juu bado watu wa Kigoma wanalia na barabara yao kuu inayounganisha mkoa kuanzia Nyakanazi mkoani Kagera mpaka Kigoma Mjini. Eneo la barabara kuanzia Manyovu –

Kasulu - Kibondo halina mradi wa ujenzi kwani bado mapitio ya usanifu yanafanywa. Kigoma ni mkoa pekee nchini ambao bado haujaunganishwa na mikoa mingine kwa barabara ya lami moja kwa moja bila maeneo ya vumbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kuwa barabara ya Kigoma – Tabora - Singida (Manyoni) – Dodoma sehemu zake muhimu zote sasa zina fedha za wafadhilli ikiwemo Nyahua – Chaya – Urambo - Kaliua na Uvinza - Malagarasi lakini kuna kilomita 41 katika Kazilambwa (Tabora) na Chagu mkoani Kigoma hazina fedha wala mradi. Serikali itazame upya vipaumbele vyake kwani haitakuwa na maana mtu asafiri kwa lami kutoka Kigoma - Dar es Salaam lakini kuwe na kilometra 41 vumbi. Serikali itafute fedha mahali kwingine na kuongeza kipande hiki katika miradi ya kuunganisha Mikoa ya Kigoma na Tabora na Mashariki mwa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudhi za ujenzi wa reli ya kati ni za kimaendeleo na hazina budi kupongezwa na kila mpenda maendeleo. Reli ina faida kubwa kwa nchi na kiongozi yeoyote anayefanya maamuzi muhimu kama haya hana budi kupongezwa kwa dhati. Hata hivyo, Serikali ni lazima ifungue masikio kusikiliza maoni mbadala katika utekelezaji wa miradi mikubwa kama hii ambayo inatumia fedha nyingi na tumeamua kutumia fedha za ndani. Uamuzi wa kutumia fedha za ndani ni uamuzi mchungu kwani maana yake badala ya kuwekeza kwenye miradi ya killimo ili kuongeza uzalishaji wa chakula na bidhaa za kuuza nje, tumeamua kujenga reli. Badala ya kuongeza vyuo vikuu na vyuo vya ufundi ili kuongeza maarifa na wataalam katika nchi yetu tumeamua kujenga reli. Badala ya kuwekeza kwenye kumaliza kabisa tatizo la mtindio wa ubongo (*stuntedness*) ambalo ni tatizo kubwa sana kwa nchi yetu kwa sasa kwani Watanzania 34 katika 100 wametindiwa ubongo tumeamua kujenga reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga ni kuchagua. Mmeamua kwa niaba yetu kutumia rasilimali fedha zetu kidogo kujenga reli (na kununua ndege) na haya mengine yasubiri kwanza. Uongozi ni uamuzi. Mmeamua, hatuna

namna. Hata hivyo, tusikilizeni sisi wawakilishi wa wananchi, mawazo yetu ni kusaidia kupunguza maumivu ya maamuzi yenu bila kuathiri utekelezaji wa miradi husika. Mimi binafsi naunga mkono uwekezaji kwenye reli lakini siungi mkono namna uwekezaji huu unavyofanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa mwaka wa tatu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam nilichagua kusoma kozi *elective* iitwayo *Transport Economics* lakini nilipoingia darasani chini ya Dkt. Natu Mwamba tulijikuta watatu tu darasani. Hatukutosha na kozi ile haikutolewa mwaka ule. Nilichagua kozi ile kwanza kwa sababu ya mwalimu aliyekuwa anafundisha hiyo kozi, wanafunzi tulimpenda sana. Pili, nimelelewa kwenye uchumi wa usafiri, Mji wa Kigoma (bandari, reli na mipaka ya Kongo na Burundi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukosa kozi ile ikabidi nisome mwenyewe na mtu aliyebadilisha kabisa mwono wangu anaitwa Ndugu Ali Karavina, alikuwa Mbunge wa Urambo. Ndugu Karavina na wenzake waliandika kuhusu 'Uchumi wa Jiografia' ukijikita kwenye faida za ujenzi wa reli ya kat. Reli ya kat i ni reli kutoka Dar es Salaam (bandarini) mpaka Kigoma (bandarini) na Tabora - Mwanza, Ruvu - Tanga na Kaliua - Mpanda ni matawi ya reli ya kat i sio reli ya kat.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika andiko lao 'Uchumi wa Jiografia Tanzania', Ndugu Ali Karavina na wenzake walishauri reli ya kat i kwa kigezo cha takwimu za mizigo na ndio maana walisema kwanza ijengwe Dar es Salaam - Kigoma kabla ya popote kutokana na mapato yatakayotokana na eneo hilo, ndio matawi yajengwe. Leo kwa mshangao mkubwa Serikali ya Awamu ya Tano imekuja na tafsiri yake ya reli ya kat i kwamba ni Dar es Salaam - Isaka - Mwanza. Mimi ni Mtanzania, sina tatizo kabisa na Mwanza kwani siku ikifika nitataka kura za watu wa Mwanza lakini mimi ni mzalendo nataka kuona kuwa maamuzi ya kutumia rasilimali za nchi yanakuwa na faida kwa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutumie shehena za mizigo

inayopita Bandari ya Dar es Salaam kujenga hoja kwamba Serikali imekengeuka na kufanya maamuzi ama kwa faida za kisilasa, maslahi ya kikanda au urafiki tu wa viongozi na kupiga teke maamuzi kwa vigezo vya faida za kiuchumi. Mwaka 2015/2016, Bandari ya Dar es Salaam ilipitisha mizigo jumla ya tani milioni tano kwenda nchi tunazopakana nazo. Katika mizigo hii, 34% ya mizigo ilikuwa ya Zambia, 34% ya DRC, 12% Rwanda, 6% Burundi na 2.6% Uganda. Lango la mizigo ya DRC na Burundi ni Bandari ya Kigoma (kimsingi kama reli inafanya kazi). Hivyo, Bandari ya Kigoma inaweza kupitisha 40% ya mizigo yote inayopita Bandari ya Dar es Salaam kwenda nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lango la mizigo ya Uganda na Rwanda yaweza kuwa Isaka na Mwanza ambayo ni takribani 15% ya mizigo yote kutoka Bandari ya Dar es Salaam. Ikumbukwe kuwa hiyo mizigo ya Rwanda na Uganda ina ushindani wa bandari ya Mombasa (ambapo wanajenga reli kwenda huko) ilhali mizigo ya Kongo DRC na Burundi haina ushindani huo na hakuna reli wala mradi wa reli unaojengwa. Sasa, Serikali itueleze sayansi gani ya uchumi waliyotumia kutumia mabillioni ya fedha za ndani kupeleka reli mahali penye mzigoto wa 15% ya mizigo yote na kuacha mahali penye mzigoto wa 40% ya mizigo yote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaweza kujenga hoja kuwa Bandari ya Mwanza itakua lakini ukitazama takwimu za reli utaona kuwa bandari inayokua kwa kasi hivi sasa kwa idadi ya mizigo inayohudumia ni Bandari ya Kigoma. Mwaka 2015/2016, Bandari ya Kigoma ilikua kwa 12% wakati Bandari ya Mwanza ilikua kwa -41.3%. Hizi sio takwimu zangu, ni takwimu za taarifa hali ya uchumi inayotolewa na Serikali yenyewe. Mkurugenzi wa Bandari (*TPA*), Mhandisi Kakoko ana ushuhuda wa juzi tu msafirishaji Azam Dewji kapata kazi ya kupeleka Kongo DRC tani 120,000 ya udongo ulaya (saraji) kwa mwaka na mzigoto huu utapita Bandari ya Kigoma kwa urahisi na wepesi wa kufikisha eneo la mteja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi, Serikali inatumia nini kufanya maamuzi? Ujasiri wa kutopeleka *SGR* Kigoma

kwanza kwa ajili ya faida za kiuchumi unatokana na nini? Serikali inajua nini ambacho sisi wengine hatujui? Njia sahihi yenye faida kwa nchi kwa reli ya katni Kigoma-Dar es Salaam na tawi la Uvinza Msongati, Burundi ili kwenda kubeba mzigo wa madini ya Nikeli. Awamu za Serikali hazina mashiko kiuchumi na ni lazima kubadilisha njia na kupeleka reli mahali penye mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kwenye reli ni hatua za ujenzi. Hivi sasa kazi ya Dar es Salaam-Morogoro imeanza, kilometra 205 kwa thamani ya dola za Marekani bilioni 1.2 (shilingi trillion 2.5). Kipande hiki cha reli kitabeba nini kutoka Morogoro kwenda Dar es Salaam na Dar es Salaam kwenda Morogoro? Mwaka 2016/2017 tumepanga bajeti ya shilingi trilioni moja lakini mwaka 2017/2018 tunapanga shilingi bilioni 900. Hivyo itachukua bajeti tatu kujenga kipande cha reli kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro cha kilometra 205. Hii reli itafika lini huko mtakapotaka ifike na muda huo uwe na uvumilivu wa kiuchumi? Serikali haioni kwamba ingekuwa na faida zaidi kama reli hii awamu hii ingefika Makutupora Dodoma, kilometra 500 halifu *TPA* wakajenga *dry port* hapo ili reli ianze kuzalisha mapato kwa kusafirisha mizigo mpaka Dodoma? Rwanda, Uganda, Burundi na DRC wachukulie mizigo yao Dodoma. Najua swali litakuwa ni fedha za kufika Dodoma. Ni lazima Serikali ianze kufikiria nje ya boksi la fedha za ndani na mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Ethiopia ilijenga bwawa la kuzalisha umeme 10,000 MW. Benki ya Dunia walikataa kuwapa fedha na China walikataa kuwapa fedha. Serikali ya Ethiopia ikawaambia wananchi wake wajenge kwa kuuza *bond* kwa wananchi na hasa wananchi wao waishio nje ya nchi hiyo (*Diaspora*). Serikali iuze *railways bond* kwa wananchi wa ndani na nje ili ku-*finance* kipande cha Morogoro – Makutupora sasa hivi. Serikali ilete Muswada Bungeni wa kuiweka *bond* hiyo kisheria kwa miaka 15 na kupanga/kutenga fedha kwenye bajeti kulipia riba ya *bond* hiyo mpaka iive ambapo tayari uchumi utakuwa umekua na kumudu malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwafanye Watanzania washiriki katika ndoto yake ya kujenga reli kwa njia hii. Tuflikishe reli hii Dodoma na kuwepo na *dry port* Dodoma kwanza ndiyo tutaweza kupunguza gharama na kuanza kupata mapato kutoka katika mradi, mapato ambayo yataanza kulipia madeni au kulipa ujenzi wa kuelekea Tabora na Kigoma na baadaye Mwanza, Uvinza, Musongati na Kaliua na Mpanda. Hayo ndiyo mawazo yangu, mnawenza kuyachukua ama kuyaacha, lakini nashukuru Mungu nimesema na watoto wetu watakuja kufukua historia na kutuhukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kwenye reli ni uchumi kufaidika wakati wa ujenzi. Miradi mikubwa kama hii huwa ina mikataba inaitwa *Offsets Agreements*. Hizi *offsets* hutumika kwenye miradi mikubwa ya kijeshi na miradi ya kiraia. Tusirudie makosa ya Bomba la Gesi la Mtwara ambapo kila kitu kilitoka China. Serikali izungumze na wakandarasi ili vitu ambavyo vinaweza kutengenezwa hapa nchini viwanda vianzishe kutengeneza vitu hivyo, lazima tutumie miradi hii kutekeleza ajenda yetu ya viwanda. Serikali inaweza kutuambia viwanda vingapi vyta ugavi kwenye bidhaa za ujenzi wa reli vitajengwa? Nashauri hili lifanyike kama halijafanyika. Haya ndio mambo ya *local content* na Serikali lazima kila mwaka ituambie ni makampuni mangapi ya Watanzania yamefaidika na ujenzi wa reli na kwa kufanya kazi gani. Wajerumani walibebesha babu zetu mataruma ya reli, Waturuki walibebesha watu wetu ujuzi na fedha tunayolipa sehemu ibakie humu nchini kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni hili la ndege. Leo nimetua uwanja wa ndege wa Dodoma nikitokea Jimboni Kigoma kwa kutumia ndege za *ATCL*. Hii ni hatua ya maendeleo kwa sababu sikuweza kufanya hivi mwaka jana tu. Ningeendesha zaidi kilomita 800 na kufika nimechoka. Hatua hii siyo ya kubeza bali ya kuungwa mkono. Hata hivyo, suala la manunuzi ya ndege za *ATCL* linahitaji uwazi mkubwa kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tumetenga fedha za ndani shilingi bilioni 500 kununua ndege na mwaka huu pia kiasi kama hicho. Tumeambiwa kuwa tayari tumelipa 30% ya dola za Marekani milioni 224 kununua *Boeng 787 -8 Dreamliner*. Jumla ya fedha za ndege kwa miaka miwili ni triliuni moja. Ni maamuzi, hatuna chakula Ghala la Taifa tunanunua ndege. Watoto wanakosa mikopo ya elimu ya juu, tunanunua ndege. Ni maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna habari kuwa ndege tuliyonunua ni sehemu ya ndege za *Boeng* zilizokataliwa na mashirika mengine duniani kwa sababu ya ubora wake. Ndege hizi zinaitwa *Terrible Teens Dreamliner* ambazo zilikuwa 12 na zilikosa soko kwa sababu ni nzito na hazina viwango. Wenzetu Ethiopia wamenunua pia ndege hizi lakini kwa punguzo kubwa la bei kwa sababu ndege hazikuwa na soko. Hata hivyo, katika tovuti ya *Boeng*, Bwana *Van Rex Gallard, Vice President, Latin America, Africa & Caribbean Sales, Boeing Commercial Airplanes*(<http://www.boeing.com/commercial/customers/air-tanzania/air-Tanzania-787-oder. page>) amesema kuwa tumenunua ndege hizi kwa USD milioni 224. Naomba maelezo ya Serikali kuhusu suala hili ili Watanzania wajue kama fedha zao zinatumika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naomba kupata majibu sahihi kuhusu masuala niliyoeleza.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ni kigezo kimojawapo cha kuongeza uchumi au kudhoofisha uchumi kwa ujumla katika Tanzania yetu. Mko wa Katavi ni mionganoni mwa mikoa ambayo imeendelea kudumaa kiuchumi na moja ya sababu ni kukosa barabara zenye uhakika na kususua kwa kuchelewa kujenga barabara na kutengewa fedha ndogo zinazochelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mpanda - Koga yenye urefu wa kilomita 1.0 na Mpanda - Uvinza zimesubiriwa na wananchi kwa muda mrefu waondokane na kero hii ya kulala barabarani kunakosababishwa na barabara mbovu na madaraja kukatika. Nini hatua ya dharura inachukuliwa

kuwakomboa wananchi ili waondoke katika kero hii? Kuchelewa kwa bidhaa katika maeneo ya biashara, mazao kuoza yakiwa njiani, je, Serikali haioni kwamba kupitia barabara hizi mbovu zinaendelea kuwafanya wananchi hawa wa Katavi kuendelea kuwa maskini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii iliyopangwa kwa mikoa hii inayoungana mitatu Tabora-Kigoma na Katavi, tulitegemea itengwe bajeti ya kueleweka ili imalize hizi barabara. Mfano barabara ya Kibaoni - Mpanda ikamilike kwa wakati lakini mpaka sasa haijulikani nini kinasababisha barabara hizi zisikamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zilizotengwa kufanyiwa marekebisho ya changarawe na udongo, Wizara ingeangalia maeneo ambayo hayapitiki kabisa yarekebishwe yote. Kwa jiografia ya Mkoa wa Katavi hakuna barabara za kuchepuka hivyo daraja linapovunjika/bomoka basi watu hawasafiri wala kuendelea na safari. Serikali hii sasa iwe na vipaumbele kutokana na mahitaji ya wananchi wake na wasifanye wanachotaka wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba changamoto hizi zifanyiwe kazi mapema:-

(i) Barabara zinazojengwa katika Manispaa ya Mpanda hazina viwango na hazina mitaro. Ni barabara mpya lakini zina viraka, je, ni kigezo gani kinatumika kila wakati kuendelea kuwapa kandarasi wakandarasi hawa?

(ii) Kucheleweshwa pesa kwa kandarasi hii inaleta shida na miradi kuchukua muda mrefu imekuwa ni kero sasa.

(iii) Usafiri wa reli Mpanda - Tabora – Dodoma, Serikali ihakikishe ujenzi wa reli ya kisasa sio siasa tu bali iingie katika utekelezaji.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa

uwezo wake mkubwa na upendo alionao juu yetu sisi sote kwa kutuwezesha kuwa mahali hapa katika kutimiza majukumu yetu ya kila siku, pia kuniwezesha nami kuchangia hotuba hii ya bajeti iliyo mbele yetu ya mwaka wa fedha 2017/2018. Vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara kwa ujumla wake kwa kuandaa bajeti nzuri yenye mlengo chanya, bajeti hii inaenda kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi, mahsus kuleta maendeleo kwa wananchi wake na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio changu cha muda mrefu ni miundombinu ya barabara na mambo mengine mengi, ila kuna hii barabara ya Makofia - Mlandizi - Mzenga, ni miaka sita (6) sasa tunazungumzia ujenzi wa barabara hii, wananchi wamekuwa wakipata shida sana katika shughuli zao za kila siku. Kutokana na hii barabara kuwa mbovu shughuli zao za kiuchumi zimekuwa zikizorota. Naiomba Serikali hii siku katika bajeti hii wakamilishe ujenzi wa barabara hii ili wananchi wale na wao waone faraja na kuanza kutumia barabara nzuri. Katika bajeti hii tunaomba fedha zitengwe na barabara hiyo iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, niipongeze Serikali kwa jitihada kubwa inazoendelea kuzifanya kwa kuleta miradi mikubwa ya barabara za juu makutano ya TAZARA, daraja jipya la Selander, ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam - Chalinze kwa kiwango cha expressway na bila kusahau ujenzi wa barabara za juu (*interchange*) kwenye makutano ya barabara ya Ubungo. Hizi ni hatua muhimu za kimaendeleo katika kukabiliana na changamoto ya msongamano wa magari. Vilevile Mji wa Mlandizi kutokana na kukua kwa kasi, kuna uhitaji wa makutano ya barabara ili kurahisisha watumiaji na kuufanya uwe wa kisasa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda mrefu sasa umepita tangu kuomba kuwekewa kivuko cha kuvukia watu pamoja na vyombo vy'a moto, *Ruvu Station*, Soga, Mpiji, Kwala na Magindu. Kukosekana kwa vivuko hivyo kunapelekea wananchi kuwa katika hali ya hatari sana kwani maeneo hayo hayana alama yoyote na kuwa kikwazo kwa wananchi

kufanya shughuli zao za kila siku pindi wanapotaka kuvuka ama kuvusha vitu mbalimbali. Naomba katika bajeti hii sasa tupewe kipaumbele kwa maeneo hayo kuwekewa vivuko. Vilevile kuna uhitaji mkubwa sana kwa maeneo tajwa hapo juu kuwa na vituo vya treni ili kuwarahisishia wananchi hawa, pindi kukiwa na vituo kutakuwepo na fursa mbalimbali katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya mawasiliano bado imekuwa kubwa hapa nchini kwetu. Jimboni kwangu Kibaha Vijijini ni wahanga wa changamoto hii kwani kuna maeneo mengi hakuna kabisa mawasiliano ya simu. Kwa kuwa hakuna hata kampuni moja ya simu inayopatikana maeneo hayo ya Dutumi, Mpelamumbi, Miyombo, Gwata na Msua. Tunaomba minara ya *Tigo*, *Vodacom* na *Airtel* maana hakuna mawasiliano kabisa. Hakika kwa wananchi wangu hii imekuwa ni kero ya muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, naipongeza Serikali kwa hatua yake nzuri ya kukamilisha Kituo Kimoja cha Kuhifadhi Taarifa na Mifumo ya Serikali (*Government Data Centre*) na Serikali haina budi kuzihamasisha Ofisi zote za Serikali kutumia mfumo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijatenda haki kama nisipoipongeza Serikali kwa hatua yake ilioichukua siku si nyingi ya kuanza mradi mkubwa kabisa wa treni ya umeme ama treni iendayo kasi kama wengi walivyozoea. Huu ni mradi mkubwa na wa kihistoria katika nchi yetu. Mradi huu utarahisisha sana usafirishaji kwenye sekta ya reli, utapunguza muda wa kusafirisha mizigo na abiria kwani treni hii itakuwa inatumia muda mfupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu na maombi kwa Wizara, naomba mradi huu usiache kuwajali vijana wetu katika kutoa ajira kwa hatua hii ya awali ya ujenzi wa reli kwa (*standard gauge*), kwa maeneo yote reli itakapopita basi watu wa maeneo yale wasiachwe nyuma, wachukuliwe na kupewa ajira kwa mujibu wa taratibu na sheria kama

zinavyosema. Haitapendeza kuona vijana wanatoka maeneo tofauti kuja kufanya kazi katika eneo ambalo nalo lina vijana wasiokuwa na ajira. Mradi huu uwe chachu na mfano kwa miradi mingine hata na nchi jirani ziweze kuiga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari yetu hasa ya Dar es Salaam imekuwa lango kuu na tegemeo kwa nchi mbalimbali zilizotuzunguka. Naipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa mageuzi makubwa ya kimkakati katika kuiboresha bandari yetu hii pia na bandari nyingine zilizopo ndani ya nchi yetu. Bandari ni chanzo kizuri cha mapato kama tu kikitumiwa vizuri na kwa uadilifu mkubwa. Hivyo basi hatua hizi zilizochukuliwa ziwe endelevu ili ziendelee kuleta tija kwa Taifa letu

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto ya kuamini na kuzikubali bandari kavu ila bandari kavu kama tukizipa kipaumbele zitakuwa na msaada mkubwa sana. Hapa nazungumzia bandari kavu za pembezoni mwa miji kama Jimboni kwangu Kibaha Vijiijini tumetenga maeneo maalum kwa ajili ya bandari kavu na kama mpango huu ukifanikiwa ina maana utapunguza msongamano ambao uko mjini. Mfano niliwahi kuishauri Serikali humu humu Bungeni kuhusu suala la bandari kavu iliyopo Kwala, bandari hii iwe maalum kwa kuegesha magari yote (*used*), kwa maana kuziondoa *yard* za kuuzia magari (*used*) ambazo zimezagaa kila kona Jijini Dar es Salaam na hivyo kuwepo sehemu maalum ya mtu akitaka magari (*used*) anajua wapi pa kwenda. Hili limefanyika katika nchi nyngi sana zilizoendelea kama Dubai na kadhalika huwezi kukuta kila kona ya mji kuna *yard* ya kuuzia magari. Hizi *yard* zimekuwa zikiharibu mandhari ya miji yetu na uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hilo pia la bandari kavu kuwepo na upatikanaji wa spea tofauti tofauti za magari pamoja na mashine mbalimbali. Hiyo itapelekea kuondokana na maeneo ya mijini kutapakaa hovyo maduka ya spea kama ilivyo hivi sasa katika Mtaa wa Shauri Moyo. Hatua hii ikikamilika watu watajua wakitaka magari yaliyotumika yote ama spea zote basi wanakwenda Kwala

Kibaha Vijijini na kufanya manunuzi. Itasaidia kuwa na sehemu moja tu ambayo utapata hitaji lako ama gari au spea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili Serikali tayari imeshaonesha nia kwa kutenga maeneo kama ilivyo jimboni kwangu, kilichobaki ni utolewaji wa elimu na uhamasishaji kwa sekta binafsi kuziona fursa hizi na kuzifanyia kazi. Hatua hii ikishakamilika, Serikali itapata fursa ya kuanzisha njia ya treni kutoka Dar es Salaam mpaka Kibaha ili kuwarahisishia wananchi watakaokuwa wakienda katika bandari kavu hiyo na Serikali kupata fedha za uendeshaji. Vilevile Mkoa wa Pwani hivi sasa umekuwa na watu wengi sana, kupatikana kwa usafiri wa treni hiyo kutawasaidia watu wengi sana na kutatua changamoto ya usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya teknolojia yamekuwa yakikua siku hadi siku na Taifa hatuwezi kukwepa ukuaji huo. Ndio maana takwimu za watumiaji wa mawasiliano zimezidi kukua siku hadi siku. Serikali imejaribu sana na inaendelea kujitahidi kuimarisha miundombinu yake na kuwasisitiza wadau wa mawasiliano pia kuzidi kuongeza jitihada mahsus kwa ajili ya kuleta tija. Leo tunaona Serikali imezitaka kampuni zote za simu za mikono kutoa hisa kwa wananchi na wao kuwa ni wamojawapo wa wamiliki wa haya makampuni lakini bado kuna changamoto katika hili kwani uhamasishaji wa kununua hisa hizo umebakil kwa makampuni yenyewe na si Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali nayo kutilia mkazo juu ya kuhamasisha wananchi ili kuleta nguvu na imani kubwa kwa wananchi wetu. Vilevile naishauri Serikali kuzidi kuchukua hatua stahiki kwa wale wote wanaokiuka sheria na taratibu zilizowekwa kisheria ili kuzifanya sekta hizi kufanya kazi zake kwa kufuata taratibu, sheria na misingi iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, naipongeza Serikali kwa juhudini ilizozifanya na inazoendelea kuzifanya kwa shirika letu la ndege. Shirika hili lina historia yake kubwa sana lakini hapa miaka ya karibuni historia hii ilitaka kufutika lakini sasa tuna ndege zetu na

nyingine zimeagizwa zinakuja muda wowote. Hatua hii ni ya kujivunia sana na ya kihistoria. Ushirikiano na makubaliano wallyokubaliana kati ya nchi mbili za Ethiopia na Tanzania katika nyaja mbalimbali hususani ya ushirikiano wa mashirika yetu haya ya ndege ni hatua nzuri ukizingatia wenzetu shirika lao ni kubwa na lina historia ndefu. Hatua hizi zote si za kubezwa kwani zitasaidia kuliimarisha shirika letu la ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ZUBEDA H. SAKURU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mchango wangu katika Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia za ujenzi wa barabara; ili kupitisha ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami hasa barabara ya Tunduru - Mangaka - Matemanga, wananchi na wakazi wa vijiji vilivyopo kwenye Tarafa ya Nakapanya, baadhi ya wakazi hawajalipwa fidia mpaka sasa licha ya kukidhi vigezo vya kulipwa fidia zao. Vilevile wahanga wa Vijiji vya Songambele, Namakambale, Nakapanya, Pacha ya Mindu, Mtanya, Misufini, Namiungo, Mnazi mmoja na Majimaji nao wanadai fidia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na malalamiko mengi juu ya utoaji wa fidia kwa wahanga, bado wakazi wa Vijiji vya Muhuwesi, Chingulungulu, Msagula, Sevuyanke, Temeke, Sisi kwa Sisi, Mkapunda, Ngalinje, Mchangani, Kalonga, Lambai na Tunduru Mjini nao wanadai fidia kutokana na ujenzi wa barabara. Je Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wakazi wa maeneo hayo wanalipwa fidia kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, upanuzi wa uwanja wa ndege Dodoma; pamoja na mahitaji makubwa ya upanuzi wa uwanja wa ndege Dodoma, bado haitoleta tija katika mipango miji na usalama wa wakazi wa maeneo ya karibu kutokana na uwanja huu kuwa karibu sana na makazi ya watu. Mpaka sasa, bado wananchi wanaendelea kubomolewa nyumba na wengine bado kulipwa fidia wakati

uwanja wa ndege wa Msalato ndiyo uliostahili kupewa kipaumbele na kuleta tija kwa matumizi sahihi ya viwanja vyta ndege. Je, Serikali imetumia vigezo gani na kuzingatia nini katika ujenzi wa kiwanja hiki karibu na makazi ya watu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano; kuna changamoto kubwa ya mawasiliano hasa ya redio na simu katika Kata ya Nalasi Wilayani Tunduru. Upatikanaji wa taarifa umekuwa ni changamoto kubwa na kusababisha wananchi kukosa mawasiliano na taarifa. Je, ni lini Serikali itaboresha huduma ya mawasiliano hasa masafa ya redio?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubovu wa barabara; akiwa Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya Serikali kujenga barabara kwa kiwango cha lami kuunganisha Wilaya ya Mbanga hadi Mbamba Bay Mkoani Ruvuma, Wilaya ya Nyasa yenye kilometra 67, wakati Rais wa Awamu ya Nne akizindua madaraja pacha ya Ruhetei A, B na C. Hali halisi ya barabara ya Mbanga hadi Mbamba Bay sasa ni mbaya, hasa ukizingatia ni kipindi cha masika. Barabara hii haipitiki na wananchi wanakwama sana. Pamoja na Serikali kila mara kueleza kuwa Serikali ipo katika hatua za mwisho za kupata Mkandarasi, ahadi hii ya barabara inaendelea kuchukua muda kutekelezwa na kusababisha hasara kubwa za kiuchumi na kijamii. Je, Serikali inatoa kauli gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. RISALA S. KABONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia. Binafsi nitoe pole kwa misiba iliyolipata Bunge letu kwa kipindi cha mwaka huu. Kipekee nikushukuru kwa upendo wako kwa Wabunge hata tunapokuwa na matatizo unakuwa mstari wa mbele kutusaidia. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi. Mheshimiwa Sitta, Mheshimiwa Hafidh na Mheshimiwa Dr. Elly Macha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuungana na Wabunge wenzangu katika kuangalia changamoto mbalimbali za miundombinu ya maeneo

mbalimbali katika nchi yetu ikiwa ni pamoja na Mkoa wangu wa Songwe ambao ni mkoa mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto za barabara katika Mkoa wa Songwe, mfano, barabara inayounganisha Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Momba inayoanzia Chapwa, kupitia Vijiji vya Nanole, Chiwezi, Msambatu, Chindi, Msagao hadi Chitete. Naomba Waziri anapohitimisha aniambie ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya barabara hii ili kusaidia maendeleo ya Mkoa mpya wa Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Taifa ya Mikumi imepitiwa na barabara kuu ya Tanzania kwenda Zambia kwa takribani urefu wa kilometra 50 kati ya eneo la Doma na Mikumi na kwamba barabara hii ilianzishwa kabla ya mwaka 1964 kabla Hifadhi ya Taifa ya Mikumi hajatangazwa. Wakati barabara hii hajawekwa lami, magari yalikuwa machache na yalipita kwa mwendo mdogo. Baada ya barabara kuwekwa lami magari yaliongezekwa sambamba na mwendokasi hivyo kusababisha ajali na vifo vingi vya binadamu na wanyamaporii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hizo, *TANAPA* mwaka 1999 walainishaa na kujenga matuta maeneo yenye mapito ya wanyama. Jumla ya matuta 12 yalijengwa na alama za barabarani kuwekwa katika kilometra 50 zilizo za hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zilizokusanywa na *TANROAD* mwaka 2012 katika kituo cha Doma zilionesha kuwa kulikuwa na magari 1,750 kwa siku yanayopita katika barabara hii ambayo asilimia 60 yalikuwa ni magari ya mizigo na mabasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aina hii ya magari ndiyo inayosababisha ajali za kuwagonga wanyama. Hifadhi kwa kushirikiana na *TAWIRI* mwaka 2014 walihesabu na kubaini idadi ya magari imeongezeka na kuwa 1,991 kwa siku. Matokeo ya utafiti 2014 yanaonesha ifikapo 2025 gari

zinazopita hifadhi zitakuwa 4,699 kwa siku. Idadi hiyo ya magari ni kubwa sana kuweza kuimudu kwa siku hivyo, ni lazima tuchukue hatua madhubuti kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua mikakati ya Serikali kwa bajeti hii ya 2017/2018 kuhusu ujenzi wa barabara mbadala ya Melela – Kilosa – Mikumi yenye urefu wa kilometa 141.78 ili kupunguza idadi ya magari yanayopita katika hifadhi na kuokoa uwepo wa Hifadhi ya Mikumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Ahsante.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na wenzangu kuunga mkono hoja. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na timu nzima ya Uongozi wa Wizara. Napongeza uamuzi wa Serikali wa kuanzisha safari za ndege Songea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya Jimbo la Peramiho:

(i) Kupandisha hadhi barabara ya Tullila-Chipole-Matomonda kuwa ya Mkoa kwa sababu inaunganisha Wilaya mbili lakini ni barabara inayotupeleka katika mradi mkubwa sana wa umeme wa maji unaotumika Songea.

(ii) Barabara ya Mkenda-Likuyufusi. Barabara hii inatajwa katika llani ya Uchaguzi, ni barabara inayotuunganisha na Nchi ya Msumbiji, ni barabara ya Taifa. Upembizi yakinifu umekamilika, usanifu tayari japo ni muda mrefu sana sasa, naomba sana tuanze kuweka lami japo kilomita 15 tu kuanzia ulipo mpaka wa Tanzania na Msumbiji.

(iii) Barabara ya Mpitimbi-Ndongosi ni ya mpakani na inahudumiwa na Mfuko wa Barabara Mkoa. Tunaomba tutengewe fedha.

(iv) Barabara ya Mkoa ya Mletewe-Matimila-Mkongo ya Mkoa hajatengewa fedha muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. HAMAD SALIM MAALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza hoja yangu kwenye suala zima la viwanja vyta ndege. Viwanja vyta ndege si suala la Muungano lakini ndani ya viwanja vyta ndege mna mambo ambayo ni ya Muungano. Suala la anga ni suala la Muungano na kwa maana hiyo utendaji wake wa kazi pia utakuwa uko chini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondosha sintofahamu ya utendaji kwa *section* hii kwa upande wa Zanzibar ningeomba Wizara husika ikaliangalia suala hili kwa kina na baadaye kupeleka mapendekezo yao kwa Serikali ya Muungano ili suala hili kwa upande wa Zanzibar libakie kama suala la Zanzibar na utendaji wake usimamiwe na SMZ.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya suala hilo sasa naomba niende moja kwa moja kwenye suala la bandari. Wafanyabiashara kwa mfano wanaoleta magari kutoka nje ya nchi na kuyateremsha kwenye Bandari ya Zanzibar hulazimika kuyalipia magari hayo kodi zote zinazostahilil. Hata hivyo, mfanyabiashara huyo huyo akiamua sasa kusafirisha gari hilo na kulipeleka Tanzania Bara pia hulazimika kulipia kodi mbalimbali Bandarini Dar es Salaam. Je, hatuoni kwamba kufanya hivyo ni kuwarudisha nyuma wafanyabiashara hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hayo tu bali hata gari iliyonunuliwa Zanzibar na baadaye kusafirishwa kupelekwa Tanzania Bara basi ushuru wake ni mkubwa sana, kwa nini hali iwe hivyo na hii yote ni nchi moja? Nashauri hili liangaliwe ipasavyo ili kuwaondolea wafanyabiashara ugumu wa biashara.

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Viongozi Makatibu Wakuu wa

Wizara na Watendaji wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, ikiwemo TANROADs kwa kazi nzuri mnayoifanya. Kazi inaonekana na jitihada pia zinaonekana. Kwa miaka zaidi ya 20 sasa wananchi wa Kongowe na Bumbuli wamekuwa wanangoja barabara ya kwanza ya lami katika eneo hilo. Wamekuwa wanaipigia kura CCM kwa matumaini hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ahadi ya barabara ya kutoka Soni – Bumbuli – Kwashemshi – Korogwe kujengwa kwa kiwango cha lami bado imebaki ahadi ya kwenye llani na kwenye Kauli za Viongozi. Wananchi hawa sasa wanakata tamaa. Mwaka jana kwenye vitabu vya bajeti barabara hii ilionesha sifuri, yaani haikupangiwa fedha. Jambo hili lilitusikitisha. Mwaka huu tumeona fedha kidogo sana kwa ajili ya kumalizia *design* kwa kipande cha mwisho. Naomba na kupendekeza kwamba, kwa kuwa kipande cha Soni – Bumbuli tayari *design* imefanyika, fedha zipangwe kuanza angalau kilomita 10 za lami mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za kupandishwa madaraja kuwa za TANROADs; vilevile tulipendekeza barabara mbili na kuzipitisha katika michakato yote husika kwa ajili ya kupandishwa madaraja. Barabara hizo ni: Kwanza, barabara ya Soni - Baga - Ngwashi - Milingano - Mashawa na pili ni Soni - Mponda - Tawota - Keronge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizi zinaunganisha Wilaya na Majimbo matatu. Tunasubiri majibu ya Wizara kwa maombi haya.

MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QASSMY: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uzima nikaweza kuchangia kwa maandishi hoja hii iliyoko mbele yetu. Vilevile sina budi kukupongeza wewe pamoja na Naibu Spika, na Wenyeviti wote kwa kuliongoza Bunge lako Tukufu kwa busara na uvumilivu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuchangia kuhusu barabara ya Chalinze na barabara sehemu

ya Mtumbatu kuelekeea Gairo kwenye kilima, kama sijasahau ni sehemu ya Ibete. Barabara ya Chalinze ni sugu na inatumia pesa nyingi kwa matengenezo, kwa ushauri wangu nahisi Serikali sehemu hizi zote mbili ambazo ni sugu ni bora Serikali ingezijenga kwa kutumia zege badala ya lami ili kuokoa pesa nyingi kwa matengenezo ya mara kwa mara. Najua zege ni pesa nyingi lakini ikitengenezwa itachukua muda mwinci bila ya kuharibika. Barabara hizi ni hatari hasa ukipita usiku zinaweza kusababisha madhara makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanja vya ndege, Serikali imefanya vizuri kwa kununua ndege, lakini viwanja vingi bado ni vibovu na vinabebwa na viwanja vikubwa vitatu tu. Viwanja vingi vinavyojengwa havifiki mwisho, Serikali inatoa pesa kidogokidogo bila ya kufikia mwisho, bora Serikali ingeshughulikia kiwanja mpaka ikakimaliza ili iweze kuleta *impact*. Kiwanja cha ndege cha Moshi kingeweza kuleta faida kubwa kama kingejengwa kwani kiko karibu sana na Mlima Kilimanjaro, ambapo watalii wengi wanakwenda kupanda, sasa ikitokea ajali inakuwa ni rahisi kuweza kupata usafiri wa haraka kuliko kwenda KIA au Arusha. Kwa kweli, Wilaya ambayo ina biashara kubwa ya utalii ni aibu kuwa haina uwanja wa uhakika na hata kwenye uwanja hapana hata gari moja ya Zimamoto, wanatumia mitungi ya gesi kwa kweli hiyo inatia aibu Serikari yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mawasiliano na miundombinu ya barabara za vijiji, tumeingia na kutangaza Serikali ya Viwanda huku tukiwa kwenye vijiji ambavyo vinalima malighafi ya hivyo viwanda vyenyewe lakini leo havifiki kwa barabara mbovu na mawasiliano hakuna, je, kweli tutafika kwenye hiyo dhamira ambayo tumekusudia? Serikali iwe *serious* kuhakikisha inajenga miundombinu ya uhakika ili tuweze kufikia malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ni muhimu sana hasa ukizingatia wanawake wengi wanaishi vijiji na wanajishughulisha na kilimo, lakini wengi wanavunjika moyo kwa kukosa barabara pamoja na mawasiliano halafu barabara hizo mbovu zinaathiri sana hasa wanawake

wajawazito wanafia njiani kwa ubovu huo. Serikali kwa umuhimu wa sekta hii ni vema ikaongeza pesa na vilevile izitoe bila ya kuchelewa.

Napenda kuwashukuru Waziri na Naibu wake kwa kujitahidi katika kazi zao pamoja na Serikali kuchelewesha fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutoa pongezi kwa Wizara kufanya kazi nzuri hadi sasa, napenda kuzungumzia barabara zifuatazo ambazo zimekuwa zikiombewa fedha kwa Serikali Kuu katika kuongeza nguvu kwenye Halmashauri kuzifanyia kazi pasipo na mafanikio:-

(i) Kitosi – Wampembe – kilometa 68, imepewa shilingi milioni 84 ambazo ni pungufu na fedha za 2016/2017 ni dhahiri kwa barabara hii hazikidhi mahitaji na ndio maana kuna maombi ya kuchukuliwa na *TANROAD*.

(ii) Nkana – Kala – kilomita 67, kijiografia Halmashauri haiwezi kuifanyia huduma katika ukamilifu wake. Serikali Kuu ni vema kuiangilia vinginevyo kwa maslahi ya wananchi wetu.

(iii) Namanyere – Ninde – kilomita 40, imekuwa ni barabara yenye maombi maalum kila mara, hii ya milioni 350 haijakamilishwa na barabara haijakamilika, hivyo Kata ya Kala haijafunguka. Tunaomba kuongezewa fedha ambazo zitakamilisha barabara hii kwa sasa.

(iv) Kasu – Katani – Miyula – kilomita 24, Mkoa wa Rukwa ni mzalishaji mkubwa wa mazao ya nafaka kwa chakula na biashara na wahuksika zaidi ni akinamama na vijana wao. Barabara hii imekuwa ni mzigo mzito kwa Halmashauri na kuwa kero kwa wananchi wetu kutowawezesha kufika kwenye soko na kusababisha mazao kuharibika. Tunaomba Serikali Kuu kuwawezesha kiwango

fulani Halmashauri ya Nkasi kuweza kuimarisha barabara hiyo kwa kunusurisha vifo kwa akinamama kufuata huduma ya afya. Kuwainua wananchi kiuchumi, kuwarahisishia kufika kwenye soko kwa uharaka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri; kwa kuwa kila Mbunge anazungumzia kupandishwa kwa barabara zao na kwenda chini ya *TANROAD* na Serikali kuona Bodi ya Wakala ya Barabara Vijijini kuanzishwa kwa tatizo hili. Naomba kutoa ushauri wangu kuwa kutokana na kazi zenye tija kubwa na uimara wake ni vema:-

- *TANROAD* ikaongezewa fedha kutoka bilioni 30 kutokana na kazi kubwa wanayofanya.

- Vema *TANROAD* kuongezewa rasilimali watu na rasilimali fedha, kwa kuzingatia kuwa huduma zao zitalazimika kufika hadi barabara za vijijini (barabara zote zilizopo hapa nchini) hakuna sababu ya kuanzisha Bodi ya Wakala wa Barabara Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano; napenda kuzungumzia Kata ya Kala kwa ujumla wake ndani ya Vijiji vya King'ombe, Mlambo, Kapumpuli, Mpasa, Kilambo, Lolesha, Kala na Tundu.

- Hawana mawasiliano ya simu na barabara.
- Eneo hili ni mpakani mwa nchi yetu na DRC – Congo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali kuona umuhimu wa kushauri na kuelekeza kampuni kadhaa maeneo hayo, nao wapate mawasiliano ya simu, ukizingatia usalama kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii, bali bajeti inakuwa finyu na kutokana na umuhimu na uharaka wa maendeleo haya

kwenye Mkoa wa Rukwa ndiyo maana tunaomba Wizara kuongezewa fedha na miradi husika kukamilika ndani ya muda mfupi na kwa kiwango cha kudumu muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kutenga fedha za matengenezo ya barabara kwa kiwango cha changarawe na udongo zipatazo shilingi 1,350,906,000.

- (i) Ntendo – Muze – kilomita 8, shilingi milioni 249,245
- (ii) Muze – Mtowisa – kilomita 7, shilingi milioni 218,089
- (iii) Mtowisa – Illemba – kilomita 20 shilingi milioni 623,111
- (iv) Illemba – Kaoze – kilomita 8.36 shilingi milioni 260,461

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizi ni maeneo ya ndani ya barabara ya Kibaoni – Muze – Mtowisa – Illemba – Kaoze – Kilyamatundu – Kamsamba – Mlowo, ambayo inaunganisha Mikoa ya Katavi – Rukwa – Songwe. Kwa azma ya Serikali ya kuunganisha mikoa hapa nchini. Naomba sasa iijipange kwa kuitoza barabara hii kwenye bajeti ya kuitengeneza kwa kiwango cha changarawe na udongo na kuiweka kwenye fungu la barabara za kiwango cha lami ili mikoa hii iweze kuunganishwa.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kiwanja cha ndege Sumbawanga. Nashukuru kwa kutengewa fedha milioni 18,400. Tunachoomba ni ukamilifu wa malipo ya fidia ya wananchi wanaotoa majengo yao kuachia upanuzi wa kiwanja hicho kwa wakati na thamani ya fedha zao kwa sasa. Tunaomba usimamizi wa ujenzi huo kuwa wa karibu zaidi na kukamilika mapema kwa kiwango takiwa ili wananchi wa Rukwa waondokane na usumbufu na adha kadhaa za kukimbilia Songwe *Airport*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. MEDARD M. KALEMANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miradi ya barabara za Mikoa inayotengenezwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, barabara kwa ajili ya *upgrading to DSDMkuyuni* kutoka Chato Mjini, eneo la Mkuyuni

imewekwa kilometra nne tu. Ukweli ni kwamba barabara hii ina urefu wa kilometra 18 kutoka Chato Mjini kuptitia Mkuyuni, Rubambangwe *JCT*, Kanyama, Illemela hadi Busarara. Barabara hii inaunganisha barabara inayotoka Nyamilembe hadi Katoke inayoungana na barabara ya Biharamulo kuelekea Bukoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa barabara hii ni muhimu katika kuunganisha barabara kuu ya kwenda Biharamulo na Bukoba na kwa kuwa, ilikuwa katika sehemu ya ahadi za Serikali tangu Bunge la Kumi katika miaka ya 2013/2014, naomba sasa ijengwe kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa 285 katika jedwali la barabara zilizotengewa fedha kwa kiwango cha lami barabara hii inaonekana kuwa kilometra nne tu ndizo zitakazojengwa kwa gharama ya millioni 300 pamoja na kwamba barabara hii haiishii hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa barabara hii ni mwendelezo wa kilometra nne zilizotajwa katika bajeti ya Wizara zinaishia njiani katika *JCT* ya Rubambungwe na kuiacha sehemu kubwa bila kujengwa kwa kiwango cha lami. Naiomba sasa Wizara ya Uchukuzi, Ujenzi na Mawasiliano waingize sehemu nzima ya barabara hii yenye jumla ya kilometra 18 ili ijengwe kwa kiwango cha lami katika mwaka huu wa bajeti 2017/2018, badala ya kujenga kilometra nne tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha hoja asisitize kuwa barabara hii itatekelezwa ili wananchi wa maeneo haya na maeneo jirani wapate unafuu wa kufanya shughuli zao za kiuchumi kwa kuwa na usafiri rafiki na rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza utendaji kazi mzuri kwa Viongozi na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TTCL*, iimarishwe zaidi kwa vitendea kazi vya kisasa ili iweze kufanikisha malengo yake kwa kufikia kutoa huduma za mawasiliano katika maeneo na vijiji vyote ndani ya Tanzania kwa ufanisi mkubwa. Mitandao ya simu ya *Tigo*, *Airtel*, *Vodacom* haina nguvu katika baadhi ya maeneo na maeneo mengine mawasiliano hakuna kabisa huko Zanzibar, hivyo waongeze nguvu ili wateja wapate huduma katika sehemu zote huko Zanzibar mfano, Chukwani, Mji Mkongwe na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi za Serikali na Taasisi zake watumie huduma za simu za *TTCL* pia wahimizwe kulipa madeni kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Posta, llongeze nguvu na kujipanga zaidi katika huduma ya kusafirisha pesa na kupokea fedha kwa njia ya haraka ili watu wavutike kutumia huduma yao badala ya kutumia mawakala wengine wa kupokea na kupeleka fedha nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nawatakieni kazi njema na nguvu katika kutekeleza majukumu ya kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana kwa kazi nzuri za kuwashudumia wananchi na kwa ushirikiano mnaonipa kuwashudumia wananchi wa Karagwe. Naomba nichangie yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru barabara ya Nyakahanga-Nyabiienza-Nyakakika imekasimishwa *TANROADS* na kutengewa shilingi milioni 150 kwa mwaka wa fedha 2017/2018, pamoja na shukrani nawaomba tena nipo chini ya miguu yenu barabara hii mniwekee nguvu

ipande officially kwenda TANROADS. Bahati nzuri wote wawili mmeshatembelea Karagwe na nimewalilia sana kwa kuonesha umuhimu wa hii barabara kwenye kukuza uchumi wa Wilaya na nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii inahudumia kambi za JWTZ, barabara hii inatuunganisha na nchi ya Rwanda. Mheshimiwa Rais aliahidi kilometra tano za lami, nimeshakaa na Madiwani na kupitia Baraza la Madiwani tumeridhia kwamba kilometra hizi za lami ziende kwenye barabara tajwa Nyakahanga-Nyabiienza-Nyakakika eneo korofi sana la Kajura Nkeito. Nawaomba sana fedha hizi zitengwe na kuletwa ili tuweze kudhibiti eneo hili korofi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kivuko *Single Custom* ili kuimarisha biashara kati ya Wilaya ya Karagwe na nchi ya Rwanda kwenye eneo la Chamhuzi Kata ya Bweranyange ambalo lipo kwenye barabara tajwa kwenye aya ya kwanza na ya pili hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine nawapongeza na kuwashukuru kwa ushirikiano mnaonipa kuwashudumia wananchi wa Wilaya ya Karagwe. Nitashukuru iwapo nitapata *reaction* yenu wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, *thanks and God bless.*

MHE. SALMA M. MWASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa Wizara imefanya mengi mazuri, kuna mambo machache ningependa kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara kuwa chini ya kiwango. Kuna barabara ambazo zimetumia hela nyingi lakini zimejengwa chini ya kiwango, hivyo basi zimepelekea upotevu wa fedha za Serikali. Sasa basi nashauri Serikali kusimamia Mainjinia na *Contractors* kwa umakini ili matatizo kama haya yasitokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchakavu wa majengo ya Serikali. Majengo mengi ya Serikali yamechakaa, kutokana na kutokarabatiwa muda mrefu. Hivyo basi, nashauri Serikali itenye fedha kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Serikali kupitia wakala wa majengo *TBA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchache wa majengo ya Serikali, majengo ya Serikali ni machache hivyo basi inasababisha watumishi wengi wa Serikali hata Mawaziri kukosa nyumba za kuishi. Hii inatokana na uuzwaji wa nyumba za Serikali kwa viongozi ambaao sasa wengi wao wamestaafu, hivyo basi napenda kuishauri Serikali itenye fedha ili kujenga nyumba nyingi ili kuziba pengo la nyumba zillizouzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati hafifu wa barabara, ukarabati wa barabara haufanyiki mara kwa mara, hivyo basi inapelekea barabara nyingi kubomoka na kupelekea kupitika kwa shida au kutopitika kabisa, hivyo basi napendekeza hela kwa ajili ya ukarabati wa barabara zitengwe za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya manunuzi kuathiri ujenzi wa barabara kwa wakati, hivyo kupelekea ongezeko la gharama za miradi ya barabara, kama vile upembuzi yakinifu kuchukua muda mrefu kupelekea ongezeko la gharama za miradi ya ujenzi wa barabara. Nashauri Wizara isimamie upembuzi yakinifu ufanyike kwa wakati na bila kuathiri miradi ya ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara Kifuru mpaka Mbezi mwisho, Wilaya ya Ubungo Mkoa wa Dar es Salaam ni kilometra sita, lakini Mkandarasi amepewa fedha za kutengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami kilometra nne tu. Sasa basi kilometra mbili zitabaki kabla ya kufika Mbezi mwisho. Hivyo naishauri Serikali itenye fedha ili kumalizia kipande hicho cha barabara cha kilometra mbili mpaka Mbezi kutoka Kifuru, kuliko ilivyo sasa haileti sura nzuri ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naipongeza Wizara, Waziri na Naibu Waziri wake pamoja na Makatibu Wakuu wa Wizara, pia nampongeza Mkurugenzi Mkuu wa Bandari kwa jitihada yake binafsi kwa kutangaza tenda ya kujenga Bandari ya Kabwe mwaka huu, pia kwa kujenga barabara ya kwenda kwenye Bandari ya Kipili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu maalum ni kuhusu mtandao wa simu katika Kata nzima ya Korongwe. Kata hii ya Korongwe haina kabisa mtandao wa simu wa aina yoyote ile, imekuwa ombi langu kubwa sana na mara kwa mara ombi hilo nazungumza moja kwa moja na Mheshimiwa Waziri Mbarawa na kweli anafanya jitihada kubwa sana kuzungumza na jamaa wa *Halotel*/lakini mpaka leo hawajatekeleza na hata dalili hakuna kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna ombi la Mkoa wa Rukwa kuhusu barabara ya Namanyere-Kirando kuweka kwa kiwango cha lami kwa kuwa *RCC* Rukwa walikwisha pendekeza na kutuma maombi barabara hiyo ya kilometa 64 ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Marine Service (MSCL)* wafanyakazi wake karibu wote hawajapata mishahara yao, Wizara ifikirie sana kuhusu *MSCL* hailipi kabisa, mishahara ya wafanyakazi mfano, wafanyakazi wa *MV Liemba* muda wa miezi 13 hawajalipwa chochote, je wataishi vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bandari ya Kirando iliyopo Wilaya ya Nkasi Mkoa wa Rukwa, kuna mtumishi wa *TPA* hapo wa kuchukua ushuru wa mizigo inayopitia hapo katika kijiji hicho. *TPA* hawajaweka huduma yoyote ile katika kijiji hicho kilichopo kando ya Ziwa Tanganyika. Kwa kuwa, wafanyakazi wengi wanapitia hapo nashauri sana *TPA* kujenga bandari ndogo ya maboti katika Kijiji hicho cha Kirando.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nategemea Mkurugenzi wa bandari atalifanya kazi suala hilo ili kutoa malalamiko ya wafanyabiashara kulipia wakati hakuna huduma kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali na Wizara ituambie ni kwa muda gani wale nyumba zao zilizopigwa (X) zilizopo au zilizokutwa na sheria ya mwaka 2007 zitafidiwa kwa kuwa sasa hawaruhusiwi kabisa kufanya maendeleo yoyote. Ni vyema wakaruhusiwa kufanya ukarabati *not* ujenzi wa nyumba hizo kwa kuwa hata zikidondoka kwa sasa hawaruhusiwi kukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ng'ombe, punda wanachungwa pembezoni mwa barabara wanababisha sana ajali, hivyo *TANROADS* kote nchini watakiwe kuweka doria kwa wanaochunga ng'ombe, punda, mbuzi, kondoo pembezoni ya barabara wachukuliwe hatua kali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, minara ya simu kwenye vijiji vyenye kuwa na tatizo la mawasiliano wasaidiwe upesi kama vile vilivyopo Babati. Mfano, Himiti, Chemchem, Imbilili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgao wa fedha za Mfuko wa Barabara *TANROAD*; asilimia 70 za fedha za Mfuko wa Barabara upunguzwe hadi asilimia 50 ili wananchi wa Tasime wenye barabara nyingi wasaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *all the best brothers.*

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano, Naibu Waziri na Timu nzima ya Wizara kwa ripoti nzuri na pia bajeti nzuri ya mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu Makamu wa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiongoza vema nchi yetu katika utekelezaji wa llani ya CCM 2015/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano ni muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu na katika kipindi cha bajeti ya 2016/2017. Serikali imefanya vizuri sana kama ifuatavyo:-

- (1) Ujenzi wa reli ya *standard gauge* umeanza;
- (2) Serikali imeendelea kulipa madeni ya wafanyakazi wa *TAZARA* ambapo shilingi billioni 16.8 zimelipwa kati ya shilingi billioni 22.9 zilizokuwa zinadaiwa;
- (3) Serikali iliingia mkataba wa ununuzi wa ndege sita, ndege mbili aina ya *Bombardier dash 8-Q400* ziliwasili nchini Septemba, 2016;
- (4) Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano;
- (5) Ujenzi wa barabara za juu kwenye makutano ya *TAZARA* unaendelea vizuri; na
- (6) Ujenzi wa barabara na madaraja mbalimbali unaoendelea nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia ya leo ya ushindani mkubwa wa kibashara umepelekea biashara ya Kimataifa kuwa ya masaa 24 na siku saba za wiki na ili kuwe na tija na ufanisi katika uchumi wetu tunahitaji uboreshaji wa miundombinu ya barabara, reli, bandari pia mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za usafirishaji na miundombinu ya bandari yamepelekea kwa kiasi kikubwa gharama kubwa za ndani (*domestic supply chain costs*) kwa bidhaa zetu na hata pembejeo za kilimo ukilinganisha na nchi zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama kubwa ya mbolea kwa mkulima wa Tanzania imebebwa na gharama za bandari, usafiri wa barabara na hata ucheleweshwaji wa kutoa mzigo bandarini. Mnyororo wa gharama za mbolea kwa mkulima wa Tanzania, hivi sasa asilimia 47 ni gharama za ndani *port charges, transportation, taxes and mark up*, wakati asilimia 53 ni gharama ya kununulia nje ya nchi *CIF* kwa kulinganisha na nchi ya Ufilipino gharama ya ndani ni asilimia 16 tu na *CIF* ni asilimia 84. Pia nchi ya Myanmar gharama za ndani za mbolea ni 23% tu wakati gharama za kununulia *CIF* ni asilimia 77, hivyo mzigo mkubwa wa bidhaa za Tanzania unatokana na uchukuzi, tozo mbalimbali za bandari na matumizi ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iboresha *TAZARA* pia ili mbolea isafirishwe kwa reli badala ya barabara ambayo ni gharama kubwa sana. Pia napendekeza Serikali iendelee kuboresha bandari ili meli kubwa ziweze kuingia kwa urahisi, vilevile shehena za mizigo ya mbolea zipewe kipaumbele cha kupakuliwa bandarini. Pia kuwepo na kituo kimoja cha huduma kwa wateja *one stop centre*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuboresha bandari ya Dar es Salaam na *TAZARA* napendekeza kujenga bandari kavu katika eneo la kimkakati la Inyala, Mbeya ili wateja wa Zambia, Malawi, DRC Congo na hata wafanyabiashara Watanzania kutoka Nyanda za Juu Kusini wasilazimike kuchukua mizigo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ndiyo chachu na tija bora hasa katika sekta ya kilimo ambayo ndiyo mhimili wa uchumi wetu wa Tanzania. Barabara za vijijini ni muhimu sana kwa kusafirisha mazao ya kilimo na pia kupunguza gharama za usafiri wa pembejeo na urahisi wa kupeleka mazao sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha usafirishaji wa mazao ya kilimo na pia kuunganisha mikoa kwa barabara za lami (*trunk roads*) napendekeza Serikali kuboresha barabara zinazounganisha Mkoa wa Mbeya na mikoa

mingine kama vile babaraba ya Isonje-Kikondo Makete - Njombe, barabara ya Mbalizi-Shigamba-Ileje inaunganisha Mbeya na Ileje - Songwe, barabara ya Mbalizi-Makongorosi inaunganisha Mbeya na Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha usafirishaji wa mazao na pembejeo, napendekeza kupandishwa hadhi barabara za kimkakati zikiwemo Kawetere-Mwabowo-Ikukwa, Mbalizi-Iwindi-Jojo, Inyala-Simambwe na Imezu – Garijimbe (*mchepuo/bypass*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali inajenga barabara ni muhimu pia kuzingatia vigezo vya kiuchumi pamoja na ahadi za Marais waliostaifu na Rais aliye madarakani, pamoja na barabara zilizotajwa hapo juu. Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne na Rais wa sasa waliahidi ujenzi wa barabara ya *mchepuo bypass* ya kilomita 40, kuanzia Mlima Nyoka Inyala-Ijombe-Swaya-Igale-Iwindi-Songwe. Pamoja na kupunguza msongamano pia ni barabara inayounganisha machimbo mapya ya umeme wa jotoardhi na mgodi mpya wa Pandahill.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za kiwanja cha ndege cha Songwe ni pamoja na kukosekana kwa uzio wa uwanja na kutokuwa na *navigational aids*, ikiwemo taa katika njia za kutua na kurukia ndege. Eneo la uwanja wa Songwe lina ukungu hususani wakati wa asubuhi na hivyo kuwa vigumu kwa marubani wa ndege kuona kiwanja vizuri. Kukosekana kwa taa kumepelekea na kusababisha usumbufu mkubwa kwa abiria na hata mashirika ya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukanda wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kuwepo kwa mazao mengi ya kilimo, hasa matunda, mbogamboga na hata maua, kuna fursa za ndege za mizigo kuchukua hayo mazao na kupeleka moja kwa moja soko la nje. Kutokana na ukosefu wa taa *navigation aids* na uzio mashirika ya ndege za mizigo yameshindwa kuanza usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kuhakikisha kabla ya mwaka wa fedha 2016/2017 kwisha, fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya taa, *navigation aids* na uzio wa kiwanja cha Songwe, zinatolewa ili kukamilisha kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyokuwa uchukuzi, na ujenzi, mawasiliano ni muhimu sana kwa wakulima vijiji. Serikali inapoangalia kuanzisha soko la mazao Tanzania, *commodities exchange market* ni muhimu sana kwa sasa kuhakikisha maeneo ya vijiji yanakuwa na minara ya mawasiliano. Napendekeza Serikali iharakishe ujenzi wa minara ya mawasiliano hasa kwa vijiji ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, vikiwemo Vijiji vya Itala, Mkuyuni, Ulenje, Wambishe, Ihango, Mashese, Nyalwela, Mwela, Shango, Ngole, Ikukwa, Ipusizi, Izyira, Shizuvi, Shisyete, Isonso na Igalukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi; Mheshimiwa Waziri kwa masikitiko makubwa sana Mkoa wa Lindi mwaka huu mmeupatia fedha chache kuliko uhalisia wa miundombinu iliyopo. Kwa nini Lindi, mkoa mkubwa kwa eneo tena bado miundombinu yake bado hajaimarika, unatengewa fedha chache kuliko mkoa wenye eneo dogo kama vile Kilimanjaro ambao umetengewa kiasi cha fedha zaidi ya triliioni 2.2 wakati Mkoa wa Lindi mmeutengea fedha chache kiasi cha shilingi bilioni 800 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Jimbo la Mchinga ambalo mimi ni Mbunge wake halijatengewa fedha hata senti moja katika fedha za maendeleo, kwa nini mgao wa rasilimali za nchi hii hauzingatii usawa kwa sehemu yote ya nchi hii? Naomba maelezo ya kina juu ya swali hili.

MHE. ALLY S. UNGANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwa maandishi katika hotuba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakapoongelea maendeleo ya nchi hii huna budi kutilia mkazo masuala ya miundombinu, Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya, hii inaonesha jinsi gani Mheshimiwa Rais wetu alivyo mzalendo katika ufanyaji kazi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, sina budi kuwapongeza Mawaziri wenyewe dhamana, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Mbunge na Naibu wake Mheshimiwa Injinia Edwin Amandus Ngonyani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Kibiti zipo changamoto nyangi hasa barabara ya Bungu – Nyamisati. Barabara hii ina jumla ya kilometra 42. Naomba Serikali yangu siku ya Chama cha Mapinduzi kuiangalia kwa jicho la huruma barabara hii. Tunailomba Serikali yangu barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami kwani kufanya hivyo inaturahisishia kwa wananchi wa maeneo ya Delta kama Nyamisati, Salale, Kiomboni, Mchingga, Mfisini na ndugu zetu majirani zetu wa Wilaya ya Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Gati la Nyamisati; naionba Serikali yangu siku suala hili lipewe kipaumbele kwani gati hili lina umuhimu sana kwa wananchi wa maeneo ya Delta na Mafia kwa ujumla. Katika Jimbo langu la Kibiti lina jumla ya Kata 16, kati ya hizo zipo tano ambazo zipo katika maeneo ya Delta, kati ya hizo ni Maparoni, Mbuchi, Salale, Msala, Kiongoroni. Katika Kata za Maparoni, Mbuchi, Salale, Msala, Kiongoroni katika Kata ya Maparoni, Mbuchi, Kiongoroni kuna barabara ya kutoka Ikwiriri – Kibiti, naomba njia hii ipewe kipaumbele kwani inatuunganisha Wilaya mbili, Kibiti na Rufiji na barabara hii ambayo inapita vijiji vingi sana ambavyo ni Mchukwi, Rungungu, Nyamatanga, Ruaruke, Kikale, Mtunda, Muyuyu, Umwe, ambapo barabara hii ina jumla ya kilometra 48. Ili kurekebisha barabara hii tuna kila wajibu wa kujenga Daraja la Ruhoi kwa *box* karavati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo ya baadhi ya vijiji vyangu hakuna mawasiliano kama Makima, Mchukwi,

Nyambunda, Ngulakula, Mngaru, Nyakinyo na maeneo mengine, tunaomba tupatiwe mawasiliano ili tuboreshe kupeana taarifa kwa njia nyepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usiposhukuru kwa kidogo hata ukipata kikubwa huwezi kushukuru. Tunashukuru Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupatia Wilaya mpya ya Kibiti, lakini tuna ombi la barabara ya lami kutoka barabara kuu hadi tunapojenga Makao Makuu ya Wilaya na kwenda kwenye kituo chetu cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Ruaruke kwenda Nyamisati. Barabara hii ina madaraja mawili ambayo ni Mkelele, Mkumbwa na Mkelele Mdogo ambayo yamesombwa na maji kwa hiyo hadi sasa barabara haipitiki kwenda Nyamisati – Ruaruke ambayo ni muhimu sana inatoka Muhoro hadi Mbwera. Barabara hii ina jumla ya kilometra 41. Awali ya yote sina budi kuishukuru Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi kwa kutupatia wafadhili wa kujenga Daraja la Mto Mbuchi na Daraja dogo la Kipoka lakini yapo maeneo ya Mkelele mchakato wa kupata mzabuni, naomba ufanyike haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishakamilisha madaraja haya mawili tunawaomba tena wafadhili hawa wa *DFIB*, tunaomba barabara yetu ya kutoka Muhoro hadi Mbwera watujengee kwa kiwango cha tuta kubwa ili kulingana na hali halisi ya mazingira ya maeneo hayo, yanahitaji makalavati kila baada ya mita 200 kwani maeneo haya ni ya sehemu ya maji njia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka njia panda ya Kingwera kuja Mchukwi hospitali ambayo ina urefu wa kilometra tano, naiomba Serikali yangu sikivu watuwekee lami kwa barabara hii, ni muhimu sana kwani inapitiwa na wagonjwa wengi amba wanakwenda kupata matibabu katika hospitali hii ya Mchukwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano, maeneo ya Delta; katika Jimbo langu la Kibiti naomba maeneo ya Delta

watuangalie kwa jicho la huruma kwani katika mazingira haya hatuna mawasiliano ya simu. Tunaomba tupatiwe mawasiliano ya simu kwani mtu akipata matatizo hakuna njia mbadala ya kupata msaada mwingine bila ya njia ya mawasiliano. Barabara ya maeneo ya Delta naomba Serikali yangu itujengee magati ya gharama nafuu na kujaza matuta katika barabara zetu za maeneo hayo.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hoja zifuatazo katika Wizara hii kuhusu Jimbo la Sikonge:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande cha barabara kutoka Mibono hadi Kipili kwenye barabara ya Sikonge – Mibono – Kipili hakijatobolewa kwa muda mrefu, wakati inaunganisha Sikonge Makao Makuu ya Wilaya na Kata mbili za Kipili na Kilumbi ambako kuna zaidi ya wakazi 45,000. Kuna uchumi mkubwa sana, maelezo aliyonipa Naibu Waziri kuwa eti kutobolewa kwa barabara hiyo kunahitaji fedha nyingi sana sh. 12,000,000,000, sasa hoja yangu nauliza ni lini Serikalini sh. 12,000,000,000 zikawa nyingi? Au kwa sababu mzigo mzito mpe Mnyamwezi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua ingekuwa maeneo mengine ya nchi ingekuwa imeshatengenezwa japo kwa kiwango cha udongo/changarawe. Naomba Serikali ijipange ili barabara hiyo itobolewe ifike hadi Kipili kama siyo mwaka huu basi mwaka ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande cha barabara kutoka Ipole hadi Lungwa ni cha muhimu sana kama kweli tunataka kuunganisha Mikoa ya Mbeya na Tabora. Lini kipande hicho kitajengwa kwa kiwango cha lami? Ndugu yangu Mheshimiwa Waziri namwambia kuwa Mbunge wa Sikonge ni mzigo mzito sana kulingana na jiografia yake na alijiona mwenyewe, mbona sijaona majibu yake kwenye hotuba yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano; nimeshaongea sana na Dkt. Sasabo ambaye ni Katibu Mkuu – Mawasiliano kuhusu kukosekana kabisa kwa mawasiliano

ya simu katika Kata za Nyahua, Igigwa, Kiloleni na Ngoywa na pia mawasiliano hafifu kabisa kwenye Kata za Kipili, Kilumbi, Kiloli, Kitunda, Mole na Ipole. Fedha za mawasiliano vijijini zinatumika lakini Sikonge tuna njaa sana ya mawasiliano. Naomba sasa kwa maandishi haya Wizara hii itutendee haki na sisi tupate mawasiliano ya uhakika kama ilivyo kwa maeneo mengine ya nchi, watu wanatumia simu lakini hawana mawasiliano ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, lakini kwa masharti ya kusikilizwa kilio cha wananchi wa Sikonge.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi; katika Mkoa wa Dar es Salaam na hasa Jimbo la Ukonga kuna mnada wa Kimataifa wa Pugu. Barabara ya kwenda mnadani ni mbovu na mwaka 2016/2017 ilipangwa kujengwa lakini hadi sasa hakuna kilichofanyika, naomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana azingatie barabara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Ukonga kuna shida ya mawasiliano hasa Kata za Msongola, Zingiriwa, Chanika, Kivule, Mzinga, Buyuni, Pugu, Pugu *Station* na Majohe, je, kwa nini Mheshimiwa Waziri asihimize uwekaji wa mitandao ya simu ili Kata hizo zipate mawasiliano ya uhakika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko mengi ya wananchi waliohamishwa kutoka Kipawa na kupelekwa Buyuni, Zavala na Kipawa Mpya. Naomba kujua mipango ya Serikali kulipa fidia wahanga na kupeleka miundombinu kama walivyokubaliana na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nichangie kidogo kwenye hoja hii iliyo mezani.

Kwanza kabisa ningependa kupata majibu ya Waziri, barabara ya Dumila – Rudewa - Kilosa – Mikumi ya kilomita 142 tu nashukuru imetengewa shilingi bilioni 5.207 ili kumaliza kipande cha Rudewa – Kilosa kilomita 18. Je, ni lini sasa Serikali itatenga pesa za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kutoka Kilosa – Mikumi kilomita 78 ambayo ni barabara ilioahidiwa na Rais aliyepita Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Mheshimiwa Magufuli wakati wa kipindi chao cha Kampeni. Hii ni barabara muhimu sana ili iweze kusaidia Kata zaidi ya 10 na kukuza uchumi wa watu wa Mikumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliomba barabara ya Ruaha Mbuyuni – Mololo Chabi – Ibanda – Uleling’ombe ipandishwe hadhi lakini siiioni katika mpango huu wa bajeti hii ya 2017/2018 na hii ni barabara inayounganisha Mikoa ya Iringa – Morogoro na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia reli ya kutoka Kiwanda cha Sukari Kilombero – Kidatu mpaka Kilosa, ilikuwa inachangia sana kuboresha uchumi wa watu wa Mikumi na kuwaunganisha na reli ya kati. Je, Serikali haionti umuhimu wa kufufua reli hii kama ilivyokuwa zamani ambapo pia kulikuwa na bandari kavu pale Mikumi ambayo ilikuwa inasaidia sana kukuza uchumi wa wananchi wa mikoani na wananchi wa Wilaya ya Kilosa kwa ujumla. Tunaiomba sana Serikali iturudishie bandari kavu ya Mikumi ili iweze kwenda na kasi ya maendeleo ya nchi yetu na kufikia uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa kuhusu mawasiliano, Jimbo la Mikumi limekuwa na matatizo makubwa sana ya mawasiliano, mfano Kata za Vidunda, Uleling’ombe, Chabima, Munisagala, Mhenda, Chonwe, Udungu, Itembe, Tindiga, Malangali, Nyameni na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba sana Serikali ituletee mawasiliano ya simu kwenye vijiji hivi na vingine vingi

vya Jimbo la Mikumi ili wananchi nao wapate fursa ya kupata mawasiliano na kukuza biashara zao na kukuza uchumi wao kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia. Barabara ya Morogoro kuanzia Mlandizi mpaka Chalinze; barabara hii imekuwa ikikarabatiwa mara kwa mara, lakini bado barabara hii haipo katika kiwango chake kwa kisingizio kwamba *water table* ipo juu, ni kwa nini wataalam wasifanye utafiti na kujenga kwa kisasa. Nchi zilizoendelea wanajenga mpaka juu ya bahari hapa Tanzania shida ni nini? Je, Mkandarasi huwa hatoi *guarantee* ni muda gani barabara itadumu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya *Old - Moshi* iliyopo Moshi kuanzia Kiboriloni- Kikarara – Kidia hadi Tsuduni, hii ni kati ya barabara iliyokuwa katika ahadi ya Mheshimiwa Rais Mstaafu Dkt. Jakaya Kikwete katika kampeni za Urais 2010 na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli wakati huo alikuwa Waziri wa Ujenzi na katika Bunge hili Tukufu kwenye hotuba yake ya bajeti 2016, aliahidi kutenga fedha kwa ajili ya barabara teule na si hivyo tu, niliuliza swali mwaka huu na nikajibowi upembuzi yakinifu umekamilika na walikuwa kwenye mchakato wa kumtafuta Mkandarasi. Je, ni muda gani unaotumika kumpata Mkandarasi. Je, barabara hii ni lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami ukizingatia barabara hii ni muhimu sana na maendeleo ya uchumi wa nchi yetu kwenye sekta ya utalii. Sababu ni njia fupi sana ya kufika kilele cha Mlima Kilimanjaro na ina vivutio kama vipepeo na ndege wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja wa Ndege wa Moshi, uwanja huu umesahaulika kwa muda mrefu hata barabara ya kuelekea *airport* imefunikwa na majani, wananchi wanalima mazao katika eneo la *airport*. Uwanja huu ni *very strategic* kwa ajili ya watalii kuja moja kwa moja

kupitia nchi jirani. Serikali imekuwa ikiahidi watakarabati kiwanja kile, je, ni lini wataanza kukikarabati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Moshi maeneo ya Kiboriloni *KDC* kumekuwepo na matatizo ya mawasiliano sasa licha ya kuwa karibu na Mjini na suala hili limeshapelekwa kwa mitandao yote ya simu, lakini hakuna kinachotendeka. Je, ni lini Serikali itatusaidia minara ya simu iwekwe pale *KDC*, Mbokomu ili wananchi wa pale waweze kupata mawasiliano.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa jinsi inavyotekeleza vema llani ya Chama cha Mapinduzi. Nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa utekelezaji wa majukumu yao. Pamoja na hayo nachangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kutenga fedha za ujenzi wa gati mita 300 shilingi bilioni 87, pia ujenzi wa gati la mafuta Shangani. Aidha, ukarabati wa gati Na. 3 tunaomba fedha hizo zitolewe kwa wakati ili miradi hiyo itekelezwe kwa muda uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami Mtwara- Newala- Masasi kipande cha kilomita 50, Mtwara- Mnivate, Mkataba wa kazi hii ni miaka miwili na thamani yake ni zaidi ya bilioni 90. Kwa fedha zilizotengwa bajeti ya mwaka jana na mwaka huu fedha zilizotengwa ni takribani shilingi bilioni 29, hivyo kama Mkandarasi atafanya kazi kwa nguvu zote na kasi kubwa hakutakuwa na fedha za kumwezesha. Naomba angalizo hili lifanyiwe kazi ili barabara hiyo ijengwe kwa muda uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ya simu. Katika Jimbo la Nanyamba kuna Kata nydingi ambazo hakuna mawasiliano ya simu. Baadhi ya Kata hizo ni Njengwa, Nitekela, Nyundo, Hinju, Mnima, Kiromba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza swali Bungeni kuhusu lini Kata hizo zitapewa mawasiliano ya simu, nikajibiwa kuwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) utagharamia ujenzi wa minara katika maeneo hayo. Naomba tena kupitia Mfuko huu kuharakisha ujenzi wa minara katika maeneo hayo ili kuwe na mawasiliano ya simu za mkononi.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na wataalam wao kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutekeleza majukumu yao. Nipongeze Serikali kwa kuanza kujenga reli kwa kiwango cha *SGR*, pia nimpongeze Waziri kwa kazi ya ujenzi na upanuzi wa barabara ya Mtwara. Naomba Serikali kuona umuhimu wa kukarabati uwanja wa ndege wa Mtwara kwani umechakaa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuiomba Serikali kuhusu kuharakisha na kuongeza kiwango cha pesa kwa barabara ya Mtwara, Newala, Masasi kwa mujibu wa mkatuba. Serikali pia ianze ujenzi wa reli ya Mtwara - Mchuchuma na Liganga Mbamba bay. Reli hii ni muhimu sana kwa uendeshaji wa bandari ya Mtwara.

MHE. DR. ANGELINA S. L. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja. Ombi langu wananchi wa Kata ya Kanyerere na Kata jirani katika Wilaya ya Magu wana tatizo kubwa la usafiri kuweza kufikia visiwa vya *base* (llemela) na kisiwa cha Mashoka – Magu. Katika Kikao cha RCCkilichofanyika Mkoa wa Mwanza Januari, 2017, waliahidi kupeleka kivuko baada ya kufanya tathmini ya abiria, mizigo na shughuli za kiuchumi zinazofanyika katika visiwa hivyo na kuona vinastahili kuwa na kivuko. Ombi langu ni utekelezaji wa ahadi hiyo.

(1) Barabara ya Sabasaba - Kiseke hadi Buswelu ilikuwa ahadi ya Waziri alipotembelea Jimbo langu, naomba barabara hiyo kuwa ni kiungo cha Makao Makuu ya Wilaya na Kata zaidi ya saba ijengwe. Aidha, barabara hiyo

itarahisisha pia kuwa kama mchepuko wa wasafiri waendao Mara na Shinyanga.

(2) Barabara ya *Airport*, Kayenze hadi Nyanguge nayo pia itasaidia mchepuo kuelekea Mara na Serengeti katika Mbuga za Wanyama na kuchochaea utalii katika maeneo hayo.

(3) Tunahitaji minara ya simu katika Kata ya Kayenze na Sangabuye hawana mawasiliano ya uhakika katika baadhi ya mitaa ya Kata hizo za Kabusungu, Igumamoyo, Imalang'ombe na kadhalika.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa utendaji wake wa kazi. Mwenyezi Mungu aendelee, kumpatia afya njema, aendelea kuimarisha Tanzania yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu Ndugu Nyamhanga na Watendaji wote wanaofanya kazi katika Wizara hii, hongereni sana na endeleeni kuchapa kazi tupo pamoja nanyi na kazi yenu Watanzania wanatambua uwezo wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri na Katibu wa Wizara hii Ndugu, Nyamhanga, kwa kusikiliza kilio cha wananchi wa Jimbo langu la Kwela, kilio cha muda mrefu, juu ya barabara sugu na yenye gharama kubwa ambayo Halmashauri haina uwezo nayo kwa maombi yangu. Kwanza ultipatia milioni 431 na bado barabara hiyo ichukuliwe na *TANROAD*. Nashukuru barabara hiyo leo imekwishachukuliwa na *TANROAD*. Ahsante sana na Mwenyezi Mungu awabariki katika kazi zenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru vilevile kwa kuanza utaratibu wa ujenzi wa daraja la Mto Momba. Daraja ambalo ni kiungo kikubwa kwa barabara ya Kibaoni - Kulyamatundu, Kamsamba, Mlowo, tunaomba kasi iendelee katika kuanza kulijenga Daraja hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali iharakishe kufanya usanifu katika barabara ya Kibaoni, Kilyamatundu, Kamsamba, Mlowo. Barabara hii ni muhimu sana kiuchumi kutokana uzalishaji wa mazao ya mpunga, mbaazi, matunda mbalimbali, samaki na mifugo. Tunaomba barabara hii itengenezwe haraka kwa kiwango cha lami ili kusaidia wananchi katika ukanda huo wa bonde la Ziwa Rukwa.

Maombi ya fedha kwa barabara ambazo Halmashauri haina uwezo nazo ambazo ni barabara ya Miangalua - Chombe - Kipeta, barabara ya Mawenzusi - Msia, barabara ya Mlimani inayounganisha Bonde la Rukwa na Sumbawanga kilomita 47. Pia maombi ya fedha ili kutengeneza daraja la Kaengesa, daraja la Laela kwenda Kituo cha Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera Waziri na timu yako yote ya Wizara kwa kuandaa hotuba hii na kuiwasilisha hapa Bungeni. Tunaipongeza Serikali kwa hatua za kuanza kuimarisha reli yetu hapa nchini pamoja na ile ya kati kwa kujengwa kwa viwango vya *standard gauge* ili kuhakikisha mizigo mizito inasafirishwa kwenye reli na kuokoa barabara zetu zinazoharibika sana. Tunashukuru Serikali kwa kutenga fedha za kumalizia kipande cha barabara ya Nyahua - Chaya kilomita 85.4 kwa mwaka huu ili kuunganisha Mkoa wa Dodoma na Tabora kwa maendeleo ya wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Urambo - Kaliua pamoja na fedha kupatikana tangu mwaka jana 2016 na Bodi ya Zabuni kukaa na kutangaza na Wakandarasi kuomba, mpaka leo hajaanza. Serikali iezeze ni kwa nini kipande hiki cha kilomita 32 ujenzi wake hajaanza mpaka sasa na ni lini hasa utaanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kaliua - Kazilambwa, kilomita 56 inayojengwa na *CHICO* ilitakiwa kukabidhiwa mapema mwaka 2017 kwa maagizo ya Waziri

Mheshimiwa Profesa Mbarawa, aliyoitoa alipotembelea mradi huu mwaka jana 2016, mpaka leo ni Mei, 2017 bado haujakamilika pamoja na kuwa kazi inaendelea. Serikali itoe agizo kwa Kampuni ya CHICO kukamilisha ujenzi huu ndani ya muda uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ile Kazilambwa - Ilunde kilomita 48 ni mbaya sana sana na kipande hiki kinaunganisha Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Kigoma. Mpango wa Serikali Kuiunganisha mikoa yote kwa barabara za lami. Pia barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi na kusafirisha mazao. Ni lini barabara hii itanza kujengwa kwa lami?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya kuunganisha Mkoa wa Katavi na Tabora, barabara ya Mpanda - Kaliua - Ulyankulu kwenda Kahama. Hii ni barabara muhimu sana kwa kusafirisha mazao na biashara kwa mikoa hii mitatu. Mwaka jana Waziri alilieleza Bunge kuwa inafanyiwa upembuzi yakinifu. Serikali ieleteze mchakato wake umefikia wapi na ni lini itanza kujengwa kwa lami?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uwepo wa reli katika Wilaya ya Kaliua wananchi wengi wa Kaliua wanakosa fursa ya kusafiri kwa treni kwa sababu ya kukosa tiketi na nafasi chache zinazotolewa kwa siku treni inapopita. Nafasi zinazotolewa ni kumi na tano tu kwa kituo na treni za express haisimami pale Kaliua na wananchi wengi wanakosa tiketi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabehewa yanayopita Kaliua kwenda Kigoma na Mpanda ni machache sana na hayakidhi mahitaji ya wananchi, pia tiketi zinalanguliwa kwa bei kubwa sana, madalali wanakata tiketi kwa bei ya Serikali wanauzu kwa bei ya kuruka na wananchi hawana namna wanunua. Mheshimiwa Waziri aliahidi kuongeza mabehewa mpaka leo bado tabu na adha inaendelea. Serikali ieleteze mkakati wa kuongeza mabehewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wastaifu wa Shirika la Reli walioachishwa kazi wakati wa EAC mpaka leo hawajalipwa

haki zao, Serikali ilete taarifa kamili za wazee kwa wananchi haki zao mpaka wamechoka na wengine wamekufa bila kupata haki zao. Hii kwa nini hawalipwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano eneo kubwa la Wilaya ya Kaliua na hususani Jimbo langu hakuna kabisa mawasiliano ya redio, wananchi wanaishi bila kujua nini kinachoendelea ndani ya nchi yao pia hakuna minara ya simu. Kata zifuatazo mawasiliano ya redio ni magumu sana mpaka radio zifungwe kwenye miti juu sana:-

Kata ya Igwisi, Kijiji cha Mpanda Mlohoka na Igwisi Center; Kata ya Usimba karibu vijiji vyote havishiki redio; Kata ya Ushokola, Kijiji cha Makubi na Mwamashimba; Kata ya Zugimbole Kijiji cha Igombe na Luyombe; Kata ya Ukumbisiganga, Kijiji cha Usimba na Ukumbi Kakonko; Kata ya Usinge, Kijiji cha Kombe; Kata ya Usonye; Vijiji vya Luganjo mtoni, Shela na Maboha. Kata ya Ugunga Vijiji vya Mkuyuni, Mpilipili na Limbula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vyote hivi mawasiliano ya simu ni ya tabu sana kwani minara iko mbali na eneo lao pia mawasiliano ya redio ni kwa tabu sana na kwingine hakuna kabisa. Naomba Serikali ileze ni lini wananchi hawa watapelekewa huduma hii muhimu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jafo dakika kumi, jiandae Mheshimiwa Ngonyani.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kwanza kumpongeza Waziri mwenye dhamana ya Ujenzi kwa hotuba nzuri na mtandao mzima wa barabara ambao wananchi wana imani kubwa kwamba Serikali ya Awamu ya Tano inatekeleza mambo mbalimbali kwa ajili ya sekta ya miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya maeneo nataka nichangie katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika baadhi ya maeneo ambayo Wabunge hasa Mheshimiwa

Mary Muro, Mheshimiwa Hasna Mwilima, Mheshimiwa Ester Bulaya na sasa hivi Mheshimiwa Julius Kalanga katika suala zima la upelekaji wa fedha za miundombinu ya barabara katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wakati mbalimbali kwamba maeneo mengine yamekuwa na changamoto kubwa na ndiyo maana Serikali kwa kipindi kirefu sasa imeamua kubadilisha utaratibu wake wa upelekaji wa fedha kuelekeza fedha nyngi katika Halmashauri zetu. Japokuwa bado hazijatosheleza angalau hali si haba, ndiyo maana hata ukiangalia kitakwimu katika Bajeti yetu ya Mwaka 2010/2011 shilingi bilioni 84 tu ndiyo zilikuwa zimetengwa kwa bajeti ya barabara lakini bajeti yetu ambayo tumeipitisha juzi hapa tumetenga karibu shilingi bilioni 272. Lengo kubwa ni kuziwezesha Halmashauri mbalimbali japo tuweze kuzifungua barabara zile ziweze kupitika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, najua kwamba changamoto ya mtandao wa barabara za Serikali za Mitaa ni mkubwa hizi fedha hazitoshi, lakini Serikali lazima tutaendelea kuangalia jinsi gani tunatafuta rasilimali fedha kuhakikisha kwamba tunaboresha. Ndiyo maana wakati mwingine tunashirikiana hasa kwa kutafuta *funds* kutoka hata kwa wenzetu wa *World Bank* ndiyo maana Halmashauri nyngi sana za Miji hivi sasa mitando ya barabara imebadilika, ni kwa ajili ya juhudhi hizo kubwa sana zinazofanyika, lengo kubwa ni kufungua barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upelekaji wa fedha, naomba ni wahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa sababu mwaka wa fedha haujawkisha, kwa zile bajeti ambazo zimetengwa katika mwaka huu wa 2016/2017, Wizara ya Fedha itakuwa inafanya harakati za kutosha kuhakikisha kwamba barabara hizi tutaziwezesha ili kazi zetu za barabara ziweze kuendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Hussein Bashe ambayo ilikuwa ikizungumzia suala zima la Wakala wa Barabara ambao unaanzishwa sasa

hivi vijijini, hoja yake ni kwamba changamoto kubwa ni fedha na jinsi gani tutaanzisha wakala ambapo sasa mgawanyo wa fedha hauko sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la kisheria, kwa sababu kwa sheria yetu tuliyonayo ni kwamba asilimia 30 ya fedha hizi zinaenda katika bajeti ya barabara za Halmashauri na asilimia 70 inaenda kwa ajili ya *TANROADS*, ndiyo maana tumekusudia kuanzisha Wakala lakini jambo hili liko katika hatua za mwisho, ilikuwa ni mapendelekezo ya Wabunge humu ndani ya Bunge, basi kama kutakuwa na mawazo mengine tofauti tutatafakari. Lengo kubwa ni kwamba wananchi wetu katika maeneo yao barabara ziweze kupitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo haya kama michango ya Waheshimiwa Wabunge yote tunayachukua kwa pamoja, jukumu kubwa la Serikali inaangalia jinsi gani itafanya kuhakikisha kwamba barabara zetu zinapitika katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Ahmed Shabiby, alikuwa akizungumzia suala zima la barabara yake pale Mjini ambapo kulikuwa na ahadi ya kilometra tano na Mheshimiwa Shabiby anasema kweli na ndiyo maana siku ya Alhamisi Mheshimiwa Shabiby anakumbuka tulikuwa Jimboni kwake. Ahadi ya Serikali ni kuhakikisha kwamba barabara ile ya kilometra tano ujenzi unakamilika na ndiyo maana juzi nilivyofika pale Gairo ujenzi wa barabara ile sasa unaendelea. Ni imani yangu kwamba Serikali katika kipindi hiki cha miaka mitano, itafanya kila liwezekanalo ule mtandao ambao ni ahadi ya Serikali, ahadi ya Mheshimiwa Rais alioitoa ya ujenzi wa kilometra tano uweze kukamilika katika eneo la Gairo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab alizungumzia suala zima la ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kilometra tatu pale Mjini Muheza. Naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab kwamba ile ahadi ya Mheshimiwa Rais ndiyo hivi sasa Ofisi ya Waziri Mkuu ilikuwa

inachukua ahadi mbalimbali. Imani yangu ni ndani ya kipindi hiki cha miaka mitano ahadi ile iweze kutekelezeka kwa sababu *commitment* ya Serikali ni kuhakikisha kwamba ahadi zote hasa za ujenzi wa miundombinu ya barabara ndani ya kipindi cha miaka mitano hii tuweze kuzikamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya Mbunge, Mheshimiwa Vedasto Ngombale ambaye amechangia nadhani kwa maandishi, Mheshimiwa Bwege naye alizungumzia ile barabara ya kwenda Kilwa Kivinje na mwaka huu kulikuwa na *commitment* ya shilingi milioni 800 ambayo ipo katika bajeti ya mwaka huu wa 2016/2017. Kwa vile juu halijachwa bado ni imani yangu kwamba zile fedha zitapatikana kwa kipindi hiki kwa kuwa ipo katika mpango huu wa bajeti, bahati nzuri Mheshimiwa Bwege ni kwamba tayari tumeshaingizwa katika bajeti, hivi sasa naamini Wizara ya Fedha, fedha hii ikishatiririka basi tutatoa maelekezo Wakandarasi waingie *site* haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kipindi hiki cha mvua hali ni mbaya na nilipokuja kule kwenu nimeona kwamba hali ya barabara ile siyo nzuri zaidi ndiyo maana *commitment* ya Serikali mwaka huu ilitenga shilingi milioni 800 hizi tutahakikisha kwamba zikishapatikana basi ujenzi utekelezwe katika ubora unaokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya dada yangu, Mheshimiwa Bonnah, kuhusu suala la ujenzi wa barabara chini ya Mradi wa *DMDP* ambao hata wewe unakuhusu katika Jimbo lako la Ilala. Mradi huu utakuwa na takribani shilingi zisizopungua bilioni 600 na nusu na kuendelea, ambapo mchakato wake kweli ilibidi uanze tokea zamani lakini kuna mambo mbalimbali yalikuwa yamekwamisha. Hata hivyo, hivi sasa tupo katika hatua nzuri, Mbunge wa Temeke na Mbunge wa Mbagala, ni mashahidi, mwezi mmoja na nusu uliopita tumekwenda kuangalia ukaguzi wa ujenzi wa barabara hizi hasa utengenezaji wa daraja lile kubwa la Twangoma ambalo lina urefu wa karibu mita 800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mchakato huu katika maeneo mengine umekwama ni kwa sababu ya lile jedwali la tathmini. Imani yetu ni kwamba kulikuwa na mchakato hapa, inaonekana hali siyo nzuri sana katika ufanyaji wa tathmini. Jambo lile likikaa vizuri kwa sababu sasa hivi Wakandarasi wameshapatikana, ni imani yangu kwamba ujenzi wa barabara hii sasa utaanza mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuhakikishie, katika Jimbo lako la Ilala nitasimamia kwa karibu zaidi na maeneo yote ya Jiji la Dar es Salaam kuhakikisha barabara zile tunazijenga. Kwa sababu barabara zile ndiyo zitakuja kufungua Mji wa Dar es Salaam nyingine ni *feeder roads* zinaunganisha katika barabara kuu yetu ya *DART*, zingine ni barabara ambazo zinapita katika mitaa yetu ya Jiji la Dar es Salaam. Sasa hivi ukiangalia hata mvua ikinyesha mitaro yetu imekuwa ni tatizo, mradi ule unakwenda kutengeneza mitaro, unatengeneza barabara halafu unafanya *settlement* katika maeneo mengine. Kwa hiyo, naomba niseme kwamba Serikali imeweka *commitment* katika maeneo haya kuhakikisha mradi huu wa *DMDP* ambao Wabunge wa Jiji la Dar es Salaam lengo letu ni kuufungua mji ule vizuri, tutakwenda kulifanya hili kwa kadri iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa zaidi naomba niwahamasishe Waheshimiwa Wabunge hasa kwa fedha tunazozipeleka katika Halmashauri zetu, tuzisimamie vizuri, kwa sababu imani yangu kubwa katika maeneo mengine hali huwa inakuwa siyo shwari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Ngonyani dakika 20.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea

kunipa uhai, nguvu, afya njema na akili timamu na kuniwezesha leo kuchangia hoja ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kwa heshima kubwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Viongozi wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao mahiri. Hakika Watanzania kwa ujumla wetu tumefarijika na uongozi wao mahiri ambao unaonesha nia ya dhati ya kuiwezesha nchi yetu kupiga hatua kubwa kimaendeleo na kufikia kiwango cha uchumi wa kati. Nami naungana na Watanzania wenzangu kuendelea kuwaombea afya njema ili waweze kuendelea kututumikia kwa mapenzi makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wengine wote wa Bunge kwa kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu. Napenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mheshimiwa Dkt. Gertrude Pangalile Rwakatare, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi, Waziri wa Katiba na Sheria walioleuliwa na Mheshimiwa Rais kuungana nasi katika Bunge hili. Nina imani kwamba sasa sote tutatekeleza kazi zetu za kuwatumikia wananchi kufuatana na kauli mbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ya 'Hapa Kazi Tu' ili tufikie malengo yetu ya kujkwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru kwa namna ya pekee wapiga kura wangu wa Wilaya ya Namtumbo, kwa namna wanavyojituma katika kuhakikisha kwamba kwa pamoja tunatatua changamoto

zinazowakabili. Pamoja na kwamba muda mwingu sipo nao kutokana na majukumu ya Kitaifa, wanajua nawawakilisha kwa kiwango kikubwa katika kutatua changamoto zao. Nawaahidi tena kwamba mambo yote niliyoyaahidi na yaliyoahidiwa ndani ya llani ya Chama cha Mapinduzi nitaendelea kuyasimamia yatekelezwe kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zote za kilimo hususan kilimo cha tumbaku na mazao mchanganyiko pamoja na masoko ya uhakika, maji, umeme, mitandao ya simu, barabara, maeneo ya kilimo na mipaka ya kiutawala zinazowakabili wakazi wa Wilaya ya Namtumbo naendelea kuzishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nishukuru familia yangu, mke wangu na watoto kwa kuniunga mkono, kunivumilia na kunitia nguvu katika kutekeleza dhamira yangu ya kuwatumikia wananchi wa Namtumbo na Watanzania wote katika nafasi hizi za Ubunge na Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru Wabunge wote kwa namna mlivyochangia, maoni na mapendekezo yenu kwetu ni maelekezo. Naomba sasa ndugu zangu, Waheshimiwa Wabunge wote, tuunge mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na naomba sasa nijielekeze katika kujibu hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamechangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombini ameongelea kuhusu kutotolewa kwa fedha za ujenzi wa viwanja vya ndege vya Kigoma, Mpanda, Tabora, Songwe, Mtwara, Sumbawanga na Shinyanga na vilevile Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani naye ameongelea kutotolewa kwa fedha za ujenzi wa jengo la tatu la abiria *JN/A Dar es Salaam* na uwanja wa Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa viwanja vya ndege vya Kigoma, Tabora, Shinyanga, Mtwara na Sumbawanga,

naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba hadi kufikia Machi 2017, ujenzi wa viwanja vya ndege tajwa ulikuwa katika hatua ya manunuzi kwa hiyo hakuna fedha iliyotolewa kwa sababu bado hatujawapata wakandarasi wa kufanya kazi zinazotakiwa kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Mpanda kwa kiwango cha lami ulikamilika mwaka 2012 na katika mwaka 2016/2017, Serikali ilitenga jumla ya shilingi milioni 700 kwa ajili ya kulipa deni la Mkandarasi. Serikali itahakikisha kuwa deni hilo la Mkandarasi linalipwa mapema. Kazi zinazoendelea katika Kiwanja cha Ndege cha Songwe ni ujenzi wa jengo kubwa la abiria na mradi unaoendelea ambapo Mkandarasi amekwishalipwa shilingi bilioni 3.3 na hadi sasa hana deni lolote analoidai Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiwanja cha ndege cha Mtwara, zabuni ya upanuzi na ukarabati wa kiwanja hicho imeshatangazwa na inatarajiwa kufunguliwa mwezi Mei, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya 2017/2018, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kulipa fidia kwa viwanja vya Kigoma, Shinyanga, Sumbawanga, Iringa, Musoma, Msalato, Bukoba, Umkajunguti na JN/A. Kwa viwanja vilivyobaki Serikali itaendelea kulipa fidia kadri ya upatikanaji wa fedha. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeweka mkakati wa kupima na kupatiwa hati miliki kwa viwanja vya ndege 15 Mwanza, Songwe, Msalato, Dodoma, Iringa, Kilwa Masoko, Mtwara, Lindi, Lake Manyara, Songea, Tabora na Shinyanga na kwa mwaka wa fedha 2017 hicho ndicho tutakachokifanya. Maombi ya kupimiwa na kupatiwa hati miliki yameshawasilishwa kwa mamlaka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze katika hoja mbalimbali za barabara. Wabunge wengi sana wameongelea barabara na muda ulivyo siyo rahisi sana kuzieleza zote, nitachukua moja moja kadri muda utakavyoniruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na barabara ya Tabora – Sikunge – Koga – Mpanda vilevile inaunganika na barabara ya Mbinga hadi Mbamba bay, barabara hizo zote ni *lot* moja, ni *project* moja inayofadhiliwa na Benki ya AFDB na fedha za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami tayari zimeshapatikana kutoka Benki ya Maendeleo ya AFDB. Zabuni za ujenzi wa barabara hii zimetangazwa na taratibu za kukamilisha manunuzi ya Mkandarasi zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kibondo – Kasulu – Mnaniila, tunatarajia kupata rasimu ya usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni mwezi Juni, 2017 kwa ajili ya kutoa maoni kabla zabuni za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kibondo – Kasulu – Manyovu hazijatangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Masasi – Nachingwea – Nanganga umepangwa kuanza mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, kulingana na Ilani ya CCM ya mwaka 2015 ambayo ndiyo tunayoitekeleza, barabara za Nachingwea hadi Liwale na barabara ya Nangurukuru hadi Liwale zinatakiwa zifanyiwe upembusi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge walioongelea hili ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande kwamba barabara hii tutaifanya upembusi yakinifu na usanifu wa kina katika kipindi hiki cha miaka mitano kabla hakijakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Butengulumasa – Iparamasa – Mbogwe – Masumbwe, Serikali imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya kufanya matengenezo na kukarabati barabara hii ili iweze kupitika katika kipindi chote cha mwaka. Ujenzi wa kiwango cha lami kwa barabara hii utafanya kadri bajeti itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kahama hadi Geita, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 12,403 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Barabara ya Mafia –

Kilindoni – Rasimkumbi; upembuzi yakinifu na usanifu wa kina utafanyika ili barabara hii ambayo pia ipo katika ahadi za Viongozi Wakuu iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Wakati fedha za ujenzi zinatafutwa, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 1.0422 katika bajeti ya 2017/2018 kwa ajili ya kuifanyia matengenezo ya aina mbalimbali barabara ya Kilindoni – Rasimkumbi ili iendelee kupitika wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara ya Makutano – Mugumu hadi Mto wa Mbu na hasa kipande cha Makutano hadi Sanzate kinachoendelea kujengwa, ujenzi wa barabara ya Makutano – Nata – Mugumu, sehemu ya Makutano hadi Sanzate umefikia hatua ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tabaka la udongo (*G 15*) ni kilometra 38 ambayo ni sawa na asilimia 76; tabaka la chini la tuta (*sub base*) kilometra 8.5; na tabaka la juu la barabara (*base course*) ni kilometra mbili, lami nyepesi (*prime course*) ni kilometra 1.2, madaraja ya makalavati makubwa na madogo asilimia 98 yamekamilika. Maendeleo ya jumla ya mradi ni asilimia 43, mradi unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Septemba, 2017. Aidha, Serikali inasimamia kwa karibu utekelezaji wa mradi huu ili kuhakikisha kuwa mkandarasi anapata ujuzi uliokusudiwa na barabara inajengwa kwa kuzingatia viwango kulingana na mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya barabara kati ya Mugumu hadi Tabora B ambayo ni kilometra 18, mpango wa Serikali ni kuijenga barabara hii mpaka Mugumu. Aidha, ujenzi kwa sehemu nyingine ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Mugumu – Tabora B – *Clensi Gate*– Loliondo itajengwa kwa kiwango cha changarawe ili kutunza mazingira ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ambapo sehemu ya Mugumu hadi Tabora B *Clensi Gate* na sehemu ya *Clensi Gate* hadi Longido zitatumika kama *buffer zone*.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipande cha Mugumu - Natta, zabuni zilitangazwa tarehe 07/09/2016 na ufunguzi wa zabuni ilikuwa tarehe 25/10/2016 lakini ulisogezwa hadi tarehe 27/02/2017. Zabuni iliypokelewa haikukidhi vigezo na hivyo mradi huu utatangazwa tena tarehe 03/05/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara Tanga - Pangani - Bagamoyo unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2017/2018. Serikali tayari imetenga shilingi bilioni 4.435 katika bajeti ya mwaka 2017/2018 na inaendelea kukamilisha taratibu za kupata fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Jumuia ya Afrika Mashariki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja jipya la Wami kwenye barabara ya Chalinze - Segera liko katika hatua ya kumpata mkandarasi wa kuanza ujenzi. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 daraja hili limetengewa shilingi bilioni 4.351 kwa ajili ya kuanza ujenzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Lindi - Morogoro, kupitia Mpango Mkakati wa Wakala wa Barabara (*TANROADS*) wa mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021, Mkoa wa Lindi umepangwa kuunganishwa na Mkoa wa Morogoro kwa kuanzia na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Nachingwea - Liwale - Ilonga - Mwaya - Mahenge kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Naibu Waziri wa TAMISEMI ameongelea barabara zote za miji mbalimbali ambazo Mheshimiwa Rais aliahidi na nimshukuru kwamba majibu yake yako sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Kiboroloni - Kiharara - Suduni - Kidia katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali ilikamilisha usanifu wa kina. Katika mwaka wa 2017/2018 Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 811 ili kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa barabara ya

Kibosho – Shine - Mto Sere ambayo ina kilometa 27.5. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 61 ili kuanza ujenzi wa kiwango cha lami kwa barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeulizwa ni hatua gani zimefikiwa katika kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Kitai - Lituhi na Lituhi -Mbamba Bay. Nimuombe Mheshimiwa Jacqueline Msongozi aondoe tishio lake la kushika shilingi kwa sababu akishika shilingi hapa mimi nitakwenda kushika shilingi Ruvuma. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Kitai - Lituhi umefikia asilimia 50. Mhandisi Mshauri amekwishawasilisha rasimu ya taarifa ya upembuzi yakinifu. Kwa barabara ya Mbamba Bay - Lituhi upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umefikia asilimia 60. Mhandisi Mshauri (*M/s H.P Gauff Ingenieure*) anaendelea kumalizia kazi ya usanifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara inayounganisha Maramba na Makao Makuu ya Wilaya ya Mkkinga yenye urefu wa kilometa 49 utatekelezwa na kukamilika kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 zimetengwa shilingi milioni 87.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kizi - Sitalike - Lyamba Lya Mfipa, Mji wa Mpanda kupitia Sitalike unaungwa na barabara mbili za Kizi - Lyamba Lya Mfipa - Sitalike ambayo ni kilometa 86.24 na Kibaoni - Sitalike ambayo ni kilometa 71.6 ambazo zote bado kujengwa kwa kiwango cha lami. Mpango uliopo kwa sasa ni kujengwa kwa kiwango cha lami barabara ya Kibaoni - Sitalike ambayo imetengewa kiasi cha shilingi milioni 480 kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. Aidha, barabara ya Kizi - Liamba Lya Mfipa - Sitalike itaendelea kupatiwa matengenezo ili kuhakikisha kuwa inapitika wakati wote. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, kiasi cha shilingi milioni 1,950 kimetengwa kwa barabara ya Lyamba Lya Mfipa - Mpanda - Uvinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kibondo – Kasulu – Mnaniila, nashukuru nimeieleza. Nachoomba tu Waheshimiwa wa Kanda ya Magharibi watuamini, siyo kweli kwamba hilo eneo tumelitelekeza, mnafahamu sasa hivi nguvu zote zinalekezwa huko na mtuamini tunachokisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Tarime - Mugumu inaendelea na usanifu. Limeulizwa swali ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii unaendelea na utakamilika mwezi Machi, 2018. Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hiyo baada ya kukamilisha usanifu wa kina na kujua gharama halisi za mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Handeni – Kiberashi - Kibaya – Singida; katika mwaka wa fedha 2017/2018 barabara hii imetengewa jumla ya shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Ni maandalizi siyo ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa barabara ya Amani - Muheza, Serikali itaendelea kutoa kipaumbele katika utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Rais.

Hata hivyo, kutokana na uhaba wa fedha, ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami utafanyika hatua kwa hatua kutegemeana na fedha zitakavyopatikana. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, barabara hii imetengewa shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niingie kwenye barabara ya Bwanga - Kalebezo. Tumepokea shukrani na nimhakikishie Serikali kuititia Wakala wa Barabara Tanzania itaendelea kumsimamia mkandarasi ili ajenge...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Dakika moja Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *TANROADS* watamsimamia mkandarasi ili ajenge barabara ya Bwanga -Kalebezo kulingana na mkataba na hivyo kukamilisha mradi kama ilivyopangwa. Aidha, Wizara itafuatilia ili kuhakikisha mkandarasi anaweka alama za barabarani na kuhakikisha usalama kwa watumiaji wa barabara na wafanyakazi wanaojenga wakati wote wa ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu minara ya simu, niwahakikishie tuna dhamira ya dhati kuhakikisha vijiji vyote Tanzania tunapeleka mawasiliano kupitia Mfuko wetu wa Mawasiliano kwa Wote, lakini vilevile kupitia Kampuni ya *Halotel* kwa mujibu wa mkataba tulioingia nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo dogo linatoka Idara ya Shughuli za Bunge kwa Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeleta fomu za maombi ya kubadili cheti cha chanjo cha kimataifa (*Form for replacement of yellow fever vaccination card*) ambayo mnatakiwa kuijaza na kuiwasilisha kwa madaktari walipo kwenye iliyokuwa zahanati ya Bunge zamani, nyuma ya Ukumbi wa Msekwa.

Sasa namwita Mheshimiwa Waziri ahitimishe hoja yake. (*Makofii*)

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa kukamilisha kazi ambayo nilianza wiki iliyopita.

Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wengine wote na Katibu

wa Bunge kwa kusimamia kwa ufanisi mkubwa majadiliano yote kwenye Mkutano huu wa Saba wa Bunge letu Tukufu. Kwa namna ya kipekee, napenda pia kumpongeza Kiongozi wa Shughuli za Bunge, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri wa hali ya juu anaoendelea kuuonyesha na kutuongoza sisi wasaidizi wake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii pia kuwashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu na Kamati ya Bajeti kwa kufanya kazi kwa karibu na Wizara yangu. Naahidi kwamba Wizara ninayoingoza itayafanya kazi yote yaliyoshauriwa na Kamati hizi ya kusimamia, kuendedesha, kuboresha na kuendeleza miundombinu na huduma za sekta ya ujenzi, uchukuzi na mawasiliano kwa weledi wa hali ya juu.

Napenda kumshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa maoni na mapendekezo yake kuhusu bajeti hii. Mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii kwa kuzungumza na kwa maandishi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu limejipanga kuwa nchi ya kipato cha uchumi wa katiba ifikapo mwaka 2020/2025. Katika kufikia lengo hili, Taifa limelipa kipaumbele sekta ya viwanda na uendelezaji rasilimali watu ili kuwezesha kufikia lengo tunalokusudia. Wizara yangu itafanya jitihada kubwa kuweka mazingira wezeshi kwa kujenga miundombinu bora ili kurahisisha uendelezaji wa viwanda hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalihakikishia Bunge lako hili Tukufu kwamba mimi na Mheshimiwa Naibu Waziri wangu pamoja na watendaji wote wa Wizara tutasimamia ujenzi wa miundombinu muhimu ya usafirishaji na ya uunganishaji maeneo ya uzalishaji wa viwanda hivyo na maeneo ya mahitaji yaani masoko ya ndani na ya nje ya nchi. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wote tuunganishe nguvu zetu ili pamoja na Serikali yetu inayoongozwa na

Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuwezeshe Taifa letu kuflikia ndoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya masuala hayo ya jumla, sasa noamba nijikite kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa kuzingatia sekta tatu yaani sekta za ujenzi, uchukuzi na mawasiliano. Mheshimiwa Naibu Waziri tayari amejibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa kuzingatia makundi ya Wabunge na maeneo ya kisekta. Kazi yangu kubwa itakuwa ni kujibu hoja kuu zilizojitokeza ambazo zitakuwa msingi wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitakwimu Waheshimiwa 29 walichangia wakati wa majadiliano ya hoja ya Waziri Mkuu na wakati wa majadiliano ya Wizara yangu tumepokea michango ya Waheshimiwa Wabunge 68 waliota maoni yao kwa kuzungumza na michango kwa maandishi 98. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilihakikishie Bunge Iako Tukufu kwamba Wizara itajibu hoja zote za Waheshimiwa Wabunge kwa maandishi na kuwapatia majibu ya maandishi kwa njia ya kitabu kitakachoandaliwa kabla ya kuanza Mkutano wa Nane wa Bunge letu Tukufu. Hivyo kwa yale ambayo hatutaweza kuyajibu hapa leo kwa sababu ya muda kutotosha, majibu yatapatikana kupitia kitabu kitakachoandaliwa na Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijikite kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge nikianzia na sekta ya mawasiliano, uchukuzi na mwisho sekta ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeamua kuanzia sekta ya mawasiliano kwa sababu wewe leo ni Mwenyekiti na ulikuwa mchangiaji wa kwanza kwenye sekta hii na hasa ulijikita kwenye suala la *TTMS*. Ulisema kwamba iko haja ya Serikali kuangalia upya mfumo wa *TTMS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilieleze Bunge lako Tukufu pamoa na Watanzania wote kwamba mfumo wa *TTMS* umejengwa kwa utaratibu wa jenga, endesha na kabidhi (*Build, Operate and Transfer - BOT*) na hivyo hakuna malipo yoyote ya awali yaliyolipwa na Serikali kwa mkandarasi wakati wa utekelezaji wa mradi huo. Mkataba wa uendeshaji ni miaka mitano na mkandarasi atakabidhi mfumo huo wa *TTMS* kwa Serikali kuititia *TCRA* mwezi Oktoba, 2018 na kuwezesha Serikali kumiliki mtambo huo kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za ujenzi wa mtambo huo kwa mkandarasi yanatokana na malipo yanayotokana na *termination fee* ya senti 25 kwa simu zinazoingia ndani ya nchi (*international incoming calls*), mgawanyo ni kama ifuatavyo:-

Mkandarasi analipwa senti nne za dola kwa ajili ya mtambo ule, senti 12 zinakwenda kwa mto huduma yaani makampuni ya simu, senti 8 zinakwenda Serikalini na senti moja ya dola inakwenda kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa ajili ya kusimamia mtambo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma zinazotolewa kwa sasa ni kama ifuatavyo; kusimamia simu za kimataifa (*international incoming calls*); kusimamia simu za ndani (*local off network monitoring*); Kusimamia ubora wa huduma (*quality of service platform*) na kusimamia au kutambua simu za ulaghai (*anti-fraud management system*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilliarifu Bunge lako Tukufu toka mtambo huo kufungwa mpaka sasa hivi tuna kesi 22 mahakamani na Serikali imepoteza pesa nyingi kuititia wizi huo wa njia za panya. Kwa mfano, mpaka sasa hivi Serikali imepoteza takribani shilingi bilioni 15.2 kuititia wizi wa mawasiliano kwa njia za panya. Kama ingekuwa hakuna mfumo wa *TTMS* tunaamini wizi ungekuwa mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mtambo huo sasa hivi unaweza kuona miamala ya fedha zote zinazopita hapa

nchini kupitia kwenye mitandao ya mawasiliano. Taarifa na takwimu za miamala ya fedha hutumiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na huwasilishwa *BoT*. *BoT* na Mamlaka ya Mapato Tanzania zote zimepewa uwezo wa kuweza kuona takwimu mbalimbali zinazopita kwenye mtambo huu hasa za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mtambo huu una uwezo wa kutambua rajisi ya namba za utambulisho wa simu za kiganjani (*Central Equipment Identification Register*). Kwa sasa mtambo huu hauna uwezo wa kutambua *revenue assurance* kwa maana ya kutambua mapato ingawa kumefungwa kifaa kwa kila *NOC* ya mtoa huduma. *Network Operative Centre* ya *Vodacom*, *Airtel*, *Tigo* kumefungwa *sensorkwa* ajili ya kupata *information* hizo lakini bahati mbaya mtambo huu mpaka sasa haujaweza kutambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini mtambo huu haujaweza kutambua *code* hiyo ni kwa sababu kulikuwa na mvutano mkubwa baina ya sisi Serikali kwa upande wa *TCRA* na mkandarasi yule kwa sababu alikuwa anasema hiyo huduma ya *revenue assurance* ilikuwa haipo kwenye mkataba. Tumevitana nao kwa zaidi ya miezi tisa na mwisho tumekubaliana kwamba aweke *platform* hiyo ya *revenue assurance* bure bila ya malipo yoyote na kazi hiyo imeanza.

Tunaamini kwamba itakapofika mwezi Agosti, mkandarasi yule atawea kuweka mfumo huo na hapo tutaweza kupata malipo sahihi ya simu zetu kupitia kwenye mtambo ule. Naomba nieleze kwamba maoni yako tumeyachukua na tutazidi kuyafanyia kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyininge uliyozungumza ni ya *TTCL* kwamba Serikali ifanye kila inavyoweza ili kuiwezesha *TTCL* kwa sababu *TTCL* ni kampuni ambayo kama itawezeshwa vizuri itakuwa na uwezo wa kuchangia sana pato la Serikali. Serikali tunakubaliana na wewe na tuko kwenye mpango madhubuti wa kuhakikisha kwamba sasa *TTCL* tunaiwezesha na kuhakikisha kwamba inachangia inavyowezekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ya msingi ambayo Serikali tumeyafanya kuiwezesha *TTCL*. La kwanza kabisa tumeiruhusu *TTCL* kutumia rasilimalizake zenyewe. *TTCL* ina rasilimali nyingi ili kuweza kukopa shilingi bilioni 96. Jambo la pili ambalo tumelifanya kwa *TTCL* kwa sababu kwenye sekta ya mawasiliano *issue* siyo pesa ni masafa, *TTCL* tumewapa masafa ya *Mhz* 1800 kwa ajili ya teknolojia ya *4G LTG*. Mpaka sasa hivi *TTCL* wameweza kufika mikoa kumi na mingine itaendelea mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *TTCL* tuna mpango wa kuwapa tena masafa mengine mapya ya 800Mhz itakapofika mwezi wa Juni, 2017. Kwa kuiwezesha *TTCL* tumeipa *Data Center* kwa ajili ya uendeshaji na inapata malipo kwa uendeshaji huo. Pia *TTCL* tumeipa kuendesha Mkongo wa Taifa na inapata malipo kupitia mkongo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ulizungumzia kuhusu *technology* ya *internet of things*, tumejipanga. *TTCL* ni kampuni ambayo itaweza kujingiza kwenye biashara hii ya *Internet of things* ambayo naamini ikienda kwenye biashara hii na kwa vile ina Mkongo wa Taifa itafanya vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza machache kuhusu sekta ya mawasiliano, naomba sasa nijikite kwenye sekta ya Uchukuzi. Wakati wa majadiliano ya hoja ya Waziri Mkuu pamoja na hoja niliyotoa tokea wiki iliyopita, michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge imegusa miundombinu ya reli, huduma za uchukuzi kwa njia ya anga, miundombinu ya bandari na miundombinu ya viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianzie na miundombinu ya reli. Reli tunayotumia sasa ya *meter gauge* imejengwa mwaka 1905 kwa ajili ya mizigo isiyozidi tani milioni tano kwa mwaka. Kwa reli hiyo treni ilikuwa inaenda mwendo kasi mdogo na ilikuwa na uwezo wa kutumia uzani wa tani 11 kwa *excel*. Mtawala wa Uingereza alipokuja yeche aliibadilisha kidogo treni hiyo badala ya kwenda kwa kutumia

mvuke akaifanya iweze kwenda kwa kutumia kwa *diesel* na ikawa na uwezo wa tani 14 kwa *excel*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, miundombinu ya treni hii kwa sasa imechakaa sana na mwendo wake mkubwa sasa inakuwa kilometa 30 kwa saa. Kwa uchumi tunaotaka kwa viwanda kwa treni hii haiwezekani. Serikali ya Awamu ya Tano imeamua sasa kujenga reli mpya ya *standard gauge* yenye uwezo wa kubeba mizigo ya tani milioni 17 kwa mwaka. Treni hii itatumia umeme, ni treni ambayo itakwenda mwendo kasi wa kilometa 160 kwa saa kwa treni ya abiria. Reli hii itahimili mizigo mkubwa wa tani 35 kwa *excel*. (*Makofj*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyofahamu Mheshimiwa Rais aliweka jiwe la msingi kwa ajili ya ujenzi wa reli hii kutoka Dar es Salaam - Morogoro. Gharama ya ujenzi wa reli hii ilikuwa ni dola bilioni 1.212 za Kimarekani sawa na shilingi trillioni 2.2. Urefu wa njia ambao tumeweka jiwe la msingi ni kilometa 300 ambapo kutoka Dar es Salaam - Morogoro ni kilometa 205 na kilomita 95 ni za mapishano ya reli hiyo. Kwa ujumla itakuwa ni kilometa 300. Katika kujenga reli hii kwa kila kilomita moja tutatumiwa dola za kimarekani milioni nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifanye kidogo *comparison* na wenzetu wa Kenya. Gharama ya ujenzi wa reli ya Kenya ya *standard gauge* kutoka Mombasa - Nairobi ni dola za kimarekani bilioni 3.8. Urefu wa njia ya reli ya kutoka Mombasa - Nairobi pamoja na maeneo ya kupishana ni kilometa 609. Kwa hiyo, kwa upande wa Kenya kilometa moja imegharimu dola za kimarekani milioni 6.23 wakati ya Tanzania kila kilometa moja imegharimu dola za kimarekani milioni nne. (*Makofj*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza tumeanza kufanya *evaluation* kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa kipande cha Morogoro - Makutupora chenye urefu wa kilometa 336. Tunaamini

mapema Juni, tutaweza kuweka jiwe la msingi kwa ajili ya ujenzi wa reli kutoka Morogoro - Makutupora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Makutupora - Tabora, Tabora - Isaka na Isaka - Mwanza zabuni zitafunguliwa mwisho wa mwezi huu. Aidha, kwa upande wa matawi ya Kaliua – Mpanda - Karema, Tabora – Kigoma, Uvinza – Msongati zabuni kwa matawi hayo zitatangazwa mara baada ya kukamilika usanifu wa kina ambao utamalizika hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, safari ya treni ya abiria kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro kwa kutumia reli ya *standard gauge* itachukua saa 1.30. Kutoka Dar es Salaam - Dodoma itatumia saa 2.45. Kutoka Dar es Salaam - Mwanza itachukua saa 7.40. Kutoka Dar es Salaam - Kigoma itachukua saa 7.45. Bado tunaangalia uwezo wa kupunguza muda huo kwa kuongeza *speed*. Tunaamini baada ya Singida tunaweza kuongeza *speed* kutoka 160 tukaenda mpaka 200 kwa sababu eneo lile lipo tambarale na tunaamini tunaweza kufanya hivyo ili Watanzania hawa sasa waweze kufika maeneo yao kwa muda mfupi zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa treni ya mizigo kwa kutumia reli hii tunayojenga itakuwa na uwezo kwa kusafirisha mizigo ya tani 10,000 kwa mara moja sawa na makontena 400 ya futi ishirini, ishirini. Hii ni sawa na *semi-trailer* 500 zenye uwezo wa kubeba tani 20 kwa kila *semi-trailer* moja. Treni hii itakuwa na mwendo kasi wa kilometra 120 kwa saa. Treni ya mizigo inakuwa tofauti na treni ya abiria, treni ya abiria inakwenda kwa kasi kuliko treni ya mizigo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge vilevile walizungumzia kidogo kuhusu *Northern Corridor* huko Kenya. Nikilinganisha na wenzetu wa *Northern Corridor*, treni ya mizigo ya wenzetu itakuwa inachukua makontena 216 kwa wakati mmoja wakati ya Tanzania itakuwa inachukua makontena 400 kwa wakati mmoja. Treni ya mizigo ya wenzetu itakuwa inakwenda mwendo wa kilometra 80 kwa

saa wakati ya Tanzania itakuwa inakwenda kilometa 120 kwa saa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kutoka Dar es Salaam - Kigali ambapo urefu ni kilometa 1,461, mzigoto kutoka bandari ya Dar es Salaam mpaka Kigali itachukua saa 13 kwa kutumia treni yetu. Kutoka Mombasa - Kigali (Rwanda) ni kilometa 1,659.3. Kwa hiyo, treni ya mzigoto kutoka bandari ya Mombasa - Kigali itachukua saa 21, mara mbili ya muda ambao itachukua treni yetu. Naamini kabisa ndani ya moyo wangu kwa kasi tunayokwenda nayo treni hii itamalizika haraka na naamini kabisa mzigoto ya Rwanda, Burundi, DRC na hata ya Uganda hapo baadaye itapita kwenye bandari yetu ya Dar es Salaam. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja juu ya fedha za ujenzi wa reli. Lengo la Serikali ni kujenga mtandao wa reli kwa kutumia fedha za ndani na za mkopo wenye masharti nafuu. Kipande cha Dar es Salaam - Morogoro katika mwaka wa fedha 2016/2017 tulitenga shilingi trilioni moja na bajeti hii ambayo tutaipitisha leo tumetenga shilingi bilioni 900. Kutokana na mahitaji makubwa ya fedha za ujenzi wa reli, Serikali imeendelea kufanya mazungumzo na wafadhili mbalimbali ikiwemo Serikali ya Uturuki, China na wengine ili kupata mikopo yenye masharti nafuu. Kwa mfano, wiki iliyopita Serikali kuititia *RAHCO* ilikuwa na mazungumzo na mabenki matano kutoka nje kuhusu kupata mkopo wa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja kuhusu ujenzi wa reli ya Mtwara – Mbamba Bay na matawi yake ya kwenda Liganga na Mchuchuma yenye urefu wa kilometa 1,000. Mwaka wa fedha 2017/2018 tunategemea kutangaza zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi, lakini reli hii tutaijenga kwa mfumo wa *PPP*.

Kuhusu ujenzi wa reli ya Tanga – Arusha - Musoma, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imetenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya kazi ya upembuzi na usanifu wa kina wa ujenzi wa reli hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja kuhusu TAZARA kwamba Serikali ina mikakati gani ya kuifanya TAZARA iweze kuijendesha kwa faida. Reli ya TAZARA iliyosanifiwa kubeba tani milioni 5 za mzigo kwa mwaka ili kusafirisha tani hizo unahitaji injini au *locomotives* 174. Kwa hivi sasa TAZARA inasafirisha tani 128,105 kwa mwaka. Sasa hivi TAZARA ina wastani wa vichwa 13 tu ambavyo vinatumika kwa mwaka. Ili TAZARA kuweza kusafirisha mzigo tani 1,273,000 zilizoweza kusafirishwa mwaka 1977/1978 inahitaji vichwa vya treni 48. Injini hizi 13 zilizopo sasa ni asilimia 27 ya vichwa vyote vinavyohitajika ambavyo vilitumika mwaka 1977/1978.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuisaidia TAZARA, Serikali tumejipanga kama ifuatavyo; kwanza, Serikali ya Tanzania kupitia bajeti hii tumepanga kuweka shilingi bilioni 26 kwa ajili ya kusaidia TAZARA. Tunaamini na wenzetu wa Zambia watatenga kiasi kama hicho ili kuweza kuisaidia TAZARA. Pili, tayari Serikali zetu mbili zimefanya mabadiliko makubwa ya viongozi wa ngazi za juu ikiwa ni pamoja na kuajiri Mtendaji Mkuu mpya, Naibu Mkurugenzi Mtendaji Mkuu mpya na Meneja wa Mkoa wa Tanzania mpya na kinachoendelea sasa ni uajiri wa Meneja wa Mkoa wa Zambia ambao uko katika hatua za mwisho za kiutawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuisaidia TAZARA iweze kufanya biashara sasa hivi tupo kwenye mpango wa kufanya marekebisho ya Sheria Na.4 ya mwaka 1995. Wataalam wa nchi zote mbili wapo kwenye hatua ya mwisho kukamilisha marekebisho hayo. Baada ya hapo marekebisho hayo yatapelekwa kwenye Baraza la Mawaziri na mwisho yatakuja kwenye Bunge lako Tukufu ambalo tunaamini litaweza kupitisha marekebisho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijikite kwenye huduma za uchukuzi kwa njia ya anga. Mwaka jana niliahidi kuanza kuchukua hatua za kulibadilisha Shirika la Ndege la Tanzania (*ATCL*) ili hatimaye liweze kuijendesha kibiashara. Tayari tumeunda Bodi mpya na Menejimenti yenye weledi na uzalendo wa hali ya juu kuijendesha kampuni hii ambapo

mpaka sasa hivi tunajua itakapofika mwaka 2018 itakuwa na ndege mpya sita. Bodi na Menejimenti ya ATCL zinaendelea na taratibu za kuirudisha kampuni hii kwenye Chama cha Watoa Huduma za Usafiri wa Anga Duniani ili mtu akiwa eneo lolote lile duniani aweze kununua tikiti bila usumbufu wowote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 zilitengwa shilingi bilioni 500 fedha za ndani kwa ajili ya ununuzi wa ndege. Tayari Serikali imenunua ndege tatu za *Bombadier Q400* zenye uwezo wa kubeba abiria 76 kila mmoja na kulipa malipo ya awali ya ndege mbili ya aina ya *CS Series 300* zenye uwezo wa kubeba abiria 127 kila moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali imelipa pesa za awali za ndege ya masafa marefu ya alna ya *Boeing 787-8 dreamliner* yenye uwezo wa kubeba abiria 262. Katika kipindi cha bajeti 2017/2018 zimetengwa shilingi bilioni 500 kwa ajili ya kukamilisha malipo ya ndege zilizotajwa hapo juu pamoja na malipo ya ndege nyingine mpya ya masafa marefu ya aina ya *Boeing 787-8 Dreamliner*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nzungumzie ndege 12 za *terrible teens*. Siku tatu zilizopita tumesikia maneno mengi hapa Bungeni na kwenye mitandao kuhusu ndege 12 za *terrible teens* ambazo zimeundwa na *Boeing*. *Terrible teens* ni ndege za mwanzo aina ya *Dreamliner 787* zilizotengenezwa na *Boeing* miaka sita, saba iliyopita huko nyuma. Ndege hizo ni nzito kidogo ikilinganishwa na ndege za kisasa za *Dreamliner 787-8*, zina uzito wa zaidi ya tani nne mpaka sita ukilinganisha na ndege za kisasa za *dreamliner*. Ndege hizi zina upungufu, kwa sababu ndege hizi ni nzito kwa hiyo zinakula mafuta zaidi ukilinganisha na ndege za kisasa. Pia ndege hizi hazina uwezo wa kwenda masafa ya mbali kwa mfano kutoka Dar es Salaam mpaka New York inabidi ziende mpaka sehemu zijaze mafuta ili ziweze kuendelea. Ndege za kisasa za *Dreamliner* zinaweza kutoka Dar es Salaam mpaka New York bila kunywa mafuta na ikafika New York na ikaanza safari kwa kunywa mafuta huko New York.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *terrible teens* zinazozungumzwa hapa, kawaida ndege tunaitaja kwa *line number* kwa hiyo mimi nitataja *line number*. *Terrible teens* zinazozungumzwa hapa ni *line number* 4 na ya pili ni *line number* 5. Ndege hizi mbili sasa hivi zinatumwa na *Boeing as a test aircraft*. Ndege nyiningine inayozungumzwa hapa ni *line number* 10 ambayo *Ethiopian Airways* wameshaonesha nia ya kuinunua. Ndege nyiningine inayozungumzwa ni *line number* 11 ambayo inatumwa na *Boeing Bussiness Jet*. Ndege nyiningine inayozungumzwa ambazo zina uzito mkubwa *Line number* 12 ambayo *Ethiopian Airways* imeonyesha *interest* ya kuichukua. Ndege nyiningine ni *Line* 13 na 14 ambazo vilevile *Ethiopian Airways* imeonyesha *interest* ya kuichukua. Ndege nyiningine ni *line* 15 ambayo kuna kampuni moja ya *Air Australia* imeichukua; *Line* 16 *Ethiopian Airways* imeonyesha nia ya kuichukua; *Line* 17 *Ethiopian Airways* imeonyesha nia ya kuichukua; *Line* 18 *Ethiopian Airways* imeonyesha nia ya kuichukua na *Line* 19 kulikuwa na maneno kwamba *Rwanda Air* inaweza kuichukua lakini mpaka sasa hivi haijawekwa vizuri na *Line* 22 kuna kampuni ya *Air Australia* imeonyesha kuichukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si kweli kwamba ndege iliyonunuliwa na Serikali kwa Shirika la Ndege la *Air Tanzania* *Boeing 787-8 Dreamlinerni* mionganoni mwa ndege 12 za *terrible teens dreamliners* ambazo zilikosa soko. Tuna ushahidi wa kutosha kuhusu jambo hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeingia mkataba na *Boeing* wa kutengeneza ndege mpya yenye *line number* 719. Ndege inayozungumzwa hapa kwamba tumeichukua ilikuwa iende *Rwanda* ina *line number* 19, yetu sisi ni *line number* 719, ni tofauti. Pia Serikali imeweka ratiba ambayo tutaifatilia ndege hiyo hatua kwa hatua. Kinachoendelea sasa hivi tunachagua injini ya ndege. *Dreamliner* inatumia injini za aina mbili, inatumia *Rolls-Royce* na *General Electric (GE)*. Kabla ya ndege kumalizika mnepewa uhuru wa kuchagua, tunalolifanya sasa hivi *ATCL* ni kuchagua injini gani tuweke kwenye ndege ile kwa vile ndege hii ni mpya sio kama maneno yaliyoletwa kwenye mitandao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wakiwa na jambo kama hili ambalo linahitaji maelezo ya kitaalam wawasiliane na sisi Serikalini. Tupo saa 24, siku saba kwa wiki, siku 365 kwa mwaka, Serikali ipo. Waheshimiwa Wabunge, elimu haina mwisho naomba tujifunze. Pia naomba sana Waheshimiwa Wabunge tushirikiane kujenga Shirika letu la Ndege la ATCL, tushirikiane kujenga nchi yetu, hatuna nchi nyngine Waheshimiwa Wabunge, maendeleo hayana chama sisi sote tunahitaji maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yaliyoelezwa katika tovuti ya *Boeing* ni sahihi katika mantiki ya kisoko maana bei iliyowekwa katika tovuti hiyo ambayo walisema Tanzania wamenunua ndege kwa pesa hizo ni sahihi. Ile bei iliyowekwa pale ni *list price*, ni bei ya ndege, lakini wakati wa kununua ndege kunakuwa na mazungumzo marefu. Pamoja na kuwekwa bei hiyo kwenye tovuti, mazungumzo marefu yalifanyika na tulipewa punguzo kubwa sana, Serikali ilipata bei nzuri. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu Serikali imenunua ndege mpya aina ya *Boeing 787-8 Dreamliner*, ndege ya kisasa na kwa bei nafuu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemaliza hilo la ndege, naomba sasa nijikite kwenye hoja ya Mheshimiwa ambaye alitaka kujua *Air Tanzania* kama tumeuza route zetu kwa South Afrika. *Route* za ndege haziuzwi ni mali ya nchi. *Route* za ndege zinapatikana kwa kuweka makubaliano ya nchi na nchi. Kwa hiyo, *route* zote za *Air Tanzania* bado ni mali ya Tanzania na wakati wowote tutaweza kuipa *Air Tanzania*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi navyozungumza na ninyi *Air Tanzania* inafanya tathmini ya njia zitakazoweza kuhudumiwa na ndege za masafa ya katni na masafa marefu. Njia hizo zitajumuisha zile zilizokuwa zikhudumiwa hapo zamani yaani njia ya kuendea Oman, Dubai, London, Entebbe, Nairobi, Johannesburg, Lusaka na Bujumbura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Mbunge alisema wenzetu wa *Kenya Airways* wameuza *route* yao kutoka Nairobi kwenda London sijui kwa dola milioni 20. Narudia tena *route* haiuzwi ni makubaliano ya nchi na nchi. Ninavyofikiria *Kenya Airways* walichowauzia *Oman Air* ni *slot* ya kuingia pale *Heathrow Airport* kwa sababu kuingia *Heathrow Airport* ni *very expensive*. Kwa kila sekunde tano *Heathrow Airport* kunaruka ndege. Walilolifanya wao ni kuzungumza na *Kenya Airways* wapate ile *slot*, lakini si kuwauzi *route*, si sahihi. Sisi tukitaka kwenda London, London kuna *Airport* tatu; *Heathrow Airport*, *City Airport* na *Luton Airport*. Hizi mbili kwa maana ya *City Airport* na *Luton* ni rahisi, bei yake sio kama *Heathrow*. Naomba kuwaambia Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwamba *ATCL* hawajauza *routes* na imejipanga kwenda *route* zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda unanikimbia lakini nizungumze tu lingine, Mheshimiwa Mbunge aliuliza kwa miaka kumi Mamlaka ya Usafiri wa Anga imekusanya kiasi gani na Zanzibar imepeleka kiasi gani? Mamlaka ya Usafiri wa Anga haikusanyi mapato, kazi yake kubwa ni kuangalia usalama wa nchi ya Tanzania. Mapato yanayokusanya na Mamlaka ya Anga yanatumiwa kwa ajili ya kununua vifaa mbalimbali vya kuangalia usalama wa anga letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008 Serikali ya Zanzibar kwa bahati mbaya sana iliamua kuchukua mapato yanayotokana na tozo za abiria kwa upande wa *Airport* ya Zanzibar, lakini Mamlaka ya Usafiri wa Anga haitakiwi kuipa Serikali ya Muungano wala Serikali ya Zanzibar. Jambo hili lipo kwenye sheria ya kuunda mamlaka hii kwa hiyo hakuna pesa yoyote kwa kipindi cha miaka kumi ambayo tumeipeleka Zanzibar sababu sheria hairuhusu hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa haraka haraka nijikite na hoja ya bandari. Kulikuwa na hoja kwamba taasisi zilizopo pale bandarini ziweze kufanya kazi saa 24. Tunavyozungumza taasisi mbalimbali zilizopo pale bandarini zinafanya kazi saa 24. Nachukua fursa hii kuwaomba wateja

wetu na mawakala wetu wa forodha kupata huduma bandarini wakati wowote ndani ya saa 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la gharama kuongezeka kutokana na VAT kwa huduma zinazotolewa kwa wakala wa mizigo inayosafirishwa kwenda nchi za jirani. Ushauri huu tumeuchukua, tunaufanya kazi na tutaupeleka Wizara ya Fedha ili uweze kufanyiwa kazi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya kupunguza tozo ya dola 23 ya Kimarekani kwa tani kwa mizigo wa shaba ambapo bandari nyingine shindani kwa mfano Durban zinatoza dola za Kimarekani 17.86. Ni kweli mizigo wa shaba hutozwa dola 23 kwa tani, hata hivyo tozo za Bandari za Dar es Salaam hufanyika kwa dola za Kimarekani wakati bandari ya Durban mizigo hutozwa kwa *rand* yaani *currency* ya South Africa. Hali hili husababisha gharama za bandari za Durban kuwa ndogo wakati sarafu hiyo inapokuwa dhaifu ikillinganishwa na dola hasa sasa hivi ambapo *exchange rate* dola moja ni *rand* 13.41.

Aidha, tozo kwa upande wa Bandari ya Dar es Salaam hupungua hadi kufikia dola 17 kutegemeana na kiasi cha mizigo na hali ya ushindani. Kwa vile hatuko *fixed* tunajaribu kuwa *flexible* na tunabadilika sana.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Nakuongeza dakika mbili lakini vilevile tujibu kuhusu *share* za Serikali ambazo ziko *Airtel*.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavoyojua Bandari ya Dar es Salaam ina changamoto kubwa kuhusu miundombinu, lakini tuna mradi ambao sasa tumejipanga kuhakikisha kwamba tunaboresha kina cha maji cha Bandari ya Dar es Salaam na pia kujenga gati mpya kwa ajili ya kuteremshia magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitakuwa na muda wa kwenda kwenye barabara lakini Mheshimiwa Naibu Waziri amezitaja nyingi. Waheshimiwa Wabunge hatutaweza kujibu kila kitu hapa muda hauwezi kuturuhusu lakini mjue tu kwamba maelezo na ushauri wenu hasa kwenye kuangalia sera ya barabara ya kuunganisha mikoa mbalimbali tumeichukua na tutaifanyia kazi kuhakikisha kwamba mikoa yote ya Tanzania inaunganishwa kwa barabara. Hatuwezi kuingia kwenye uchumi wa kati bila kuunganisha mikoa yetu yote na barabara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema kuwa bajeti ya Wizara yangu mwaka 2017/2018 ni bajeti ya kuanza kuweka mazingira ya uwekezaji kwenye sekta ya viwanda na kuinua uchumi wa nchi yetu kijumla ili uchumi wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2020/2025 uweze kufikiwa. Kama nilivyoliomba Bunge lako Tukufu mwanzo wa hotuba yangu ndivyo ninavyomalizia kwa kuwaomba tuunganishe nguvu zetu kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge katika kutekeleza malengo ya Wizara yangu. Kwa kufanya hivyo, nchi yetu itafikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2020/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri subiri kwanza, *share* za Serikali ziko *Airtel* zinafanya nini? *Airtel*/mpaka leo haijatoa faida kwa nini msizichukue mkazipeleka *TTCL*? (*Makof*)

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni Mwenyekiti ukiuliza swalii lazima nilijibu. Kwa heshima yako, tumelichukua wazo lako kuhusu *share* za Serikali ndani ya *Airtel*/na tunalifanyia kazi. Ni jambo ambalo tunatakiwa tufanye utafiti wa kina, tufanye mambo mengi ya kitaalam, siyo jambo ambalo naweza kutoa jawabu hapa kwa sababu jambo la *shares* watu ile ni *business* yao. Hata hivyo, tumelichukua na tutalifanyia kazi tu haina shida. (*Makof*)

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imeungwa mkono, Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 68 – Mawasiliano

Kif.1001 - *Administration and HR Management*Shs.1,716,521,000/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tayari nina orodha yenu, Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka ufanuzi kwenye mshahara wa Waziri kuhusu suala la reli hapa naona ni mawasiliano.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sakaya huu ndiyo mshahara wa Waziri, huko mbele hakuna mshahara wa Waziri.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati nachangia....

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hii Wizara ina mafungu matatu haina Wizara tatu. Kwa hiyo, kila mwenye hoja ikiwa ni ya reli, ndege, simu zote ni hapa, baada ya hapa hakuna tena mshahara wa Waziri.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye mchango wangu wa maandishi nilipenda Waziri atusaidie. Ndani ya Wilaya yetu ya Kaliua kwenye suala la reli pamoja na kwamba tunaipongeza Serekali inajenga reli lakini upande wa Kaliua wananchi wanaosafari kwa treni ni wachache sana kutokana na uchache wa mabehewa yanayotolewa. Kwa kituo cha Kaliua wananchi wanaosafiri kwa siku moja wakati wa treni inapita ni watu 15 tu wakati zaidi ya watu 100 wangependa kusafiri kwa treni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wakati alikuja Kaliua aliahidi kuongeza mabehewa lakini mpaka tunapoongea sasa hivi tatizo limeendelea kuwa kubwa kiasi kwamba tiketi ya treni sasa hivi inauzwa zaidi ya basi kutokana na kwamba wananchi wanaosafiri ni wengi na nafasi ni chache.

Naomba Serikali itusaidie mpango mkakati kuhakikisha kwamba wanaongeza mabehewa ili wananchi wa Kaliua waweze kusafiri vizuri kwa kutumia treni kwa sababu ndio usafiri rahisi lakini pia unachukua mizigo kwa wingi. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sakaya unajua kwenye mshahara na wewe ni Mbunge wa zamanii unatakiwa uzungumze masuala ya sera. Nitaruhusu Waziri alijibu kwa sababu linagusa watu wako, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nilikwenda kule na nilimuahidi ingawa tuna changamoto ya mabehewa, lakini tutajitahidi kuhakikisha tunampelekeea mabehewa. Vilevile kwa muda mrefu tumejipanga kuongeza kununua mabehewa mapya ambapo tutaweza kulimaliza kabisa tatizo hilo la mabehewa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ngwali.

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu siku ya Ijumaa nilizungumzia hasa kuhusu usajili wa meli za kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna meli ambazo zinasajiliwa na Serikali ya Zanzibar ambazo zimelitia doa Taifa hili. Mfano, meli za Iran 39 zilizoshajiliwa ambapo Iran ilikuwa imewekewa vikwazo na Umoja wa Mataifa kwa sababu ya vinu vyake vya *nuclear*, Serikali tukadhani ni bahati mbaya, wakaachia. Baadaye ikakamatwa meli nydingine katika maji ya Uingereza ambayo ilikuwa imekamatwa na *cocaine* tani tatu, Serikali ikanyamaza tukasema ni bahati mbaya. Ikakamatwa meli nydingine ya *Goldstar* katika maji ya Italy ikiwa na tani 30 za bangi, Serikali ikanyamaza kimya, tukasema bado ni bahati mbaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni zilikamatwa meli 45 za Korea Kaskazini ambayo imewekewa vikwazo na Umoja wa Mataifa. Kwa hiyo, Tanzania inapata taswira mbaya, watu wake wanaonekana ni wahalifu na hawafuati sheria. Waziri wa Mawasiliano yupo, Mwanasheria Mkuu yupo, Waziri wa Mambo ya Nje yupo, Waziri wa Sheria na Katiba yupo na Mawaziri wote wapo lakini hakuna majibu ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitapata jibu la uhakika leo nitazuia shilingi ya Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubali kwamba kumeshawahi kutokea changamoto kama hizo ambapo baadhi ya meli zilizokuwa zimesajiliwa Zanzibar ziliweza kuharibu taswira ya nchi yetu. Baada ya matukio hayo tukaja na mfumo ambao unatumika sasa ambapo meli ikisajiliwa Zanzibar kwanza inabidi tuione huku Dar es Salaam, tuna mfumo ambao sehemu zote za Muungano tunaweza kuona, kama meli tuna wasiwasi nayo moja kwa moja haiwezi

kusajiliwa. Tunaendelea kufanya hivyo kila siku, Zanzibar hawawezi kusajili meli bila *SUMATRA* kuziona. Kwa hiyo, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Watanzania kwamba tutasimamia mfumo huu ambao haupo Tanzania tu umeunganishwa mpaka na *International Marine Organization - IMO* kuhakikisha kwamba hizi meli ambazo zilikuwa zimekatazwa kutohana na sheria za Umoja wa Mataifa haziwezi kusajiliwa hapa Tanzania na kuharibu jina letu zuri la Tanzania. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ngwali.

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Waziri sehemu ndogo sana, lakini nachosema suala la kusajili meli za kimataifa ni la kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Zanzibar. Kwa mujibu wa *Maritime Transport Act* ya Zanzibar kifungu cha 8(1)(a) kinasema Zanzibar itasajili meli za kimataifa, kwa maana hiyo inavunja hata Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika orodha ya mambo ya Muungano kipengele cha 2 kinachosema kwamba Zanzibar hairuhusiwi kutunga sheria katika mambo ya Muungano. Sasa unapoweka sheria kwamba *international ship* unazisajili wewe maana yake ni kwamba unakwenda kinyume na utaratibu hata wa Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado sijaridhika na majibu ya Waziri nataka Waziri aniambie Serikali ina msimamo gani katika jambo hili?

MWENYEKITI: Toa hoja.

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja tujadili.

MWENYEKITI: Haya, watakaochangia hoja hii ni Mheshimiwa Dkt. Selemain, Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Chumi, Mheshimiwa Khatib, Mheshimiwa Manyanya, Mheshimiwa AG atakuwa wa mwisho, Mheshimiwa Khamis, watu wa meli mmekwisha? Haya Mheshimiwa Dkt. Suleiman.

MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kuungana au namuunga mkono Mheshimiwa Ngwali hoja yake, ni hoja ya msingi sana. Kwa sababu ikiwa meli zinasajiliwa katika nchi, na majambazi ambao wanahusika na kuuza dawa za kulevyia, hii ni dhambi kubwa sana ambayo haiwezi kusamehewa, inachafua taswira ya nchi yetu, si Zanzibar pekee bali inaichafua Tanzania nzima. Kwa hali hiyo mtu yejote ambaye ana akili hawezi akaliunga mkono suala hilo na hasa ukiangalia kwamba suala hili ni uvunjaji wa Katiba ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ngwali. (*Makofii*)

MWENYEKTI: Ahsante. Mheshimiwa Masoud jiandae Mheshimiwa Manyanya.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kaeni makini kweli kwa hilo, naanza sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali Mbunge makini. Naunga mkono kwa sababu zifuatazo; kama kuna meli ambazo zimekamatwa na cocaine, kuna meli ambazo zimekamatwa na bangi, lakini hivi karibuni meli 45, mwaka 2016 meli hizi nazo zikasajiliwa kinyume na taswira, kwamba meli hizi Korea Kaskazini tayari ilikwishawekewa vikwazo na Umoja wa Mataifa lakini sisi ina maana kwamba hatuheshimu hata ile mipaka ya Umoja wa Mataifa? Hii ni kuitia doa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuambie baadhi ya meli katika meli 45 hizo aibu ambayo ipo na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wakati wako ukifika jambo hili kaa mkao wa kula. Angalia meli zifuatazo, *Ji Shun 2, Hong Xin 9, Jin Heng Hai, Jin Bai Hai 3, New Fu Shun na Towg De mna IMO number* na kila kitu. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni msululu mzima wa aibu tulioipata huko nje kwenye sura za Kimataifa ninyi

mnakaa mnataka kulindana lindana nyie wenyewe, hili halilindiki. Hata ukienda kwenye diplomasia za kiuchumi jamani hili ni baya kweli, Mheshimiwa Waziri Mbarawa aibu hii utuambie vipi tutatoka nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii, Serikali lazima itoe jibu mahsus tujue tunakwenda wapi. Nashukuru sana. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Manyanya, jiandae Chumi.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana mimi nitaungana nae mkono kwa sehemu ndogo tu kwamba suala la meli zinazosajiliwa, kutiliwa mkazo na kuhakikisha kwamba zinakuwa ni zile ambazo zinafanya shughuli zake kwa taratibu na sheria ndiyo suala la msingi. Lakini kusema kwamba wanaosajili ni majambazi badala ya kusema wale wenye mali zile ndio majambazi naona hilo halijawa sawa.

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio*)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili...

MWENYEKITI: Waheshimiwa muacheni ajibu, ninyi mmesema watu wamekaa kimya. Na leo tumekubaliana wote familia moja humu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kweli kabisa nizamu ni kitu cha bure na naomba mzingatie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba suala la meli zinazosajiliwa kuhakikisha kwamba zinaendana kwa mujibu sheria ni suala la msingi lakini hata hivi karibuni tu, mwaka 2015 tulipitisha Sheria ya Dawa za Kulevyo ambayo sasa tunaangalia meli zote, ziwe za ndani ziwe za kimataifa, kuhakikisha kwamba zinaondokana na shughuli zinazohusiana na dawa za kulevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile masuala haya yaliyozungumzwa ya Muungano ni masuala ambayo kimsingi wote tunaona umuhimu wake na ndio maana wakati wa utungaji wa Katiba iliyokuwa inapendekezwa watu wote ambao wana nia njema na nchi hii wasingewenza kutoka.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kupata nafasi. Hoja ya Mheshimiwa Ngwali kimsingi tunapoangalia mahusiano ya kimataifa na *image* ya Taifa kwa ujumla ni hoja ya msingi, ni hoja ambayo siyo ya kupuuza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nishauri pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri aliyyoatoa kama taratibu zinaruhusu Serikali ifanye *review* ya meli zote ambazo zimesajiliwa na ikibidi kama taratibu zinaruhusu usajili huo uftutwe na uanze upya, lakini *all in all* ni jambo la msingi na nimuombe Mheshimiwa Ngwali kama ataridhia ili kuipa Serikali nafasi arejeshe shilingi lakini umakini uwe ni mkubwa kwa sababu jambo hili ki ukweli linaharibu *image* ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Khatib.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ngwali, halafu nikuambie kwamba mimi ni muumini wa Muungano kweli kweli, na juzi nilimsikia Mheshimiwa Rais akisema kwamba atakayeuchezza na kujaribu kuuning'nia Muungano huu atavunjika yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nionavyo hawa viongozi waandamizi kwa mujibu nilivyomsikia mtoa hoja akisema viongozi waandamizi wa Zanzibar wanahuksika na uchafu huu,

hawa ndio watakaovunja Muungano. Tunahitaji bendera ya Tanzania ipepewe na akina Simbu walete hapa sifa kwa Tanzania, isipepewe kwa wauza dawa za kulevyta, ni aibu iliyopitiliza kwamba jambo hili la kwamba bendera ya Tanzania, *image* ya Watanzania, *passport* ya Matanzania anapoonekana popote sasa hivi anaingizwa katika wigo huu. Hii ni aibu na Wabunge wote wenye nia njema tusikubali kisingizio cha kwamba wanalinda Muungano waweze kufanya watakavyo wao, ni bora jinamizi la Muungano liniangukie, sikubaliani nao. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Khamis, jiandae Mheshimiwa AG.

MHE. ALI SALIM KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Ngwali kwa kweli ni jambo la kusikitisha kwa sababu imani yangu naamini kwamba Waziri na Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano inafahamu mchezo huu ambao unafanyika na suala hili bado inaonekana kwamba ni jambo la kawaida, lakini pia usajili wa meli huo uliosajiliwa hayo manufaa ya hayo mapato yanayopatikana kwa ajili ya meli hizo wala hayaendi Serikalini moja kwa moja. Lakini hadi leo hii, Katibu Mkuu wa hii Wizara yupo kazini anafanya kazi, wala hajaulizwa kitu chochote, wala hakuna maelezo yoyote, imekaa tu kama hii si nchi yenye mamlaka kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni hatua gani ambazo amezichukua kwa sababu jambo hili wanalifahamu jinsi ambavyo linaendelea na ushahidi upo wa kutosha atuambie hapa hawa watu wamechukuliwa hatua gani kwa ajili ya kulitia doa Taifa letu? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa AG.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hatuna ushahidi kwamba kweli wanaoidhinisha usajili au wanaonufaika na usajili wa hizi meli ni viongozi waandamizi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

na Bunge hili sio mamlaka ya nidhamu kwa viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sasa hoja ya Mheshimiwa Ngwali ni ya msingi sana kwamba, usajili wowote ambao unawezesha tukafikia hatua tukasajili, kwa sababu katika Jumuiya ya Kimataifa hakuna Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wala Serikali ya Tanganyika ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria, meli ambayo inashukiwa kwa uhalifu, ili ikamatwe *Attorney General* ndiye anayeidhinisha na hiyo meli anayoisema Mheshimiwa Ngwali nilliidhinisha mimi ikakamatwa, na mwezi wa tatu nimeidhinisha meli nydingine nayo ikakamatwa. Sasa Waziri ameелеza, kwamba tumbaini hili tatizo, Serikali hizi mbili zitakaa, lakini kubwa pia amelisema Waziri kwamba tayari Serikali wameweka utaratibu kwamba wanajiridhisha, Zanzibar halweze sasa ili kukwepa huo udhaifu uliojitokeza wana-*verify* ili kusudi Taifa letu lisije likapata sifa mbaya kwenye Jumuiya ya Kimataifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo na kwa sababu kama alivyoseme Mheshimiwa Ngwali liko kwenye Sheria ya Serikali na Bunge ambayo imetungwa inayotumika Zanzibar, Serikali ya Jamhuri haiwezi kulazimisha tu kwamba kafute ile, ni masuala ya kuzungumza na tumeanza kuchukua hatua haya ndiyo mambo pia tunazungumza kwenye Kamati ile ya masuala ya Muungano. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kushauri kwamba, Mheshimiwa Ngwali maadam Serikali inalitambua hili tatizo na inachukua hatua amrudishie shilingi Mheshimiwa Waziri, haya yanafanyiwa kazi kwa sababu sisi wote hatutaki kuaibika mbele ya Jumuiya ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikubaliane na Mheshimiwa Ngwali hizo meli walizosema, lakini yule Wakala kwa sababu Zanzibar walitumia Wakala ambaye anaitwa Filtex yule

wakala mwenyewe amefutwa kabisa, hafanyi kazi yoyote ya usajili kwa meli za Zanzibar na meli zote zile zimefutwa na sasa hivi Umoja wa Mataifa hauna matatizo na Zanzibar, Ubalozi wa Korea ambao walikuwa wanalalamika sana Korea Kusini hauna matatizo na Tanzania, Wamarekani hawana matatizo na Tanzania na kikitokea meli yoyote ambayo ina matatizo tunapewa taarifa na tunaifuta moja kwa moja. Mtambo wetu ama mfumo wetu ni mzuri na tutaendelea kuusimamia kuhakikisha kwamba hizi meli hizo hazisajiliwi tena huko Zanzibar. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Ngwali hoja yako ni ya msingi inakubalika na Serikali imetoa majibu sahihi japo sasa hakuna tena matatizo. Kwa hiyo, ni kumrudishia tu shilingi yake kwa sababu tukipiga kura itakuwa hailete ile hoja ya kuondoka nayo ili kuibana Serikali, ikitokea tena tutauliza imekuwaje.

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba jambo hili lipo na AG kakiri kwamba jambo hili lipo basi mimi nitamrudishia shilingi yake lakini niseme Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge ikutane ijadili jambo hili. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Ngonyani Stephen, Profesa Maji Marefu.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kwa jinsi Waziri alivyokuwa anaeleza, lakini mimi nimekuwa na llani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilichangia hapa kwa maandishi pamoja na kuchangia kwa kutamka, mimi ningetaka kujua Serikali katika utaratibu wake wote wa reli wameongea masuala ya reli na watu wamewaelewa, lakini mpaka sasa hivi sijajua utaratibu wa reli ya kutoka Tanga kwenda Moshi kuititia Arusha kwenda mpaka Musoma imetengewa kiasi gani cha fedha, na itaanza lini kufanyiwa marekebisho, kama vile ilivyofanyiwa reli ya katika na kuwekwa jiwe la msingi pale Dar es Salaam? Kinyume cha hapo

nisipopata maneno mazuri kutoka kwa Waziri, nashika mshahara wake mpaka anihakikishie kwamba Serikali imetenga pesa kiasi gani kwa reli ya Tanga - Moshi - Arusha mpaka Musoma. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemuelewa Mheshimiwa Stephen Ngonyani ama Profesa Maji Marefu na hoja yake nimeielewa. Lakini nadhani ambacho ningependa akielewe vilevile kwa upande wetu ni kwamba reli ya kutoka Tanga hadi Musoma ni moja kati ya vipaumbele vyetu ndani ya Serikali. Na kwa sasa kipande hicho kinafanyiwa upembuzi yakinifu, na kwa vyovyote vile hatungeweza kuanza kutenga fedha kabla kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina haijakkamilika. Kwa hiyo, nadhani amewaalsha mno, asubiri kazi hii ya upembuzi yakinifu ikamiliike, aje aone Serikali inafanya kitu gani katika reli hii. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maji Marefu.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, haya waliyoyaweka ndani ya llani ya Uchaguzi ya mwaka 2010/2015, 2015/2020 basi wayaondoe kwa sababu toka mwaka 2010 reli ya Tanga iliwekwa kipaumbele kwamba itatengewa kiwango safi na sio kwamba unatafuta reli nyingine, reli ya zamani ipo, sehemu ya kupita reli mpya ipo, wenzetu wanapitisha kando ya reli ya zamani, wenzetu wa TAZARA wanapitisha reli ya kati na watu wamefanya upembuzi na sasa hivi reli za wenzetu zinapitika, Tanga ilikuwa inapitika hata reli ya mizigo, leo tunasema kwamba hatuwezi kutenga pesa. Hamuoni kwamba hamtutendei haki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashika shilingi nataka mpaka waniambie Serikali wametenga kiasi gani kwa reli ya Tanga - Moshi - Arusha na Musoma. Natoa hoja Bungeni niungwe mkono. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Adadi mtu wa Tanga, Mheshimiwa Japhary inakuja Moshi huko, Mheshimiwa Shangazi, Mheshimiwa Boni, mnatosha jamani, mnatosha tayari. Mheshimiwa Adadi.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kupata nafasi naunga mkono hoja ya Profesa Maji Marefu. *(Makofii)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli hii ya Tanga - Arusha mpaka Musoma ni reli ya siku nyingi sana, na ni reli ambayo ukichukulia maanani sasa hivi tumepata bomba la mafuta Tanga na tuna bandari Tanga, sasa na sisi tulitaka tupate hii *bullet train*, tulitaka tupate hii *train* ya kisasa, sasa najua kwamba gharama kubwa imekwenda kwenye reli ya katil, lakini ni muhimu pia waangalie reli hii ili ziweze kwenda sambamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshukuru sana kama Mheshimiwa Waziri angefikiria aweze kuangalia uwezekano wa kutenga hata hela kidogo, unajua upembuzi yakinifu ni mwanzo, lakini ni vizuri pia akataja *amount* ambazo ameziweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana Mwenyekiti. *(Makofii)*

MWENYEKITI: Ahsante Waheshimiwa, naongeza muda, naongeza nusu saa kwa mujibu wa Kanuni. Tunakwenda kwa Mheshimiwa Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi nimesimama kuunga hoja ya Ndugu yangu Profesa Maji Marefu kwamba tumekuwa tukikaa kwenye bajeti tunatenga kuonyesha kwamba kuna dhamira ya dhati ya kujenga hii reli ya Tanga - Arusha - Musoma. Mwaka 2015/2016 Serikali tulitenga shilingi bilioni 5.2 kwa ajili ya hii reli, lakini hazikuweza kutoka hata senti tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza mwaka huu wametenga shilingi bilioni moja, sasa naunga hoja mkono Serikali ituambie ni lini itatoa kipaumbele kwenye hii reli na kuwekeza fedha nyingi ambazo zitaenda kurahisisha sio tu usafirishaji bali itaenda kukuza uchumi wa haya maeneo kwa kuleta hii reli. Kwa hiyo, naunga hoja mkono ya Profesa Maji Marefu mtueleze ni lini mtawekeza hela nyingi kwenye hii reli. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Boni.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante na mimi naunga mkono hoja ya Profesa Maji Marefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme tu nikiwa mdogo mwaka 1975 Mheshimiwa Wasira akiwa Mkuu wa Mkoa wa Mara, akaanza kueleza watu namna gani reli ya kutoka Tanga kuja Musoma itajengwa, mwaka 1975 sijui niko darasa la ngapi hivi, toka muda wote huo mpaka leo tunapewa hadithi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba anafanya kazi nzuri, lakini ni vizuri mkiangalia ukanda wa maeneo unaendaje, hii Mikoa ya Tanga, Mikoa ya Musoma, Mikoa ya Arusha inaenda kufa, kuna maeneo mengine ukitazama vizuri yanaenda kufa, hakuna kitu kinaendelea huku. Miaka nenda rudi ni ahadi tu, upembuzi yakinifu umekuwa ni hadithi miaka nenda rudi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukubaliane leo kwamba hii reli itakuwepo? Kwa sababu kuna mambo mengine hapa Bungeni tunakubaliana kwamba sasa tutoe bajeti hapa tuongeze hapa, hili tukubaliane kwamba reli itakuwepo au haitakuwepo? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jafo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi

naomba nichangie hapo ni kwamba mimi nimeelewa dhamira nzuri ya Mheshimiwa Ngonyani ya suala zima la reli na bahati nzuri amefanya *reference* katika llani ya Chama cha Mapinduzi na hili nikijua wazi llani hii ni utekelezaji wa miaka hii mitano tuliyokuwa nayo ya mwaka 2015 - 2020 na kwa vile Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana amesema wazi kwamba, hivi sasa upembizi yakinifu sasa unaendelea, imani yangu kubwa ni kwamba *commitment* ya Chama cha Mapinduzi katika utekelezaji wa llani yake katika miaka hii mitano jambo hilo litatekelezeza. Ni jukumu letu na sisi Waheshimiwa Wabunge tuko humu ndani na dhamira ni nzuri katika ukanda ule kwa sababu suala la bomba la gesi na uchumi wa maendeleo na suala zima viwanda ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Mheshimiwa Ngonyani akuballane na Mheshimiwa Waziri kwamba jambo hili liko katika utekelezaji na kwa vile Serikali imeonesha dhamira katika suala zima la Sekta ya anga, ujenzi wa reli na miundombinu na hili litafanyika mwisho wa siku ni kwamba *commitment* ya Serikali itakuwa kote uko ambako wameweza kulitekeleza kwa hiyo naomba Mheshimiwa Ngonyani uliridhie kwamba *commitment* ya Mheshimiwa Waziri kwa vile upembizi yakinifu unaenda kufanyika kwa kina nini kitafanyika.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Japhary, jiandae Mheshimiwa Shangazi.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, pamoja na kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu na najua kwamba kuna dhamira ya kujenga hiyo reli ya Tanga mpaka Musoma na najua vikwazo vinavyosababisha kwa sasa tusifikie hapo, lakini nilikuwa naomba sana kuishauri Serikali ili kutimiza hiyo azma ya Mheshimiwa Ngonyani na umuhimu ya ile reli ya Tanga - Musoma ni vizuri basi kwa sasa tuone haja ya kutumia *PPP* kwa ajili ya kujenga ile reli kwa maana ya kutafuta fedha, ndiyo yalikuwa maoni yangu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Shangazi, jiandae Mheshimiwa Mbarouk, atamalizia Mheshimiwa Laizer.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante na mimi naunga mkono hoja ya Profesa Maji Marefu kwamba hii reli ilikuwa inapigwa danadana siku nyingi na lakini tu niseme kwamba wakati huu sasa ni wakati muafaka zaidi kwa sababu Taifa la Sudan Kusini limejumuishwa katika Jumuiya ya Nchi za Afrika Mashariki. Kwa hiyo, uwepo wa reli hii utakwenda kusaidia pia kupeleka mizigo nchi ya Uganda ambayo tayari tuna bomba lakini pia kufufua, kutengeneza mashirikiano mapya ya kiuchumi na Taifa la Sudan Kusini. Kwa hiyo tunasema Tanga kunani? Hii reli ndiyo ya kwanza kujengwa na wakoloni wa Kijerumanii kwa nini leo inakuwa ya mwisho? Tunaomba Serikali itoe *commitment*.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mbarouk tunamalizia na Mheshimiwa Laizer.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Ngonyani, lakini vilevile niikumbushe Serikali kwa maana ya kwamba Tanga inarudi katika enzi yake ya viwanda, sasa hivi pia kuna Kampuni ya *GBP* ambayo mafuta ya Mikoa ya Musoma, Kilimanjaro na Arusha yanashushwa Tanga. Lakini sio hivyo, kuna viwanda vya *cement* vinavyotaka kujengwa Tanga, sasa ikiwa tutakuwa tuna ujenzi au reli ile ile ya zamana itakuwa hamkututendea haki. Tunachoomba tunataka mtuambie leo hapa reli ya Tanga - Kilimanjaro - Arusha hadi Musoma itajengwa nayo katika kiwango cha *standard gauge* au vipi kwa sababu tunapitisha bajeti hapa ni Waziri kusema tu tuongeze kutoka bilioni moja upembuzi yakinifu twende kwenye bilioni tano ujenzi wa reli uanze.

MWENYEKITI: Ahsante, ahsante, Mheshimiwa Laizer.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu kwamba reli hii ni muhimu sana na kwa kweli maendeleo ni wivu na sisi tunaona wivu tunavyosikia kuna maeneo mengine wanajenga reli lakini hii

ya muhimu kwa kiwango hiki haijengwi. Lakini kinachotusikisha kabisa mwaka 2015/2016 ilitengewa bilioni tano haijatolewa hata senti tano, mwaka huu 2016/2017 haikutengewa kabisa, mwaka huu mnasema mtaitengea bilioni moja ya kufanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naona kabisa kwamba hakuna dhamira ya kweli kwa sababu kama miaka ya nyuma ilipita ukaitengea bilioni tano leo unaitengea bilioni moja maana yake nini, utaifanyia kazi gani. Na kule mnasema kabisa kuna bomba la mafuta linajengwa Tanga pale Engaruka kuna magadi ya kutosha na tunashangaa kama Waziri wa Viwanda hatasimama kuitetea hii reli, asipoisimamia hii reli na mimi kule kwenye eneo la kukaa kwa ajili ya kujenga kiwanda...

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwijage Waziri wa Viwanda.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia nafasi na nipende kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge kama alivyosema Mheshimiwa Laizer mdau mkuu na namba moja wa reli ya Tanga kwenda Arusha na Musoma ni mimi. Engaruka tutazalisha magadi tani milioni nne kwa mwaka, huwezi kuzisafirisha kwa malori. Kwa hiyo, mtulie ile *demand* yenye we italazimisha reli kuwepo, pesa iliyotengwa ya upembizi yakinifu itafanya kazi yake na niwaeleze katika kutafuta wawekezaji wa Engaruka mojawapo ya mambo wanayoyaangalia ni miundombinu ya kusafirisha malighafi. Kwa hiyo chonde chonde mumpe shilingi yake Mheshimiwa Waziri aendelee na kazi lakini reli ya kwetu Tanga ni lazima.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mtu anayebisha reli ya kutoka Tanga - Arusha mpaka Musoma ni muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu, bila reli hatuwezi kuwa na viwanda imara. Kwenye bajeti yetu ya mwaka huu

tumetenga shilingi billioni moja kwa ajili ya kukamilisha *feasibility study*. Na huwezi ukajenga reli bila au chochote bila kuweka kufanya *feasibility study* huwezi kujua reli hiyo ita-*cost* shilingi ngapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa atuachie shilingi ili tukafanye kazi hiyo kuhakikisha kwamba tunafanya *feasibility study* halafu tuanze kupanga pesa kwa ajili ya kujenga reli ya *standard gauge*.

MWENYEKITI: Hoja yao mwaka jana mlitenga bilioni tano hamkutoa, mwaka huu, ngoja, ngoja, ngoja! Hoja ya Mheshimiwa Mbunge anasema mwaka jana mmetenga shilingi bilioni tano hamkutao, mwaka huu mmeweka bilioni moja wanaona kama vile bado haitoshi kwa hiyo kazi. Cha msingi hapa Mheshimiwa Ngonyani hii ni hoja mahsus, kama Kiti tunaichukua hoja hii tunapeleka Kamati ya Bajeti na Mwenyekiti yuko hapa ili Kamati ya Bajeti itaiita Serikali na wadau wa maeneo hayo kuja kukaa kufanya *engagement* na Serikali kujua sasa *commitment* ya Serikali ni ipi. Kwa maneno hayo nakuomba umrudishie shilingi yake hali yenewe unaoina sasa hivi. (*Makof/Kicheko*)

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina tatizo na Wizara hii wala sina tatizo na Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu wake na Makatibu wake Wakuu wanafanya kazi nzuri. Kwa maneno hao uliyoniambia na aliyoongea Mheshimiwa Waziri namrudishia shilingi. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mchengerwa.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nitambue mchango wa *macampions* wa uchumi nchini ambapo wao walijitolea nyakati zile za uhuru mwaka 1961 kujenga uchumi wa nchi yetu kwa kuboresha miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kubwa ni kwamba nimeona kabisa Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ukurasa wa 252 amekiuka Ibara ya 2(2) ya Katiba kwa

kuligawa eneo la Rufiji kuwa Kibiti na kati ya barabara hizo ni barabara ya Nyamwage -Utete kuifanya barabara hii kuwa ni barabara ya Kibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 4 cha Sheria ya Uanzishwaji wa Mikoa na Wilaya, Sura ya 397 ni Rais pekee mwenye mamlaka ya kufanya hayo. Naomba taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri aniambie kwamba, je, Wizara yake ilidhamiria kuigawa Wilaya ya Rufiji kuwa Kibiti au ni mapungufu ambayo yalifanywa na watendaji wake?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe radhi Mheshimiwa Mchengerwa, hilo ni kosa la kiufundi ukikuta katika Wilaya zile ambazo zimegawanyika mara nyingi watu wa *TANROADS* wanatumia ramani zile ambazo wakati mwingine yale marekebisho ya Mikoa na Wilaya hayajaingizwa. Mradi barabara imetajwa kama ambavyo ilivyo sidhani kama itakwenda Kibiti, kama Kibiti sasa hivi ni tofauti na Rufiji. Kwa hiyo, mimi nadhani ni kosa la kiufundi na linatokana na ramani tunazozitumia na ramani ambazo zingine bado hazizingatii Wilaya mpya zilizoanzishwa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mchengerwa hukutoa shilingi imekwisha biashara yako.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Nilitoa Mheshimiwa.

MWENYEKITI: Halafu na jibu hili ni *technical*, we umeuliza swali la msingi, swali *very pertinent* na yeye jibu lake ameomba radhi ni makosa ambayo yatarekebishwa.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nikushukuru lakini pia nimuombe Mheshimiwa Waziri atambue kwamba Kibiti na Rufiji ni ndugu lakini pia Rufiji ilianzishwa toka nyakati za mkoloni ni Wilaya ya sita wakati wa mkoloni nimuombe Mheshimiwa Waziri sasa

alizungumzie hili suala la barabara ya Nyamwage - Utete ili tuweze kupata...

MWENYEKITI: Aaah, sasa hiyo mtakutana kantini baadaye. Mheshimiwa Mipata. (*Kicheko*)

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi, katika mchango wangu wa maandishi niliweze kuzungumza juu ya umuhimu wa mawasiliano ya simu katika mipaka ya nchi yetu, ili kuimarisha usalama wa nchi yetu hasa katika mipaka mirefu ya Ziwa Tanganyika ambapo nchi yetu imepakana na nchi ambazo hazijatengamaa sana kiusalama kule. Nikatoa mfano wa kata moja na tarafa ya Wampembe na kata ya Kala ambapo mara nydingi sana kama Mbunge wa maeneo hayo nimikuwa nikiwasiliana na Waziri kumwandikia barua Katibu Mkuu wake na kwenda Ofisiini mara kwa mara lakini sijapata majibu yanayoridhisha na mpaka sasa mawasiliano yamebaki pekee maeneo hayo hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikasema kwa sababu katika ufanuzi wa Waziri hajanijibu naomba sasa anipe maelezo ya kutosha asiponipa maelezo ya kutosha nitaweza kuchukua shilingi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa hilo swali lako sio la kisera, ni *specific* kwenye eneo lako.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maeneo ya mpakani kunahitaji usalama mkubwa sana katika suala zima la usalama na siku zote tumekuwa tunazungumza hapa kama ni sera yetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewahi kweli kuzungumza na Mheshimiwa Mipata kwa muda mara mbili, mara tatu hivi kweli tuna changamoto kubwa katika maeneo ya mpakani kuhusu mawasiliano na maeneo ya mpakani ni muhimu sana

katika ulinzi wa nchi yetu. Sasa hivi tuna mpango maalum ambao tunautayarisha kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ambao tutayachukua maeneo yote ya mpakani ya nchi yetu kuhakikisha tunawapelekea mawasiliano haraka iwezekanavyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mipata jibu hilo wana *commitment* ya Serikali ndiyo hiyo.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nitaafatilia kwa makini zaidi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Oscar Mukasa.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru suala langu liko kwenye ile *distribution* ya *road fund* 70% barabara kuu; 30% barabara za Wilaya, lakini kwa sababu shughuli za uchumi ziko vijijini, vitongojini kabisa na ile 30% inaishia kutengeneza barabara za ngazi ya kata na vijiji vichache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni namna gani Waziri anatupa *comfort kwamba* tunaweza kufanya *reallocation* ama *mfumo maalum* *special agency* au *special arrangement* ya kufanya barabara za vitongojini ziflike ili mihogo, mahindi, mchele vinavyolimwa huko vitongojini Biharamulo viweze kuondoka kule ili wakulima wetu washiriki kwenye uchumi?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunakubali kuna mchango huo yaani mgawanyo huo wa 30% na 70%. Kwa kweli 70% zinazopelekwa kwenye *TANROADS* ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara kubwa pamoja na vivuko. Lakini 80% zinazokwenda huko kwa bahati mbaya hazifanyi kazi ambayo pengine haifanyiki kazi nzuri kwa sababu ambazo pengine si rahisi kuzifahamu, lakini tunalolifanya kama Serikali ambalo tutalifanya tutaendelea kuzisimamia hiyo 30%

inayopelekwa huko iweze kufanya kazi inayokusudiwa kwa sababu unaweza kupeleka 30% na hata kazi yenye we isiweze kufanyika. Mimi naamini kama tutaipeleka 30% kwa muda unaotakiwa na tukaweza kuisimamia vizuri ninaamini tutapata matokeo mazuri.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dau.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi nasimama kwa mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Nchi yetu imejaaliwa kuwa na visiwa vingi sana kwenye bahari na maziwa na ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba usafiri katika maeneo hayo unakuwa ni wa uhakika na wa salama. Lakini kwa bahati mbaya sana jukumu hili Serikali imekuwa hailifanyi ipasavyo katika baadhi ya maeneo. Kwa mfano, katika kisiwa cha Mafia ambacho kina wakazi takribani 70,000 mpaka hii leo wananchi wa Mafia hawana usafiri wa boti wa uhakika. Sasa nilikuwa nataka nipate maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, ni lini sasa Serikali itakuja na mkakati?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Dau ni ya msingi, ni hoja nzito mimi mwenyewe nimefika Mafia, kona moja ya Kaskazini hadi ya Kusini ni hoja nzito, nimhakikishie tu Mheshimiwa Dau yale ambayo tumeyaahidi tutayatekeleza. Hatua inayofanywa sasa kwanza ni kupitia ile njia ambayo kuwe na uhakika njia ya uhakika ya kupita kivuko au meli tuijue, lakini kubwa lingine ni kuhakikisha sehemu hizi mbili ni moja tu kule Mafia ndio kumejengwa gati, lakini kule ambako inatakiwa iunge na bara huku ambako ni Kibiti haijajengwa gati ya Nyamisati, tumeliongea hili na nimhakikishie kwamba gati ya Nyamisati na unafahamu kwamba inaendelea iko katika hatua nzuri. Lakini vilevile suala la uwanja wa ndege unayafahamu haya yote tumeongea.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri inatosha.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mimi nikuombe...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri inatosha, anataka masuala ya meli sasa ndege za nini tena. Mheshimiwa Maufi. (*Kicheko*)

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante mimi ninakuja kwa shilingi ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ye ye anafahamu wazi kwamba Halmashauri zetu uwezo wa kifedha ni mdogo na daima Wabunge wote wakismama wanaomba barabara zao ziende *TANROADS* na sisi Mkao wa Rukwa tukiwa ni wamojawapo lakini kuna kigugumizi cha barabara hizi kutokuchukuliwa na *TANROADS*. Barabara ya Kitosi - Wampembe, barabara ya Nkana - Nkara...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maufi kwa vile wewe bado ni mgeni ungezungukazunguka barabara ya Dodoma - Kilosa wapi halafu baadaye ungerudi. Sasa unaelekea moja kwa moja kwenye *issue* ambayo sio ya sera.

MHE. SILAFU J. MAUFI Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuja mpaka huko lakini ninasema hivi ya kwamba ni bora nianze huku kabla nikifika huko nikapoteza muda wangu na wewe ukaniambia nisimame, ndio maana nimeifanya hivyo moja kwa moja.

Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze kwamba hivi kuna kigugumizi gani kwa Serikali kuzichukua barabara hizi kwa *TANROADS* ili ziweze kuwa imara na akina mama zangu waweze kuondokana na vifo vinavyowakabili hivi sasa? (*Makofj*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu suala la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuna maombi mengi kwa ajili ya kuzipandisha hadhi barabara mbalimbali, lakini kupandisha hadhi barabara ni pesa, tulikuwa tungalifurahi sana tungalikuwa na bajeti kubwa barabara zote za Tanzania tukaweza kuzipandisha hadhi, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuna vigezo maalumu ambavyo tunavifuata. Sasa bila ya kuvikidhi hivyo vigezo hivyo inakuwa ni vigumu sisi kuipandisha hadhi barabara husika. Lakini tutaongea na Mheshimiwa Mbunge nizungumze naye kuhusu barabara aliyoitaja tuangalie kama imekidhi vigezo *then* tutafanya utaratibu unaohusika. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, muhimu sana, Mheshimiwa Laizer.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na wenzangu katika jambo hili la upelekaji wa fedha za miradi ya maendeleo katika Halmashauri zetu, tunajua kabisa kwamba Halmashauri katika mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Barabara zimetengewa 30% tu lakini ni mfuko huu peke yake ambao ni *reinforced* kwamba Serikali fedha zake zinalindwa, lakini tatizo ni kwamba fedha zakehaziendi tunataka majibu ya Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Laizer hebu kaa kwanza, *issue* yako hiyo imeshajibowi na...

MBUNGE FULANI: Bado!

MWENYEKITI: Aaah! Imeulizwa kule na nani, *no, no, no, no!* Mimi nasimamia kanuni hapa.

Mheshimiwa Paresso sikiliza, suala ambalo limeshatolewa majibu na Serikali haliwezi tena likaja kwa njia hiyo hiyo. Tunaendelea Mheshimiwa Sannda.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niipongeze Serikali kwa kazi nzuri ya ujenzi unaoendelea wa barabara nchi nzima, lakini nataka kusema

jambo moja, katika ujenzi huu kuna jambo ambalo halifanywi vizuri kuhusiana na alama za barabarani pale ambapo ujenzi unaendelea. Hali hiyo inasababisha usumbufu mkubwa maeneo mengine imesababisha ajali, mfano hii barabara ya kutoka Dodoma kwenda mpaka Babati ni kilometra chache sana zimebaki, lakini hakuna alama kabisa pale. Unakwenda unatembea mpaka kilometra tano ndiyo inabidi urudi nyuma. Wakati mwagine na ajali zimetokea watu wamepoteza maisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tena nitashika mshahara wako kama sitaridhishwa na maeleo. Nataja kujua kuna mikakati na utaratibu gani wa kuhakikisha yale masharti ya mikataba yanasmamiwa na yanatekelezwa kwa hawa wakandarasi kuweka alama za barabarani? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zote tunazozilenga katika mkataba lazima kuna mpango wa kuweka alama za barabarani. Barabara anayoizungumzia ni kutoka Dodoma mpaka Babati bado iko katika hatua za ujenzi, lakini mara itakapomalizika alama zote za barabarani zitawekwa na ni sehemu ya mkataba wa barabara yoyote inayojengwa hapa Tanzania. Ni muhimu kabisa kuhakikisha kwamba barabara zetu zote zina alama kwa sababu hiyo itapunguza sana ajali na mambo mengine ambayo yanatokea barabarani.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sannda, barabara bado iko kwenye *warranty* haijawkisha.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Mheshimiwa Waziri hatujaelewana kidogo. Najua baada ya kumaliza barabara, wakati wa ujenzi wa barabara tunatakiwa tuoneshwe kuna *diversion* kuna nini, usije ukaenda mahali kilometra tano halafu inabidi urudi nyuma kuchepuka tena. Ndiyo ninachozungumzia, alama za barabarani wakati wa ujenzi, sio baada ya ujenzi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kubali tu hilo.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Mheshimiwa Mwenyekiti tunakubaliana nae kwamba barabara ikijengwa lazima kuwe na alama hizo, *diversion* na nini vinginevyo itakuwa ni hatari. Haina shida. Tunakubaliana na Mheshimiwa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sannda umeridhika nakushukuru. Mheshimiwa Hasunga.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia juu ya umuhimu wa reli ya *TAZARA* na naomba nizungumzie kidogo kuhusu hili suala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jithada ambazo Serikali imekuwa ikichukua katika kuimarisha hizi reli ikiwemo reli ya *TAZARA* nimeona Serikali imetenga shilingi bilioni 26 ambazo ni kwa ajili ya kulipa madeni. Lakini mimi naona hii reli ni muhimu sana katika kusaidia maendeleo ya Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na reli hii ndiyo inayotumika na nchi ya Zambia, Malawi na Congo na inasaidia sana katika kusaidia mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba wataleta sheria ya kurekebisha. Nataka kujua ni mkakati gani ambao upo badala ya kulipa madeni, sasa hizi fedha ziende kununua vichwa vya treni ili viweze kusaidia katika kuweza kusafirisha hii mizigo na kuweza kuimarisha hii *TAZARA* ambayo itasaidia sana katika kuleta maendeleo? Kama sitapata maelezo ya kutosha nitashika mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri mshahara huo.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali kuwa ni kweli hizo pesa tulizotenga ni kwa ajili ya madeni lakini tuna

mpango maalum ambao kuna mazungumzo sasa hivi yanaendelea baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Zambia na wenzetu wa China kuhakikisha kwamba tunapata vifaa muhimu ikiwemo vichwa vya treni ili kuhakikisha kwamba treni yetu ya TAZARA inaweza kufanya kazi inavyotakiwa. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hasunga.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naridhika na majibu aliyoyatoa lakini naomba niseme wajaribu kuharakisha ili kufikia mwezi Oktoba tupate majibu kamili nini hatua ya Serikali...

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Vulu.

MHE. ZAYNABU M. VULU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa mujibu wa sera tunayokwenda nayo ya uchumi wa viwanda umuhimu wa barabara ni kitu kimoja ambacho lazima kipewe kipaumbele na hili limetokana na ahadi nyingi zilizotolewa na viongozi wetu wakuu, Rais wa Awamu ya Nne na Awamu ya Tano.

Swali langu nataka kujua hizi ahadi ambazo zimetolewa katika ujenzi wa barabara ikiwemo barabara ya kutoka Mpuyani kwenda Vikumbulu, Mzenga kwenda Mlandizi, Mlandizi kwenda Maneromango, Makofia kwenda Mlandizi, Kisiju mpaka Mkuranga, Bungu mpaka Nyamisati, ni lini Mheshimiwa Waziri atatuambia zitajengwa ili nisichukue mshahara wake? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaelewa anachokiongea Mheshimiwa Vulu na nimhakikishie tu ahadi zote ambazo viongozi wetu wakuu walizitoa Serikali ya Awamu ya Tano na ya Nne, zote tutazitekeleza kwa awamu kwa kadri ambavyo bajeti tunazipanga. Hatuwezi kufanya vyote kwa wakati mmoja au mwaka mmoja wa fedha,

ukiangalia bajeti ya mwaka huu iko tofauti na ya mwaka jana na bajeti itakayofuata mwaka unaofuata itakuwa tofauti na hii na yote hii tunalenga kutekeleza ahadi ya viongozi wetu wakuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizi zote alizozitaja najua Mheshimiwa Jafo yuko hapa tutashirikiana nae na kuhakikisha kila fedha wanayopata kutoka Mfuko wa Barabara zinatumika vizuri kuhakikisha tunatekeleza ahadi hizo za Mheshimiwa Rais.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ryoba Chacha.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu kwakuongea niliongela mambo mawili; barabara ya Tarime -Mugumu ambayo inasaidia kuleta watalii wanaotoka *Kenyatta International Airport*, lakini pia niliongelea barabara ya Mkoa wa Mara inayounganisha Mkoa wa Mara na Mkoa wa Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sera za ujenzi wa barabara za lami *priority* ya kwanza ni kuunganisha Mkoa na Mkoa. Hapa tulikuwa tunabishana kuhusu ujenzi wa reli ya kutoka Tanga kwenda Musoma haieleweki! Nimekuwa niko mdogo naisikia, sasa kuunganisha barabara ya lami kati ya Mkoa wa Mara na Mkoa wa Arusha nayo bado inasua sua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitachukua shilingi kama sikupata maelezo ya kueleweka kwamba mwaka jana...

MWENYEKITI: Mheshimiwa umeshachukua shilingi na muda wenyewe umeisha. Ngoja majibu. Mheshimiwa Waziri. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mbunge wa Serengeti, Mheshimiwa Chacha Ryoba kwamba ni kweli tumechelewa sana kufikiria ni namna gani tutaunganisha Mkoa wa Mara na Arusha na hii inatokana na uwepo wa mbuga zetu za wanyama ambazo zinaangaliwa kimataifa na kuna Mashirika mengi ya Kimataifa yanayoangalia hizo mbuga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani unafahamu kwamba kutokana na *pressure* tulioita sisi kuitia Serikali ya Awamu ya Nne, sasa tumekubaliana, Wajerumani wanatusaidia kutafuta *southern bypass* itakayotuwezesha sasa kuunganisha Mkoa wa Arusha na Mara kama ambavyo tumekusudia muda mrefu. Anafahamu kuna bajeti ipo na hiyo barabara anazifahamu na vipande vingine vimeshaanza kujengwa. Nikuombe tu tuna nia ya dhati ya kukamilisha kujenqa hiyo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa hivi *KfW* wanaendelea na *feasibility study and detailed design* kuanza kuamua katika zile barabara mbili ipi ikubalike na Wajerumani kwamba hiyo ndiyo itakuwa *southern bypass* na tayari watu wako kazini *field* wanaifanya hiyo kazi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ryoba, Serikali imeshaweka *commitment* muda wetu umekwisha na Kanuni zinaruhusu kufunga mijadala.

Kwa hiyo, baadae utakaan naye na mimi nitakusaidia ukae nae akupe majibu ya ziada. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaingia kwenye *guillotine*.

Kif. 1001 – Administration and

HR Management Shs. 1,716,521,000/-

Kif. 1002 – Finance and Accounts Shs. 279,314,000/=

Kif.1003 – Policy and Planning Shs. 294,942,000/=

Kif. 1004 – Internal Audit UnitShs. 180,643,000/=

Kif. 1005 – Legal Unit Shs. 105,220,000/=

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kif. 1006 – *Government Comm. Unit* Shs. 229,454,000/=
Kif. 1007 – *Procurement Mgt. Unit* Shs. 208,669,000/=
Kif. 1008 – *Management Infor. System* Shs. 139,552,000/=
Kif. 2001 – *Communication Division* Shs. 588,952,000/=
Kif. 2002 – *Information, Communication
and Technology* Shs. 360,872,000/=
Kif. 3003 – *Science and Technology* Shs. 0/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 98 – Ujenzi

Kif. 1001 – *Administration and
HR Management* Shs. 2,262,142,082/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit* Shs. 405,447,500/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning Division* Shs. 318,448,900/=
Kif. 1004 – *Government Comm. Unit* Shs. 132,661,800/=
Kif. 1005 – *Procurement Mgt. Unit* Shs. 160,473,700/=
Kif. 1006 – *Internal Audit Unit* Shs. 105,050,600/=
Kif. 1007 – *Legal Services Unit* Shs. 102,604,700/=
Kif. 1008 – *Information Comm.Techn.* Shs. 98,055,800/=
Kif. 2002 – *Technical Services Divison* Shs. 13,285,340,700/=
Kif. 2005 – *Roads Development Div.* Shs. 16,843,785,118/=
Kif. 5002 – *Safety and Environ. Div.* Shs. 301,963,400/=
Kif. 6001 – *Airport Construction Unit* Shs. 107,267,700/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 62 - Uchukuzi

Kif. 1001 – *Administration and
HR Management* Shs. 1,839,085,000/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts* Shs. 440,113,000/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning* Shs. 656,939,000/=
Kif. 1004 – *Government Comm.Unit* Shs. 128,929,000/=
Kif. 1005 – *Procurement Mgt. Unit* Shs. 125,995,000/=
Kif. 1006 – *Internal Audit Unit* Shs. 137,240,000/=
Kif. 1007 – *Legal Services Unit* Shs. 151,446,000/=

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kif. 1008 – *Info.and Comm. Tech. Unit*Shs. 173,291,000/=
Kif. 2005 – *Transport Infrastructure Div.*Shs. 227,007,000/=
Kif. 2006 – *Transport Services Division*Shs. 86,967,431,000/=
Kif. 5002 – *Transport Safety and Environment Division*Shs. 294,549,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 62 – Uchukuzi

Kif.1003 - *Policy and Planning* Shs. 8,285,183,000/=
Kif. 2005 – *Transport Infrast. Div.*Shs. 1,887,850,000,000/=
Kif. 2006 – *Transport Services Div.*Shs. 581,796,000,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 68 – Mawasiliano

Kif. 1003 – *Policy and Planning* Shs. 200,000,000/=
Kif. 2001 – *Communication Division* Shs. 3,800,000/
=
Kif. 2002 – *Information, Communication
and Technology*.... Shs. 10,000,000,000/=
Kif. 3003 – *Science and Technology* Shs. 0/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 98 – Ujenzi

Kif. 1003 – *Policy and Planning Div.* Shs. 250,000,000/=
Kif. 2002 – *Technical Services Division* ...Shs. 22,450,000,000/=
Kif. 2005 – *Roads Develop. Div.*.... Shs. 1,694,013,792,000/=
Kif. 5002 – *Safety and Environment Div.* ... Shs. 2,500,000,000/=

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kif. 6001 – *Airport Construction Unit* ... Shs.176,368,640,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

NDG. NENELWA M. WANKANGA – KATIBU MEZANI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(*Bunge Lilirudia*)

MWENYEKITI: Tukae. Mtoa hoja.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge limekaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi yake. Naomba kwamba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(*Makofii*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi,
Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka 2017/2018
yalipitishwa na Bunge*)

MWENYEKITI: Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wako kwa kazi nzuri mliyofanya na majibu sahihi mliyoyatoa. Inaonesha Wizara hii mnaitendea haki na tunategema pesa zilizotengwa mwaka huu zote zitakuja na zifanye kazi kama inavyotakiwa.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, kwenye mshahara wa Waziri, mengi ambayo yameombwa sio masuala ya kisera. Kwa vile tunajifunza, Kiti kinajaribu tu ku-accommodate lakin naomba kila siku tujaribu kujifunza, tuwe na maswali ya kisera ambayo yataweza kuifanya Serikali iwe na *commitment* za dhati kwenye *issue* ambazo zinawakuta kwenye maeneo yenu ambayo mpo.

Lakini na mimi nawashukuru Wabunge kwa kazi nzuri mlizofanya toka Bajeti ya Wizara hii ianze. Mmefanya kazi nzuri sana na niwashukuru wote. (*Makofi*)

Naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 2.13 Usiku Bunge lilahirishwa Mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 3 Mei, 2017, Saa Tatu Asubuhi)